

**UTENDAJI KATIKA NYIMBO ZA NGOMA YA WASAMBAA: MIFANO  
KUTOKA *MDUMANGE* NCHINI TANZANIA**

**NA**

**RAMADHANI THOMAS KADALLAH**

**Tasnifu hii imewasilishwa katika Kitivo cha Fani na Sayansi za Kijamii ili  
kutimiza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Idara ya Kiswahili  
na Lugha Nyingine za Kiafrika**

**Chuo Kikuu cha Moi**

**Novemba, 2018**

## **IKIRARI**

### **Ikirari ya Mzamifu**

Kazi hii ni utafiti wangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada yoyote. Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kutoleshwa nakala bila idhini na ridhaa ya mzamifu na (au) Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi.....Tarehe.....

**Ramadhani Thomas Kadallah**  
(SASS/DPHIL/KIS/04/14)

### **Ikirari ya Wasimamizi**

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi.....Tarehe.....

Dkt. Mwanakombo Noordin  
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika  
Chuo Kikuu cha Moi

Sahihi.....Tarehe.....

Dkt. Magdaline Wafula  
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika  
Chuo Kikuu cha Moi

**HAKIMILIKI**

Sehemu yoyote ya tasnifu hii, hairuhusiwi kubadilishwa, kwa njia yoyote iwayo, iwe ya kieletroniki, kunakilisha, au ya kurudufu, bila ya kupata idhini ya maandishi, kutoka kwa mwandishi wa Tasnifu hii au Chuo Kikuu cha Moi kwa niaba yake.

## **TABARUKU**

Ninaitabaruku kazi hii kwa wazazi pamoja na walezi wangu wapendwa kwa juhudi zao za kunilea na kunielimisha hadi kufikia hatua hii. Kwanza ninaitabaruku kazi hii kwa baba yangu mpendwa, marehemu mzee Thomas Kadallah. Pili, ninaitabaruku kazi hii kwa mama yangu mpendwa, marehemu Bi. Mwanahamisi Juma ambaye pia aliaga dunia mwaka 2008. Tatu, ninaitabaruku kazi hii kwa baba yangu mlezi Mzee Said Kikwa aliyenilea tangu 1990 mpaka mwaka 2016 alipoaga dunia. Ingawa mlishatangulia mbele ya haki, ninaamini kuwa sala zenu kwangu zimenisaidia sana maishani hata mpaka nimefikia hatua hii.

Pumzikeneni kwa amani.

## SHUKURANI

Awali ya yote ninatoa shukrani zangu za pekee kwa Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbinu na ardhi kwa kunipa nguvu na uwezo wa kukamilisha kazi hii. Kisha, shukrani zangu zisizo na kifani ziwaendee wasimamizi wangu kutoka Chuo Kikuu cha Moi, ambao ni Dkt. Mwanakombo Noordin na Dkt. Magdaline Wafula. Kutokana na mawaidha na ushauri wa wasimamizi hawa nimepata busara, mwongozo na mwelekeo angavu nilipopatwa na vuguvugu la kutofahamu njia ambayo ningefuata katika bahari hii ya usomi na utafiti. Kwa pamoja ninatoa pongezi zangu za dhati kwenu kwa namna mlivyoniipatia changamoto mbalimbali za kazi yangu kwa makini na kuniwezesha kuukamilisha utafiti wangu hadi kufikia hatua hii. Aidha, mawaidha yenu mema yalinitia ari na mshawasha wa kuwaza, kutafakari zaidi na kuandika kazi hii. Mola akuzidishieni umri na kulipeni kila la kheri muzidi kuelekeza umma juu ya hekima ihusuyo tafakuri ulimwengu.

Shukrani pia za pekee nazitoa kwa Mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi, Dkt. Mosol Kandagor. Kutokana na ukarimu wake hakuchoka kusoma kazi yangu na kunipatia maoni mbalimbali. Mara kwa mara alinipatia uhakiki pamoja na maoni ambayo ninakiri kuwa yaliupatia utafiti huu sura iliyo nayo. Kwa masahihisho na mawaidha yake namshukuru na kumwomba Mola azidi kumpa maarifa na neema zaidi. Kadhalika, utafiti huu umekamilika baada ya kupata ushauri wa kitaalamu na kiusomi kutoka kwa wahadhiri mbalimbali kutoka Chuo Kikuu cha Moi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Nakupeni shukrani kwa kazi bora ya mwongozo mlionipatia katika harakati yangu ya kusomea shahada ya uzamifu.

## IKISIRI

Licha ya maendeleo ya sayansi, teknolojia na habari bado turathi za kifasihi simulizi zikiwemo nyimbo zingali zinaheshimiwa na jamii nyingi za Kiafrika kwa kuwa ni tunu inayotumika kuhifadhi historia, kuendeleza amali za jamii na pia ni chemchemi ya burudani. Kutokana na umuhimu wa nyimbo katika jamii, utafiti huu umechunguza utendaji wa nyimbo za *mdumange* kutoka jamii ya Wasambaa wa Lushoto, Tanga – Tanzania kwa minajili ya kutathmini nafasi ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika mwonoulimwengu wa Wasambaa. Madhumuni mahsusi ya utafiti huu yalikuwa: (i) Kupambanua jinsi miktadha ya kijamii inavyochochea utendaji wa nyimbo za *mdumange*; (ii) Kuchanganua usawiri wa maisha ya Wasambaa kupitia mitindo ya lugha inayotumika katika nyimbo za *mdumange* na; (iii) Kujadili nafasi ya mitindo ya viziada lugha kwa wasanii wa nyimbo za *mdumange* na jamii ya Wasambaa kwa ujumla. Data zilikusanywa nyanjani kwa kutumia mikakati ya uchunguzi shiriki, usaili na mijadala ya vikundi. Vifaa vilivyotumika vilikuwa kamera, kinasa sauti na redio kaseti. Uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia za Utendaji wa Maigizo pamoja na Semiotiki ya Kijamii. Kulingana na Nadharia ya Utendaji wa Maigizo, utendaji ni tukio la aina yoyote ile linalowajumuisha hadhira pamoja na fanani wake kwa minajili ya kuigiza au kuonyesha tabia za wanadamu. Nadharia hii ilichaguliwa kwa kuwa katika jamii nyingi za Kiafrika utendaji ni mojawapo ya kanuni za maisha ya kila siku. Kutokana na mihimili ya Nadharia hii, utendaji unachukuliwa kuwa ndicho kiungo cha fasihi simulizi chenye uwezo wa kudhihirisha ujumi na diskosi za wanajamii. Kwa upande mwingine, Nadharia ya Semiotiki ya Kijamii ilitumika kwa minajili ya kupambanua misimbo au ishara zinazohusika wakati wa utendaji. Wafuasi wa Nadharia hii wanaeleza kuwa Semiotiki huchunguza maana katika ishara pamoja na kuonyesha uhusiano kati ya ishara husika na mifumo mbalimbali ya jamii. Kimsingi, kupitia utafiti huu imegundulika kuwa nyimbo za *mdumange* ni sanaa thabiti ya Wasambaa iliyosheheni vipashio mbalimbali vya ujumi, hususan lugha na viziada lugha. Kadhalika, kupitia utafiti huu imedhihirishwa kuwa utendaji wa fanani na hadhira unaimarishwa na mitindo ya lugha na viziada lugha. Kwa kutumia mitindo hiyo, fanani na hadhira wanajadili itikadi mbalimbali za maisha ya Wasambaa kijamii, kisiasa, na kiuchumi. Kwa ujumla, utafiti huu umegundua kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* umekuwa ukichochea na miktadha anuai ya Wasambaa kama vile turathi simulizi, mwingiliano na jamii nyingine pamoja na mfumo wa maisha ya Wasambaa unaodhihirika kwenye sherehe za harusi, dini na siasa. Imegundulika pia kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* una nafasi kubwa katika jamii ya sasa ya Wasambaa. Nyimbo hizo hutumika kwa minajili ya kuburudisha, kuelimisha, kuhifadhi turathi na kufasiri mwonoulimwengu wa Wasambaa. Pamoja na matokeo haya, utafiti huu umependekeza kuwa ipo haja ya kuchunguza utendaji wa nyimbo nyingine za jamii, hususan nyimbo za maombolezo.

## ABSTRACT

In spite of the development of science, technology and information, orally transmitted cultural heritage including songs are perfectly sound as they are respected by many African communities because they are precious values that are being used for historical preservation, promoting social values as well as for exploring entertainment aesthetics. Due to significant roles played by songs in the society, this research has examined the performance of *mdumange* songs from Sambia community of Lushoto, Tanga – Tanzania. The purpose of the study was to assess the significance of *mdumange* songs performance in reflecting and affecting the Sambia worldviews. In addition, the objectives of this study were (i) to discern the way social contexts have promoted the emergence of *mdumange* songs performance; (ii) to analyse the role of language styles in songs transmission and reflecting the Sambia worldview; and (iii) to discuss the significance of paralinguistic devices in *mdumange* songs performance among the artists and the Sambia community in general. The data was collected in the field by using participatory, interviews and group discussion methods. Devices used were camera, audio recorder and radio cassette. Data analysis was guided by the theories of Theatre Performance and Social Semiotics. According to the theory of Theatre Performance, performance is any event involving the artist and his audience for play or displaying human behavior. This theory was chosen because in many African communities performance is one of the principles of everyday life. In short, from the beams of this theory, the performance is considered as the literary link capable of exploring aesthetics and various discourses concerning worldviews of the society. On the other hand, Social Semiotics theory was used for describing the symbols or codes used in the song performance. Supporters of this theory point out that Social Semiotic theory investigate the symbols reflected in literature. Briefly, this theory has informed us that *mdumange* songs performance is highly related to the social context of the Sambia community. The results indicate that the performance of the *mdumange* songs by the Sambia people is characterised with the use of the language and paralinguistic aesthetics. It has been found that the performance of the songs of *mdumange* have a great role in the current society of the Sambia. These songs are to entertain, to educate, to preserve heritage and interpret Sambia worldviews. With these results, the study suggests that there is a need to investigate the performance of other songs, especially dirge songs.

## YALIYOMO

|   |          |
|---|----------|
| IKIRARI .....   | ii       |
| HAKIMILIKI.....   | iii      |
| TABARUKU .....  | iv       |
| SHUKURANI.....  | v        |
| IKISIRI .....   | vi       |
| ABSTRACT.....   | vii      |
| YALIYOMO.....   | viii     |
| ORODHA YA MAJEDWALI.....                                  | xiii     |
| ORODHA YA VIELELEZO.....                                  | xiv      |
| VIFUPISHO.....  | xv       |
| UFAFANUZI WA ISTILAHI ZILIZOTUMIKA .....                  | xvi      |
| <b>SURA YA KWANZA .....</b>                               | <b>1</b> |
| <b>MISINGI YA UTAFITI .....</b>                           | <b>1</b> |
| 1.0 Utangulizi.....                                       | 1        |
| 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti .....                       | 1        |
| 1.1.1 Historia Fupi ya Wasambaa .....                     | 3        |
| 1.1.2 Shughuli za Kiuchumi katika Jamii ya Wasambaa ..... | 4        |
| 1.1.3 Mila na Desturi za Wasambaa.....                    | 5        |
| 1.1.4 Utafiti wa Fasihi Simulizi ya Wasambaa .....        | 8        |
| 1.1.5 Utendaji katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika .....   | 11       |
| 1.2 Suala la Utafiti .....                                | 13       |
| 1.3 Madhumuni ya Utafiti.....                             | 14       |
| 1.4 Maswali ya Utafiti.....                               | 15       |
| 1.5 Mawanda ya Utafiti.....                               | 15       |
| 1.6 Sababu za Uteuzi wa Mada ya Utafiti.....              | 16       |
| 1.7 Mbinu za Utafiti .....                                | 18       |
| 1.7.1 Uteuzi wa Sampuli .....                             | 19       |
| 1.7.1.1 Mikakati ya Sampuli Kimakusudi .....              | 19       |
| 1.7.1.2 Sampuli Bahati Nasibu .....                       | 22       |
| 1.7.2 Vifaa vya Utafiti .....                             | 24       |
| 1.7.2.1 Watafiti Wasaidizi .....                          | 25       |
| 1.7.2.2 Redio Kaseti na Kinasa Sauti .....                | 26       |



|   |           |
|---|-----------|
| 1.7.2.3 Kamera ya Kidijitali .....  | 27        |
| 1.7.3 Mikakati ya Ukusanyaji Data .....   | 27        |
| 1.7.3.1 Uchunguzi Shiriki.....  | 28        |
| 1.7.3.2 Usaili .....  | 28        |
| 1.7.3.3 Majadiliano ya Vikundi.....   | 29        |
| 1.7.4 Uchambuzi wa Data .....   | 31        |
| 1.8 Itikeli.....  | 32        |
| 1.9 Hitimisho.....  | 32        |
| <b>SURA YA PILI.....</b>  | <b>33</b> |
| <b>MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA KINADHARIA .....</b>                                  | <b>33</b> |
| 2.0 Utangulizi.....   | 33        |
| 2.1 Historia na Ethnografia ya Wasambaa.....  | 33        |
| 2.2 Sanaa Jadiya na Sanaa za Maonyesho .....  | 37        |
| 2.2.1 Sanaa Jadiya ya Kiafrika .....  | 37        |
| 2.2.2 Sanaa za Maonyesho .....  | 43        |
| 2.3 Nyimbo kama Utanzu wa Sanaa za Maonyesho na Fasihi Simulizi.....                        | 48        |
| 2.3.1 Nyimbo Kama Utanzu wa Sanaa za Maonyesho .....  | 49        |
| 2.3.2 Nyimbo Kama Utanzu wa Fasihi Simulizi.....  | 56        |
| 2.4 Misingi ya Ujumi wa Nyimbo .....  | 63        |
| 2.4.1 Misingi ya Kimwingiliano Matini .....   | 64        |
| 2.4.2 Misingi ya Kiuamilifu .....   | 69        |
| 2.4.3 Misingi ya Utendaji .....   | 74        |
| 2.5 Kiunzi cha KiNadharia .....   | 82        |
| 2.5.1 Nadharia ya Utendaji wa Maigizo.....  | 83        |
| 2.5.2 Nadharia ya Semiotiki ya Kijamii .....  | 87        |
| 2.6 Hitimisho.....  | 91        |
| <b>SURA YA TATU.....</b>  | <b>92</b> |
| <b>UTENDAJI WA NYIMBO ZA MDUMANGE KATIKA MIKTADHA ANUWAI<br/>YA JAMII YA WASAMBAA .....</b> | <b>92</b> |
| 3.0 Utangulizi.....   | 92        |
| 3.1 Turathi Simulizi za Wasambaa .....  | 92        |
| 3.2 Mtagusano wa Kijamii .....  | 100       |
| 3.3 Matukio ya Sherehe za Wasambaa .....  | 104       |
| 3.3.1 Harusi .....  | 105       |

|  |            |
|--|------------|
| 3.3.2 Sikukuu za Kidini .....                                    | 108        |
| 3.3.3 Hafla za Kisiasa.....                                      | 114        |
| 3.3.3.1 Kampeni za Uchaguzi .....                                | 115        |
| 3.3.3.2 Hafla za Sikukuu ya Wafanyakazi .....                    | 120        |
| 3.3.3.3 Hafla za Mbio za Mwenge .....                            | 122        |
| 3.4 Hitimisho.....   | 125        |
| <b>SURA YA NNE .....</b>   | <b>126</b> |
| <b>MITINDO YA LUGHA NA DHIMA YAKE KATIKA KUWASILISHA</b>         |            |
| <b>UJUMBE KWA HADHIRA .....</b>                                  | <b>126</b> |
| 4.0 Utangulizi.....  | 126        |
| 4.1 Mtindo wa Kuchanganya Misimbo.....                           | 126        |
| 4.1.1 Kisambaa na Kiswahili.....                                 | 127        |
| 4.1.2 Kiswahili na Kingereza .....                               | 129        |
| 4.1.3 Kisambaa na Kingereza.....                                 | 130        |
| 4.2 Mitindo ya Arudhi za Kishairi .....                          | 132        |
| 4.2.1 Vina na Mizani .....                                       | 134        |
| 4.2.2 Mshororo, Ubeti na Kibwagizo .....                         | 137        |
| 4.2.2.1 Mwimbaji Mkuu Mmoja na Waitikiaji .....                  | 138        |
| 4.2.2.2 Waimbaji Wakuu Wawili na Waitikiaji .....                | 142        |
| 4.3 Mtindo wa Mianza na Miisho ya Kifomula.....                  | 145        |
| 4.3.1 Fomula za Ufunguzi .....                                   | 145        |
| 4.3.2 Fomula za Uhitimishaji .....                               | 148        |
| 4.3.3 Fomula za Kibwagizo cha Kubadilishia Wimbo.....            | 150        |
| 4.4 Mitindo ya Tamathali za Usemi, Methali, Nahau na Misemo..... | 152        |
| 4.4.1 Tamathali za Usemi.....                                    | 152        |
| 4.4.1.1 Tanakali za Sauti .....                                  | 152        |
| 4.4.1.2 Tashititi.....   | 154        |
| 4.4.1.3 Tasfida .....  | 159        |
| 4.4.1.4 Tashihisi .....  | 163        |
| 4.4.2 Matumizi ya Methali .....                                  | 164        |
| 4.4.3 Matumizi ya Misemo na Nahau .....                          | 167        |
| 4.5 Hitimisho.....   | 170        |

|   |            |
|---|------------|
| <b>SURA YA TANO .....</b>   | <b>171</b> |
| <b>NAFASI YA MITINDO YA VIZIADA LUGHA KWA WASANII NA JAMII YA WASAMBAA KWA UJUMLA .....</b> | <b>171</b> |
| 5.0 Utangulizi.....   | 171        |
| 5.1 Miondoko ya Fanani na Hadhira.....  | 171        |
| 5.1.1 Miondoko Inayofafanua Ujumbe wa Nyimbo.....   | 172        |
| 5.1.2 Miondoko ya Hadhira Kupongeza Utendaji wa Fanani .....                                | 177        |
| 5.1.3 Miondoko Inayoweza Mawasiliano Miongoni mwa Fanani.....                               | 179        |
| 5.2 Utendaji wa Kimuziki .....  | 182        |
| 5.2.1 Muziki wa Sauti za Uimbaji.....   | 183        |
| 5.2.2 Muziki wa Ala katika Nyimbo za Mdumange .....   | 189        |
| 5.2.2.1 Ala Zinazotoa Sauti za Kimuziki kwa Njia ya Kupigwa .....                           | 189        |
| 5.2.2.1.1 Ngoma za Asili .....  | 189        |
| 5.2.2.1.2 Ngoma za Kisasa.....  | 194        |
| 5.2.2.1.3 Manyanga.....   | 195        |
| 5.2.2.2 Ala Zinazotoa Muziki kwa Njia ya Kupulizwa.....                                     | 196        |
| 5.2.2.2.1 Tarumbeta .....   | 196        |
| 5.2.2.2.2 Filimbi, Gunda na Kipaza sauti .....  | 198        |
| 5.3 Maleba na Vifaa vya Kuigizia .....  | 201        |
| 5.3.1 Maleba ya Wasanii na Washiriki.....   | 201        |
| 5.3.2 Vifaa vya Ugizaji wa Fanani .....   | 210        |
| 5.4 Jukwaa na Uchezaji Dansi .....  | 214        |
| 5.4.1 Miundo ya Jukwaa la Utendaji .....  | 214        |
| 5.4.1.1 Jukwaa la Muundo wa Duara .....   | 215        |
| 5.4.1.2 Jukwaa la Muundo wa Steji.....  | 216        |
| 5.4.2 Mitindo ya Uchezaji Dansi.....  | 220        |
| 5.5 Hitimisho.....  | 224        |
| <b>SURA YA SITA.....</b>  | <b>225</b> |
| <b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>  | <b>225</b> |
| 6.0 Utangulizi.....   | 225        |
| 6.1 Muhtasari wa Tasnifu .....  | 225        |
| 6.2 Mahitimisho ya Utafiti.....   | 228        |
| 6.2.1 Jinsi Miktadha ya Kijamii Iliyochochea Utendaji wa Nyimbo .....                       | 229        |
| 6.2.2 Mitindo ya Lugha na Dhima yake katika Kuwasilisha Ujumbe .....                        | 232        |

|  |     |
|--|-----|
| 6.2.3 Nafasi ya Mitindo ya Viziada Lugha kwa Wasanii na Jamii .....            | 233 |
| 6.3 Mchango wa Utafiti .....   | 234 |
| 6.4 Mapendekezo ya Utafiti huu .....   | 234 |
| 6.5 Mapendekezo kwa Ajili ya Tafiti za Baadaye .....                           | 235 |
| MAREJELEO .....  | 236 |
| VIAMBATISHO.....   | 243 |
| Kiambatisho cha 1: Mwongozo wa Maswali Ya Usaili Nyanjani .....                | 243 |
| Kiambatisho na. 2: Mwongozo wa Maswali katika Mijadala ya Vikundi .....        | 247 |
| Kiambatisho na. 3: Watafitiwa Walioshiriki Usaili na Mijadala ya Vikundi ..... | 248 |
| Kiambatisho cha 4: Nyimbo za <i>Mdumange</i> .....                             | 249 |
| Kiambatisho na. 5: Fomula za Ufunguzi .....                                    | 281 |
| Kiambatisho na. 6: Fomula za Uhitimishaji .....                                | 283 |
| Kiambatisho na. 7: Kibwagizo cha Kuhitimishia au Kubadilishia Wimbo .....      | 285 |
| Kiambatisho cha 8: Vibali vya Utafiti.....                                     | 290 |
| 8.1: Idhini ya Kufanya Utafiti Nyanjani Kutoka Chuo Kikuu Cha Moi .....        | 290 |
| 8.2: Barua ya Kuomba Kibali cha Utafiti katika Wilaya ya Lushoto.....          | 291 |
| 8.3: Kibali cha Utafiti kutoka kwa Afisa Utamaduni wa Wilaya ya Lushoto.....   | 292 |
| 8.4: Idhini ya Watafitiwa.....   | 293 |

**ORODHA YA MAJEDWALI**

|  |    |
|--|----|
| Jedwali na 1: Sampuli ya Vijiji vya Utafiti na Idadi ya Wasailiwa .....  | 21 |
| Jedwali na 2: Sampuli ya Maonyesho na Hafla za Utafiti .....             | 22 |
| Jedwali na 3: Sampuli ya Nyimbo za <i>Mdumange</i> Zilizochambuliwa..... | 24 |

## ORODHA YA VIELELEZO

|  |     |
|--|-----|
| Kielelezo na 3.1: Wasanii wakiwa wamechuchumaa wakati wa kuimba.....             | 96  |
| Kielelezo na 5.1: Picha Inayoonyesha Ushiriki wa Hadhira.....                    | 177 |
| Kielelezo na 5.2: Picha Inayoonyesha Hadhira ikipeana Mikono na Wachezaji .....  | 178 |
| Kielelezo na 5.3: Picha Inayoonyesha Mawasiliano ya Wasanii kwa ishara .....     | 180 |
| Kielelezo na 5.4: MK akiwaamrisha wasanii .....                                  | 181 |
| Kielelezo na 5.5: Maumbo ya ngoma za Utendaji wa Nyimbo za <i>Mdumange</i> ..... | 190 |
| Kielelezo na 5.6: Picha Inayoonyesha Wanawake wakipiga ngoma.....                | 193 |
| Kielelezo na 5.7: Picha Zinazoonyesha Ngoma ya Bendi .....                       | 195 |
| Kielelezo na 5.8: Picha ya Msanii anayepuliza Manyanga.....                      | 196 |
| Kielelezo na 5.9: Matumizi ya Tarumbeta katika Nyimbo za <i>Mdumange</i> .....   | 197 |
| Kielelezo na 5.10: Picha Zinazoonyesha Kofia ya Usinga na y a Kishadda .....     | 202 |
| Kielelezo na 5.11: Picha Zinazoonyesha Kibwebwe .....                            | 204 |
| Kielelezo na 5.12: Picha za Wasanii waliovaa Masegele .....                      | 205 |
| Kielelezo na 5.13: Picha Zinazoonyesha Wasanii waliovaa Sare ya Kaniki .....     | 206 |
| Kielelezo na 5.14: Picha Zinazoonyesha Sare Maalum za Watendaji.....             | 208 |
| Kielelezo na 5.15: Picha inayoonyesha msanii aliyeshika mwengo.....              | 211 |
| Kielelezo na 5.16: Picha za Pembe na Gunda.....                                  | 212 |
| Kielelezo na 5.17: Picha inayoonyesha Muundo wa Ngao ya Sheuta.....              | 213 |
| Kielelezo na 5.18: Muundo wa Jukwaa (Nusu duara) .....                           | 215 |
| Kielelezo na 5.19: Muundo wa Jukwaa (duara kamili) .....                         | 216 |
| Kielelezo na 5.20: Muundo wa Jukwaa la Steji .....                               | 217 |
| Kielelezo na 5.21: Mistari ya Wachezaji katika Jukwaa la Steji .....             | 218 |

**VIFUPISHO**

|                 |                                   |
|-----------------|-----------------------------------|
| <b>CCM:</b>     | Chama cha Mapinduzi               |
| <b>CHADEMA:</b> | Chama cha Demokrasia na Maendeleo |
| <b>KE:</b>      | Mwanamke                          |
| <b>Khj:</b>     | kama hapo juu/keshatajwa          |
| <b>Kur.</b>     | Kurasa                            |
| <b>MBF:</b>     | Muziki wa Bongo Flewa             |
| <b>ME:</b>      | Mwanamume                         |
| <b>Mhar.</b>    | Mhariri                           |
| <b>MK:</b>      | Mwimbaji Kiongozi                 |
| <b>MUK:</b>     | Mshororo Uliimbwa kwa Kiswahili   |
| <b>Uk.</b>      | Ukurasa                           |
| <b>UKIMWI:</b>  | Ukosefu wa Kinga Mwilini          |
| <b>Wahr.</b>    | Wahariri                          |
| <b>WK:</b>      | Waimbaji Wasaidizi                |

## UFAFANUZI WA ISTILAHU ZILIZOTUMIKA

- Diskosi:** Ni mukhtadha wa kipekee katika mawasiliano.
- Kibwebwe:** Ni vazi la kisanaa linalovaliwa na wasanii wa nyimbo za mdumange. Vazi hili huvaliwa na wanaume pamoja na wanawake ambapo wawaaji wake hukunja kanga/kitenge au nguo nyingine na kisha huizunguka katika viuno vyao. Vazi hili hunoghesha utendaji kwa vile huwafanya wasanii wake waonekane na viuno vikubwa kuliko kawaida.
- Kidembwa:** Ngoma asili ya Wasambaa inayochezwa na wanawake peke yao. Nyimbo zinazoimbwa wakati wa utendaji wa ngoma hii huitwa ‘Nyimbo za Kidembwa’
- Mdumange :** Ngoma asili ya jamii ya Wasambaa, ambayo huambatana na uimbaji pamoja na uchezaji. Ngoma hii huchezwa ama na watu wa rika zote. Pia mara nyingi huwashirikisha wanaume na wanawake lakini mara chache huchezwa na wanaume peke yao. Katika utafiti huu tumetumia dhana ya ‘Nyimbo za *Mdumange*’ imetumika kurejelea nyimbo zinazoimbwa wakati wa kucheza ngoma hii.
- Msimbo:** Ni aina ya ujumbe unaoeleweka kwa kundi fulani la watu na kamwe haiwezi kueleweka na kundi lingine.
- Mwingilianotanzu:** Ni kuchanganyikana kwa matawi ya fasihi simulizi wakati wa utendaji. Mwingilianotanzu ni uimbaji wa maana kamili ya utanzu kutokana na utanzu mwingine. Hii ni hali ya tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiafrika kuvunja mipaka na kuchanganyikana wakati wa utendaji wake. Hali hii huiwezesha Fasihi Simulizi ya Kiafrika kutekeleza



wajibu wake. Kwa mfano, hadithi inapotongolewa inaweza kubeba tanzu kama vile methali, misemo na misimu ndani mwake; na hata wakati mwingine, kubadilika na kuwa wimbo badala ya hadithi

**Mwonoulimwengu** ni ufafanuzi au maelezo ya kimantiki kuhusu mpangilio wa mambo katika jamii na jinsi unavyoathiri maisha ya watu na mazingira yao. Maelezo hayo huanza kwa mtu mmoja mmoja kisha mawazo ya mtu binafsi husambazwa kwa watu wengine kupitia njia anuwai fasihi simulizi ikiwemo. Kutokana na mabadiliko yanayotokea katika jamii mawazo mapya huchipuka na kuchukua mahali pa mawazo yaliyotangulia au mawazo ya kale huimarishwa na kuwa bora zaidi. Mfumo huu wa mawazo hutupa picha au taswira ya jumla kuihusu hiyo jamii.

**Segele:** Ni vazi la kisanii lililotengenezwa kwa kutumia majani ya miti inayofanana na majani ya migomba na ambalo huvaliwa wakati wa kuwasilisha nyimbo za mdumange. Vazi hili huvaliwa na wanaume pamoja na wanawake ambapo majani husika husukwa vyema na kuzungushwa kiunoni. Wakati wa utendaji, segele hutoa sauti ya namna fulani.

**Ujumi:** Ni elimu ya sheria na kanuni za sanaa. Hii ni tawi la falsafa linaloshughulika na uzuri, ubaya au ladha.

**Utendaji:** Ni urudiaji wa kitendo cha kisanaa kwa namna mpya.

**Vipokeo:** Nyimbo zinazoimbwa na wanaume pamoja na wanawake wakati wa kuomboleza. Nyimbo hizi haziambatani na matumizi yoyote ya ala.

## **SURA YA KWANZA**

### **MISINGI YA UTAFITI**

#### **1.0 Utangulizi**

Katika utafiti huu tumeshughulikia mitindo ya utendaji wa nyimbo za ngoma ya Wasambaa iitwayo *mdumange*. Aidha, azma kuu ya utafiti huu ni kuchunguza nafasi ya mitindo ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika kusawiri na kuathiri maisha au ulimwengu wa Wasambaa. Sura hii ya kwanza imeangazia usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, umuhimu wa utafiti, maswali ya utafiti, mbinu pamoja na upeo wa utafiti.

#### **1.1 Usuli wa Suala la Utafiti**

Licha ya maendeleo ya sayansi, teknolojia na habari, turathi za kifasihi simulizi zingali zinaheshimiwa na kuenziwa na jamii nyingi za Kiafrika. Katika jamii za Kiafrika, turathi za kifasihi simulizi ni tunu adhimu sana kwa kuwa hutumika kama chemchemi ya kuhifadhi na kuendeleza amali za jamii. Kwa mujibu wa Finnegan (1970) na Owomoyela (2008) turathi za kifasihi simulizi zina umuhimu wa kipekee katika jamii nyingi za Kiafrika kutokana na jinsi muundo wake wa kiujumi ulivyofungamana na mfumo wa maisha ya Waafrika. Wataalamu hawa wanaeleza kuwa takribani kila tukio katika maisha ya Waafrika linaambatana na utendaji wa tanzu mbalimbali za kifasihi simulizi. Kulingana na Kobia (2008), katika jamii nyingi za Kiafrika utendaji ulijumuisha shughuli za kawaida za kila siku kama vile sherehe za kuzaliwa na kupewa jina kwa mtoto, tohara, mazishi na kutoa kafara kwa miungu. Hoja hii pia inasisitizwa na Matti (2009) anaposema kuwa katika jamii za Kiafrika, utendaji ni sehemu ya maisha ya kila siku.

Kushamiri kwa turathi za kifasihi simulizi tangu zamani mpaka wakati huu wa sayansi na teknolojia kunatufanya tuhoji sababu zinazowafanya Waafrika waendeleo kuzithamini. Aidha, utafiti huu unakusudia kudadisi kuwa kwa nini licha ya ugunduzi wa teknolojia mpya ya mawasiliano (uandishi, simu, komputa na runinga) jamii za Kiafrika zinaendelea kung'ang'ania turathi zake za tangu kale? Kulingana na Schechner (2013) kusudio la kuwasilisha kazi ya kisanaa mbele ya hadhira ni kuathiri na kubadili muelekeo wa jamii na sanaa inayotendwa. Ingawa Schechner anaona kuwa fasihi ina uwezo wa kuathiri na kubadili muelekeo wa jamii, kwa upande mwingine hata jamii inao uwezo wa kuathiri na kubadili muelekeo wa fasihi kadri jamii inavyobadilika kulingana na wakati. Kimsingi, ili kuona namna ambavyo nyimbo za *mdumange* zimeathiri na kuathiriwa na jamii ya Wasambaa, utafiti huu umeangazia uhusiano baina ya miktadha ya jamii ya Wasambaa na mitindo ya utendaji wa nyimbo katika kusawiri masuala mbalimbali yanayohusu ulimwengu wa Wasambaa.

Kadhalika, tumeangazia utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika jamii ya Wasambaa ili kupambanua sifa mahsusi za utendaji wa nyimbo husika kulingana na muktadha wa utamaduni wa Wasambaa. Tumefanya hivyo kwa sababu watafiti waliotangulia walisisitiza kuwa fasihi na utamaduni ni vitu viwili vinavyohusiana sana (Abdallah, 1973; Kezilahabi, 1981; Senkoro, 1988; Finnegan, 2007; na Mulokozi, 2002). Kwa kuzingatia kuwa muktadha wa utamaduni wa jamii huathiri muundo wa utendaji na uwasilishaji wa fasihi, katika sehemu ifuatayo tumefafanua muktadha wa Wasambaa kwa kujikita katika historia, uchumi, mila na desturi, na fasihi simulizi.

### 1.1.1 Historia Fupi ya Wasambaa

Masuala mbalimbali yanayohusu historia ya Wasambaa yamejadiliwa na wataalamu kadhaa wakiwemo Feierman (1972, 1974, 2000 na 2008). Kulingana na mtaalamu huyu Wasambaa ni Wabantu wanaoishi katika safu za milima ya Usambara, Kaskazini – Mashariki mwa Tanzania katika Wilaya ya Lushoto, mkoa wa Tanga (Kristina, 2009). Kiutawala eneo hili limegawanywa katika Wilaya tatu za Korogwe, Lushoto na Muheza. Utafiti huu umefanyikia katika Wilaya ya Lushoto. Aidha, kutokana na utaratibu wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wilaya ya Lushoto pia imegawanywa katika majimbo mawili ya uchaguzi: Lushoto na Mlalo. Kadhalika, tumehusisha vijiji mbalimbali kutoka majimbo yote mawili ya uchaguzi ndani ya Wilaya ya Lushoto.

Kwa ujumla, lugha inayotumika katika mawasiliano ya kila siku miongoni mwa Wasambaa ni Kisambaa.<sup>1</sup> Kulingana na Nkondokaya (2006), kando na Kisambaa, lugha nyingine zinazopatikana Lushoto ni Kichasu na Kimbugu. Nkondokaya anaendelea kueleza kuwa Kichasu kilitokana na Wapare waliohamia Lushoto kutoka Upareni mwaka 1780. Aidha, Wambugu waliohamia Lushoto kutoka Kenya mwaka 1890 walileta lugha ya Kimbugu.

Kwa upande wake Lawrence (2009), anaeleza kuwa Wasambaa ni kundi la jamii za Waswahili wanaopatikana katika mwambao wa Afrika Mashariki. Maelezo ya Lawrence (2009) yanaafikiana na hali halisi iliyopo katika jamii hii kwa sababu

---

<sup>1</sup> Lugha ya Kisambaa na jamii ya Wasambaa hutamkwa kwa namna tofauti tofauti kutegemea lahaja, athari za Kiswahili sanifu na athari za wageni hususan wakoloni. Kwa mfano, wakati wenyeji wa Wilaya ya Lushoto hupendelea kujiita Washambaa, na kuliita eneo lao Shambaai, maandiko mengi yaliyoandikwa na wageni yanataja matamshi kama vile *Wasambara*, *Washambala* na *Wasambaa* kuirejelea jamii ya Wasambaa. Vile vile maandiko hayo ya wageni yanataja *Sambaani* au *Usambaani*, *Shambalai*, na *Usambara* kurejelea eneo lote la Wilaya ya Lushoto (Feierman 1990). Katika utafiti huu tumetumia istilahi za *Wasambaa*, *Kisambaa* na *Usambaani* kurejelea jamii, lugha wanayotumia na eneo wanamoishi.

ingawa Kisambaa huzungumzwa katika mawasiliano ya kila siku, matumizi ya Kiswahili pia ni makubwa sana ndani ya jamii hii. Aidha, kuenea na kukua kwa Kiswahili ndani ya jamii hii kumetokana na biashara ya watumwa, mfumo wa elimu ya kikoloni, pamoja na harakati za kisiasa na mageuzi ya elimu baada ya uhuru. Mambo yote haya yamechochea kuongezeka kwa idadi ya watu katika Wilaya ya Lushoto, kukua kwa Kiswahili na kuingia kwa lugha nyinginezo katika Wilaya ya Lushoto hasa Kichasu na Kimbugu.

Kwa mujibu wa Feierman (1972) Wapare wanahusiana sana na Wasambaa kwa kuwa wote ni jamii za Kibantu, ilhali jamii ya Wambugu huhusiana na Wasambaa kwa kiwango kidogo sana kwa kuwa wao si Wabantu. Turathi za fasihi simulizi ya Wasambaa zinaonyesha kuwa Wambugu walihamia Lushoto kwa minajili ya kutafuta malisho ya mifugo wao. Aidha, Feierman (2000) anafafanua kuwa Wambugu walihamia Lushoto mwaka 1890 na kwamba asili yao ni eneo moja liitwalo Laikipya nchini Kenya. Kiini cha wageni hawa kuhamia Lushoto ni kufuata udongo wenye rutuba pamoja na mpangilio mzuri wa uongozi wa machifu wa kijadi.

Ufafanuzi wa Feierman pia unaelekeza kuwa kijiografia, Wilaya ya Lushoto inapatikana nchini Tanzania mkoa wa Tanga. Eneo hili linapakana na Wilaya ya Muheza na nchi ya Kenya upande wa Kaskazini. Upande wa Mashariki-Kusini imepakana na Wilaya ya Korogwe. Upande wa Magharibi imepakana na Wilaya ya Korogwe na Mkoa wa Kilimanjaro.

### **1.1.2 Shughuli za Kiuchumi katika Jamii ya Wasambaa**

Kwa mujibu wa Feierman (2008), udongo wenye rutuba pamoja na mvua ya kutosha ni mambo yaliyosaidia kuimarisha uchumi wa Wasambaa hususan kupitia shughuli za kilimo na biashara. Feierman (2008) anaongeza kuwa kutokana na hali hii, shughuli

kuu ya kiuchumi kwa Wasambaa ni kilimo cha mazao ya chakula na biashara. Mazao ya chakula yanayolimwa Lushoto ni mihogo, mahindi, maharagwe, mboga, na matunda. Aidha, mazao ya biashara yanayolimwa Lushoto ni chai, katani na miti ya mbao. Kutokana na kujihusisha mno na shughuli za kilimo, jamii ya Wasambaa kama zilivyo jamii nyingine za Kiafrika inathamini sana matumizi bora ya ardhi na utunzaji wa mazingira. Aidha, fasihi simulizi hususan nyimbo na ngoma za asili zimetumika sana kuelimisha jamii kuhusu madhara ya kuchafua mazingira pamoja na faida zitokanazo na utunzaji wa mazingira.

Aidha, mfumo huu wa uchumi pia umewafanya Wasambaa wathamini sana umuhimu wa ardhi, uwajibikaji na nafasi ya viongozi wa kijadi katika kusimamia nidhamu ya jamii. Viongozi wa kijadi walihusishwa na masuala ya kutabiri hali ya anga na kwamba kila mtu alipaswa kuonyesha heshima ya hali ya juu kwa viongozi hao. Kulingana na imani ya Wasambaa, heshima kwa kiongozi huleta neema na uasi kwa kiongozi ulileta balaa. Kutokana na imani hii, Wasambaa walijijengea utamaduni wa kufanya ibada za kuabudu miungu ya kijadi, na kufuata maelekezo yote ya kiongozi wao. Hali hiyo, iliimarisha umoja wa jamii na uthabiti wao kiutawala, kiutamaduni na kiuchumi.

### **1.1.3 Mila na Desturi za Wasambaa**

Mila na desturi ni vipashio vikuu vinavyojenga utamaduni wa jamii mbalimbali duniani. Aidha, suala la utamaduni ni muhimu sana katika utafiti huu kwa kuwa ndilo linalofungamana moja kwa moja na namna jamii inavyofafanua mwonoulimwengu wake. Kulingana na Vansina (1985) pamoja na Lewis (2002) tamaduni zote huwakilisha na kuwasilisha mwonoulimwengu fulani. Kadhalika, Winstone (2006) anaongeza kwa kusema kuwa tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ikiwemo ngano na

nyimbo zina uwezo mkubwa wa kusawiri mwonoulimwengu wa jamii za Kiafrika kupitia utendaji wake. Maelezo ya wataalamu hawa yanadokeza kuwa huwezi kufasiri barabara mwonoulimwengu wa watu fulani ikiwa hujauielewa utamaduni wao. Hii ni kwa sababu kila kundi la watu huulinda na kuusambaza utamaduni kwa njia mbalimbali kwa kutumia ngano, nyimbo, mashairi, sanaa ya uchoraji, na matambiko. Utafiti huu umechunguza namna utendaji wa nyimbo za *mdumange* umewazesha wasanii na hadhira kuumba dunia yao kisanaa na kuiwasilisha wakati wa utendaji mbele ya hadhira.

Ajjemy (1978) anaeleza kuwa miongoni mwa mambo yanayosisitizwa na jamii ya Wasambaa ni heshima. Aidha, suala la heshima lilitiliwa mkazo si tu katika ngazi ya kiutawala bali pia katika ngazi ya familia. Jamii ya Wasambaa huendesha mambo yake kwa kufuata mfumodume. Kulingana na Ngadala (2003), katika mfumodume mwanamume ndiye mwenye mamlaka ya juu ikilinganishwa na mwanamke. Mamlaka ya mwanamume yanadhihirika kwenye uhusiano wa ndoa, umiliki wa raslimali na usimamizi wa familia kwa ujumla. Kwa hiyo, baba wa familia ndiye kiongozi mkuu wa wanafamilia wengine, ikiwemo mama pamoja na watoto. Pia, mwanamume aliruhusiwa kuoza zaidi ya mke mmoja. Utamaduni huu uliimarisha imani kwamba, kuwa na idadi kubwa ya wanawake na watoto ilikuwa ishara ya utajiri alio nao mwanamume wa Kisambaa.

Kwa upande mwingine, Kitogo (2005) anaeleza kuwa mamlaka ya chini aliyonayo mwanamke yalidhihirika kupitia matukio mbalimbali yaliyofanywa na mwanamume pamoja na wanafamilia wengine dhidi yake. Hadhi na heshima ya mwanamke ilipatikana baada ya kuolewa. Mwanamke asiyeolewa alihesabika kuwa ni mtoto licha ya umri wake kuwa mkubwa. Wakati wa kuolewa ni lazima mwanamume atoe mahari

(ng'ombe na mbuzi) kwa wazazi wa mwanamke anayeolewa. Baada ya kuolewa mwanamke alipaswa kuzaa watoto wengi kwa minajili ya kuongeza kizazi cha ukoo wa mwanamume pamoja na kuongeza nguvu kazi ya familia. Kwa ujumla, uwajibikaji ni sifa kuu ambayo ilimfanya mwanamke wa Kisambaa aheshimike katika familia. Ikiwa mwanamke ataonyesha hali ya kutowajibika katika kazi za shambani, kuchunga mifugo na kulea/kuzaa watoto, hurejeshwa kwao. Hii inaonyesha kuwa katika jamii ya Wasambaa mwanamume ndiye mwenye mamlaka ya kumuoa na kumuacha mwanamke.

Kulingana na utamaduni huu, tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya jamii hii ikiwemo nyimbo na ngano zilitumika kuhamasisha malezi yanayojali utamaduni wa jamii ya Wasambaa (Ajjemy, 1978). Aidha, Ajjemmy anazidi kufafanua kuwa katika utambaji wa ngano, dhamira ya utii ilipewa kipaumbele, uzazi na malezi pia vilisisitizwa sana. Vilevile, dhamira ya kutunza mazingira ilipewa nafasi ya juu zaidi. Suala la uwajibikaji liliangaziwa kwa nafasi ya kipekee zaidi. Kwa kufanya hivyo, ustawi wa jamii uliimarishwa kupitia utambaji wa ngano, uimbaji wa nyimbo na uchezaji wa ngoma.

Kadhalika, katika utamaduni wa Wasambaa na Afrika kwa ujumla masuala ya malezi, uzazi na uwajibikaji yalihakimizwa sana. Kwa hiyo, kando na kujihusisha na dhamira za utunzaji mazingira, nyimbo, ngano na ngoma za Wasambaa zinatumika kuendeleza malezi, uzazi na uwajibikaji kwa mujibu wa utamaduni wa jamii husika. Ili kujadili umuhimu wa nyimbo za *mdumange* katika jamii ya Wasambaa, utafiti huu umechunguza mitindo mbalimbali ya utendaji wa nyimbo husika. Kwa ufupi, katika utafiti huu tumejikita katika kuchunguza dhima na nafasi ya mitindo ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika ulimwengu wa Wasambaa.



#### **1.1.4 Utafiti wa Fasihi Simulizi ya Wasambaa**

Kulingana na Matteredu (2000) historia ya utafiti wa fasihi simulizi ya Kiafrika ikiwemo jamii ya Wasambaa imepitia katika mihula mikuu mitatu, yaani kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na wakati wa uhuru. Kabla ya ukoloni, Wasambaa waliendesha mambo yao chini ya utawala wa kijadi ulioongozwa na machifu. Viongozi wa kijadi wanaokumbukwa zaidi katika jamii ya Wasambaa ni Mbega pamoja na Kimweri. Katika kipindi hiki fasihi simulizi iliimarishwa kwa kuwasilishwa na kutendwa kwenye hafla na sherehe za kijamii kama vile jando na unyago. Kipindi hiki, fasihi simulizi ilipevuka sana kwani kila tukio la kijamii liliambatana na utendaji wa sanaa mbalimbali za kifasihi simulizi.

Utawala wa kijadi ulikoma katika Karne ya 19 watawala wa kikoloni waliposhika hatamu za uongozi. Tangu 1885 mpaka 1914, Wasambaa walikuwa chini ya utawala wa Wajerumani. Mara baada ya kuangushwa kwa utawala wa Wajerumani, Wasambaa walikuwa chini ya utawala wa serikali ya Waingereza kuanzia mwaka 1914 mpaka 1960. Mifumo yote miwili ya serikali za kikoloni iliathiri makuzi na maendeleo ya fasihi simulizi ya Wasambaa. Kupitia mifumo ya dini na elimu, serikali ya Kijerumani ilifanikiwa kwa kiasi kikubwa kukusanya na kuweka fasihi na lugha ya Kisambaa katika maandishi. Kwa mujibu wa Beshu (1986), shirika la Bethel Mission kutoka Ujerumani lilifanya kazi kubwa ya kukusanya, kurekodi na kuweka msingi wa kuandika lugha ya Kisambaa. Wajerumani walikusanya na kuandika mambo ya Wasambaa yaliyohusu utawala, dini, na utamaduni kwa ajili ya kuandaa vitabu vya kufundishia katika shule za msingi.

Mbali na kuandika kuhusu dini, utawala na fasihi simulizi, Wajerumani pia waliiweka lugha ya Kisambaa katika maandishi kupitia miradi ya utunzi wa kamusi pamoja na

tafsiri ya kitabu kitakatifu cha Biblia (LangHeirinch, 1921). Mchango wa serikali ya Kijerumani katika kukuza na kuendeleza lugha na fasihi ya Kisambaa unaonekana kupitia ukusanyaji na uandishi wa msamiati wa lugha hii. Kutokana na juhudi hizo Wajerumani walifanikiwa kuandika na kuchapisha kamusi moja ya Kisambaa – Kijerumani (LangHeirinch, 1921).

Pamoja na kamusi hiyo, Wajerumani pia waliweka msingi imara wa kuandikwa kwa Kisambaa kwa kupendekeza utaratibu maalum wa maandishi. Tullemans (2006) anaeleza kuwa kutokana na jitihada hizo, mwaka 1969, shirika la Biblia Tanzania lilifanikiwa kuchapisha tafsiri ya Biblia ya Agano Jipya katika Kisambaa. Hata hivyo, wakati wa utawala wa serikali ya Waingereza jitihada hizi hazikuendelezwa na huo ukawa ndio mwanzo wa kuanguka na kufifia kwa utunzaji na utafiti wa fasihi simulizi ya Wasambaa.

Nchini Tanzania, utawala wa kikoloni ulikoma mwaka 1960. Kutoka kipindi hicho hali ya kutafiti na kuhifadhi fasihi simulizi ya makabila mbalimbali likiwemo kabila la Wasambaa ilidorora. Katika kipindi cha uongozi wa Mwalimu Nyerere kwa mfano, lugha za asili ikiwemo Kisambaa hazikupewa nafasi. Kiswahili pekee ndicho kilichosisitizwa kutumika katika elimu, vyombo vya habari na katika uongozi na siasa. Pia chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere Kiswahili kilitumika kuimarisha mfumo wa ujamaa uliolenga kustawisha undugu wa Watanzania. Hatimaye hata sera za lugha zilipendekeza matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kitaifa na lugha ya kufundishia. Kwa hivyo, tangu utawala wa Nyerere, Mwinyi, Mkapa na Kikwete turathi simulizi za Kiafrika nchini Tanzania hazijaimarishwa ipasavyo. Hali hii imerutubisha maendeleo ya Kiswahili kwa upande mmoja, na imezorotesha maendeleo ya turathi zinazoelezwa kwa lugha asili kwa upande mwingine (Rugemarila na Muzale, 2008).

Katika kipindi hiki, kudorora kwa fasihi simulizi ya Wasambaa na makabila mengine nchini Tanzania pia kumechochewa na mabadiliko ya kijamii yaliyozuka wakati huo. Miongoni mwa mabadiliko ya kijamii yaliyochangia kuzorota kwa uchunguzi wa turathi simulizi za Kiafrika baada ya uhuru ni maendeleo ya sayansi, teknolojia ya habari, mawasiliano na kukua kwa miji. Hatimaye, mabadiliko haya yamesababisha mielekeo mipya ya utunzi, uwasilishaji na upokezi wa fasihi simulizi. Kwa hivyo basi, utafiti huu umefanywa kwa minajili ya kuziba pengo hili la kupuuzwa kwa fasihi simulizi ya Wasambaa.

Kupuuzwa kwa umuhimu wa turathi simulizi za Kiafrika kuna misingi yake katika mifumo ya biashara ya utumwa na utawala wa kikoloni. Mifumo yote miwili iliwahusu watu wa mataifa ya Ulaya waliohakikisha kuwa wanawakandamiza Waafrika kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha, ndani ya mifumo hii, turathi za Kizungu zilieniwa kama kielelezo cha ustaarabu, ilhali turathi za Kiafrika zilibeza kwa madai kuwa zilikuwa ni za kishenzi, na watu wake hawakuwa wamestaarabika.

Kimsingi, wanazuoni kutoka nje ya Afrika hususan Wanaanthropolojia na Wanahistoria waliamini kuwa bara la Afrika halikuwa na historia wala fasihi. Kulingana na Frazer (1890), fasihi simulizi ya Kiafrika ilikuwa duni na haikufaa kuendelezwa ilhali fasihi andishi ya Kizungu ilikuwa bora na kielelezo cha ustaarabu uliotukuka. Mtazamo huu uliwafanya watawala wa kikoloni watilie mkazo maendeleo ya fasihi andishi kwa upande mmoja na wapuuze maendeleo ya fasihi simulizi ya Kiafrika kwa upande mwingine.

Kwa bahati mbaya, hata baada ya uhuru serikali nyingi za Kiafrika ikiwemo Tanzania hazikuweka misingi imara ya kuendeleza fasihi simulizi ya jamii zao. Mielekeo iliyoongoza uchunguzi wa historia na utamaduni wa Mwafrika wakati wa ukoloni na

muda mfupi baada ya uhuru ilishindwa kutambua umuhimu wa fasihi simulizi ya Kiafrika hasa kwa kuwa wachunguzi hao hawakuelewa kuwa utendaji ndio mhimili wa fasihi ya Mwafrika. Ili kuupambanua vyema ujumi wa fasihi ya Wasambaa, utafiti huu umechunguza utendaji wa nyimbo za *mdumange* kama kielelezo cha fasihi simulizi ya Wasambaa. Aidha, chukulizi ya utafiti huu ni kuwa bila kuutambua utendaji kama mhimili unaojenga na kufasiri ujumi wa fasihi simulizi ya Kiafrika, upekee wa fasihi hiyo hauwezi kudhihirika.

### **1.1.5 Utendaji katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika**

Utendaji ni dhana telezi na ya kidhahania mno. Kutokana na hali hii, maelezo mengi yametolewa na wanazuoni mbalimbali katika kuifasili na kuelezea viambajengo vyake. Hivyo, dhana hii imewashughulisha wengi miongoni mwa wataalamu wa taaluma za Anthropolojia (Gennep, 1960; Turner, 1969 na 1982), Isimu na Isimu Jamii (Chomsky, 2007; Hymes, 2013 na Halliday, 2014), Maigizo (Schechner, 1988, 1993 na 2013; Bauman & Briggs, 2003 na Bauman & Sherzer, 2011) na wataalamu wa taaluma ya Sosholojia (Goffman, 1959, 1963 na 1974).

Katika utafiti huu dhana hii imetumika kulingana na jinsi ilivyofafanuliwa na Wanaisimu, Wanaisimu Jamii pamoja na Utendaji wa Maigizo. Katika isimu, dhana ya utendaji inahusishwa na mawazo ya Chomsky (2007) yasemayo kuwa utendaji ni michakato ya kiisimu inayodhihirishwa na wanajamii lugha wakati wa kutumia lugha yao. Aidha, Chomsky alitumia dhana ya utendaji kwa kuitofautisha na dhana ya umilisi. Tofauti na utendaji, umilisi ni uwezo alio nao mwanajamii lugha katika kutunga na kutambua tungo sahihi za lugha yake.

Chomsky alihitimisha kuwa utendaji si kipengele muhimu katika taaluma ya isimu kwa sababu ulidhihirisha matumizi ya lugha badala ya kudhihirisha sifa mahsusi

zinazotawala misingi ya sarufi. Ni kutokana na msingi huu ambapo Chomsky alitoa maelekezo kuwa wanaisimu wanapaswa kushughulikia umilisi badala ya utendaji kama njia sahihi ya kuchunguza na kuchanganua michakato ya kiisimu katika lugha mahsusi.

Ingawa kwa muda wa miongo kadhaa Nadharia tete zilizopendekezwa na Chomsky kuhusu uhusiano uliopo baina ya umilisi na utendaji zilitumika kama dira ya kuchunguzia lugha, wanaisimu waliokuja baada yake walizipinga. Miongoni mwa wanaisimu waliohakiki mawazo ya Chomsky ni Hymes (2013) na Halliday (2014). Kwa mfano, Hymes alitoa hoja kuwa kando na kanuni za kiisimu zinazodhihirika katika lugha kuna kanuni za kimawasiliano zinazopaswa kutawala uchunguzi wa kiisimu. Kamwe kanuni za kiisimu katika lugha haziwezi kuwa na maana endapo wanaisimu hawatazitambua na kuzichunguza kanuni za kimawasiliano. Kwa upande wake Halliday aliona kuwa taaluma ya isimu haipaswi kuchunguza sentensi peke yake bali inapaswa kuchunguza michakato ya uumbaji na ubadilishanaji maana (Diskosi) kati ya mwanajamii lugha mmoja na mwingine.

Hivyo, maelezo ya Hymes na Halliday yanaelekeza kuwa katika isimu utendaji na umilisi ni vitu viwili tofauti lakini vinavyohusiana sana na vinapaswa kuchunguzwa kwa pamoja. Vilevile maelezo yao yanatufahamisha kuwa dhana ya utendaji ilitumiwa na wanaisimu kurejelea uwezo wa kutumia lugha katika kufanikisha mchakato wa mawasiliano kati ya mwanajamii lugha mmoja na mwingine.

Aidha, mtazamo wa Hymes na Halliday kuhusu utendaji kwa namna fulani unaelekeana na mtazamo wa Goffman (1959), Turner (2008) na Schechner (2013). Kwa mfano, kulingana na Schechner (2013), utendaji ni urudiaji wa kitendo cha kisanaa kwa namna mpya. Mtaalamu huyu anaona kuwa urudiaji ni msingi mkuu wa

kudhihirisha utendaji katika tabia za wanadamu. Fasili hii inaakisi maana ya utendaji iliyoenezwa na Halliday kwa kuwa ingawa ni kweli kuwa utendaji huambatana na urudiaji lakini urudiaji wa kitendo uliofanywa mara ya kwanza hutofautiana na udhihirikaji wa kitendo unapofanywa kwa mara ya pili.

Kadhalika, kwa mujibu wa Goffman (1959) utendaji ni utolewaji upya wa matendo au tabia. Hii ina maana kuwa utendaji ni udhihirishwaji wa matendo ya kawaida kwa njia ya kisanaa. Kwa ujumla, katika utafiti huu dhana ya utendaji imetumika kurejelea mchakato mahsusi wa kisanaa unaowajumuisha pamoja fanani na hadhira ili kutekeleza wajibu mahsusi wa kijamii. Kwa hiyo, utendaji si lazima uwe urudiaji wa kitendo kimoja kwa namna ileile.

Kulingana na maelezo haya ni dhahiri kuwa dhima na nafasi ya utendaji katika kudhihirisha ujumi wa fasihi simulizi ya Kiafrika ni kubwa. Licha ya umuhimu wake, nafasi na sifa zake mahsusi katika muktadha wa jamii ya Wasambaa haijachunguzwa. Kutozingatiwa kwa mitindo mbalimbali ya utendaji kumefanya watafiti wa awali kupuuzua sanaa husika. Turathi za Wasambaa zilienziwa vyema katika kipindi cha kabla ya ukoloni pekee na tangu kuingia kwa wakoloni, wakati wa uhuru, ujamaa mpaka wakati wa sasa hakuna jitihada madhubuti zilizofanywa na wanajamii katika kuziendeleza na kuzihifadhi turathi hizi.

## **1.2 Suala la Utafiti**

Utendaji unaelekea kuwa kiambajengo muhimu cha ujumi wa tanzu nyingi za fasihi simulizi ikiwemo nyimbo za ngoma. Kama ilivyo kwa tanzu nyingine za fasihi simulizi, ujumi wa nyimbo pia unaimarishwa na mitindo ya utendaji wa fanani na hadhira hususan matumizi ya lugha, muziki, uchezaji wa dansi na maleba. Ni kutokana na uwasilishwaji wenye sifa za kiutendaji ndipo umuhimu wa fasihi simulizi

hudhihirika kutegemea muktadha wa jamii mahsusi. Kwa bahati mbaya tafiti zilizokwishafanywa hazijatambua umuhimu wa utendaji katika fasihi simulizi kwani Nadharia zilizoongoza tafiti hizo zilielemea zaidi katika fasihi andishi kuliko fasihi simulizi. Kutotambuliwa kwa utendaji kulizua hitimisho kuwa fasihi simulizi ya Kiafrika ni sanaa duni ikilinganishwa na fasihi andishi.

Utafiti huu basi ni uchanganuzi wa nyimbo za *mdumange* ambazo ni sehemu muhimu ya fasihi simulizi ya Wasambaa kama amali imara na thabiti iliyosheheni mbinu mbalimbali za kisanaa. Mbinu hizo za kisanaa hutumiwa na fanani pamoja na hadhira katika kuumba maana na kubadilishana maana au jumbe za namna mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii kihistoria, kijamii na kiutamaduni. Kadhalika, katika utafiti huu tumeangazia nyimbo za *mdumange* kutoka jamii ya Wasambaa kwa kuwa tafiti zilizotangulia zinaelekea kusisitiza kwamba utendaji hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Utafiti huu vilevile ulipambanua mikakati ya utendaji, dhima yake na jinsi watendaji wanavyotumia utendaji huo kujadili masuala mbalimbali yahasuyo maisha na ulimwengu wa Wasambaa kwa ujumla.

### **1.3 Madhumuni ya Utafiti**

Azma kuu ya utafiti huu ni kutathmini nafasi ya mitindo ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika mwonoulimwengu ya Wasambaa. Ili kutekeleza azma hii, madhumuni mahsusi yafuatayo yameshughulikiwa:

- (i) Kupambanua jinsi miktadha ya kijamii inavyochochea utendaji wa nyimbo za *mdumange*.
- (ii) Kuchanganua usawiri wa maisha ya Wasambaa kupitia mitindo ya lugha inayotumika katika nyimbo za *mdumange*.
- (iii) Kujadili nafasi ya mitindo ya viziada lugha kwa wasanii wa nyimbo za *mdumange* na jamii ya Wasambaa kwa ujumla.

#### 1.4 Maswali ya Utafiti

Ili kutimiza madhumuni yaliyoainishwa, mtafiti ameongozwa na maswali yafuatayo:

- (i) Ni kwa namna gani miktadha ya jamii ya Wasambaa imechochea utendaji wa nyimbo za *mdumange*?
- (ii) Je, ni ipi dhima ya mitindo ya lugha katika kuwasilisha nyimbo na kusawiri maisha ya Wasambaa?
- (iii) Je, mitindo ya viziada lugha ina nafasi gani kwa wasanii na jamii ya Wasambaa kwa ujumla?

#### 1.5 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu umeshughulikia utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika jamii ya Wasambaa. Aidha, azma kuu ilikuwa kuchunguza nafasi ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika maisha ya Wasambaa. Katika kutekeleza jukumu hili, mtafiti alijiegemeza kwenye vipengele mahsusi vya uchunguzi kijiografia, kiutanzu na kiwakati kama ifuatavyo:

Licha ya kuwa sanaa ya nyimbo za *mdumange* inapatikana pia katika Wilaya nyingine wanakoishi Wasambaa kama vile Muheza na Korogwe, utafiti huu ulimakinikia eneo la Wilaya ya Lushoto peke yake. Ili kupata data mahsusi yenye muumano wa hoja na ithibati, mtafiti hakukusanya data kutoka katika Wilaya za Muheza na Korogwe. Aidha, eneo la Wilaya ya Lushoto lilipewa kipaumbele kutokana na tajriba ya mtafiti kuhusu jiografia, mila na tamaduni za watafitiwa aliyoipata wakati wa uchunguzi wa awali. Tajriba alizonazo mtafiti kuhusu eneo la utafiti zina mchango mkubwa katika kufanikisha upatikanaji wa watafitiwa na idhini ya kukusanya data kwa uhuru na kujiamini.



Kadhalika, licha ya kuwa jamii ya Wasambaa wa Lushoto wanazo tanzu mbalimbali za sanaa za maonyesho na fasihi simulizi kama vile ngano, vitendawili, methali na miviga, utafiti huu umechunguza mashairi nyimbo za *mdumange* peke yake. Uteuzi wa nyimbo hizi umetokana na upekee wake pamoja na malengo yaliyokusudiwa na utafiti huu. Nyimbo za *mdumange* zinatofautiana sana na aina nyingine za nyimbo zinazopatikana katika jamii ya Wasambaa kama vile vipokeo, bembelezi, kidembwa na pungwa kiutendaji. Miongoni mwa sifa zinazozipambanua nyimbo za *mdumange* dhidi ya aina nyingine za nyimbo ni pamoja na kujumuisha jamii yote bila kujali tofauti zao kijinsia na kiumri, kuwasilishwa katika muktadha mpana wa sherehe na hafla za harusi, siasa na sikukuu za kidini. Kwa hivyo, nyimbo za *mdumange* zilichunguzwa kwa kuwa sifa zilizotajwa zingeweza kukidhi haja ya malengo mahsusi ya utafiti huu.

Mwisho, ili kubaini utendaji hai wa nyimbo za *mdumange*, data zilikusanywa kutoka maskani asilia ya Wasambaa. Mtafiti hakushughulikia utendaji wa nyimbo za *mdumange* unaofanyika katika maeneo ya mijini kwa sababu utendaji unaodhihirika huko si asilia. Kwa ufupi, sababu ya kujikita vijijini ni kuwa huko ndiko utamaduni wa Wasambaa unazingatiwa zaidi ikilinganishwa na maeneo ya mijini.

### **1.6 Sababu za Uteuzi wa Mada ya Utafiti**

Haja ya kufanyika kwa utafiti huu imechochewa na shauku ya mtafiti ya kutaka kukuza na kuendeleza turathi za Kiafrika kupitia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi, hususan nyimbo. Kwa minajili hiyo, kupitia utafiti huu tunatarajia kuchangia ukuzaji wa maarifa ya utunzi, uwasilishaji, utafiti, ufundishaji, upokezi na uhifadhi wa sanaa jadiya ya nyimbo na ushairi simulizi kwa ujumla kwa namna mbalimbali.

Pia, utafiti huu umechochewa na ukweli kuwa kuna tafiti chache sana zilizoshughulikia vipengele mbalimbali vya utendaji wa fasihi simulizi kama vile mikakati ya utunzi na uwasilishaji wake. Kwa hiyo utafiti unaohusu utendaji wa nyimbo za ngoma katika jamii ya Wasambaa utachangia kuongezeka kwa marejeleo ya nyimbo na tanzu nyingine za ushairi simulizi.

Vilevile, mada ya utafiti huu iliteuliwa kwa sababu mtafiti aliona kuwa fasihi simulizi ya Kiafrika inakabiliwa na changamoto ya kutokuweco kwa matumizi ya mbinu linganishi katika shughuli za kiutafiti. Kwa hiyo, data pamoja na matokeo ya utafiti huu itatumika katika kufanyia tafiti linganishi kati ya mitindo ya utendaji wa fasihi ya Wasambaa na mitindo ya utendaji wa jamii nyinginezo za Kiafrika. Ingawa tumejikita katika nyimbo za *mdumange* peke yake, matokeo na mapendekezo yaliyotolewa yanaweza kuchochea uchunguzi zaidi kwenye vipengele vingine vya fasihi simulizi na sanaa jadiya sio tu katika jamii ya Wasambaa bali pia kuhusu jamii nyingine za Kiafrika.

Kwa upande mwingine, mada ya utafiti huu ni muhimu kwa sababu utaimarisha jitihada za ufundishaji wa fasihi simulizi katika ngazi mbalimbali za elimu nchini Tanzania na mahali kwingineko ambako fasihi ya Kiafrika hufunzwa. Kwa kuzingatia kuwa ufundishaji wa fasihi simulizi ya Kiafrika unakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na data za kutosha, utafiti huu utasukuma mbele jitihada za ufundishwaji wa fasihi hii kiNadharia na kivitendo.

Vilevile, mada ya utafiti huu imeteuliwa kwa sababu matokeo yake yatachochea usambazaji na upokezi wa fasihi simulizi ya Wasambaa katika hadhira pana ya Waswahili na ulimwengu wote kwa ujumla. Mpaka sasa, sehemu kubwa ya fasihi ya jamii nyingi za Kiafrika imejibana mno katika hadhira finyu kwa kuwa inawasilishwa

kwa kutumia lugha za wazawa peke yake. Kwa kutafsiri nyimbo na utamaduni wa Wasambaa katika Kiswahili na kupambanua utendaji wake kupitia utafiti huu tunapanua hadhira yake na hivyo kuikuza na kuiendeleza kijiografia.

Kufuatia kasi ya mabadiliko ya kijamii yatokanayo na nguvu za sayansi, teknolojia na utandawazi, kuna hofu ya kupotea kwa turathi mbalimbali za Kiafrika kama vile nyimbo, hadithi na miviga. Tofauti na wanajamii wa zamani ambao waliitumia fasihi simulizi kwa kiwango kikubwa, jamii ya sasa inakabiliwa na changamoto ya kupuuza matumizi ya fasihi simulizi kutokana na kukithiri kwa matumizi ya vyombo kama vile redio, televisheni na intaneti. Kutokana na hofu hii, utafiti huu utachangia katika kuhifadhi sehemu kubwa ya turathi za kijadi zinazopotea kila uchao. Kwa hivyo, ripoti ya utafiti huu itakuwa ghala la kuzihifadhi, kuzilinda na kuziendeleza turathi za Kiafrika, hususan nyimbo za ngoma ya *mdumange*. Data zihusuzo nyimbo za *mdumange*, msamiati wa lugha ya Kisambaa, utamaduni na historia ya Wasambaa kwa ujumla ni muhimu kwa kizazi cha sasa na cha baadaye.

Kwa kuzingatia kuwa kila jamii ina fasihi yake inayoweza kuelezwa vyema kwa kutumia lugha na utamaduni wake, utafiti huu umedhihirisha kuwa nyimbo za *mdumange* zina dhima ya kipekee katika utamaduni wa Wasambaa kiuchumi, kiutamaduni na kiujumi. Kulingana na hoja hii, utafiti huu ni muhimu kwa kuwa utachochea na kuhamasisha wataalamu kuchunguza fasihi simulizi ya jamii nyingine ndani na nje ya bara la Afrika.

### **1.7 Mbinu za Utafiti**

Mbinu za utafiti ni kanuni au kaida za kiuchunguzi zinazotumiwa na mtafiti tangu hatua ya kukusanya mpaka hatua ya kuchambua data. Aghalabu, mbinu hizo hutofautiana kutoka utafiti mmoja hadi mwingine kutegemea mkabala mahsusni wa

kiutafiti . Katika utafiti huu, mbinu anuai za utafiti ziliteuliwa kwa kuzingatia mihimili ya mkabala wa kistahilifu au kitaamuli. Mkabala huu umetuwezesha kuteua mikakati mahsusi ya kiutafiti kama vile uteuzi wa sampuli, vifaa vya utafiti, njia za kukusanyia data pamoja na mikakati ya uchambuzi wa data kama ifuatavyo:

### **1.7.1 Uteuzi wa Sampuli**

Sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalowakilisha sifa na tabia ya jamii nzima inayotarajiwa kutafitiwa (Bryman, 2004). Kwa upande mwingine, Bryman (*keshatajwa*) anafafanua kuwa usampulishaji ni mchakato wa kiutafiti ambapo mtafiti hutumia mikakati mahsusi ya kuteua sampuli inayofaa kutekelezea azma ya utafiti. Michakato ya sampuli na usampulishaji imemsaidia mtafiti kukabiliana na changamoto za uteuzi wa idadi ya watafitiwa, idadi ya nyimbo za *mdumange* pamoja na idadi ya vijiji vya utafiti katika Wilaya ya Lushoto, mkoa wa Tanga – Tanzania. Kwa ujumla, mikakati ya kimakusudi na kibahati nasibu ilitumika wakati wa kuteua sampuli za utafiti.

#### **1.7.1.1 Mikakati ya Sampuli Kimakusudi**

Mikakati ya kimakusudi hufuata utaratibu maalum ambapo sampuli ndogo huteuliwa kutoka chanzo kikuu cha data kwa kudhamiria (Kothari, 2004). Sampuli hiyo huteuliwa kulingana na sifa zake zinazochangia katika upatikanaji wa data. Aina hii ya usampulishaji ilitumika kubainishia na kuteulia eneo la utafiti hususan vijiji vya Wilaya ya Lushoto, ambako kuna watu mbalimbali wanaofanya sherehe zao kwa kutumia nyimbo za *mdumange*.

Aidha, katika kupata sampuli ya utafiti, mtafiti alifanya uchunguzi wa awali kwa kuzuru eneo la utafiti, hususan vijiji vya Wilaya ya Lushoto kabla ukusanyaji wa data haujaanza. Tangu tarehe 15 Mei 2015 hadi 20 Juni 2015 mtafiti alifanya ziara ndani

ya Wilaya ya Lushoto kwa minajili ya kupata taarifa za awali kuhusu upatikanaji wa data. Ziara ilianza katika ofisi ya mkuu wa Wilaya ya Lushoto ambaye alitutambulisha kwa Afisa Utamaduni wa Wilaya. Kwa kutumia barua ya utambulisho tuliyokuwa nayo kutoka Chuo Kikuu cha Moi, Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika tulimfahamisha Afisa Utamaduni wa Wilaya azma na matarajio ya utafiti wetu. Kwa ufupi, Afisa Utamaduni wa Wilaya alitupa orodha ya vijiji vya Wilaya ya Lushoto ambako wanapatikana wasanii wa nyimbo za *mdumange*. Kadhalika, Afisa Utamaduni wa Wilaya alitupatia ratiba ya hafla zilizotarajiwa kufanyika siku za usoni ambapo vikundi mbalimbali vya sanaa za kijadi (ikiwemo nyimbo za *mdumange*) vingevalikwa na kushiriki kwa kuonyesha utendaji wao.

Uchunguzi wa awali ulionyesha kuwa nyimbo za *mdumange* hupatikana kwa wingi zaidi ndani ya Wilaya ya Lushoto, ikilinganishwa na Wilaya nyinginezo za mkoa wa Tanga. Kwa hivyo, Wilaya ya Lushoto ilituuliwa kimakusudi, kwa sababu ina idadi kubwa ya vijiji vyenye vikundi vya wasanii wa nyimbo za *mdumange*. Jumla ya vijiji kumi na viwili (12) viliteuliwa kimakusudi kwa ajili ya utafiti huu. Kwa upande mwingine, sampuli ya kimakusudi ilitumika kuteulia idadi ya watafitiwa waliotumika katika majadiliano ya vikundi na usaili. Watu wawili kutoka kila kijiji waliteuliwa kulingana na ushiriki wao kama ifuatavyo:

**Jedwali na 1: Sampuli ya Vijiji vya Utafiti na Idadi ya Wasailiwa**

| Kijiji    | Watafitiwa |    | Kijiji      | Watafitiwa |    |
|-----------|------------|----|-------------|------------|----|
|           | ME         | KE |             | ME         | KE |
| Kihitu    | 2          | 0  | Magoma      | 1          | 1  |
| Kivilicha | 2          | 0  | Mbuzii/Ngua | 1          | 1  |
| Kwemhafa  | 1          | 1  | Mgwashi     | 1          | 1  |
| Kwezindo  | 1          | 1  | Mlalo Kaya  | 1          | 1  |
| Lushoto   | 1          | 1  | Mtae        | 1          | 1  |
| Lwandai   | 1          | 1  | Soni        | 1          | 1  |

*Jumla Vijiji Teule = 12, Jumla Watafitiwa = 24*

Jedwali nambari moja hapo juu linaonyesha kuwa idadi ya vijiji vilivyoteuliwa kimakusudi ni kumi na viwili (12) na idadi ya watafitiwa walioteuliwa kwa kutumia njia hii ni ishirini na wane (24).

Vilevile, uchunguzi wa awali ulionyesha kuwa nyimbo za *mdumange* hutendwa katika hafla za harusi, kidini na kisiasa. Kwa hivyo, kutokana na ratiba ya hafla

kutoka kwa Afisa Utamaduni mtafiti aliteua kimakusudi maonyesho ishirini (20) ya utendwaji wa nyimbo za *mdumange*. Maonyesho hayo yalijumuisha hafla zilizobainishwa katika jedwali nambari mbili kama ifuatavyo:

**Jedwali na 2: Sampuli ya Maonyesho na Hafla za Utafiti**

| <b>Sherehe au hafla</b>                                  | <b>Idadi ya maonyesho yaliyoshuhudiwa</b> |
|--|---|
| Harusi   | 05  |
| Ubarikio   | 05  |
| Krismasi   | 01  |
| Id el-fitri  | 01  |
| Mbio za mwenge   | 03  |
| Sherehe za Wafanyakazi                                   | 02  |
| Kampeni za uchaguzi mkuu                                 | 03  |
| <i>Jumla ya Maonyesho Yaliyoteuliwa ni ishirini (20)</i> |   |

Kama inavyoonekana hapo juu, jedwali la maonyesho ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* lina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inaonyesha aina ya sherehe na sehemu ya pili inaonyesha idadi ya maonyesho yaliyotumika wakati wa ukusanyaji data. Kwa ujumla, idadi ya maonyesho iliteuliwa kimakusudi kulingana na kiwango cha utendwaji wa nyimbo.

**1.7.1.2 Sampuli Bahati Nasibu**

Sampuli bahati nasibu ni mbinu ya utafiti ambapo idadi maalum ya vijelezi vya kiutafiti kutoka chanzo kikuu cha data huteuliwa bila utaratibu maalum. Katika mbinu hii, vitu au watu wote katika chanzo kikuu cha data wanakuwa na nafasi sawa ya kuchaguliwa na kuingizwa katika sampuli ya utafiti (Bryman, 2004). Kwa ujumla, mbinu hii ya uteuzi wa sampuli ni faafu kwenye utafiti kwa kuwa huondoa upendeleo wa mtafiti kuingiza data katika sampuli kwa matakwa yake binafsi.

Kulingana na Kothari (2004) pamoja na Silverman (2005) kuna aina kuu tatu za sampuli bahati nasibu. Aina hizo ni usampulishaji nasibu sahili, tabakishi na taratibishi. Usampulishaji bahati nasibu sahili huhusisha uteuzi wa sampuli kutoka

kwenye kundi lote linalotafitiwa bila kufuata utaratibu maalum. Kwa upande mwingine, usampulishaji bahati nasibu tabakishi ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ambapo chanzo kikuu cha data hugawanywa katika safu mbalimbali kulingana na vigezo au ruwaza maalum za data. Baada ya kuunda safu, sampuli huteuliwa katika safu hizo kinasibu ili kuunda sampuli ya utafiti. Aidha, usampulishaji bahati nasibu taratibishi ni mbinu ya utafiti ambapo sampuli huteuliwa kutoka chanzo kikuu cha data kinasibu lakini kwa kufuata utaratibu uliowekwa na mtafiti wa kuruka idadi maalum ya vitu au watu (Bryman, 2004 na Kothari, 2004).

Mbinu ya usampulishaji tabakishi ilitumika kuteulia nyimbo za *mdumange* kwa ajili ya uchambuzi. Nyimbo zilizoteuliwa ni zile zilizowasilishwa kwenye vijiji vya utafiti wakati wa hafla za harusi, dini na siasa. Kupitia utendwaji wa nyimbo uliofanywa kwenye hafla zilizoainishwa mtafiti alikusanya jumla ya nyimbo mia mbili na arobaini (240) za *mdumange*. Aidha, ili kupata sampuli ya utafiti, nyimbo zilizokusanywa ziligawanywa katika makundi tisa (09) kulingana na dhamira. Kwa kila kundi idadi maalum ya nyimbo ilitoteuliwa kutegemea kiwango cha nyimbo zinazoelezea dhamira husika. Muhtasari wa uteuzi wa sampuli ya nyimbo za *mdumange* umewasilishwa kwenye jedwali nambari tatu kama ifuatavyo:



**Jedwali na 3: Sampuli ya Nyimbo za *Mdumange* Zilizochambuliwa**

| <b>Kategoria za Nyimbo kulingana na dhamira</b> | <b>Idadi ya nyimbo zilizokusanywa</b> | <b>Idadi ya nyimbo zilizoteuliwa katika sampuli</b> |
|---|---------------------------------------|---|
| Afya  | 24                                    | 05  |
| Dini  | 12                                    | 05  |
| Fomula  | 34                                    | 20  |
| Furaha/pongezi                                  | 28                                    | 05  |
| Huzuni/kero                                     | 36                                    | 20  |
| Mapenzi   | 47                                    | 20  |
| Maudhui ya jumla                                | 20                                    | 05  |
| Mazingira                                       | 10                                    | 05  |
| Siasa/uongozi                                   | 29                                    | 05  |
| <i>Nyimbo zote ni 240</i>                       |                                       | <i>Nyimbo zilizoteuliwa ni 90</i>                   |

Kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu, makundi ya dhamira yaliyokuwa na nyimbo chini ya thelathini (30) nyimbo tano (5) pekee ziliteuliwa ilhali katika makundi ya dhamira zilizokuwa na nyimbo zaidi ya thelathini (30) nyimbo zilizoteuliwa ni ishirini (20). Kwa kutumia utaratibu huu mtafiti alifanikiwa kuteua nyimbo tisini (90) kwa ajili ya sampuli. Nyimbo zilizoteuliwa ni zile zilizokuwa na miundo tofauti tofauti pamoja na dhamira mbalimbali kuhusu maisha ya Wasambaa.

**1.7.2 Vifaa vya Utafiti**

Vifaa vya utafiti ni jumla ya zana zitumiwazo na mtafiti katika kukusanya, kuhifadhi na kuchambua data. Kwa hiyo, uandaaji na uteuzi wa vifaa vya utafiti ni mbinu muhimu sana katika utafiti. Kwa mujibu wa Mulokozi (2002) uteuzi wa mbinu za utafiti unaongozwa na mambo manne: (i) mada ya utafiti, (ii) shabaha za utafiti, (iii) uwezo wa mtafiti kifedha na kitaaluma; na (iv) mazingira ya utafiti kijiografia na kiutamaduni. Pamoja na maelezo mazuri ya Mulokozi kuhusu vigezo vya kufuata

wakati wa kuteua vifaa vya utafiti, katika utafiti huu tumeteua vifaa vya utafiti kutegemea majukumu yake katika utafiti. Sehemu ifuatayo tumefafanua aina mbalimbali za vifaa vilivyotumika ndani ya utafiti huu kulingana na majukumu yatekelezwayo na vifaa husika.

### **1.7.2.1 Watafiti Wasaidizi**

Watafiti wasaidizi ni watu maalum walioteuliwa na kupewa maelekezo muhimu ya namna ya kushirikiana na mtafiti mkuu. Aghalabu maelekezo yanayotolewa kwa watafiti wasaidizi hokusudiwa kuwapatia wasaidizi hao ujuzi wa namna ya kukabiliana na majukumu ya kiutafiti wakiwa nyanjani. Uandaaji wa watafiti wasaidizi ni moja kati ya hatua muhimu za awali zinazopaswa kufanywa na mtafiti kabla ya kukusanya data. Katika utafiti huu, tulitumia watafiti wasaidizi wawili (mmoja wa kiume na mwingine wa kike) kwa sababu pamoja na mambo mengine tulihitaji kupata data za kiutendaji na kiethnografia kutoka kwa wasaidizi hao. Watafiti wasaidizi pia walitumika kama watafiti wakuu ambao wamechangia pa kubwa kupatikana kwa data za utafiti huu.

Ubainishaji na uteuzi wa watafiti wasaidizi uliongozwa na maelekezo au taarifa tulizozipata kutoka kwa viongozi wa serikali za vijiji husika. Taarifa hizi zilituhakikishia kuwa watu hawa walikuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu jiografia ya Lushoto, utamaduni wa Wasambaa na tajriba ya nyimbo za *mdumange*. Aidha, tuliona kwamba ni bora kuwa na mtafiti msaidizi mwanamke na mwanamme kwa sababu licha ya kuwa waliotongoa nyimbo ni wanaume peke yao, uchezaji na upigaji ala za muziki ulihusisha watu wa jinsia zote.

Licha ya uzoefu waliokuwa nao watafiti wasaidizi, ilimbidi mtafiti awape maelekezo ya kutumia kamera katika kunasa mwonekano wa fanani, hadhira na jukwaa la

utendaji. Kwa ujumla, mbali na kuwajibika kama watafiti wasaidizi, watu hawa pia walikuwa sehemu ya watafitiwa na waliwajibika kutoa taarifa mbalimbali za utafiti kama watoa taarifa wakuu. Ingawa tuliwapa posho kutokana na msaada wao mkubwa, tuliwahakikishia kuwa ushiriki wao ulikuwa wa hiari na kwamba wangeweza kujitoa muda wowote katika utafiti. Kwa bahati nzuri, watafiti wote wasaidizi walishirikiana na mtafiti mkuu tangu mwanzo wa kukusanya data nyanjani hadi mwisho.

### **1.7.2.2 Redio Kaseti na Kinasa Sauti**

Mtafiti alikusudia kuchunguza utendaji wa nyimbo za *mdumange*, kwa hivyo ili kutimiza lengo hili vifaa mbalimbali vya kunasia sauti, maneno na mwonekano wa muktadha wa utendaji vilitumika. Katika jitihada za kunasa utendaji wa sauti zilizotolewa na fanani na hadhira wakati wa uwasilishwaji wa nyimbo tulitumia vifaa vya aina mbili: kinasa sauti na redio kaseti. Vilevile vifaa hivi vilitumika kukusanyia data wakati wa usaili wa ana kwa ana baina ya mtafiti na watafitiwa. Kuna wakati vifaa hivi vilitumika vyote kwa pamoja na kuna wakati ambapo kila kifaa kilitumika kwa wakati wake mahsusni.

Matumizi ya redio kaseti na kinasa sauti yalileta tija kubwa katika utafiti huu. Kwanza yaliwahamasisha watafitiwa na kuwafanya wavutiwe zaidi na utongoaji wa nyimbo, hususan baada ya kusikiliza sauti zao mara kwa mara. Pili, vifaa hivi vina uwezo wa kurekodi utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika kiwango cha sauti. Baadhi ya vipengele vya utendaji wa sauti za watafitiwa vilivyopatikana kutokana na matumizi ya vifaa hivi ni pamoja na kiimbo na toni za nyimbo husika. Tatu, vifaa hivi ni mwafaka zaidi kutumia kwa kuwa vilimwezesha mtafiti kufanya mambo mengi kwa wakati mmoja. Kwa kutumia redio kaseti na kinasa sauti mtafiti alikusanya data kwa njia za usaili, ushuhudiaji kwa pamoja kama njia ya kudhibiti uharibifu na upotevu wa

data. Baadaye mtafiti alisikiliza nyimbo na mahojiano na kisha kuyanukuu kwa utulivu katika kompyuta.

### **1.7.2.3 Kamera ya Kidijitali**

Utafiti kama huu ambao umekusudia kuchunguza utendaji wa nyimbo za *mdumange* ambazo pia ni sehemu ya mashairi simulizi ya Wasambaa usingekamilika bila kutumia kifaa chenye uwezo wa kunasa hali za mwonekano wa utendaji. Mwonekano huo ulijumuisha maleba yao, sura zao, mandhari na jukwaa wakati wa utendaji. Ili kufanikisha jambo hili, mtafiti alitumia kamera ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua picha za video na za kawaida.

Kamera ni kifaa cha kisasa ambacho kimeleta mapinduzi makubwa katika tafiti za kifasihi simulizi. Matumizi ya kamera ya kidijitali katika utafiti huu yaliruhusu uhamishaji wa data kutoka kifaa kimoja hadi kingine kwa urahisi. Kwa mfano, punde tu ushuhudiaji na ushiriki ulipokamilika picha na video zilizorekodiwa kwenye kamera zilihamishiwa kwenye kompyuta kwa ajili ya uchambuzi. Ubora wa kifaa hiki pia ulitokana na ukweli kuwa kifaa hiki kilikuwa na uwezo wa kufanya kazi zaidi ya moja. Ingawa katika utafiti huu tulitumia katika kukusanyia data nyanjani wakati wa ushiriki na ushuhudiaji, kifaa hiki pia kina uwezo wa kurekodi sauti za waimbaji na mahojiano wakati wa usaili.

### **1.7.3 Mikakati ya Ukusanyaji Data**

Msingi wa data za utafiti huu ni nyimbo za *mdumange* zinazopatikana katika jamii ya Wasambaa. Nyimbo hizo zilitokana na maonyesho yaliyofanyika katika hafla za kijamii hususan sherehe za harusi, sikukuu za kidini, na hafla za mikutano ya kisiasa kama vile kampeni za uchaguzi. Aidha, katika utafiti huu ngoma ya Wasambaa, “*mdumange*” ndiyo iliyotumika kama chemchemi ya ukusanyaji wa data zilizohusu

utendaji wa nyimbo husika. Data za utafiti huu zimekusanywa kutoka nyanjani kwenye maskani halisi ya jamii ya Wasambaa. Ukusanyaji huu ulifanyika tangu 05/08/2015 mpaka 15/03/2016. Hii ina maana kuwa mchakato wa kukusanya data ulidumu kwa muda wa miezi minane na siku kumi.

Kwa ujumla, njia zilizotumika katika kukusanyia data za utafiti huu zilijumuisha uchunguzi shiriki, usaili na majadiliano ya vikundi. Mtafiti ametumia njia zaidi ya moja ili kudhibiti dosari ndogo ndogo zinazoambatana na njia husika. Kwa hiyo, njia zote tatu zilitumika kwa pamoja katika hali ya kukamilishana kama ifuatavyo:

#### **1.7.3.1 Uchunguzi Shiriki**

Uchunguzi shiriki ni mbinu ya ukusanyaji data ambapo mtafiti anakuwa sehemu ya jamii inayochunguzwa. Katika mbinu hii, mtafiti hukusanya data kwa kushuhudia na kushiriki matendo au tabia za watafitiwa katika utendaji hai. Mtafiti alitumia mbinu hii kwa kushuhudia na kushiriki maonyesho ya utendwaji wa nyimbo za *mdumange* kwenye sherehe za harusi, dini na siasa. Kwa kutumia njia hii mtafiti alikusanya data kwa kurekodi mienendo ya utongoaji wa nyimbo, upigaji, uchezaji ngoma na uigizaji ulivyotendeka katika mazingira halisi.

#### **1.7.3.2 Usaili**

Usaili ni mbinu ya kukusanya data kwa kuhojiana na watafitiwa kwa minajili ya kupata data za suala linaloshughulikiwa. Usaili huo unaweza kufanyika ama ana kwa ana au kwa kutumia mawasiliano ya simu na mitandao ya kijamii. Katika utafiti huu tumetumia usaili wa ana kwa ana ambapo mtafiti alipata fursa ya kutagusana na watafitiwa kwa kiwango kikubwa.

Lengo la kutumia mbinu hii lilikuwa kukusanya data zilizohusu masuala ya kiethnografia na kihistoria katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Ili kufahamu vyema historia na maana ya mitindo ya utendaji mtafiti aliwahoji wasanii wa aina mbili. Kwanza aliwahoji wasanii wapya, ambao wengi wao ni vijana na kwamba hadi sasa wangali wanajihusisha na shughuli za usanii wa nyimbo za *mdumange*. Kutokana na mahojiano hayo ilibainika kuwa vijana wengi wanaoshiriki katika nyimbo za *mdumange* hawafahamu historia ya *mdumange* pamoja na mitindo yake.

Kwa upande mwingine, mtafiti aliwahoji wasanii wa nyimbo za *mdumange* ambao ni wazee. Baadhi ya wazee waliohojiwa wangali wanaendelea na utongoaji wa nyimbo ilhali wengine kutokana na sababu mbalimbali za kiafya na kijamii walishaachana na shughuli hizo.

Maswali yaliyoulizwa wakati wa usaili yaliangazia masuala anuai ya kiutafiti kama vile mitindo ya utendaji, maana za mitindo hiyo, dhamira na itikadi katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Kimuundo maswali hayo yalikuwa wazi kiasi cha kuwaruhusu watafitiwa kutoa hisia na maoni yao bila kizuizi. Mtafiti alifanikiwa kufanya mahojiano na watafitiwa ishirini na wanne (24) katika vijiji kumi na viwili (12) vya utafiti. Kama inavyoonekana katika jedwali nambari moja watafitiwa waliohojiwa walihusisha watu wa jinsia za kiume na kike kutegemea ushiriki wao kwenye utendaji wa nyimbo za *mdumange*.

### **1.7.3.3 Majadiliano ya Vikundi**

Haja ya kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi imekuwa kubwa sana katika tafiti zenye kufuata mkabala wa kistahilifu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa tafiti za namna hii, hulenga kufahamu tajriba za wanajamii, maana ya tajriba hizo na namna wanajamii wanavyotumia tajriba hizo kufasiri ulimwengu wao. Kwa mujibu wa Guba

(1981), ili kulifikia lengo hili mtafiti hana budi kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi. Aidha, Esposito (2001) anaongeza kuwa mbinu ya majadiliano ya vikundi inasaidia sana kuzalisha na kukusanya data za utafiti kutoka kwa watafitiwa kwa muda mfupi. Kwa kuzingatia madhumuni na mahitaji ya utafiti huu, tulitumia majadiliano ya vikundi kama mbinu ya kukusanya data mpya na pia kama mbinu ya kusawazishia data zilizokusanywa kwa kutumia njia za ushuhudiaji na usaili.

Kwa mujibu wa Kitzinger (2000) matumizi ya mbinu ya majadiliano ya vikundi hayana budi kufanywa kulingana na mila na tamaduni za jamii inayochunguzwa. Kutokana na maoni ya mtaalamu huyu, mtafiti aliandaa majadiliano ya vikundi yaliyojali na kulinda taratibu za utamaduni wa Wasambaa. Katika jamii ya Wasambaa, aghalabu vijana na wazee hawatangamani katika mazungumzo yao ya kila siku. Kutokana na hali hii ili kupata majadiliano yenye tija majadiliano ya vikundi yalizingatia tofauti za umri wa watafitiwa.

Fursa ilitolewa kwa kila kijiji kuunda vikundi viwili vya wazee na vijana. Kila kikundi kilijumuisha pamoja wanawake na wanaume. Kutokana na utaratibu huu, mtafiti alipata vikundi vidogovidogo ishirini na vinne (24) kutoka katika vijiji kumi na viwili (12) vya utafiti. Muda ulitengwa kwa kila kikundi kushiriki majadiliano yaliyohusu utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Lengo la kuendesha majadiliano haya ni kujazilia data ambazo tayari zilishapatikana kwa kutumia njia za uchunguzi shiriki na usaili. Kwa kutumia mbinu zilizofafanuliwa katika sehemu hii, mtafiti alifanikiwa kukusanya taarifa mbalimbali kuhusu nyimbo za *mdumange*. Data kuhusu utendaji wa nyimbo zilirekodiwa katika redio kaseti, kinasa sauti, na katika kamera.

#### 1.7.4 Uchambuzi wa Data

Baada ya kukusanya data, mikakati mahsusi ya uchambuzi wa data ilifanyika. Kwa ujumla, data ziliwasilishwa kwa kutumia matini ya nyimbo za *mdumange* na maelezo yalitolewa kwa kuweka tafsiri yake kwa Kiswahili. Kadhalika, uwasilishaji wa data za mitindo ya viziada lugha kama vile miondoko, uchezaji na uigizaji umefanywa kwa kutumia picha za fanani, hadhira, mandhari na jukwaa la utendaji.

Kando na mikakati hii, uchambuzi wa data za utafiti huu pia ulihusisha hatua kuu nne za kunukuu, kuhariri, kutafsiri na uwekaji misimbo. Katika hatua ya awali, mtafiti alichakata data kwa kunukuu nyimbo za ngoma ya *mdumange*. Kutokana na mchakato huu, mtafiti alifanikiwa kutengeneza data iliyo katika maandishi. Kati ya nyimbo mia mbili na arobaini (240) zilizorekodiwa, nyimbo zilizonukuliwa kwa ajili ya uchambuzi zilikuwa tisini (90) tu.

Katika hatua ya pili mtafiti alihariri matini zilizozalishwa kupitia mchakato wa kunukuu masimulizi kuwa maandishi. Uhariri huo ulifanyika kwa njia ya kulinganisha matini andishi kwa upande mmoja na rekodi mbalimbali za nyimbo kwa upande mwingine. Lengo la mchakato huu ni kuhakikisha kuwa kinachotokea katika redio kaseti, kinasa sauti, simu na kamera ndicho kinachoonekana katika matini andishi.

Hatua ya tatu ilikuwa kutafsiri. Matini za nyimbo pamoja na masimulizi yaliyonukuliwa katika lugha ya Kisambaa yalitafsiriwa kwa Kiswahili. Uzalishaji wa data katika tafsiri ulitilia maanani ishara na misimbo ya kiutamaduni iliyodhihirika wakati wa utendaji nyanjani.

Hatua ya nne na ya mwisho ni kuweka misimbo. Mchakato huu ulijumuisha ugawanyaji data katika makundi anuai kutegemea madhumuni mahsusi ya utafiti.



Kwa kuzingatia madhumuni mahsusi ya utafiti huu, uwekaji misimbo ulijumuisha data za namna tatu: (i) miktadha ya jamii ya Wasambaa iliyochochea utendaji wa nyimbo za *mdumange*; (ii) mitindo ya lugha iliyotumika katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*; na (iii) mitindo ya viziada lugha pamoja na nafasi yake kwa wasanii na Wasambaa kwa ujumla.

### **1.8 Itikeli**

Katika utafiti huu nilihakikisha kwamba nimepata idhini ya watafitiwa. Katika kufanya hivyo, watafitiwa waliosailiwa na ambao walishiriki kwenye mijadala ya vikundi walinipatia ruhusa ya kutumia picha zao zilizopigwa moja kwa moja. Aidha, nyimbo zao pia zilinukuliwa moja kwa moja baada ya kupata ruhusa ya washiriki kupitia kwa wawakilishi (viongozi) wao.

### **1.9 Hitimisho**

Katika sura hii vipengele muhimu vya utafiti vimewasilishwa na kujadiliwa. Vipengele hivyo ni pamoja na usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, na umuhimu wa utafiti. Katika sura inayofuata tumehakiki maandishi mbalimbali yahasuyo fasihi simulizi ya Wasambaa, utendaji na viunzi vya Nadharia zilizotumika katika utafiti huu.

## SURA YA PILI

### MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA KINADHARIA

#### 2.0 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya maandishi ya watafiti mbalimbali walioshughulikia utendaji katika sanaa jadiya, sanaa za maonyesho na fasihi simulizi ya Kiafrika. Aidha, katika sura hii tumetalii misingi ya kiNadharia iliyotumika katika utafiti hususan Nadharia za Utendaji wa Maigizo na Semiotiki ya Kijamii. Kwa ufupi, masuala yaliyojadiliwa yamejumuisha historia na ethnografia ya Wasambaa, muumano wa sanaa jadiya na sanaa za maonyesho, vijenzi vya ujumi wa nyimbo pamoja na misingi ya kiNadharia.

#### 2.1 Historia na Ethnografia ya Wasambaa

Kuna wataalamu mbalimbali waliowahi kujishughulisha na uchunguzi wa historia, utamaduni na fasihi simulizi ya Wasambaa. Miongoni mwa wataalamu hao ni Feierman (1974; 2008), Ajjemy (1978), Nkondokaya (2006) na Peter (2013). Kulingana na Peter (2013), Wasambaa ni kundi la jamii za Waswahili wanaopatikana katika mwambao wa Afrika Mashariki. Peter (*Keshatajwa*) alichunguza mabadiliko ya utamaduni wa jamii hii na kueleza kuwa hapo awali utamaduni wa Wasambaa ulijipambanua kwa kutumia lugha ya Kisambaa peke yake. Hata hivyo, kutokana na biashara ya utumwa, ukoloni na kuongezeka kwa watu utamaduni wa jamii hii umebadilika sana. Kwa mujibu wa Peter (*Keshatajwa*), miongoni mwa mabadiliko makuu katika utamaduni wa Wasambaa ni kushamiri kwa matumizi ya Kiswahili kwa upande mmoja na kupungua kwa matumizi ya Kisambaa kwa upande mwingine.

Katika utafiti huu tumenufaika mno kutokana na utafiti wa Peter (2013), kwa sababu kulingana na mtaalamu huyu imebainika kuwa, ingawa Kisambaa huzungumzwa na Wasambaa katika mawasiliano ya kila siku, matumizi ya Kiswahili pia ni makubwa miongoni mwa wanajamii. Suala la matumizi ya lugha zaidi ya moja linadokeza kuwa wingi lugha ni mojawapo ya mkakati wa kimawasiliano miongoni mwa Wasambaa. Aidha, pamoja na mambo mengine katika utafiti huu pia tumejadili dhima ya mitindo ya lugha itokanayo na muktadha wa jamii yenye wingi lugha. Mitindo hiyo imejadiliwa na kupambanuliwa kama mojawapo ya mikakati ya kimawasiliano inayotumiwa na wasanii katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Kadhalika, utafiti wa Peter (*Keshatajwa*), umeimarisha fikra za utafiti huu kwa sababu umebainisha na kuchanganua masuala ya kijamii yaliyozua kutokea kwa hali ya wingi lugha miongoni mwa Wasambaa kama vile biashara ya utumwa, utawala na utamaduni.

Ingawa utafiti wa Peter unashabihiana na utafiti huu, kwa upande mwingine utafiti huu ni tofauti na wa kwake kutokana na sababu mbalimbali. Wakati katika utafiti huu tumejadili kwa kina utendaji wa nyimbo za *mdumange*, katika utafiti wa Peter (*Keshatajwa*) suala lililojadiliwa lilikuwa matumizi ya lugha peke yake. Kadhalika, utafiti huu ni wa kipekee zaidi kwa kuwa mbali na kujadili dhima ya miktadha ya jamii ya Wasambaa katika kuchochea utendaji wa nyimbo za *mdumange*, pia tumejadili athari ya mitindo ya lugha na viziada lugha. Kwa mujibu wa Nkondokaya (2006), jamii lugha zinazoishi katika Wilaya ya Lushoto ni Wasambaa, Wapare na Wambugu. Nkondokaya anaongeza kwa kusema kuwa isipokuwa jamii ya Wambugu, Wasambaa na Wapare ni jamii ambazo zimechimbuka kutokana na asili moja ya ukoo wa mhenga wa kale aliyeitwa Sheuta. Kwa hiyo, utafiti huu utaimarisha hoja za Peter kuwa Wasambaa si wakazi pekee wa Lushoto na kwamba lugha ya Kisambaa

inatumiwa na jamii hizi sanjari na lugha nyingine, yaani Kiswahili, Kimbugu na Kichasu.

Feierman (1974; 2008) alifanya utafiti wa kiethnografia kuhusu historia na utamaduni wa Wasambaa. Kusudio la Feierman lilikuwa ni kuchunguza namna turathi simulizi kama vile ngano, methali, visasili, na nyimbo zingeweza kutumika kama chemchemi ya kuhifadhia historia. Katika utafiti wake, Feierman alitoa maelezo kadhaa. Kwa kutumia turathi hizo, alibaini kuwa shughuli kuu ya kiuchumi miongoni mwa Wasambaa ni kilimo cha mazao ya chakula kama vile mihogo, mahindi, maharagwe, mboga na matunda na biashara. Mazao ya biashara yanayolimwa na jamii hii yalijumuisha misitu, katani na chai. Pamoja na kufafanua mfumo wa kiuchumi katika jamii hii, Feierman pia ameelezea kuwa kiutawala Wasambaa walijiimarisha vyema chini ya uongozi wa machifu wa kijadi. Aidha, uongozi wa kijadi katika jamii ya Wasambaa umechimbuka kutokana na ukoo wa Wakilindi ambapo Feierman anaeleza kuwa viongozi maarufu walikuwa Chifu Mbega na Kimweri.

Mambo mengine yaliyowasilishwa na Feierman ni masuala ya kijamii kama vile mfumo wa malezi, ndoa na dini. Kwa ufupi, mtaalamu huyu anaelezea kuwa jamii ya Wasambaa inaishi kwa kufuata itikadi za mfumodume ambapo wanaume wamepewa mamlaka ya juu zaidi kuliko wanawake katika maamuzi ya kisiasa, ndoa, talaka na mirathi. Kwa upande mwingine, jamii hii ilithamini turathi simulizi (ikiwemo nyimbo) kama nguzo imara ya kurithisha amali zake kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Utafiti wa Feierman umechochea mambo kadhaa yahusianayo na utafiti wetu. Kwanza, kulingana na utafiti alioufanya nafasi ya turathi simulizi imeonekana katika kuhifadhi historia, maadili, utawala na uchumi wa jamii. Ni kutokana na umuhimu wa

amali hizo ndipo utafiti huu umefanyika ili kutathmini dhima ya utendaji wa nyimbo kama turathi kongwe ya Wasambaa. Tofauti na utafiti wa Feierman, matokeo ya utafiti huu yanabainisha jinsi nyimbo za *mdumange* zilivyo na umuhimu wa kipekee katika jamii ya Wasambaa. Masuala yaliyoangaziwa wakati wa kujadili dhima ya nyimbo hizi ni jinsi mikakati yake ya utendaji ikiwemo muktadha, lugha na viziada lugha husaidia kupambanua ujumi na itikadi za ulimwengu wa Wasambaa. Pamoja na mchango mzuri tulioupata kutokana na utafiti wa Feierman, kuna mambo kadhaa yanayotofautisha utafiti wake na utafiti huu. Kulingana na makusudio yake, yeye alichunguza zaidi jinsi turathi simulizi zinafanya kazi ya kuhifadhi historia na kamwe hakuchunguza nyimbo kama kazi ya kisanaa iliyosheheni vipashio maalum vya kiuji. Kwa upande mwingine, utafiti huu ni wa kipekee zaidi ikilinganishwa na wa kwake kwa kuwa katika utafiti huu tumejikita katika utendaji wa nyimbo na dhima yake katika jamii ya Wasambaa. Kwa hivyo, utafiti wetu utaongeza maarifa yahasuyo mikakati ya kiutendaji, dhima ya nyimbo na uhusiano wa utendaji wa nyimbo na muktadha wa kijamii.

Ajjemy (1978) alifanya utafiti wa kiisimu kuhusiana na lugha ya Kisambaa. Pamoja na mambo mengine, Ajjemmy anafafanua kuwa eneo la Wilaya ya Lushoto lina jamii lugha za namna tatu: (i) Wasambaa, (ii) Wapare na (iii) Wambugu. Kulingana na Ajjemmy, Wapare wanahusiana sana na Wasambaa kwa kuwa wote ni jamii za Kibantu, ilhali jamii ya Wambugu huhusiana na Wasambaa kwa kiwango kidogo sana kwa kuwa wao si Wabantu bali ni Wanailoti. Kutokana na utafiti wa Ajjemmy tunapata kufahamu kuwa mapisi mbalimbali ya fasihi simulizi ya jamii hii yanasimulia kuwa Wambugu walihamia Lushoto kwa minajili ya kutafuta malisho ya mifugo wao. Aidha, inasimuliwa pia kuwa asili ya Wambugu ni eneo moja liitwalo Laikipia, linalopatikana katika nchi ya Kenya. Kiini cha wageni kuhamia Lushoto ni udongo

wenye rutuba pamoja na mpangilio wa uongozi wa machifu wa kijadi, hususan chifu Mbega na Kimweri.

Utafiti wa Ajjemmy (*Keshatajwa*) unashabihiana na uliofanywa na watangulizi wake hususan Feierman (1974). Hii ni kwa sababu wote wanaelekea kukubali kuwa utamaduni wa Wasambaa umechangiwa na nguvu za kijamii kutoka ndani na nje ya Lushoto. Kwa ufupi, wote wanasisitiza nafasi ya wageni katika kustawi kwa utamaduni wa Wasambaa. Katika utafiti huu tumenufaika na mambo anuai yaliyojadiliwa na Ajjemmy kama vile miundo ya lugha ya Kisambaa, matamshi yake na sarufi yake kwa ujumla. Hata hivyo, katika utafiti huu tumepiga hatua mbele zaidi kwa kuchunguza fasihi simulizi ya Wasambaa.

## **2.2 Sanaa Jadiya na Sanaa za Maonyesho**

Wataalamu mbalimbali wamependekeza kuwa tunapojadili utendaji wa nyimbo za ngoma hatuwezi kuacha kujadili dhana za sanaa jadiya na sanaa za maonyesho (Kipury, 1983; Miruka, 1994; Kobia, 2004 na Matti, 2009). Hii ni kwa sababu licha ya kuwa dhana zilizotajwa zina umuhimu wa kipekee katika utafiti huu, kimaana dhana hizi zinategemeana na kukamilishana. Aidha, katika kutalii yaliyoandikwa kuhusu dhana hizi, tumeangazia ufafanuzi wa dhana husika, Nadharia zilizoongoza ufafanuzi huo pamoja na athari yake katika kufasiri ujumi na ulimwengu wa Waafrika.

### **2.2.1 Sanaa Jadiya ya Kiafrika**

Kuna mitazamo mikuu miwili ya kuelezea sanaa jadiya ya Kiafrika. Mitazamo hii inajumuisha mawazo yanayoichukulia dhana ya sanaa jadiya ya Kiafrika kwa mtazamo hasi na mtazamo chanya. Aidha, mawazo yanayoichukulia dhana hii kwa mtazamo hasi yanawakilishwa na fikra za wanazuoni wa Kimagharibi pamoja na

mwenendo mzima wa Nadharia zilizoibuka na kushamiri katika kipindi cha Karne ya kumi na tisa. Kwa upande mwingine, mawazo yanayoichukulia dhana ya sanaa jadiya kwa mtazamo chanya yanawakilishwa na fikra za wanazuoni pamoja na wanaharakati wa mkabala wa Kimax walioibuka mwanzoni mwa Karne ya ishirini.

Mtazamo wa kwanza unaeleza kuwa sanaa jadiya ni jumla ya mambo yanayojenga mfumo wa maisha ya watu wasiostaarabika. Kwa mujibu wa Lang (katika Almabrok, 2004) mtazamo huu unashikilia kuwa sanaa jadiya ni aina ya ustaarabu unaopatikana katika jamii zilizo nyuma kimaendeleo kama vile jamii za Kiafrika, ilhali jamii zilizoendelea kisayansi, kiutamaduni na kihistoria zilikuwa na ustaarabu wa kipekee. Katika kufafanua vyema hoja hii, Almabrok anaonyesha kuwa sanaa jadiya inatajikana itokane na jamii ambayo imeendelea kama ilivyonukuliwa hapa chini:

sanaa jadiya inahusika tu na visakale, desturi, imani za kundi la watu wa jamii fulani walioathiriwa na mfumo wa elimu kwa kiwango kidogo, na ambao wana kiwango kidogo cha maendeleo (Almabrok, 2004:98).

Katika nukuu hapo juu, tunaona jinsi sanaa jadiya ilivyohusishwa na wakulima, watu wa tabaka la chini na wasiokuwa na maendeleo katika sekta ya elimu. Tofauti na mawazo haya, Dundes (1971) anaeleza kuwa sanaa jadiya ni utaratibu wa maisha ya jamii za kale, zilizoendelea na zilizostaarabika. Licha ya maelezo yao, bado dhana ya sanaa jadiya haijabainishwa waziwazi. Kulingana na ufafanuzi wa wataalamu hawa tunaona kuwa kila mmoja ametoa fasili yake, tena fasili zenyewe zinapingana.

Katika utafiti huu tunatoa hoja kuwa kuwepo kwa utata katika matumizi ya “sanaa jadiya” kumetokana na kutofahamika kwa neno “jadi” pamoja na mtazamo finyu wa Nadharia zilizotumika kufasili “sanaa jadiya”. Kimsingi, dhana ya ujadi ni mojawapo ya sababu iliyo zua utata katika kufasili maana ya sanaa jadiya. Kuna wanaofikiri kuwa neno ‘jadi’ linarejelea kundi la watu wa jamii mahsusi badala ya mtu binafsi.

Kwa sababu hiyo sanaa jadiya hurejelea amali mahsusi zinazotambulisha watu wa jamii mahsusi, sio mtu mmoja.

Kwa upande mwingine kuna wanaofikiri kuwa neno jadi linarejelea ama (i) hali ya kudumu kwa muda mrefu au (ii) hali ya kutobadilika wala kuendelea. Mawazo haya huzua maswali kadhaa tunapowaza namna ya kuifasiri vyema dhana ya sanaa jadiya. Swali kuu linalozuka katika mjadala huu ni kuwa ni upi ukomo wa ujadi katika fasihi na sanaa kwa ujumla? Je, ujadi wa fasihi unatofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine?

Katika kulijibu swali hili, Dundes (1971) amethubutu kutenganisha na kutofautisha sanaa jadiya ya jamii za Ulaya, Afrika na Wahindi wanaoishi Amerika. Aidha, katika uainishaji wake, Dundes anaona kuwa jamii za watu wa Ulaya zina sanaa jadiya ilhali jamii za Waafrika pamoja na Wahindi wanaoishi Marekani hazina sanaa jadiya kwa kuwa bado watu wake hawajaendelea. Kulingana na maoni yake, sanaa jadiya ni aina ya ustaarabu au turathi inayopaswa kustawi katika jamii iliyoimarika kiuchumi, kisiasa, na kiteknolojia. Kamwe, sanaa jadiya si utamaduni wa watu wasiostaarabika, na wasiondelea.

Wazo la Dundes linapingana na Forster (2007) anayedai kuwa kuna sanaa jadiya halisi na sanaa jadiya bandia. Sanaa jadiya halisi hupatikana katika jamii zilizoendelea kiviwanda kama vile Marekani, Uingereza, Ujerumani, na Kanada ilhali sanaa jadiya bandia hupatikana katika jamii ambazo bado hazijaendelea, hususan jamii za Bara la Afrika na Ulimwengu wa tatu kwa ujumla.

Ingawa Forster anasisitiza kuwa sanaa jadiya hupatikana katika kila jamii na kwamba hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine, fasili yake bado inadokeza hali ya upendeleo na utabaka wa kikoloni. Hii ni kutokana na hitimisho analolitoa kuwa,



kadri muda unavyosonga na kadri maendeleo ya viwanda yanavyozidi kushamiri ndivyo sanaa jadiya inavyozidi kutoweka duniani. Kulingana na hitimisho hili, sanaa jadiya hupatikana katika jamii zisizoendelea na kamwe haitarajiwi kupatikana katika jamii zilizoendelea, hususan jamii zilizopitia katika mfumo wa mapinduzi na mageuzi ya viwanda.

Wenye mtazamo huu bado hawajafanikiwa kuifasili vyema dhana hii, hususan katika muktadha wa utamaduni na ujumi wa Kiafrika. Kama ilivyodokezwa hapo awali, utata huu ulichangiwa sana na matumizi ya neno ‘jadi’ na kwamba katika utafiti huu tumependekeza kuwa ili kuifasili vyema dhana ya sanaa jadiya, neno “jadi” linapaswa kubadilishwa kwa kutafutiwa kisawe kingine kinachojitosheleza kimaana.

Jambo lingine lililochangia kuwepo kwa utata wa maana ya “sanaa jadiya” ni athari ya Nadharia za Kimagharibi zenye mwelekeo wa kikoloni. Wazo hili litaeleweka vyema kama tukidhukuru hitimisho la Dundes pamoja na Forster kuhusu maana na aina za sanaa jadiya. Wao wanatoa hitimisho kuwa ama sanaa jadiya huwahusu watu walioendelea au watu wasioendelea. Kimsingi, hitimisho hili lina msingi wake katika mkondo wa Nadharia za Kimagharibi unaoshikilia kuwa daima ustaarabu unaweza tu kupatikana na kusambaa kutoka jamii zenye nguvu na zilizoendelea kuelekea kwenye jamii zisizoendelea (Sengo, 2009).

Mkondo huu wa kiNadharia unashabihiana sana na mkondo wa Nadharia uliotumiwa na wanazuoni wa Kijerumani (German Grimm brothers) walipochunguza tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiafrika na Ulaya. Kwa mfano, katika uchunguzi wao walifafanua kuwa asili ya ngano za Afrika ni Ulaya. Kutokana na maelezo yao utamaduni wa kusimulia hadithi za kingano barani Afrika uliletwa na Wazungu

kutoka Ulaya katika kipindi cha biashara ya utumwa na kwamba kabla ya hapo Waafrika hawakuwa na uwezo wa kutamba hadithi (Okpwewho, 1992).

Kwa upande mwingine, wanazuoni wa Kijerumani, Forster pamoja na Dundes wanaweza kujumuishwa katika kundi la waumini wa Nadharia ya Msambao (Diffusion Theory). Kulingana na Nadharia ya Msambao, ikiwa kutakuwa na kushabihiana kwa namna yoyote kwa jamii mbili zinazoishi katika maeneo tofauti basi kufanana huko kunaashiria kuwa jamii hizo ziliwahi kukutana. Katika muktadha huo, jamii zilizokuwa imara na zenye nguvu ziliziathiri jamii dhaifu na zisizostaarabika (Okpwewho, 1992).

Kama tulivyotangulia kusema hapo awali, fasili zilizotolewa hapo juu kurejelea dhana ya sanaa jadiya zina uvulivuli mwingi, hasa kuhusiana na muktadha wa lugha ya Kiswahili na utamaduni wake. Ili kuweka bayana maana ya dhana hii, mambo mawili yanafaa kufanyiwa kazi. Mosi, ni kutumia neno lingine badala ya neno ‘jadi’ wakati wa kurejelea ‘sanaa jadiya’. Neno hilo litumike kwa minajili ya kurejelea aina ya sanaa, amali au mienendo ya maisha inayowahusu watu wengi badala ya mtu binafsi.

Pili, kwa kuwa amali zinazokusudiwa kurejelewa hapa ni zile zinazowahusu watu wote na kwamba kila mwanajamii anao uhuru wa kutumia amali hizo jinsi atakavyo. Maana ya sanaa jadiya inayopendekezwa na utafiti huu inakaribiana na maana iliyowahi kutolewa na Dundes (1971) kuwa sanaa jadiya ni mkusanyiko wa taratibu za maisha ya jamii mahsusi wenye sifa mahsusi na unaotambulisha jamii husika. Mawazo ya Dundes yanawakilisha maoni ya wanaharakati wa Kiafrika wanaotetea kuwa sanaa jadiya ni amali inayopatikana katika jamii zote duniani. Kulingana na fasili hii, sanaa jadiya hujumuisha kaida anuai za kimaisha ikiwemo lugha, fasihi, siasa, utawala, uchumi, sayansi na teknolojia. Aidha, fasili hii inapanua mawanda ya

uwanja wa sanaa jadiya na kwamba badala ya kuwa amali mahsusi za jamii zilizoendelea peke yake, sasa sanaa jadiya inahusisha hata amali za jamii zisizoendelea.

Kadhalika, kwa maoni yetu fasili zilizotolewa na Dundes (1971) na Sengo (2009) ni mwafaka zaidi. Kutokana na fasili hizi, sanaa jadiya hujumuisha mfumo wa mawasiliano na matendo ya wanajamii kwenye muktadha wa kijamii. Kwa hivyo, tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kama vile ngano, vitendawili, methali na nyimbo ni sehemu moja tu ya sanaa jadiya za Kiafrika. Sehemu nyingine kubwa ya sanaa jadiya ya Kiafrika inawakilishwa na mifumo mingine kama vile dini, siasa, kilimo, biashara, utawala na aina nyingine za sanaa hususan uashi, uchoraji, ujenzi, useremala na uashi.

Kutokana na maelezo haya tunaweza kusema kuwa sanaa jadiya ya Kiafrika ina matawi makuu mawili: (i) amali zinazotumia lugha, ikiwemo fasihi simulizi na (ii) amali zisizotumia lugha, kama vile ujenzi, uchoraji na uchongaji. Sehemu kubwa ya amali za kundi la pili hutumika pia katika kutambulishia aina ya sanaa ambazo ujumi wake unapatikana kwa kutazama (sanaa za maonyesho). Mtazamo wa Dundes na Sengo, na ambao unawakilisha fikra za Kiafrika umetufanya tuzitazame sanaa jadiya katika mawanda mapana yanayohusisha suala la utendaji.

Imebainika kupitia maelezo ya wataalamu hawa kuwa fasihi simulizi ni aina moja tu kati ya aina nyingi za sanaa jadiya. Isitoshe, aina hizi za sanaa jadiya hutegemeana na hukamilishana. Kwa mfano, tanzu mbalimbali za fasihi simulizi hujadili masuala mengine ya kijamii (sanaa jadiya zisizotumia lugha) kama vile utawala, ndoa, na historia. Kwa upande mwingine, sanaa jadiya zisizotumia lugha (kama vile siasa,

historia, ndoa, dini na nyinginezo) huchangia katika kujenga muktadha wa utendwaji wa fasihi simulizi.

Ni kutokana na msingi huu ndipo utafiti huu umedhamiria kujadili jinsi suala la muktadha lilivyochochea utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Aidha, hoja hii inaonyesha kuwa utafiti huu unahusiana na dhana ya sanaa jadiya kwa kuwa tumechunguza kipengele cha fasihi simulizi (nyimbo) ili kuonyesha namna kipengele hicho kinahusiana na vipengele vingine vya sanaa jadiya ya Wasambaa.

### **2.2.2 Sanaa za Maonyesho**

Wataalamu mbalimbali wamejadili namna sanaa za maonyesho zinavyotokea na kuwasilishwa katika jamii. Aidha, sanaa za maonyesho ni mojawapo ya tanzu za sanaa jadiya ambazo ujumi wake unadhihirika kupitia utazamaji zaidi kuliko usikilizaji. Kutokana na hali hii, dhana ya sanaa za maonyesho mara nyingine hutumiwa kama kisawe cha sanaa za kimaigizo (maigizo). Hata hivyo, Nadharia nyingi zilizoelezea kuhusu maigizo ya jamii mbalimbali duniani zimejikita katika kigezo cha utokeaji na uwasilishwaji. Akizungumzia mazingira yanayorutubisha utokeaji au uwepo wa sanaa za maonyesho Brecht (1990:3) anasema:

Sanaa za maonyesho hutokea wakati waigizaji wanapotenda mbele ya hadhira [.....] sanaa hiyo inawasilisha tajriba za ndani na za nje katika jamii kwa kutumia maneno na matendo. Inahitaji wasanii wengi ili iweze kutengenezwa, muigizaji, mtunzi wa tamthiliya, mwongozaji, mandhari, msanifu, mpambaji.

Fasili hii inaeleza misingi ya utokeaji wa sanaa za maonyesho za Kimagharibi zinazozingatia zaidi maigizo ya kidrama. Katika sanaa hizo, tajriba za maisha ya mwanadamu zinasawiriwa katika umbo la simulio la hadithi likiambatana na unenaji pamoja na uigizaji wa matendo. Aidha, fasili hii pia inadokeza kuwa hadithi au simulio la kidrama linahitaji ushirikiano wa rasilimali mbalimbali ili liweze

kuwasilishwa mbele ya hadhira. Rasilimali hizo ni pamoja na waigizaji, mwongozaji, mandhari na mtunzi au mwandishi wa tamthiliya.

Mtazamo wa Brecht kuhusu sanaa za maonyesho unashabihiana na mtazamo wa Melnitz (1955) pamoja na Baumgardt (2002). Kwa mfano, kulingana na Melnitz (1955) uwasilishaji wa drama ni sharti ufanyike kwa njia ya maandishi. Katika kuelezea ujumi wa sanaa za maonyesho Melnitz (*Keshatajwa*) anasema:

Tunaweza kusema kuwa, sanaa za maonyesho hutokea tunapokuwa na tamthiliya iliyoandikwa, inayotendwa na waigizaji katika ukumbi maalum wa sanaa, jukwaa, mandhari na mwanga au baadhi ya vitu hivi.

Katika nukuu hapo juu, suala la maandishi ya michezo ya kuigiza linasisitizwa pamoja na jukwaa au jengo maalum la sanaa za maonyesho zinazohusika. Kwa ujumla, katika fasili zote vigezo vya sanaa za maonyesho zitokanazo na sanaa jadiya ya Kimagharibi husisitizwa. Aidha, inahalisi hapa kusisitiza kuwa kutokana na msuko wa sanaa hizo, suala la jukwaa au jengo maalum la kuonyeshea lilikuwa muhimu sana.

Kwa upande mwingine, sanaa za maonyesho za Kiafrika hazikujifunga katika maandishi wala jengo maalum la kuonyeshea (jukwaa) bali zilisisitiza sifa ya ushiriki wa hadhira katika utendekaji wake. Kwa hiyo, fasili zilizotolewa hazikidhi vigezo vya sanaa za maonyesho za Kiafrika. Kwa ujumla, sanaa za maonyesho ni utanzu wa sanaa jadiya unaopatikana Afrika na katika jamii mbalimbali duniani. Kila jamii ina misingi yake ya uundaji na uwasilishwaji wa sanaa hizo. Katika fasili za wataalamu wa Kimagharibi, misingi ya utokeaji wa sanaa za maonyesho kwa kiasi kikubwa inaakisi muundo wa drama na maigizo ya Kimagharibi. Hata hivyo, japo fasili za Kimagharibi zimeegemea katika sanaa za maonyesho za kifasihi andishi zaidi, kuna

baadhi ya vipengele ambavyo vinaafikiana na utendaji wa sanaa za maonyesho za Kiafrika ambazo hazijaandikwa. Vipengele hivyo ni jukwaa, hadhira na lugha.

Ijapokuwa nyimbo nyingi za Kiafrika hazijaandikwa, utendaji wake haukamiliki bila kuwasilishwa katika mandhari au jukwaa mahsusi. Katika fasili ya sanaa za maonyesho iliyotolewa na Melnitz suala la jukwaa linapewa umuhimu wa kipekee kabisa. Jambo ambalo yafaa litahadharishwe hapa ni kuwa ingawa hata sanaa za maonyesho za Kiafrika kama vile nyimbo hutendwa katika mandhari na mahali mahsusi kutegemea kusudio lake, lakini dhana ya mandhari na jukwaa ni tofauti na ile ya sanaa za maonyesho za Kimagharibi. Jukwaa linalozungumziwa na Melnitz (1955) ni la drama za Kimagharibi kwa sababu anarejelea jukwaa kama jengo mahsusi lililoandaliwa kwa ajili ya kuonyesha sanaa mbalimbali za kimaigizo.

Ingawa jukwaa la sanaa za maonyesho za Kimagharibi ni tofauti na jukwaa la sanaa za Kiafrika, wazo la kuchunguza kipengele hiki ni muhimu kwa sababu hata utendaji wa nyimbo hufanyika katika mandhari maalum. Kwa hiyo, katika utafiti huu tunadadisi na kujadili jinsi nyimbo za *mdumange* zinavyotendwa na namna jukwaa lilivyoundwa. Kusudio letu ni kutaka kufahamu iwapo jukwaa hilo linaathiri utendaji wa fanani na hadhira na ni kwa namna gani katika fasihi za Kiafrika miundo ya jukwaa inafanikisha utendwaji wa sanaa husika.

Aidha, vipengele vya utokeaji wa sanaa za maonyesho vinavyojadiliwa na wataalamu hawa havitoshelezi kuifafanua sanaa ya maonyesho ya Kiafrika na maeneo mengine ya ulimwengu kama vile Japani na China. Matalan, hoja ya Brecht (1990) kuwa ‘maigizo husawiri tajriba kwa kutumia usemaji na matendo’ haiwezi kukidhi kuelezea hali halisi ya utokeaji wa sanaa za maigizo au maigizo ya China yaitwayo Peking Opera. Hali ilivyo ni kuwa maigizo ya sanaa za maonyesho huko China yajulikanayo

kama Peking Opera huwasilisha fikra au tajriba za maisha sio tu kwa kutumia unenaji na matendo, bali pia hutumia muziki na uchezaji wa dansi. Hivyo hivyo, sanaa mbalimbali za Kiafrika kama vile utambaji wa hadithi, uimbaji wa nyimbo, matambiko na sherehe mbalimbali utendaji wake hutumia unenaji, uigizaji wa matendo, muziki, uchezaji wa dansi, na uigizaji bubu. Katika utafiti huu tunachunguza utendaji wa nyimbo za *mdumange* ili kuona ni kwa kiwango gani mitindo yote iliyotajwa hapa inajitokeza na inafanya kazi gani katika kuwasilisha ujumbe.

Kadhalika, si lazima sanaa za maonyesho za Kiafrika ziwasilishwe kupitia maandishi. Sanaa za maonyesho ambazo ni mpya na za kisasa zinaweza kuwasilishwa kwa maandishi, lakini kwa kiwango kikubwa sanaa nyingi za maonyesho zinawasilishwa kwa kutumia Utendaji wa Maigizo, unaokiuka misingi ya utendaji wa kidrama. Kwa hivyo, maoni ya Melnitz (1955) kuwa “sanaa za maonyesho hutokea tunapokuwa na tamthiliya au mchezo wa kuigizwa ulioandikwa” yanaashiria kuwa fasili yao ilijibana mno katika muktadha wa maigizo ya Kimagharibi. Katika muktadha wa jamii za Kiafrika, fasili hii haiwezi kukidhi vigezo vya kuwasilisha fasihi ambayo haijaandikwa. Hii ni kwa sababu utendaji wa nyimbo na tanzu nyingine za kifasihi simulizi umeelezwa na kuendelezwa kwa kutumia masimulizi na maongezi ya mdomo. Utafiti huu basi umefanywa ili kuhakiki jinsi utendaji wa nyimbo unavyothubutu kuvuka mipaka ya utendaji wa maigizo ya Kimagharibi, ambayo yanategemea sana maandishi.

Kwa kiwango kikubwa dhana ya sanaa za maonyesho tuliyoitumia katika utafiti wetu imetokana na mawazo ya Mlama (1983) pamoja na Brecht (1990). Kwa mujibu wa wataalamu hawa, ni muhimu kuzingatia muktadha na uhusiano baina ya jamii na

fasihi katika kuchunguza utendaji wa sanaa za maonyesho na sanaa jadiya kwa ujumla. Pamoja na kuisitiza muktadha na uhusiano wa fasihi na jamii, wanaNadharia hawa hususan Mlama, ameonyesha jinsi jukwaa la sanaa za maonyesho za Kiafrika linapaswa kuwa na athari ya mikakati ya kiutendaji kwa hadhira.

Akizungumzia jukwaa la maigizo ya Kiafrika, Mlama (*Keshatajwa*) anasema kuwa sanaa za maonyesho za Kiafrika hazitumii kumbi wala majumba maalum ya kuonyesha sanaa kwa kuwa sanaa hizi zinatendwa kama sehemu muhimu ya shughuli nyingine za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kwa hiyo, hata suala la mahali au jukwaa la kutendea hutegemea dhima ya utendwaji wa sanaa husika.

Kwa upande mwingine, baada ya kuona aina nyingine za drama zisizo za Kimagharibi, hususan za China, Brecht alikiri kuwa sanaa za maonyesho ni utanzu wa kifasihi wenye vipengele vingi vya kiujumi ambavyo vinapaswa kuelezwa sio tu kwa misingi ya drama ya Kimagharibi, bali pia kwa kutumia misingi ya ujumi wa jamii husika. Brecht anapendekeza kuwa njia sahihi ya kuwasilisha tajriba za kimaisha katika maigizo ni kutumia mbinu za kiukengeushi. Katika mbinu hizi, watendaji pamoja na fanani wa maigizo walitakiwa kujitenga na hisia zinazowakilishwa katika fasihi. Brecht anaona kuwa maigizo na tanzu nyingine za sanaa za maonyesho zingeweza kugusa na kuathiri jamii kwa kiwango kikubwa kama mbinu mbalimbali za kiukengeushi zingetumika. Baadhi ya mbinu hizo ni pamoja na matumzi ya muziki, korasi, usimulizi na ukinzani baina ya maneno, matendo na uigizaji wa wahusika.

Ijapokuwa mawazo ya Brecht yalikusudia kuendeleza maigizo ya Kimagharibi kwa kutengeneza maigizo yaliyoathiri matendo ya jamii (drama tendi), mawazo yake yana tija kubwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu, mawazo yake yanasisitiza umuhimu wa mikakati ya kiutendaji katika kufanikisha uwasilishwaji wa sanaa za maonyesho.



Katika utafiti huu tunachunguza utendaji wa nyimbo za *mdumange* ili kupambanua sifa mahsusi za mikakati ya utendaji wa fanani na hadhira katika kujenga maana mbalimbali.

Vilevile, Nadharia za Brecht na Mlama zimechangia pa kubwa katika kuimarisha utafiti huu kwa kuwa zimeonyesha namna tunavyoweza kuichukulia sanaa jadiya kama chombo cha kiukombozi. Ukombozi huo unaweza kuwa wa kifikra, kiitikadi, au kisiasa. Suala hili linahusiana mno na utafiti huu kwa kuwa pamoja na mambo mengine utafiti huu pia unadhamiria kujadili dhima (majukumu) ya utendwaji wa nyimbo katika jamii. Miongoni mwa majukumu hayo ni kuonyesha namna utendwaji wa nyimbo za *mdumange* unavyoakisi mivutano ya kijamii katika ngazi mbalimbali za kijamii kama vile familia (ndoa na malezi), na utawala (migogoro ya kisiasa).

Aidha, kitendo cha kuhusisha suala la utendaji na dhima za kiukombozi katika jamii kimesaidia kutambulisha namna sanaa za maonyesho zinavyohusiana na sanaa jadiya nyingine za jamii kama vile mfumo wa malezi, siasa na uchumi. Katika utafiti huu, nyimbo za *mdumange* zimetazamwa kama chemchemi na jukwaa la majadiliano na maridhiano ya wanajamii katika ngazi mbalimbali za mahusiano.

### **2.3 Nyimbo kama Utanzu wa Sanaa za Maonyesho na Fasihi Simulizi**

Kulingana na fasili zilizotolewa kuhusu sanaa za maonyesho ni wazi kuwa nafasi ya nyimbo imetazamwa katika mitazamo miwili: kwanza kama utanzu wa sanaa za maonyesho na pili kama utanzu wa fasihi simulizi. Mitazamo hii imetokana na hali halisi ya utendaji wa nyimbo ambapo wasanii huchanganya nyenzo za kiutazamaji na kiusikilizaji. Nyenzo za kiutazamaji kama vile jukwaa, hadhira, fanani na maleba ndizo hupambanua sanaa za maonyesho dhidi ya tanzu nyingine za fasihi simulizi. Kwa kuwa utendaji wa nyimbo hutekelezwa kwa kutumia nyenzo za namna zote

mbili, katika sehemu ifuatayo tumeelezea hoja za mitazamo yote miwili katika kupambanua nyimbo kwa jamii.

### **2.3.1 Nyimbo Kama Utanzu wa Sanaa za Maonyesho**

Katika sehemu iliyopita tumefafanua dhana za sanaa za maonyesho na sanaa jadiya pamoja na nafasi yake katika utafiti huu. Aidha, imeelezwa kuwa sanaa za maonyesho ni sehemu ya sanaa jadiya ambazo kiwango kikubwa cha ujumi wake kinadhihirika kupitia nyenzo za kiutazamaji zaidi kuliko za kiusikilizaji. Kulingana na jinsi utendaji wa nyimbo unavyofanyika kuna baadhi ya wataalamu wanaoona kuwa nyimbo ni utanzu wa sanaa za maonyesho kwa kuwa hutumia nyenzo za kiutazamaji katika kudhihirisha ujumi wake. Miongoni mwa wataalamu hao ni Askew (2002), Omari (2009) na Brunott (2013).

Askew (*Keshatajwa*) alichunguza uhusiano baina ya utendaji katika muziki na ujenzi wa utamaduni, utambulisho na itikadi mbalimbali nchini Tanzania. Katika utafiti wake, Askew amechambua aina tatu za sanaa za kimuziki na kuonyesha namna sanaa hizo zilivyotumiwa na wanajamii katika mihula mbalimbali kuunda na kusawiri itikadi, utamaduni na utambulisho wa taifa la Tanzania. Utafiti wa Askew umebainisha kuwa kuna aina kuu mbili za muziki: (i) muziki wa kijadi; na (ii) muziki wa kisasa.

Kulingana na utafiti wa Askew, muziki wa kijadi hujumuisha sanaa mbalimbali hususan ngoma na nyimbo. Kwa upande mwingine, muziki wa kisasa hujumisha muziki wa dansi na taarabu. Maelezo haya yanadokeza kuwa katika aina zote za muziki nyimbo hutumiwa kwa njia moja ama nyingine. Aidha, katika utafiti wake Askew aligundua kuwa utendaji wa sanaa hizo za kimuziki umechangia kwa kiasi kikubwa katika mabadiliko ya utamaduni na utambulisho katika nyakati tofautitofauti

kutegemea aina ya utawala uliokuwa madarakani. Mihula anayoitaja Askew ni pamoja na muhula wa ukoloni, harakati za kudai uhuru, ujamaa, na utandawazi. Anasema kuwa katika mihula yote hii, muziki umehochea shughuli za kisiasa kwa kiwango kikubwa. Kwa ufupi, Askew anasisitiza athari ya nyimbo na sanaa ya muziki katika kuunda utamaduni na mahusiano ya mamlaka ya kisiasa nchini Tanzania tangu kipindi cha ukoloni hadi kipindi cha uhuru na utandawazi.

Utafiti wa Askew umetupatia mawanda mapana yanayohusiana na utafiti wetu katika nyanja za historia ya nyimbo, muziki na uhusiano baina ya fasihi na jamii kwa ujumla. Askew pamoja na mambo mengine amefanikiwa pia kutujua kuhusu masuala ya kijinsia yanayoambatana na utendwaji wa muziki wa taarabu na muziki wa asili (ngoma). Anasema kuwa katika utendaji wa muziki kuna mavazi maalum ya wanawake na wanaume na pia kuna mgawanyo wa majukumu baina ya jinsia hizi mbili.

Kutokana na utafiti wa Askew imebainika kuwa, wanaume walishiriki kwa njia ya kupiga na kutumia ala za muziki ilhali wasanii wa kike walishiriki kwa njia ya kuimba na kcheza. Aidha, kila kundi lilivaa mavazi maalum kutambulisha majukumu yao wakati wa utendaji. Hatimaye, kazi ya Askew imefanikiwa kutupatia mwanga kuhusu dhima ya ngoma za asili, muziki wa taarabu na dansi katika kusuluhisha migogoro na kueneza itikadi za wanasiasa tangu wakati wa ukoloni mpaka kipindi cha baada ya uhuru. Katika utafiti huu tunatafiti na kuchunguza utendaji wa nyimbo za ngoma ya Wasambaa ya “*mdumange*” ili kuona jinsi muumano wa sanaa na utamaduni, itikadi na siasa unavyojitokeza.

Kwa upande mwingine, Askew alitafiti nyimbo na kuona kuwa nyimbo ni sehemu ya sanaa za maonyesho ambazo ujumi wake unategemea mapigo ya kimuziki pamoja na

utendaji wa fanani na hadhira. Aidha, utafiti wake ulifanyika na kuhusisha zama za kuanzia wakati wa ukoloni. Hii inaonyesha kuwa utafiti wake haukugusia jambo lolote linalohusu utendaji wa nyimbo na muziki wa asili katika kipindi cha kabla ya ukoloni. Kwa kuzingatia kuwa jamii za Kiafrika zilikuwa na sanaa zake mbalimbali kama vile ngoma, nyimbo, hadithi na nyinginezo nyingi, utafiti huu unakusudia kuziba pengo hili kwa kuchunguza nyimbo za *mdumange* ambazo chukulizi ya utafiti huu ni kuwa ni za kale zaidi.

Kwa kuwa nyimbo zinazochunguzwa katika utafiti huu ni za kale zaidi, zina nafasi kubwa ya kutufahamisha jinsi utamaduni, utambulisho, itikadi na aina nyingine ya diskosi za kijamii ilivyokuwa sio tu wakati wa ukoloni bali hata katika kipindi cha nyuma zaidi, wakati kabla ya ukoloni. Kwa hiyo, utafiti huu ni daraja mwafaka la kitaaluma linalotarajiwa kujadili na kudadisi nafasi ya utendwaji wa nyimbo za *mdumange* katika jamii ya Wasambaa, tangu zamani mpaka leo. Tofauti na Askew, utafiti huu unaona kuwa nyimbo ni utanzu mahsusi wa fasihi simulizi unaojipambanua kwa mitindo mahsusi ya kiutendaji, ikiwemo suala la utendaji wa kimuziki unaodhihirika kwa kuimba na matumizi ya ala za muziki.

Mtaalamu mwingine aliyechunguza nyimbo kama utanzu wa sanaa za maonyesho ni Omari (2009). Kwa ujumla, Omari alichunguza nyimbo na kutoa hoja kuwa nyimbo ni sanaa ya maonyesho inayowasilishwa kwa kutumia mitindo ya utendaji wa kimuziki. Nyimbo alizochunguza Omari zilitokana na muziki unaojulikana kwa jina maarufu la Muziki wa Bongo Flewa (MBF). Omari aliibua hoja kuwa katika siku za awali (miaka ya 1990) nyimbo pamoja na utendaji wa MBF ulionekana kama sanaa ya vijana wahuni na wasio na mwenendo bora katika jamii. Hii ina maana kuwa katika kipindi cha awali nyimbo na utendaji wa MBF haukupewa hadhi ya kuonekana kama kazi ya kisanaa. Wazee, hususan waliotokea maeneo ya vijijini walikebehi na

kudharau sanaa hii. Kundi dogo tu la vijana kutoka maeneo ya mjini ndilo lililoenzi na kutukuza utunzi na uwasilishaji wa nyimbo za MBF. Hata hivyo, Omari anaelezea kuwa kadri siku zilivyosonga, muelekeo wa jamii ulibadilika na kuanza kuheshimu na kupenda muziki wa MBF.

Kwa ufupi, utafiti wa Omari ulidhamiria kuchunguza masuala ya kisanaa na kijamii yaliyosababisha mabadiliko katika MBF. Kwa hivyo, Omari alikusudia kudadisi na kuthibitisha sababu zilizoufanya MBF ukubalike na uwe sehemu muhimu ya fasihi pendwa ya Watanzania kunako miaka ya 2000. Katika uchunguzi wake, Omari aligundua kuwa sababu zilizoufanya MBF ukubalike na uwe maarufu kiasi cha kuwa sehemu ya fasihi pendwa ya Watanzania miongoni mwa hadhira ya vijana na wazee ni utashi wa fanani katika kubuni nyimbo zinazovutia hadhira na maudhui yanayogusia hisia au tajriba za wanajamii. MBF imekuwa maarufu miaka ya 2000 kutokana na utendaji wake kusheheni vionjo mbalimbali vya kiutendaji kama vile matumizi ya lugha ya kishairi, mbinu za utendaji wa maigizo kama vile uigizaji na uchezaji, ubunifu wa mavazi na matumizi ya ala za muziki.

Kadhalika, kulingana na Omari (2009), maendeleo ya sayansi na teknolojia katika kipindi cha utandawazi pia yamechochea sana mwamko mpya wa jamii kuhusiana na sanaa ya MBF. Omari anahitimisha kuwa kutokana na sababu hizi MBF imekuwa maarufu sio tu maeneo ya mijini bali hata katika maeneo ya vijijini ambako hapo kabla hali haikuwa hivyo.

Ingawa utafiti wa Omari haukuchunguza utendaji kwa kina, umetubainishia vipengele mbalimbali vya kifani na kimaudhui vya nyimbo za MBF. Vipengele hivyo vimetokana na vyanzo vikuu viwili: utamaduni wa fasihi pendwa ya Kimagharibi hususan Marekani na utamaduni wa fasihi simulizi ya Kiafrika. Akijadili kuhusu

athari ya utamaduni wa Kimagharibi katika MBF Omari anasema kuwa wasanii wa MBF wameiga mitindo ya utendaji kutoka kwa wasanii wa muziki wa Hip Hop (Marekani). Miongoni mwa mitindo hiyo ni matumizi ya lugha ya Kingereza pamoja na mavazi yasiositiri vyema maungo ya wasanii,

Kwa upande mwingine, Omari anaelezea kuwa ili kunogesha utendaji wao, wasanii wa MBF pia hutumia mitindo ya utendaji itokanayo na utamaduni wa fasihi simulizi ya Kiafrika kama vile mavazi ya kimasai na lugha za kikabila. Kwa hiyo, kupitia kazi ya Omari sio tu kuwa tunapata kufahamu miundo na dhima ya vipengele vya utendaji katika sanaa ya nyimbo, bali pia tunapata fursa ya kutambua usuli na historia ya baadhi ya miundo hiyo. Utafiti huu basi umefanyika ili kuona jinsi nyimbo za *mdumange* zimeazima mitindo ya utendaji kutoka sanaa jadiya ya Kiafrika na katika fasihi pendwa ya kisasa nchini Tanzania kwa ujumla.

Aidha, utafiti huu umechunguza nyimbo ambazo ni sehemu ya fasihi kongwe ya Wasambaa. Nyimbo zilizochunguzwa katika utafiti huu zina uasilia zaidi kwa sababu zinatokana na muktadha halisi wa jamii ya Wasambaa. Hii ni tofauti na hali ilivyo katika nyimbo za MBF zilizochunguzwa na Omari ambazo zinatokana na fasihi ya mataifa mengine ya Marekani na Ulaya. Hivyo, nyimbo za *mdumange* zimechunguzwa ili kuona upekee wa sanaa jadiya ya Kiafrika katika misingi ya utendaji wake, muktadha na ujenzi wa diskosi anuai miongoni mwa jamii ya Wasambaa. Licha ya kuwa Omari alizichunguza nyimbo kama utanzu wa sanaa za maonyesho, kwa namna fulani anaelekea kusesitiza kuwa utendaji wa nyimbo unazifanya zionekane kama utanzu wa fasihi simulizi zaidi.

Brunott (2013) amechunguza uhusiano baina ya ngoma na mitindo mbalimbali ya utendaji kama vile uimbaji, uchezaji na mavazi katika jamii ya Wapemba huko

Zanzibar. Katika utafiti wake, Brunott alijadili na kuonyesha namna muktadha wa utendaji wa ngoma za asili ulivyobadilika katika nyakati mbalimbali za kihistoria. Mbali na kuonyesha sababu za mabadiliko hayo, Brunott pia amejadili athari za mabadiliko ya utendaji katika jamii na katika sanaa ya ngoma. Kwa mujibu wa Brunott, zamani ngoma zilichezwa katika matukio ya kijadi kama vile harusi, matambiko na sherehe za mwaka kogwa. Watendaji hawakuwasilisha sanaa zao kwa ajili ya kupata fedha na walikuwa huru zaidi kisanaa kwa kuwa walikuwa na uwezo wa kutunga na kuwasilisha sanaa yao papo kwa papo bila maandalizi yoyote.

Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi hali ya utendaji wa sanaa ya ngoma pia imebadilika. Kwa mfano, katika wakati huu wa utandawazi ngoma huchezwa pia katika mahoteli na viwanja maalum kwa ajili ya kuwaburudisha watalii. Kwa ujumla, katika muktadha huu mpya vitendo na nia ya utendaji wa ngoma imebadilika. Akifafanua zaidi Brunott anasema kuwa mabadiliko yaliyojitokeza katika utendaji wa ngoma za asili yamechochewa na mwamko mpya wa serikali za Kiafrika kutaka kuinua fasihi jadiya kwa kuihusisha na harakati za siasa na jamii.

Vilevile mabadiliko hayo yametokana na mikakati ya serikali ambayo imethubutu kuwawekea wasanii mipaka wakati wa maandalizi ya uwasilishaji wa ngoma zao. Mipaka hiyo inahusu uteuzi wa ngoma za kucheza, nyimbo za kuimba na mitindo ya uchezaji inayofaa. Hatimaye, kutokana na kuingiliwa huko na siasa, uhuru katika vitendo vyote vinavyohusika na ngoma ulipungua kabisa. Mitindo ya uimbaji na uchezaji iliyotumika zamani ilianza kusakamwa na udhibiti kutoka kwa viongozi wa kisiasa ambao walikuwa wanatumia njia ya ngoma kuwafahamisha raia mipango ya kisiasa na mambo ya kijamii.

Hali hii imezua mtazamo hasi kwa wanajamii kuhusiana na ujumi wa ngoma za asili. Kwa mfano, wasanii wanaonekana leo hii wakicheza ngoma kwa njia ya kukata viuno wanaonekana wahuni mbele ya watu wenye mtazamo wa kulinda maadili ya jamii na taifa kwa ujumla. Hivyo, siasa na utandawazi viliathiri namna ya kucheza na hata nyimbo zilizoimbwa katika ngoma.

Utafiti wa Brunott (2013) ni muhimu sana katika utafiti wetu kwa sababu umeonyesha namna mitindo ya utendaji wa fasihi ya Kiafrika (ngoma) unahusiana na mfanyiko wa masuala anuai ya kijamii. Kupitia kazi yake tunapata kujua kuwa mitindo ya utendaji kama vile uimbaji, upigaji ngoma, na uchezaji inahusiana sana na ujumbe unaotolewa.

Kadhalika, utafiti wa Brunott (2013) umetufaa sana kwenye utafiti huu kwa sababu unaonyesha dhima ya nyimbo katika kuchambua masuala mbalimbali ya kijamii ambayo bila kutumia nyimbo hayawezi kupatikana. Akizungumzia umuhimu wa ngoma katika jamii Brunott anatoa hoja kuwa vipengele mbalimbali vya fasihi kama vile ngoma za asili vina umuhimu mkubwa katika jamii kwa kuwa husawiri mambo yaliyofichama katika jamii kwa njia isio ya waziwazi.

Katika utafiti huu wazo linalozuliwa na Brunott limetufaa sana kwa kuwa tumechunguza namna utendaji wa nyimbo za *mdumange* unatoa fursa ya kusema masuala anuai kuhusu masuala ambayo hayazungumzwi waziwazi katika maisha ya kila siku ya Wasambaa. Baadhi ya masuala yanayojadiliwa katika nyimbo za *mdumange* yanahusu jinsia, siasa, mapenzi na utamaduni. Kwa hiyo, kwa kutumia utendaji wa nyimbo za *mdumange* sauti ambazo kwa kawaida hazipati fursa ya kusikilizwa hupata nguvu ya kufanya hivyo. Utafiti wa Brunott umetufaa kwa kuwa pia umesisitiza uwezo mkubwa wa kuonyesha au kuzungumza kwa njia ya kisanii katika sanaa jadiya ya Kiafrika, ikiwemo nyimbo za *mdumange*.



Pamoja na mchango mzuri wa kazi ya Brunott, utafiti wake ni tofauti na utafiti wetu kwa kuwa yeye ameegemea zaidi katika kuonyesha mchango wa vyombo vya dola na utandawazi katika utendaji wa fasihi jadiya ya Wazanzibar. Katika utafiti wetu, badala ya kushughulikia jambo hili moja kwa moja, tumechunguza athari za utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika kujenga itikadi mbalimbali za Wasambaa. Vilevile, Brunott hakuonyesha dhahiri mikakati kiNadharia inayoweza kupambanua upekee wa nyimbo na ngoma. Kadhalika, utafiti wake hauelezi bayana mikakati ya kisanaa inayoweza kuinua ari na mwamko wa kutunga na kuwasilisha fasihi jadiya ya Kiafrika katika muktadha wake asilia.

Ili kubaini upekee wa nyimbo za *mdumange* tumeongozwa na misingi ya Nadharia za Utendaji wa Maigizo na Semiotiki ya Kijamii. Nadharia hizi zimemuewezesha mtafiti kufafanua upekee wa nyimbo za *mdumange* katika misingi ya utendaji wake mbele ya hadhira. Vipengele vya sanaa za maonyesho vinavyopatikana katika nyimbo havizifanyi nyimbo ziwe sanaa za maonyesho bali vinanogesha utendaji wake, ambao msingi wake mkuu unategemea vionjo vya kifasihi simulizi, hususan ushairi wa namna mbalimbali.

### **2.3.2 Nyimbo Kama Utanzu wa Fasihi Simulizi**

Pamoja na kutumia nyenzo za sanaa za maonyesho, nyimbo pia hutumia nyenzo za fasihi simulizi, hususan ushairi simulizi katika kufikisha ujumbe kwa hadhira. Mtazamo wa namna hii unashikiliwa na wengi miongoni mwa wataalamu kama vile Fenton (2003), Pongwen (2007), Tsiu (2008), na Hoffman (2013). Kwa mujibu wa Hoffman (*Keshatajwa*) ushairi simulizi ni sanaa iliyojengwa kwa kutumia ujumi maalum wa matumizi ya lugha. Hoffman anaendelea kuelezea kuwa lengo la mtunzi wa ushairi simulizi ni kuuwasilisha ujumbe kwa njia inayogusa na kuathiri hisia za

hadhira. Kulingana na ufafanuzi huu, nyimbo za *mdumange* ni sehemu ya ushairi simulizi wa jamii ya Wasambaa kwa kuwa uwasilishwaji wake ni wa kiutendaji na kwa kiwango kikubwa unatumia mapigo ya sauti na muziki.

Aidha, kulingana na Fenton (2003) kuna aina kuu mbili za ushairi: (i) ushairi pendwa na (ii) ushairi wa kijadi. Fenton anafafanua kuwa ushairi pendwa hutungwa ndani ya kipindi kifupi cha muda kulingana na matukio ya kila siku. Katika kipindi chote hicho, aina hii ya ushairi hubakia kuwa na umbo la namna moja lisilobadilika. Kwa upande mwingine, ushairi wa kijadi hutungwa katika kipindi kirefu cha wakati na hukumbwa na mabadiliko mbalimbali.

Ingawa katika uainishaji wake Fenton hajumuishi nyimbo katika kundi lolote la ushairi, Tsiu (2008) anadai kuwa nyimbo zinaingia katika kundi la ushairi pendwa kwa kuwa hutungwa na kuwasilishwa katika kipindi kifupi cha kihistoria na kwa kiwango kikubwa umbo lake halibadiliki sana.

Kulingana na Tsiu (*Keshatajwa*), kipengele kimojawapo kinachoonyesha kuwa nyimbo ni amali ya kijamii inayosawiri sifa za ushairi simulizi ni kuwa kwa kiwango kikubwa watunzi wa nyimbo za fasihi simulizi hawajulikani, badala yake nyimbo hizo zinatambulishwa kwa kurejelea aina ya wanajamii wanaohusika na utunzi au uwasilishwaji wake. Ni kutokana na mtazamo huu ambapo nyimbo za kiasili hufikiriwa kuwa ni aina ya fasihi isiokuwa na mtunzi wala mmiliki mahsusi, bali hubakia kuwa mali ya jamii nzima. Utambulisho wa nyimbo ni wa kijamii zaidi kuliko mtunzi mahsusi. Katika muktadha huu, nyimbo za *mdumange* zimetafitiwa kama sehemu ya fasihi pendwa ya Wasambaa kwa kuwa suala la nani alitunga wimbo halipewi uzito mkubwa. Lililo muhimu ni maudhui na ufundi wa mitindo ya uwasilishaji (lugha na viziada lugha).

Sifa nyingine ya ushairi simulizi inayojadiliwa na wataalamu hawa ni mabadiliko. Kulingana na Pongwen (2007), ushairi simulizi ni fasihi isio na umbo la kudumu, na kwa hivyo ujumi wake unajengwa na kuundwa kila wakati. Katika utafiti huu suala la mabadiliko limejadiliwa kwa kuhusishwa na mikakati ya utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Kulingana na mtazamo wa Tsiu na Pongwen, dhana za wimbo na ushairi zinahusiana sana kiasi kwamba dhana moja inaweza kuwakilisha dhana nyingine. Mtazamo unaoongoza utafiti huu ni kuwa licha ya kuwa dhana hizi zinahusiana, ushairi ni dhana pana na wimbo ni dhana mahsusi. Vilevile, wimbo hujitokeza zaidi katika muktadha wa fasihi simulizi ilhali ushairi hujitokeza zaidi katika fasihi andishi. Aidha, dhana ya ushairi inapotumika katika muktadha wa fasihi simulizi hurejelea aina mbalimbali za nyimbo kama vile majigambo, ngonjera, mbolezi na nyiso.

Licha ya tofauti zilizoainishwa kati ya dhana ya ushairi na wimbo, dhana hizi hufanana katika misingi ya kimwingiliano matini. Mosi, zote zinatungwa kwa minajili ya kutekeleza madhumuni mahsusi katika jamii ambayo ni ama kuburudisha au kuelimisha. Pili, nyimbo na ushairi huathiriwa na uwepo wa hadhira (kuna msomaji/msikilizaji). Kutokana na uhusiano huu Fenton (2003), anahitimisha kuwa nyimbo na ushairi ni tanzu zinazofungamana kwa kiasi kikubwa na sio rahisi kuzitenganisha. Kwa sehemu kubwa, ujumi wa nyimbo huwasilishwa kwa kutumia vipashio vya kiushairi kama vile takriri na tamathali za usemi.

Maelezo haya yanaonyesha kuwa sifa pambanuzi ya nyimbo mbali na kutokuwa na majina ya watunzi mahsusi ni uhusiano wa karibu kati yake na ushairi. Hii ni kwa sababu dhamira ya kwanza ya fasihi pendwa inatendwa kwa minajili ya kuifanya hadhira yake ikumbuke mambo yanayoelezwa. Njia mojawapo ya kuzifanya nyimbo hizo zikumbukike kwa urahisi ni kutumia vipashio mbalimbali vya kiushairi kama

vile takriri, toni na melodi. Kutokana na mfungamano huu, katika fasihi simulizi ya Kiafrika si rahisi kutofautisha kikamilifu wimbo, shairi na muziki hasa kwa kuwa ndani ya arudhi za kiushairi kuna mapigo ya kimuziki na matumizi ya ala za muziki.

Suala hili ni muhimu kulihusisha na utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwa kuwa katika nyimbo hizo, mwimbaji ambaye ndiye mshairi na mwanamuziki hawatenganishiki. Hii inaonyesha kuwa kulingana na mtazamo wa Kiafrika, Wasambaa wakiwemo dhana za mshairi na mwanamuziki zinafumbatwa pamoja katika suala zima la utendaji. Ni kutokana na muktadha huu ambapo yeli (griot) wa tendi za Kiafrika walijulikana kama wanamuziki wabobezi (professional musician) kutokana na ujuzi wao wa kutongoa na kuwasilisha tendi mbele ya hadhira (Tsiu, 2008).

Fikra kuwa ushairi hutunza kumbukumbu ni muhimu pia katika utafiti huu kwa kuwa pamoja na mambo mengine utafiti huu unahoji kuhusu dhima ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika kutunza kumbukumbu za Wasambaa. Utafiti huu unahoji namna ambavyo uwasilishwaji wa nyimbo za *mdumange* unakuwa ghala la kuhifadhia na kuendeleza amali za jamii na historia yao. Kwa hivyo, utafiti unazichunguza nyimbo za *mdumange* kama aina mahsusi ya mfumo wa mawasiliano ambapo wanajamii hujiieleza, na wakati huohuo huonyesha migogoro ya namna mbalimbali.

Samwel (2012) ni mmoja kati ya watafiti waliochunguza ushairi simulizi wa Kiafrika. Utafiti wa Samwel ulimakinikia mabadiliko yaliyojitokeza baina ya majigambo ya kijadi na ya kisasa. Katika utafiti wake, Samwel aliyachukulia majigambo ya kijadi kama kijejezi cha kuhakikia Nadharia tete iliyodai kuwa tanzu mpya za kifasihi huzuka kutokana na misingi ya tanzu za zamani za kifasihi. Kwa mujibu wa Samwel (2012), majigambo ya kisasa yanayoonekana katika MBF yameibuka kutokana na

misingi ya majigambo ya kijadi yaliyokuwa yakitendwa katika jamii mbalimbali nchini Tanzania.

Aidha, Samwel anatoa hoja kwamba licha ya kuwa majigambo ya kijadi ndiyo yaliyosababisha kuzuka kwa majigambo ya kisasa, kuna tofauti mbalimbali za kifani na kimaudhui zinazodhihirika baina yake. Tofauti hizo zimejikita katika vipengele vinavyohusiana na malipo, muundo wa jukwaa, mavazi pamoja na hadhira. Hata hivyo, Samwel anaelekea kutushawishi tuamini kuwa majigambo ya kijadi yalikuwa na nguvu ya kuweza kuathiri majigambo ya kisasa. Kwa upande mwingine, utafiti wa Samwel unaelekea kusesitiza kuwa majigambo ya kijadi yamekuwa imara kiasi kwamba licha ya kuingiliana na utanzu mpya wa ushairi simulizi (MBF) kwa muda mrefu hayakuathiriwa.

Hii ina maana kuwa, nyimbo za majigambo ya kisasa (MBF) zina uwezo wa kupokea tu mabadiliko kutoka kwa nyimbo za majigambo ya jadi, na kamwe nyimbo za majigambo ya kijadi hazijaathiriwa na nyimbo za majigambo ya kisasa. Ikiwa ni kweli kuwa tanzu mpya za kifasihi huzuka kutokana na misingi ya tanzu zilizopo, basi hapana shaka kuwa tanzu hizo mpya pia zina nafasi ya kuzua mabadiliko mbalimbali katika tanzu kongwe. Kwa upande mwingine, utafiti huu unadai kuwa mabadiliko ya kijamii na muktadha ambamo nyimbo za *mdumange* zinafanyika huchangia mabadiliko katika utendaji wake na dhima yake.

Ingawa utafiti wa Samwel umefanikiwa kujadili nduni za kifani na kimaudhui za nyimbo za majigambo ya kijadi na kisasa, suala la utendaji halijapewa hadhi na nafasi inayostahiki. Hii ni kwa sababu kati ya nduni alizojadili, vipengele mbalimbali vya utendaji wa nyimbo za majigambo ya kijadi na ya kisasa vimewekwa katika kundi la nduni za kifani. Mgawanyo na ufafanuzi huu unaonyesha namna ambavyo mwandishi

alivyolichukulia suala la utendaji kuwa lina nafasi sawa na vipengele vingine vya kifasihi katika nyimbo alizotafiti.

Utafiti huu unatoa hoja kuwa mbinu na vipengele mbalimbali vya utendaji havipaswi kuwekwa katika makundi ya fani wala maudhui, pia mbinu hizo hazipaswi kutenganishwa na maana ya kazi ya kifasihi. Kwa hivyo, mbinu na mitindo ya utendaji katika ushairi simulizi (nyimbo zikiwemo) zinafaa zichukuliwe kama mhimili mkuu wa sanaa husika uliopo baina ya fani, maudhui na maana au ujumbe wa sanaa husika. Azma ya kuchunguza vipengele vya utendaji katika utafiti huu ni kujadili na kutathmini muumano uliopo baina ya mitindo ya utendaji na ujenzi wa diskosi za kijamii. Kwa hivyo, katika utafiti huu suala la utendaji limetazamwa katika mawanda mapana zaidi, badala ya kuchukuliwa kama ama mbinu za kifani au mbinu za kimaudhui.

Kimsingi, mawazo ya Samwel kuhusu mabadiliko katika fasihi simulizi yamechochea fikra za kiudadisi na kiuchunguzi katika utafiti wetu. Kadhalika, kazi yake imetufaa kwa kuwa hata kama haikuhusu utendaji wa nyimbo moja kwa moja lakini katika kazi yake amekuwa akigusia na kudokeza masuala mbalimbali ya utendaji katika ushairi wa majigambo. Baadhi ya vipengele hivyo ni kama vile hadhira, fanani, sauti, mavazi, ala zinazotumika na mitindo ya uchezaji. Pia, kazi yake ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu kupitia hitimisho lake kuwa tanzu mpya za kifasihi huzuka kutokana na misingi ya tanzu za zamani za kifasihi tumepata kufahamu na kuendelea kudadisi jinsi fasihi simulizi ilivyo hai. Fasihi hii inakuwa na kubadilika kwa haraka zaidi ikilinganishwa na fasihi andishi.

Kutokana na mabadiliko hayo hata idadi ya tanzu za fasihi simulizi huongezeka na hupungua kila uchao. Hii ni kwa sababu licha ya kuongezeka kwa tanzu za fasihi

simulizi, mabadiliko katika fasihi simulizi pia huweza kuchochea kufa na kupotea kwa baadhi ya tanzu. Utafiti huu umefanywa ili kunusuru hatari ya kupotea au kufa kwa tanzu au mitindo ya utendaji na pia ili kuchunguza dhima ya mitindo ya utendaji katika kuzua mabadiliko mbalimbali ya jamii ya Wasambaa.

Hata hivyo, Samwel anafikiri kuwa mabadiliko katika fashi simulizi huzuka kiholela kutokana na misingi ya tanzu za kifasihi zilizochunguzwa. Katika utafiti huu, kuzuka kwa mabadiliko katika fasihi simulizi kumehusishwa na mchakato wa utendaji wa sanaa husika, hususan nyimbo za ngoma ya *mdumange*. Utendaji wa tanzu mbalimbali za kifasihi simulizi kama vile nyimbo unaweza kuzua mabadiliko chanya au hasi kwa fasihi yenyewe au kwa jamii. Samwel anagusia mabadiliko lakini hakuyahusisha na suala la utendaji. Kutokana na kutohusisha na utendaji, ndio maana Samwel anaishia tu kujadili kuzuka kwa tanzu mpya kama mojawapo ya mabadiliko katika ushairi simulizi. Katika utafiti huu tumepiga hatua mbele zaidi kwa kujadili sio tu kuzuka kwa vionjo vya kifasihi bali pia hata kutoweka kwa ama vionjo au utanzu mahsusi wa kifasihi.

Kadhalika, ingawa utafiti wa Samwel una mchango mkubwa katika utafiti wetu, kwa kiwango kikubwa kazi yake ni tofauti na kazi hii kwa kuwa yeye aliongozwa na misingi ya Nadharia za Umatini zaidi ilhali katika utafiti huu tumeongozwa na misingi ya Nadharia za Kiutendaji. Kuna hatari kadhaa zinazoweza kutukia endapo mhakiki ama mtafiti wa fasihi simulizi ataongozwa na misingi ya Nadharia zenye muelekeo wa Nadharia za Umatini.

Mojawapo ya hatari hizo ni kupuuza mihimili imara ya utokeaji wa fasihi simulizi na hivyo kusababisha kuwako kwa hitimisho lisilokuwa na mashiko. Hiki ndicho kilichotokea katika utafiti wa Samwel kwa kuwa katika kazi yake anaelekea kuamini

kuwa mkabala wa matini una faida kubwa katika uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi ikilinganishwa na mkabala wa muktadha. Kwa hiyo, anapendekeza kuwa katika kutambua kama utanzu wa fasihi simulizi unatendwa na wanaume ama wanawake peke yao au wote kwa pamoja tusitazame muktadha wa utokeaji wake badala yake tutazame umbo la matini ya utanzu huo kifani na kimaudhui. Kwa maoni yetu huu si msimamo mwafaka katika fasihi simulizi ya Kiafrika.

Hoja zinazojengwa na Samwel zinakosa mashiko kwa kuwa yeye mwenyewe anakiri kuwa muktadha unabadilika kwa haraka zaidi kuliko matini. Katika utafiti huu tunatoa hoja kuwa si sahihi kujiegemeza katika kigezo cha matini wakati wa kuamua mitindo ya utendaji wa utanzu mahsusi wa fasihi simulizi. Jambo muhimu ni kuwa muktadha ni kiambajengo muhimu cha utendaji na hivyo kinapaswa kuchunguzwa. Katika utafiti huu, tumeongozwa na vigezo vya kimuktadha katika kubainisha mitindo mbalimbali ya utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Kutokana na vigezo hivyo, tumeshuhudia wanaume na wanawake wakishiriki utendaji wa nyimbo za *mdumange* ama katika nyakati tofautitofau au katika wakati mmoja.

Kwa hivyo, katika utafiti huu tumeonyesha aina za watu wanaoshiriki utendaji wa nyimbo za *mdumange* pamoja na athari ya ushiriki wao katika utendaji huo. Suala la kutambua aina ya wanaoshiriki utendaji wa nyimbo limeshughulikiwa kwa kutumia ushahidi kutoka nyanjani katika muktadha wa uwasilishaji, na si kutokana na matini au dhamira ya nyimbo za *mdumange*.

#### **2.4 Misingi ya Ujumi wa Nyimbo**

Ingawa tumedokeza katika sehemu zilizotangulia kuwa nyimbo za *mdumange* zimechunguzwa kama aina mahsusi ya kipera cha fasihi simulizi badala ya kipera cha sanaa za maonyesho ni vema pia kusisitiza hapa kuwa tanzu hizi (yaani fasihi simulizi



na sanaa za maonyesho) huingiliana sana. Kutokana na mwingiliano huo utendaji wa sanaa za maonyesho hutumia pia vipengele vya kifasihi simulizi, hususan utambaji wa ngano na uimbaji wa nyimbo. Vivyo hivyo utendaji wa fasihi simulizi hutumia pia vipengele vya sanaa za maonyesho. Kutokana na hali hii, sehemu ifuatayo inajadili sifa pambanuzi za ujumi wa nyimbo kulingana na misingi ya kimwingiliano matini, kiuamilifu na kiutendaji.

#### **2.4.1 Misingi ya Kimwingiliano Matini**

Wataalamu mbalimbali wanaona kuwa ujumi wa nyimbo unapatikana kwa kutumia kanuni au mchakato wa kimwingiliano matini. Miongoni mwa wataalamu hao ni Karim (1999), Jameson (2005) na Brown (2016). Kwa mfano, ili kuelezea ujumi wa nyimbo au ushairi simulizi Brown (2016) alichunguza mwingiliano wa fasihi simulizi na fasihi andishi katika misingi ya utendaji wake. Hoja kuu ya Brown ni kuwa katika jamii ya Wakhoikhoi, fasihi simulizi na fasihi andishi zimeathiriana sana kupitia utendaji wa tanzu mbalimbali za ushairi simulizi hususan nyimbo. Ni kutokana na tabia hii ya kuathiriana ambapo Brown anajadili matumizi ya mbinu za usimulizi katika ushairi andishi wa jamii hiyo kunako miaka ya 1970. Aidha, utafiti wa Brown pia umeonyesha namna utendaji wa mashairi simulizi ulivyoshamiri katika majukwaa ya kisiasa miaka ya 1980.

Kwa ujumla, utafiti wa Brown unahusiana na utafiti wetu katika baadhi ya mambo kama vile utashi wa fanani na hadhira kubuni na kubadilisha utendaji kutegemea matakwa ya hadhira na jamii kwa jumla. Katika kazi hiyo, Brown anaelezea jinsi wasanii wa nyimbo walivyofanikiwa kutumia vipaji vyao kutekeleza majukumu mbalimbali ya kijamii kama vile kuwasifu viongozi wao, kuhifadhi mila na desturi zao, pamoja na kuburudisha jamii. Mashairi hayo yalitongolewa katika miktadha

halisi ya kijamii kwa kutumia lugha za wazawa, na yaliwasilishwa kwa kutumia mbinu za kiutendaji.

Brown anazidi kufafanua kuwa hata baada ya kuja kwa wageni katika jamii hii, utongoaji wa nyimbo (ushairi simulizi) haukukoma, badala yake uliendelea sanjari na utungaji wa mashairi (ya fasihi andishi). Kazi ya Brown pia imetuwezesha kufahamu athari ya dini na serikali za kigeni katika fasihi simulizi. Anasema kuwa kutokana na kuja kwa Wamisionari, fasihi simulizi ya jamii za Kiafrika iliathiriwa kifani na kimaudhui. Mifumo mipya ya kiutawala na kidini iliathiri utendaji wa nyimbo na aina nyingine za fasihi simulizi. Kwa mfano, kuja kwa wageni kulizua tanzu za ushairi simulizi (nyimbo) zilizosifu sio viongozi wala miungu ya kijadi peke yake bali pia zilijitokeza tanzu za ushairi simulizi uliotukuza Wazungu na dini ya Kikristo.

Kadhalika, utafiti wa Brown umetufaa sana kwa kuwa umefafanua athari za kukua kwa miji katika fasihi ya jamii za Afrika ya Kusini. Kukua kwa miji katika jamii hii kuliendana na shughuli za uchimbaji madini, hamahama ya watu na kuimarika kwa miundo mbinu ya usafiri na mawasiliano. Kutokana na muktadha huu, ushairi simulizi ulibadilika na kuzua utanzu mpya wa nyimbo (sefela) ambazo ni nyimbo zilizotongolewa na wachimba madini kwa minajili ya kuelezea hisia zao za kuupinga unyonyaji uliofanywa na makaburu. Kwa ujumla, Brown amefanikiwa sana katika kuonyesha uhusiano baina ya ushairi na muktadha wa kijamii.

Kimuktadha, utafiti wa Brown ni tofauti na wetu kwa kuwa yeye aliangalia namna ushairi simulizi unavyotendwa katika jamii iliyoendelea katika viwanda, sayansi na teknolojia. Hii ni tofauti na utafiti wetu kwa kuwa muktadha uliochochea kutokea kwa nyimbo za *mdumange* katika jamii ya Wasambaa ni wa jamii ya wakulima, wafugaji na ni muktadha wa vijijini sio wa mjini. Kwa hiyo, ikilinganishwa na utafiti

wa Brown utafiti wetu ni wa kipekee kwa sababu umeangazia jinsi hali ilivyo katika jamii zisizo na viwanda.

Utafiti wa Brown uliangazia athari ya muktadha wa mapinduzi ya viwanda katika utendaji wa ushairi huko Afrika ya Kusini. Katika utafiti huu hali ni tofauti kwa kuwa tunaangazia mchango wa sherehe za harusi, dini na siasa katika utendaji wa nyimbo. Tofauti za kimuktadha baina ya jamii hizi mbili zinatarajiwa kutupatia aina tofauti za mitindo ya utendaji na hatimaye kuzua mwitiko tofauti wa hadhira. Kwa hiyo, utafiti huu umetujaza mengi kuhusu itikadi ya jamii ya wakulima, jamii ambayo haina viwanda.

Karim (1999) alichunguza ushairi wa fasihi simulizi ya jamii ya Wayoruba kutoka Afrika Magharibi. Katika utafiti wake, Karim anatoa hoja kuwa tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Wayoruba huingiliana sana na kuwa aina moja ya utanzu wa kifasihi ina uwezo wa kusawiri na kuwasilisha diskosi nyingi kwa wakati mmoja. Kiutendaji, tanzu za ngano hutofautiana na ushairi simulizi kwa kuwa utendaji wa ngano katika jamii ya Wayoruba huwaruhusu watu wote kutoka katika rika tofautitofauti kutongoa na kusikiliza ngano. Hii inaashiria kuwa katika jamii ya Wayoruba, kuna demokrasia kubwa ya kutamba na kutongoa ngano kuliko katika kutongoa aina mbalimbali za mashairi kama vile majigambo na ushairi wa kidini.

Hali hii imetokana na namna maudhui ya ngano yanavyohusishwa na jamii nzima kama vile ujirani mwema, uaminifu na urafiki. Mashairi ya kidini yanatongolewa na wataalamu mahsusi waliobobea katika jadi ya uganga. Hata hivyo, ingawa si watu wote wanaruhusiwa kutongoa mashairi ya kidini, Karim anatoa hoja kuwa utongoaji wa mashairi haya pia hutumia vionjo vya utambaji wa ngano kama vile majina ya wahenga, koo/mbari na visasili.

Kwa upande mwingine, utendaji wa mashairi simulizi ya kimajigambo unafanana sana na utendaji ngano pamoja na mashairi ya kidini. Ili kudhihirisha kuwa tanzu hizi zimeathiriwa na utendaji wa kimwingiliano matini, Karim anasema kuwa utendaji wa tanzu zote zilizoainishwa hapa unatekelezwa kwa kutumia lugha za Kiyoruba, taswira za kijamii na urudiaji wa fomula mbalimbali mwanzoni na mwishoni mwa utendaji.

Hata hivyo kila moja kati ya tanzu hizi ina msisitizo wa aina yake kimaudhui. Majigambo husisitiza sifa za mashujaa, viongozi mashuhuri, na utamaduni wa kufanya kafara. Kwa upande mwingine ushairi wa kidini unahusu magonjwa na matibabu kwa wagonjwa wanaotaka kuombewa kwa wahenga. Ushairi wa kidini pia hutendwa na watu maalum. Ngano zinawasilisha dhamira mbalimbali za maisha binafsi na maisha ya jamii nzima kama vile umoja, urafiki, na migogoro.

Hoja nzuri inayotolewa na Karim na ambayo imechangia pa kubwa kuimarisha utafiti huu ni kuwa tanzu za fasihi simulizi huingiliana na huathiriana. Sifa hii ya kuingiliana kwa tanzu za fasihi simulizi imeangaziwa pia katika utafiti wetu. Katika utafiti huu tumehoji jinsi utendaji wa nyimbo za *mdumange* unafanyika kwa kutumia mikakati mbalimbali ya kimwingiliano matini kama vile uchanganyaji wa nyimbo, ngoma, methali na maigizo wakati wa kuwasilisha nyimbo za *mdumange*.

Pamoja na mchango mzuri wa kazi ya Karim, ni dhahiri kuwa utafiti wake unatofautiana na utafiti wetu kwa sababu yeye aliangazia ulinganishi wa ngano, majigambo na matabano (ushairi wa kidini au uganga) katika jamii ya Wayoruba. Tofauti na alivyofanya Karim, katika utafiti huu tumeangazia ushairi simulizi peke yake, hususan nyimbo zinazoimbwa kwenye muktadha wa sherehe. Tofauti hizi zinatazamiwa kutupatia matokeo tofauti na ya pekee kuhusu sifa mahsusi za mikakati ya utendaji, dhima ya mikakati hiyo na dhima ya nyimbo katika jamii ya Wasambaa.

Mtaalamu mwingine aliyechunguza mwingiliano matini kama sifa mahsusi ya ujumi wa ushairi simulizi wa Kiafrika ni Jameson (2005). Katika utafiti wake, Jameson amejadili chimbuko la vipengele mbalimbali vya Utendaji wa Maigizo katika ushairi wa Kiafrika. Kwa mujibu wa Jameson (*Keshatajwa*), haiwezekani kugawa ushairi wa Kiafrika katika mihula mahsusi isiotegemeana wala kuathiriana. Hii ni kwa sababu aina moja ya ushairi imejengwa kutokana na misingi ya aina nyingine ya ushairi iliyowahi kuwako kabla yake. Aidha, Jameson anaendelea kufafanua kuwa jitihada zinazofanywa katika kutenganisha na kutofautisha fasihi andishi na fasihi simulizi kamwe hazitafanikiwa (Honko, 2000; na Harding, 2002). Hii ni kwa kuwa si rahisi kuweka mpaka ulio wazi kati yake.

Madai ya Jameson ni mazuri kwa kuwa yanaonyesha namna vijenzi mbalimbali vya utendaji wa fasihi simulizi vimejitokeza katika ushairi andishi. Hata hivyo, mawazo yake yanakabiliwa na changamoto ya kukosa kuaminika kwa kuwa hayakutokana na utafiti yakinifu uliochunguza ushairi simulizi, badala yake hitimisho lake limetokana na uchunguzi wa ushairi andishi. Katika utafiti huu tumejikita katika nyimbo ambazo ni aina mojawapo ya kipera cha utanzu wa ushairi simulizi.

Simiyu (2015) alichunguza mwingilianotanzu katika fasihi simulizi ya jamii za Wamakunduchi na Babukusu. Katika utafiti wake alirejelea mila na desturi za jamii husika hususan sherehe ya *mwaka kogwa* kutoka jamii ya Wamakunduchi na tambiko la *Embalu* miongoni mwa Babukusu. Kimsingi, utafiti wa Simiyu (*keshatajwa*) ulitumia miviga ya *mwaka kogwa* katika kubainisha namna tanzu zinavyoingiliana katika utendaji. Aidha, utafiti huo umeshughulikia miviga ya *embalu* ambayo ni sehemu ya fasihi simulizi ya Babukusu.

Fasihi Simulizi ya Babukusu inajumulisha *chingano* (ngano), *kimienea* (nyimbo), *chisimo* (semi) na *kimilukha* (miviga). Ilibainika kuwa tanzu mbalimbali za miviga iliyochunguzwa hazina majina maalum ya kuzitofautisha, ila muainisho ambao umekuwa ukifanyika unatokana na tajiriba ya uainishaji wa fasihi za kigeni na hata zile za Waswahili. Kutokana na utafiti wake, Simiyu alihitimisha kuwa Wamakunduchi na Babukusu hawakuona haja ya kuigawa fasihi yao kuipa majina maalum, kwani zote zilitekeleza majukumu yaleyale.

Utafiti wa Simiyu (2015) ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa pamoja na mambo mengine umeonyesha kuwa kutokana na sifa ya mwingiliano tanzu wimbo mmoja unaweza ukawa wa aina nyingi ndani yake kutegemea muktadha na malengo ya uwasilishaji wake. Mawazo haya yanajenga msingi imara wa utafiti huu unaolenga kuchunguza utendaji wa nyimbo za mdumange miongoni mwa Wasambaa. Ni kutokana na msingi huo ambapo nyimbo za mdumange zinatarajiwa kudhihirisha ndani yake tanzu nyingine za fasihi hasa wakati wa utendaji. Kimsingi, utafiti huu basi utaonyesha ikiwa kuna haja ya kutenganisha tanzu za fasihi wakati wa utendaji au la.

Tofauti na utafiti wa Simiyu (2015) ambao ulitumia jukwaa la tohara (*embalu*) utafiti huu ni wa kipekee kwa kuwa unatumia jukwaa la sherehe mbalimbali za Wasambaa kama vile harusi, siasa, mwaka mpya na dini kama mfano wa miviga kutoka kwenye kongoo kuu la fasihi simulizi ya Wasambaa, kwa madhumuni ya kudhihirisha utendaji na dhima yake katika fasihi simulizi ya Kiafrika.

#### **2.4.2 Misingi ya Kiuamilifu**

Wataalamu mbalimbali wamejadili vipengele vinavyojenga ujumi wa nyimbo, hususan nyimbo na nafasi yake katika jamii (Sebeok, 1959; Jakobson, 1960; Rirash,

1992 na Fabb, 2009). Kwa mujibu wa Jakobson, nyimbo au ushairi ni muhimu sana katika jamii sawa na jinsi lugha ilivyo kuwa na umuhimu. Akifafanua zaidi umuhimu wa sanaa ya ushairi, Jakobson anasema kuwa kama ilivyo kwa sanaa ya uchoraji na upakaji rangi ambayo huwasilisha ujumbe kwa njia ya kuona, sanaa ya ushairi ni muhimu kwa kuwa huwasilisha ujumbe kwa kutumia lugha (Jakobson, 1960).

Jakobson anasisitiza kuwa ushairi unapaswa kuzingatiwa kama sanaa muhimu na ya maana sana inayofanya kazi ya kutathmini vipengele vyote vya kiisimu vitumikavyo katika kuwasilisha ujumbe. Kutokana na mawazo ya mwanaNadharia huyu, sanaa ya ushairi imelinganishwa na kuhusishwa na vipengele mbalimbali vya kiisimu. Kwa hivyo, ili kuchanganua sanaa hii kwa ufanisi zaidi ni vyema kwanza mhakiki aelewe na afafanue misingi ya matumizi ya lugha katika matini husika. Hoja hii iliwahi kupendekezwa pia na Sebeok (*Keshatajwa*) aliyesema kuwa ili kuweza kujua umuhimu wa kila mshororo katika nyimbo, kwanza ni jambo la maana kwa mhakiki kuelewa ujumbe unaowasilishwa kwa kutumia muundo wa sentensi au lugha.

Aidha, mawazo ya Sebeok pia yanaendana na mawazo ya Jakobson anayedai kuwa muundo wa ushairi wa jamii fulani hauna budi kuhusishwa na muundo wa fonolojia ya lugha husika (Jakobson, 1960). Mawazo yanayopendekezwa na Jakobson na wenzake yanashadidia kuwa sanaa ya ushairi inahusiana na taaluma ya isimu kwa kuwa utunzi na uwasilishaji wa mashairi hutumia vipengele mbalimbali vya kiisimu kwa kufuata sarufi ya lugha husika. Hata hivyo, si wataalamu wote wanaoamini katika Nadharia hii. Wengine wanaona kuwa ingawa ni kweli kuwa ushairi hutumia vipengele mbalimbali vya kiisimu kuna wakati ambapo ushairi huwasilishwa bila kutumia vipengele vya kiisimu.

Mtazamo kuwa kuna uwezekano wa kuwasilisha ushairi bila kutumia vipashio vya kiisimu unaendelezwa na kusisitizwa na Fabb (2009). Katika kufafanua hoja hii Fabb anasema kuwa tofauti na nathari ambazo hazina ushikamani, sanaa ya ushairi hutumia vipashio mbalimbali visivyo vya kiisimu kujenga ushikamani kati ya maneno, sentensi na dhamira. Baadhi ya vipengele visivyo vya kiisimu vinavyotumika kujengea ushikamani katika ushairi ni mizani, vina vya kati na vya mwisho. Vipengele hivi kwa kawaida vinakengeuka misingi ya matumizi ya lugha ya kishairi na kujiegemeza zaidi katika matumizi ya lugha inayotumiwa katika mawasiliano ya kawaida katika maisha ya kila siku (Fabb, 2009). Mawazo ya wataalam hawa ni muhimu kwa kuwa nyimbo za *mdumange* ni sehemu ya ushairi simulizi wa jamii ya Wasambaa. Kwa hiyo, tumechunguza utendaji wa nyimbo hizi kwa kuangazia matumizi ya lugha, muziki, uchezaji na miondoko ya watendaji.

Dhima nyingine ya ushairi katika jamii ni kutunza na kuendeleza utamaduni wa jamii. Kwa muda mrefu, ushairi umepewa jukumu la kuzilinda na kuziendeleza turathi za kijamii kama vile lugha, mavazi, uongozi na historia. Kutokana na umuhimu huu, baadhi ya wanazuoni wanafikiri kuwa maudhui ya ushairi simulizi ni muhimu zaidi kuliko mbinu zake za uwasilishaji kwa kuwa katika maudhui kuna amali mbalimbali za kijamii kama vile visasili, malezi na historia. Mtazamo huu unashikiliwa na mwanazuoni wa Kimagharibi aliyeitwa Lord (1960). Akitetea hoja yake, Lord (1960) anasema kuwa maudhui ya kijadi yanaelekea kudumisha msimamo wa jamii na kuhifadhi mashairi husika. Kwa hiyo, mashairi simulizi ni muhimu kwa kuwa yana dhima kubwa ya kulinda na kuendeleza utamaduni wa jamii. Kwa mtazamo huu, mashairi hatazamwi kama msanii tu bali anatazamwa kama mhenga na mzalendo wa taifa ambamo anabuni na kutongolea mashairi yake.



Hoja kuwa ushairi ni hazina ya kutunza na kuendeleza jadi na tamaduni za jamii inaendelezwa na kuimarishwa na Njogu na Chimera (1999). Njogu na Chimera wanaona kuwa ushairi simulizi ni kama insaiklopedia ya jamii. Anasema kuwa mpaka kufikia nusu ya pili ya Karne ya 15 katika bara Ulaya taaluma za sheria, usimamizi wa biashara na kilimo zilitakiwa zishabihiane na kanuni ama elimu iliyoelezwa katika utamaduni wa turathi simulizi. Aidha, Njogu na Chimera wanasisitiza kuwa hata mashairi ya tendi za Homer huko Ugiriki yalikuwa na dhima kuu mbili: (i) kuburudisha na (ii) kuwa insaiklopedia inayohifadhi amali za kijamii.

Mtazamo wa Lord kuhusu suala la ujadi na dhima ya ushairi simulizi katika kulinda na kuendeleza tamaduni za jamii ni kuwa tendi simulizi zilikuwa na muelekeo wa kidiakronia ambapo michakato mbalimbali ya mabadiliko ya kijamii hujitokeza wakati huohuo jitihada za kubakisha na kuhifadhi amali ambazo zingali na umuhimu kwa jamii hufanyika (Foley, 1988). Ni kutokana na umuhimu huu wa nyimbo katika jamii ndipo utafiti huu umeangazia nyimbo za *mdumange*.

Rirash (1992) alichunguza ushairi simulizi wa jamii ya Wasomali. Uchunguzi wake ulikusudia kufafanua namna ushairi simulizi unatumika kama mbinu ya kuelewa na kusuluhisha migogoro katika jamii za wafugaji. Anafafanua kuwa, katika jamii za wafugaji ushairi simulizi pamoja na aina nyingine ya fasihi simulizi ndicho chombo kikuu cha mawasiliano kwa kuwa jamii hizi bado hazijapata fursa ya kuwa na ujuzi wa kusoma na kuandika. Jamii za wafugaji hutumia ushairi simulizi sio tu kuelezea migogoro bali pia kuhifadhi historia yao ya matukio ya kila siku.

Rirash anazidi kuelezea kuwa jamii ya Wasomali imefanikiwa kutumia ushairi simulizi kama dafina ya kuhifadhi historia yao kwa sababu kila mwanajamii anaanza kujifunza na kukariri mashairi tangu akiwa mtoto mdogo. Matukio mbalimbali

yahusuyo malezi ya watoto yalifanywa na mama, dada na wanafamilia wengine kwa kutumia nyimbo mbalimbali. Pia, jamii iliimba nyimbo katika shughuli za pamoja kama vile kulima na kutwanga mahindi, kuchunga ng'ombe na ndama. Rirash anaelezea kuwa utashi wa kuimba na kutongoa mashairi miongoni mwa Wasomali ni mkubwa kwa kuwa ujuzi huo huendelezwa mpaka wanapokuwa watu wazima.

Utafiti wa Rirash umetufahamisha chimbuko na maendeleo ya nyimbo au ushairi simulizi wa jamii ya Wasomali. Pia katika utafiti huu tumefanikiwa kuweka bayana dhima za nyimbo katika jamii ikiwa ni pamoja na kufafanua chimbuko la migogoro inayotokea katika jamii za wafugaji. Tunaelezwa kuwa migogoro hiyo inahusu vyanzo vya maji, maeneo ya kuchungia wanyama na mashamba ya kulima. Pia migogoro hiyo ilichimbuka kutokana na ongezeko la idadi ya watu linalohitaji serikali kuratibu njia sahihi ya kutatua migogoro. Pia, utafiti wa Rirash umetufaa kwa namna ilivyofafanuliwa kuwa jamii hii ilirithisha jadi ya mashairi simulizi kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya kukariri.

Mashairi simulizi miongoni mwa jamii ya Wasomali yalikaaririwa na watoto na baadaye watoto hao walipokuwa watu wazima waliyaendeleza na kuyatongoa kwenye hafla za kijamii zikiwemo mikutano ya siasa, harusi na kwenye misiba. Kama ilivyo kwa Wasomali, Wasambaa pia wanategemea kilimo na ufugaji kama shughuli kuu za kiuchumi. Aidha, Wasambaa pia wanategemea sana turathi za kifasihi simulizi kurithisha amali za jamii. Kutokana na kushabihiana kwa jamii hizi kiutamaduni masuala yanayojitokeza kwa Wasomali yana mchango mkubwa katika utafiti huu kwani yanasaidia kulinganisha jinsi nyimbo zinafanya kazi katika maeneo haya mawili.

Kwa upande mwingine, pamoja na uzito wa hoja za Rirash bado utafiti wake ni tofauti na wa kwetu kwa kuwa yeye alimakinikia zaidi kipengele cha maudhui ya migogoro katika ushairi simulizi. Pia utafiti wake ulikabiliwa na changamoto ya kutoa hitimisho la jumla kuwa katika jamii ya wafugaji takribani kila mtu ni mshairi. Tofauti na alivyofanya Rirash, utafiti huu unatoa hoja kuwa ingawa ushairi simulizi hutumika sana katika jamii za wafugaji na ambazo hazina maandishi haifai kuhitimisha kuwa kila mtu ni mshairi kwa kuwa usanii wa washairi hutofautiana toka msanii mmoja na mwingine. Katika utafiti huu tumejadili zaidi suala la viwango vya ubunifu wa wasanii na watendaji katika nyimbo kupitia utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Masuala yaliyosisitizwa zaidi kwenye utendaji huo ni muktadha, mitindo ya utendaji pamoja na dhima ya utendaji wa nyimbo katika kufasiri ulimwengu wa Wasambaa.

### **2.4.3 Misingi ya Utendaji**

Miongoni mwa wataalamu walioshughulikia utendaji wa nyimbo ni Mvula (1994), Mulokozi (2002) na Tsiu (2008). Mvula (1994) alichunguza mitindo ya utendaji katika nyimbo zinazoimbwa na wanawake miongoni mwa jamii ya Wangoni. Aidha, wanawake waliimba nyimbo hizo wakati wa kutwanga mahindi. Mvula anasema kuwa utafiti wake uliongozwa na mtazamo wa Bauman (1975) kuwa maendeleo makubwa katika utafiti wa sanaa jadiya ya Kiafrika yamesababisha watafiti kutozitazama sanaa jadiya kama masalia ya kale badala yake tafiti za sasa zinatazama sanaa jadiya kama mchakato wa kimawasiliano. Katika mkabala huu, sanaa jadiya huongozwa na kanuni za kiutamaduni ili kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wanadamu. Kutokana na msingi huu, Mvula anaongeza kwa kusema kuwa mitindo ya utendaji inayotumiwa katika nyimbo za kutwanga mahindi ina dhima ya kuwawezesha wanawake kuwasilisha hisia na fikra zao kwa jamii.

Licha ya kuwa Mvula alishughulikia mbinu za utendaji katika nyimbo za jamii ya Wangoni, kwa namna moja ama nyingine utafiti wake unahusiana na utafiti huu. Utafiti wake ulidhamiria kufafanua mitindo ya utendaji wa nyimbo za wanawake katika jamii ya Wangoni. Katika kufafanua mitindo hiyo, Mvula anasema kuwa watendaji wa nyimbo husika hutumia mbinu mbalimbali kama vile tanakali za sauti, taswira, ushirikishwaji wa hadhira, ucheshi pamoja na dialojia. Kwa ujumla, wasanii hutumia jukwaa la utendaji wa nyimbo husika kuelezea hisia zao kama vile hisia za kukejeli waume zao pamoja na kuonyana wao kwa wao.

Kwa mujibu wa Finnegan (1977) nyimbo (ushairi) wa namna hii yafaa uwekwe katika kundi la sanaa yenye kazi maalum kwa kuwa huwapatia wanawake fursa ya kuwasilisha dhamira mahsusi za ndoa, urafiki, na mapenzi. Washiriki wake hutumia mbinu mbalimbali za kiutendaji kutekeleza malengo yao. Kwa hiyo kuna uhusiano mkubwa baina ya mitindo ya utendaji na malengo au azma ya fanani wa fasihi simulizi. Ni kutokana na uhusiano huo ndio maana Mvula anasema kuwa kufanikiwa ama kutofanikiwa kwa wanawake katika utendaji wa nyimbo zao kunategemea utashi wao wa kutumia vyema mbinu husika za utendaji.

Ingawa utafiti wa Mvula umesaidia kutufahamisha mitindo ya kiisimu na kiutamaduni katika utendaji wa nyimbo miongoni mwa Wangoni, bado ipo haja ya kutafiti zaidi utendaji wa aina nyingine za nyimbo katika jamii za Kiafrika. Nyimbo alizochunguza zinaimbwa katika muktadha wa kutwanga mahindi na huimbwa na wanawake peke yao. Hii ni tofauti na ilivyo katika nyimbo za *mdumange* ambazo huimbwa na wanawake pamoja na wanaume katika mandhari mamoja. Utafiti huu unafanywa ili kuona ni kwa namna gani mitindo ya utendaji inatambulisha nyimbo za *mdumange* kama utanzu mahsusi wa fasihi simulizi ya Wasambaa. Pia, utafiti huu unaangazia

dhima ya mitindo husika katika kuwawezesha wanajamii kujenga na kuwasilisha diskosi za namna mbalimbali.

Isitoshe, utafiti wa Mvula umetusaidia kufahamu kuwa mitindo mbalimbai ya utendaji kama vile tanakali za sauti husaidia kujenga taswira zenye hisia mwafaka kwa hadhira. Aidha, utendaji wa nyimbo hizo husaidia kuondoa uchovu katika kazi na huchochea wanawake kufanya kazi kwa bidii. Hii inaonyesha kuwa kuna uhusiano mkubwa baina ya fasihi na nyanja nyingine za kimaisha kama vile uchumi, malezi na mapenzi. Ingawa nyimbo za *mdumange* haziimbwi wakati wa kutwanga mahindi wala kazi nyingine yoyote, chukulizi ya mtafiti ni kuwa diskosi zinazojengwa kupitia nyimbo za *mdumange* zinachochea hamasa ya uzalishaji mali, umiliki raslimali, na malezi pamoja na mapenzi. Kwa hiyo, utafiti huu umefanywa ili kujadili na kutathmini muumano uliopo baina ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* na maisha ya kila siku miongoni mwa Wasambaa, wanaume kwa wanawake.

Mulokozi (2002) alichunguza ushairi simulizi wa jamii ya Wahaya kutoka Tanzania kwa kujikita katika ushairi uliosimulia visa na matendo ya mashujaa wa jamii hiyo (tendi). Baadhi ya vipengele vilivyoshughulikiwa na Mulokozi ni pamoja na sifa za utokeaji na uwasilishaji wa tendi simulizi, dhima ya tendi hizo pamoja na nafasi ya utamaduni katika kuvyaza na kuathiri ujumi wa kifasihi. Kadhalika, Mulokozi alikusudia kuonyesha nduni bainifu zinazojenga utanzu wa tendi simulizi katika jamii ya Wahaya, Tanzania.

Ili kuyafikia malengo yake, Mulokozi aliongozwa na Nadharia ya Mukstadha wa Utendaji. Aidha, Mulokozi anaanza kwa kuonyesha udhaifu wa mikabala ya kiNadharia iliyotumiwa na wataalamu waliowahi kuchunguza tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Kiafrika. Kwa mujibu wa Mulokozi (2002) tafiti za awali

zilizofanywa na wataalamu kama vile Finnegan (1992 & 2015) zilishindwa kufafanua vyema misingi ya ujumi wa fasihi simulizi ya Kiafrika kwa kuwa zilipuuza umuhimu wa muktadha wa utendaji. Kutokana na kupuuza suala la muktadha wa utendaji katika fasihi simulizi ya Kiafrika, tafiti hizo ziliishia katika kutoa mahitimisho finyu na potofu.

Kwa mfano, kulingana na Mulokozi tatizo lililomfanya Finnegan (1970) ahitimishe kuwa Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara hakuna tendi ni kuwa alitumia vigezo vya Nadharia ya Ki-Aristotle kujadili fasihi ya Kiafrika. Mulokozi anasema kuwa Afrika ni bara lenye utamaduni wake mahsusi unaotofautiana na utamaduni wa jamii za Kimagharibi. Kwa misingi hiyo basi, hata fasihi yake haipaswi kuhakikiwa kwa misingi ya ujumi wa fasihi andishi ya Kimagharibi, badala yake fasihi hiyo inapaswa kuhakikiwa kwa kutumia misingi inayotokana na ujumi wa Kiafrika.

Kulingana na Mulokozi misingi ya ujumi wa fasihi simulizi ya Kiafrika imejumuisha utendaji hai, hadhira shiriki, na kuwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo. Kutokana na mawazo ya Mulokozi, ni dhahiri kuwa nyimbo pamoja na tanzu nyingine za fasihi simulizi ya Kiafrika zinahitaji kuchanganuliwa kwa kutumia misingi ya kiNadharia itokanayo na ujumi wa jamii husika. Katika utafiti huu, tumefaidika kutokana na mawazo ya Mulokozi kwa kuwa mbali na kutumia Nadharia ya Semiotiki vilevile tumetumia Nadharia ya Utendaji kujadili muktadha na mitindo ya utendaji katika nyimbo za *mdumange*.

Kwa upande mwingine, Mulokozi amefanikiwa kuonyesha udhaifu wa Nadharia zisizoongozwa na misingi ya utendaji wa fasihi simulizi. Mulokozi anaelezea kuwa ili watafiti wafanikiwe kupambanua vyema ujumi wa fasihi simulizi ya Kiafrika hawana budi kufahamu kuwa utendaji ndio uti wa mgongo wa fasihi hiyo. Ni kutokana na

msingi huu ambapo utafiti huu umefanywa ili kuchunguza utendaji wa nyimbo za mdumange.

Kwa mujibu wa Mulokozi, utanzu wowote wa fasihi simulizi ya Kiafrika unafaa uchukuliwe kama sanaa inayotendwa katika muktadha mahsusi wa kijamii unaojumuisha fanani, hadhira, tukio au shughuli ya kijamii. Kwa hivyo, nduni za kifani na kimaudhui za utanzu huo zafaa zitazamwe kulingana na mahitaji ya muktadha wake wa utendaji. Utafiti huu wa Mulokozi umetufaa kwa kuwa umetujaza misingi ya utendaji wa ushairi simulizi (tendi) na nafasi ya muktadha katika utendaji wa ushairi huo.

Kutokana na kazi ya Mulokozi, tumepata kufahamu baadhi ya mitindo ya utendaji inayotumiwa na wasanii wa tendi simulizi kama vile matumizi ya ala za muziki, sauti mbalimbali za usimulizi pamoja na matumizi ya fomula simulizi. Mulokozi anashadidia kuwa tendi simulizi za jamii ya Wahaya zinatumia fomula simulizi pamoja na sauti za usimulizi kuchochea ushiriki wa hadhira, kujenga maudhui na kujenga taharuki. Katika utafiti wetu, tumetumia Nadharia iliyopendekezwa na Mulokozi ili kuchunguza namna utendaji katika nyimbo za *mdumange* unafanyika kimuktadha.

Tofauti na Mulokozi, utafiti wetu unachunguza jamii ya Wasambaa. Vilevile, Mulokozi alimakinikia tendi, ilhali katika utafiti wetu tunashughulikia nyimbo za ngoma. Licha ya tofauti hizi, tunadhukuru kuwa, kwa vile nyimbo za ngoma na tendi simulizi zote ni tanzu za ushairi simulizi kuna baadhi ya vipengele vya utendaji vitakuwa vinafanana baina ya tanzu hizi. Kwa kuchunguza nyimbo za ngoma tunadhamiria kuonyesha upekee wa utendaji wa nyimbo husika ikilinganishwa na utendaji wa tendi simulizi za Kiafrika. Kadhalika, utafiti wa Mulokozi ulimakinikia

suala la diskosi za jamii ya Wahaya kwa kiwango kidogo sana. Katika utafiti wetu, suala la utendaji limehusishwa na namna diskosi za jamii ya Wasambaa zinajengwa na mabadiliko yanayotokea baina ya muktadha mmoja hadi mwingine hususan katika miktadha ya siasa, harusi, na sikukuu za dini.

Tsiu (2008) alichunguza hali ya utendaji wa ushairi simulizi wa jamii ya Walesotho katika Karne ya ishirini na moja. Utafiti wa Tsiu ulimakinikia aina tatu za ushairi simulizi kwa pamoja. Aina hizo ni majigambo (dithoko), nyimbo za wachimba madini (difela), na nyimbo za mbari au koo (diboko). Kwa ujumla, Tsiu aliongozwa na Nadharia ya Fasihi Linganishi kwa kuwa alilinganisha utendaji wa aina mahsusi za ushairi simulizi katika mihula anuai ya kihistoria.

Tsiu aligundua kuwa aina hizi za mashairi zimebadilika sana katika mitindo ya utendaji, muktadha na dhamira zake. Anaendelea kwa kusema kuwa, hapo zamani aina zote tatu za mashairi simulizi zilitongolewa kwenye muktadha halisi ilhali katika kipindi cha mwanzo wa Karne ya ishirini na moja utendaji wa nyimbo hizi ulifanyika nje ya muktadha halisi hususan katika sherehe au matamasha maalum ya kijamii.

Mabadiliko pia yameonekana katika dhamira na hisia za fanani wakati wa uwasilishaji mashairi husika. Katika Karne ya ishirini na moja, watendaji hawakuwa na hisia kali za hasira au furaha, hawakuvaa mavazi maalum na hawakuwasifu mashujaa wa vita bali walijisifu wenyewe na pia waliwasifu viongozi wao wa kijadi. Hata hivyo, Tsiu anakubali kuwa kasi ya mabadiliko inatofautiana kutoka utanzu mmoja hadi mwingine. Kwa mfano, kidhamira utanzu wa diboko bado ulikuwa unajadili historia ya jamii kwa kuhifadhi majina ya wahenga, majina ya koo, na matambiko yahasuyo kuasisiwa kwa mbari mbalimbali za jamii ya Walesotho.



Utafiti wa Tsiu ni muafaka sana katika kazi yetu kwa kuwa mbali na kutuwezesha kujadili na kufahamu dhima ya ushairi simulizi katika jamii, pia kazi yake imetufahamisha tabia ya mabadiliko katika ushairi simulizi. Kadhalika, utafiti wake umetambulisha kuwa kwa kawaida tanzu za fasihi simulizi huingiliana sana. Hali ya kuingiliana kwa tanzu za ushairi simulizi imejitokeza katika utendaji wa ushairi simulizi wa Wasotho ambapo tumeelezwa kuwa waimbaji wa nyimbo za difela walitongoa sanaa yao kwa kutumia vipashio mbalimbali vya nyimbo za majigambo na mashairi ya mbari.

Kadhalika, utafiti wa Tsiu umetufaa sana kwa kuwa umetufahamisha kuhusu vipengele vya utendaji wa mashairi simulizi ya Walesotho. Vipengele hivyo ni pamoja na sauti, lugha ishara, ujumbe pamoja na ala au vifaa vya kimuziki. Aidha, pamoja na kuchunguza vipengele hivi, Tsiu amesisitiza kuwa ni muhimu kujadili namna hadhira na fanani wanashirikiana katika kuukamilisha utendaji wao. Utafiti huu umefanywa ili kujadili hali ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* miongoni mwa Wasambaa kwa kuzingatia muktadha wa utendaji. Kadhalika, utafiti huu unahoji na kuhakiki madai ya Tsiu kuwa katika fasihi simulizi muktadha na dhamira hukumbwa na mabadiliko makubwa kwa haraka zaidi kuliko mitindo ya utendaji.

Aidha, pamoja na hoja nzuri za Tsiu kuhusu dhima ya mitindo ya utendaji katika ushairi simulizi wa jamii ya Walesotho, utafiti wake ni tofauti na utafiti wetu kwa kuwa tafiti hizi zimefanyika katika miktadha tofauti kijiografia na kiwakati. Utafiti wa Tsiu ulifanyikia katika jamii ya Walesotho miaka takriban kumi iliyopita ilhali utafiti huu unahusu jamii ya Wasambaa na umefanyika hivi karibuni zaidi. Vilevile, Tsiu alishughulikia ushairi wa majigambo, mbari, na wa wachimba madini ilhali katika utafiti huu tumechunguza utendaji katika mashairi simulizi ya nyimbo zinazoimbwa kwenye ngoma na sherehe za Wasambaa.

Kutokana na ukweli kuwa muktadha alioutumia Tsiu ulitokana na jamii yenye viwanda na ukuaji wa miji, hata data zake zimeathiriwa sana na muktadha huo. Aina ya nyimbo alizochunguza pamoja na matokeo aliyoyapata yanaonyesha jinsi fasihi simulizi ilivyoathiriwa na fasihi andishi na teknolojia ya viwanda. Katika utafiti wetu tumechunguza nyimbo za jamii ya Wasambaa. Jamii hii bado haina viwanda na kutokana na hali hiyo chukulizi ya utafiti huu ni kwamba athari ya fasihi andishi ndani ya fasihi simulizi ya Wasambaa ni ndogo. Kwa hiyo, tumechunguza nyimbo za *mdumange* ili kuona ni kwa namna gani utendaji unafanyika na unatumika kutekeleza majukumu gani katika jamii isio na viwanda.

Vilevile, tafiti hizi mbili zilikuwa na malengo tofauti na ziliongozwa na misingi tofauti ya kiNadharia. Wakati Tsiu aliongozwa na misingi ya Nadharia ya Fasihi Linganishi, utafiti wetu umeongozwa na misingi ya Nadharia za Utendaji wa Maigizo na Semiotiki ya Kijamii. Kwa kutumia Nadharia hizi tumedadavua vyema utendaji wa nyimbo za ngoma ya *mdumange*, muktadha wake na dhima mbalimbali za mitindo ya utendaji.

Rajwayi (2009) alichunguza maudhui na mtindo katika nyimbo za msanii Faustin Munishi. Mtafiti huyu ameangazia suala la mabadiliko katika utendaji wa nyimbo za dini. Kulingana na utafiti huo kabla ya miaka ya sitini nchini Kenya na kwingineko Afrika nyimbo za dini hazikutumia ala za muziki bali zilitumia gita peke yake. Pia imeelezwa kuwa kimaudhui nyimbo hizo zilijihusisha na mahubiri ya dini peke yake. Ilichukuliwa kuwa ala nyingine za muziki kama vile ngoma zilifaa kutumika katika kunogesha utendaji wa nyimbo za kiulimwengu na sio za kiroho. Utafiti wa Rajwayi unabainisha kuwa kunako miaka ya sabini na tisini nyimbo hizo zilikumbwa na mabadiliko kadhaa. Miongoni mwa mabadiliko hayo ni kuingizwa kwa maudhui ya dhamira za kiulimwengu na matumizi ya ngoma katika utendaji wake. Mtafiti huyu

amechunguza nyimbo za msanii Faustin Munishi kama kielelezo cha mabadiliko hayo.

Ingawa utafiti wa Rajwayi unaonyesha hali ya mabadiliko katika nyimbo za kidini kwa kuingiza maudhui ya kiulimwengu na kutumia ala za muziki katika uendaji wake ni dhahiri kuwa nyimbo hizo zilitendwa kwenye muktadha wa mahubiri. Tofauti na utafiti wa Rajwayi, utafiti huu unaagalia suala la utendaji kwenye nyimbo za *mdumange* ambazo hutendwa kwenye muktadha wa sherehe za kijamii, nje au kando na muktadha wa mahubiri. Aidha, utafiti huo umekuwa muhimu kwetu kwa kuwa umedokeza na kuthibitisha kuwa suala la mabadiliko katika fasihi haliepukiki na linaenda sambamba na hali halisi ya kijamii. Msimamo wa mtafiti huyu ni kuwa tofauti na ilivyokuwa zamani hivi sasa waimbaji wengi wa nyimbo za kidini wanachanganya maudhui ya kiroho na ya kiulimwengu. Hivyo hivyo katika utendaji wake, nyimbo hizo hutawaliwa na matumizi ya ala nyingine za kimuziki. Ili kuona ni kwa namna gani nyimbo za *mdumange* zimekumbwa na mabadiliko yanayozungumzwa na Rajwayi (2009), utafiti huu umejikita kwenye utendaji unaotokea katika sherehe mbalimbali zinazoambatana na nyimbo husika. Sherehe hizo ni pamoja na dini hususan dini ya Kikristo (ubarikio) na Kiislamu (idil fitri).

## **2.5 Kiunzi cha KiNadharia**

Kuna Nadharia mbalimbali zilizowahi kutumika katika kuchunguza udhihirikaji wa matendo ya wanadamu ndani na nje ya muktadha wa kifasihi. Baadhi ya Nadharia hizo ni Nadharia ya Fomula Simulizi, Uamali, Korasi, Utendaji na Semiotiki. Kama ilivyodokezwa katika sehemu iliyotangulia (2.5.3) madhumuni yetu katika utafiti huu yamechambuliwa kwa kutumia misingi ya Nadharia za Utendaji wa Maigizo pamoja na Semiotiki ya Kijamii. Aidha, misingi ya Nadharia hizi pamoja na matumizi yake

katika utafiti huu yamejadiliwa katika sehemu 2.6.1 na 2.6.2 mutawalia kama ifuatavyo.

### **2.5.1 Nadharia ya Utendaji wa Maigizo**

Waasisi wa Nadharia ya utendaji kama vile Bauman (1975), Foley (1995) na Schechner (2013) ambao wanashikilia kuwa wahakiki sharti wachunguze zaidi ya matini moja na kuhakiki utendaji unaoambatana na matini husika. Waasisi hawa wametambua na kupendekeza mihimili kadhaa inayosaidia na kutumika katika kuumba, kuwasilisha na kufasiri tajriba za wanadamu katika kazi ya kifasihi. Mihimili hiyo ni pamoja na imani kuwa uumbaji, uwasilishaji na upokezi wa fasihi simulizi unajengwa na:

- (i) Muundo wa tukio la kiutendaji kulingana na muktadha wa uwasilishaji.
- (ii) Utangamano wa fanani na hadhira wakati wa uwasilishaji wa fasihi.
- (iii) Mfanyiko wa kimawasiliano kulingana na kaida za utamaduni wa jamii inayochunguzwa.

Kwa mujibu wa Schechner (2013) utendaji ni tukio la aina yoyote ile linalowajumuisha hadhira pamoja na fanani wake kwa minajili ya kuigiza au kuonyesha tabia za wanadamu. Kutokana na maelezo yake, mipaka kati ya utendaji unaotokea katika kazi za kisanaa kwa upande mmoja na utendaji unaotokea katika shughuli za kila siku kwa upande mwingine ni wa kidhahania. Aidha, Matti (2009) anaona kuwa katika jamii za Kiafrika utendaji ulikuwa mojawapo ya kanuni za maisha ya kila siku.

Ingawa maelezo ya wataalamu hawa hayaelekei kutenganisha baina ya utendaji wa kifasihi na usio wa kifasihi madai yetu katika utafiti huu ni kuwa licha ya kuwako kwa uhusiano wa karibu baina ya aina hizi za utendaji, kila aina ya utendaji ina

kanuni zake na inajitegemea. Faida moja tunayoipata kutokana na maelezo ya wataalamu hawa ni kuwa aina zote za utendaji zina dhima yake kwa wanajamii. Aidha, kutokana na Alembi (2002) pamoja na Mulokozi (2002), uhakiki wa fasihi simulizi ya Kiafrika unapaswa kuzingatia namna fasihi hiyo inavyotendwa kwa kuwasilishwa mbele ya hadhira. Kwa ufupi, Mulokozi anaonelea kuwa msingi mkuu wa Nadharia ya Utendaji ni muktadha unaojumuisha fanani, hadhira, tukio na lugha.

Kwa upande mwingine, Alembi na Mulokozi, wanatoa mawazo kuwa utendaji ni uti wa mgongo wa fasihi simulizi. Ndani ya utendaji huo, fanani huanzisha mawasiliano na pia hadhira hushiriki moja kwa moja katika kukamilisha mawasiliano kwa njia za kuuliza, kuelekeza, kuimba, na kujibu maswali ya fanani. Kadhalika, fanani anaweza kuupa nguvu utendaji wake kwa kutumia sio tu lugha ya maneno ya mdomo, bali pia hata kwa kutumia mitindo ya viziada lugha kama vile ishara za uso, mikono, kichwa na sauti wakati wa kuwasilisha sanaa yake.

Utendaji ndio uti wa mgongo wa fasihi simulizi kwa kuwa hufanikisha uwasilishaji wa ujumbe na hivyo kuwezesha mawasiliano baina ya mwasilishaji na hadhira yake. Katika jamii nyingi za Kiafrika, utendaji ulijumuisha shughuli za kawaida za kila siku kama vile kuzaliwa kwa mtoto, kupewa jina mtoto, kuoja na kadhalika.

Kwa upande wake Okpewho (1992) anaona kuwa utendaji wa fasihi simulizi ya Kiafrika unapaswa kuzingatia sio tu maneno yanayotamkwa kwa kutumia lugha ya mdomo bali pia ujumbe unaowasilishwa kwa kutumia lugha ya ishara au viziada lugha. Hii ni mbinu ya mawasiliano inayotumia ishara za uso, mikono, uchezaji pamoja na sauti, hususan sauti za kimuziki. Mtaalamu huyu anasisitiza kuwa mbali na maneno ya mdomo, wasanii wa kifasihi simulizi hutumia mbinu mbadala katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa.

Katika kuchunguza utendaji wa nyimbo za *mdumange*, mawazo ya Okpewho yametumika kwa kiwango kikubwa. Mawazo haya yametumika katika kuchanganulia mikakati ya utendaji unaofanywa kwa kutumia lugha, muziki na uigizaji ndani ya nyimbo hizo. Hii ni kwa sababu uwasilishaji wa nyimbo za *mdumange* unahusisha pamoja na mambo mengine matumizi ya sauti na mapigo ya kimuziki kwa njia ya uimbaji na matumizi ya ala za muziki. Matumizi ya mbinu za uchezaji na uigizaji pia yamechunguzwa kwa kutumia kanuni na mhimili wa Nadharia ya Utendaji uliopendekezwa na Okpewho. Mbinu hizo hutumia mikakati anuai ya viziada lugha kama vile muziki na uigizaji. Utafiti huu umechunguza jinsi fanani wanavyowasilisha ujumbe kwa kutumia lugha mbinu mbalimbali za viziada lugha.

Mtazamo wa Okpewho (1992) kuhusu utendaji umetufaa kwa sababu viziada lugha huonyesha mambo yanayofanywa na viungo mbalimbali vya mwili wa mwanadamu. Mitindo hii pia ni muhimu sana hasa katika kufanikisha mawasiliano baina ya fanani na hadhira. Hakuna mawasiliano yoyote mwafaka yanayokosa matumizi ya viziada lugha kwani mawasiliano huhitaji matumizi ya ala ongezi ambazo huchuja mawasiliano. Mbinu za kiutendaji ambazo hutawaliwa na uzungumzaji wa fanani na hadhira katika nyimbo za *mdumange* miongoni mwa jamii ya Wasambaa hujumuisha uimbaji, ala za muziki, maleba, vigelegele, ishara-uso na uchezaji.

Kimsingi, matumizi ya viziada lugha huzifanya nyimbo zivutie na kuufanya utendaji wake uwe hai zaidi. Katika utafiti huu tumetumia Nadharia ya Utendaji ili kupambanulia miktadha ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* pamoja na matumizi ya lugha na viziada lugha katika kujenga ujumi wa nyimbo na diskosi ya Wasambaa. Aidha, wakati wa uchanganuzi wa data uchunguzi uliohusu matumizi ya viziada lugha ulijikita katika vipashio mahsusi vya kisanaa kama vile ishara za viungo vya mwili

(uso, mikono, miguu na kichwa), uchezaji dansi, maleba, ala za muziki pamoja na uigizaji.

Kwa ujumla, utafiti huu umetumia Nadharia ya Utendaji wa Maigizo kama ilivyopendekezwa na Bauman (1975). Kulingana na Kobia utendaji hauna budi kujumuisha pamoja dhana za muktadha, lugha, na maana. Akifafanua maana ya utendaji, Bauman (*Keshatajwa*) anasema kuwa utendaji ni mchakato unaotumia lugha katika kuwezesha mfanyiko wa mawasiliano (maana au ujumbe) baina ya fanani na hadhira kwenye muktadha mahsusi wa kijamii.

Kulingana na maoni Wanaisimu jamii (Austin, 1965: Hymes, 2007), nyenzo za kimawasiliano (lugha na viziada lugha), ujumbe na muktadha ni vijelezi muhimu vinavyojenga tukio la kiutendaji. Katika utafiti huu tumechunguza matumizi ya lugha ya kisanaa na kawaida kama mojawapo ya sifa pambanuzi za utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Hii ni kutokana na Bauman (*Keshatajwa*) alivyopendekeza kuwa utendaji hujumisha usemi kama kitendo katika muktadha mahsusi. Dhana ya usemi hapa imetumika kurejelea mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha kati ya fanani na hadhira katika kuumba maana au ujumbe.

Mihimili ya Nadharia ya Utendaji iliyoelezwa katika sehemu hii imetuwezesha kupambanua ujumi wa nyimbo za *mdumange* kulingana na mikakati yake ya kiutendaji. Mikakati hiyo imejumuisha muktadha, matumizi ya lugha na viziada lugha. Mihimili hii imetufaa sana kwa kuwa kwayo tumeweza kufasiri tajriba za Wasambaa kupitia utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Katika utafiti huu imebainika wazi jinsi mikakati mahsusi ya utendaji inatumiwa na fanani pamoja na hadhira katika kutongoa na kuwasilisha nyimbo zinazovutia na kuathiri jamii kwa kiwango kikubwa. Matumizi ya Nadharia hii yamethibitisha mtazamo wa Bauman (1975) kuwa kila

utendaji sharti uishawishi hadhira kuzingatia na kufuatilia tukio la kiutendaji kwa umakini mkubwa. Ni kwa njia hiyo tu ambapo mawasiliano baina ya fanani na hadhira (utendaji) hufanikiwa.

Katika kutumia Nadharia ya Utendaji wa Maigizo ndani ya utafiti huu, masuala anuai yamejadiliwa hususan namna uwasilishwaji wa nyimbo za *mdumange* unaambatana na vipashio mbalimbali vya kimaigizo. Miongoni mwa vipashio vya kimaigizo ambavyo vimedhihirika wakati wa kujadili utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni pamoja na:

- (i) Matumizi ya miundo mbalimbali ya jukwaa.
- (ii) Maleba au mavazi maalum ya kisanii.
- (iii) Matumizi ya ala au vifaa vya kiutamaduni kama vile mwengo, kofia ya usinga na kofia ya kishadda.
- (iv) Uimbaji kwa njia ya Upokezanaji zamu (dialogia).
- (v) Ushirikishwaji wa hadhira katika kuimba, kucheza na kushangilia.

Kwa ufupi, kutokana na misingi ya Nadharia hii, utafiti huu unatoa hoja kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* unashabihiana sana na utendaji wa sanaa za maonyesho za Kimagharibi (tamthiliya). Hata hivyo, kama itakavyoonyeshwa kwenye sura zijazo, ujumi wa nyimbo zilizochunguzwa ni wa kipekee mno hasa ikizingatiwa kuwa ujumi huo unategemea muktadha hai na utendaji wa ana kwa ana baina ya fanani na hadhira.

### **2.5.2 Nadharia ya Semiotiki ya Kijamii**

Licha ya kufaa kwa Nadharia ya Utendaji wa Maigizo, kuna wakati tulishindwa kutambua maana ya misimbo au ishara zilizowasilishwa katika nyimbo za *mdumange*.



Ili kuona ni kwa namna gani misimbo na ishara hizo zinahusiana na utendaji pamoja na maana au ujumbe tulitumia pia Nadharia ya Semiotiki ya Kijamii.

Semiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara au uashiriaji. Kihistoria, kuibuka kwa Nadharia ya Semiotiki kunahusishwa na mawazo ya Ferdinand de Saussure na Charles S. Peirce katika Karne ya 20 (Fenner 2010). Kwa mujibu wa de Saussure katika Fenner (2010) Semiotiki ni Nadharia inayochunguza uhusiano baina ya miundo ya ndani na miundo ya nje katika mifumo ya kijamii. Kulingana na Barthes (1964) Nadharia ya Semiotiki inaundwa na vitu vitatu: (i) kitajwa; (ii) ishara; na (iii) kirejelewa. Katika Nadharia ya Semiotiki, dhana hizi hufanya kazi kutokana na athari za ushirikiano wa ishara, kitajwa na kirejelewa. Kwa ujumla, Semiotiki inasaidia kuchanganua miundo ya mifumo anuai ya kijamii kama vile lugha, fasihi, siasa, na uchumi. Ili kuelewa vyema aina mahsusi ya mfumo wa kijamii tunapaswa kuchunguza namna umbo la ndani linahusiana na umbo la nje. Umbo la ndani hurejelea maana na umbo la nje hurejelea ishara au elementi ndogondogo zinazojenga mfumo husika.

Hata hivyo, mkabala wa de Saussure kuhusu Semiotiki una dosari kwa kuwa haujazingatia nafasi ya utendaji unaohusisha matendo ya wanadamu katika kusimba na kusimbua michakato ya kimawasiliano. Hali ilivyo ni kuwa, utendaji wa tanzu nyingi za fasihi simulizi ya Kiafrika, nyimbo za *mdumange* zikiwemo, matendo ya wanadamu yana nafasi kubwa sana na hivyo nafasi yao haiwezi kupuuzwa.

Wahakiki wa Kisemiotiki ambao mitazamo yao inakidhi haja na matakwa ya utendaji unaotokea katika fasihi simulizi ni pamoja na Barthes (1964) na Eco (1984). Kwa mujibu wa Eco ishara ni kila kitu kinachoweza kutumika kuwakilishia kitu kingine. Mtazamo huu unashabiana na wa Barthes (*Keshatajwa*) ambaye anafikiri kuwa ishara

ni dhana inayorejelea hali ya kukifanya kitu kimoja kusimama badala ya kitu kingine. Kwa mujibu wa Barthes (*Keshatajwa*), ishara za kisemiotiki zinaundwa na kitendwa (*object*) na kibainishi (*modifier*).

Mitazamo ya Eco na Barthes kuhusu Nadharia ya Semiotiki ina tija kubwa katika utafiti huu kwa kuwa muelekeo wake unaihusisha jamii. Aidha, maelezo ya wataalamu hawa yamezingatia hali halisi ya dhana ya udhihirikaji wa Semiotiki katika kazi za kifasihi. Kutokana na mtazamo huu, ishara sio lazima zitokane na misimbo ya kiisimu, bali zinaweza kuwa kitu chochote kinachotumika kupashia maana katika mchakato wa kimawasiliano. Hivyo, kuna utangamano mkubwa baina ya muktadha, maana na ishara. Tumechanganua utangamano huu kwa kuzingatia misimbo inayotokana na matumizi ya lugha, na viziada lugha. Kulingana na mhimili huu, kitu chochote kinaweza kuwa ishara ikiwa watu wa jamii fulani wata kifasiri kama kirejelea kinachosimama kwa niaba ya kitu kingine. Kwa ujumla, Nadharia hii inatufundisha namna ya kufahamu matumizi ya lugha na viziada lugha kwa kutumia utamaduni wa jamii mahsusni.

Kwa ujumla, katika utafiti huu tumeitumia mihimili ya Nadharia ya Semiotiki ya Kijamii kama iliyopendekezwa na mhakiki wa kifasihi, Roland Barthes. Kwa mujibu wa Barthes (1964) lengo la Nadharia hii ni kuchunguza uhusiano baina ya maana ya kazi ya kifasihi na vijenzi vya kimuundo vilivyozua maana hizo. Katika utafiti wetu, Nadharia ya Semiotiki imetumika ili kufafanua maana mbalimbali zinazowakilishwa na ishara zinazotumika katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Vilevile, Nadharia ya Semiotiki imetuwezesha kuchambua aina mbalimbali za misimbo inayopatikana katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* pamoja na dhima yake kwa jamii.

Kulingana na Barthes (*Keshatajwa*), misimbo ya Kisemiotiki inayojadiliwa katika kazi za kifasihi ina akisi muundo wa ndani wa fasihi husika. Kwa hiyo uhakiki wa Kisemiotiki unamhitaji mhakiki kuivunja kazi ya kifasihi katika sehemu zake ndogondogo (leksia). Kila leksia hudhihirisha misimbo na kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri kazi ya kifasihi. Aidha, kutokana na Barthes, uhakiki wa kifasihi unaoongozwa na Nadharia ya Semiotiki hauna budi kubainisha, kuchanganua na kufafanua misimbo mikuu ya Kisemiotiki inayojitokeza katika kazi ya kifasihi. Misimbo hiyo imejumuisha matukio, anwani, maneno ya lugha na utamaduni.

Aina ya kwanza ni msimbo wa matukio. Msimbo huu unahusu jinsi ishara zinazojengwa kutokana na mpangilio wa matukio au visa katika hadithi au simulizi fulani. Kwa kutumia msimbo huu mtunzi anajenga visa na matukio kwa njia ya ishara. Msimbo wa pili unajulikana kama msimbo wa kihemenitiki. Huu ni msimbo unaojengwa katika kazi ya kifasihi kupitia anwani ya kazi husika. Anwani hiyo inaweza kuwa jina la kitabu, shairi, igizo au jina la mhusika. Kutokana na anwani hiyo mtunzi hujenga taharuki akilini mwa hadhira. Aidha, kwa kutumia msimbo wa kihemenitiki tunaweza kufahamu maana na kusudio la mtunzi kwa kudadisi kile kinachorejelewa na mtunzi katika kazi yake ya fasihi.

Aina ya tatu ni msimbo wa kiseme. Huu ni msimbo ambao unajengwa kwa kutumia maneno yenye kutoa maana ya kisemantiki. Maana ya kisemantiki hupatikana kwa kurejelea vipengele nasibishi vya kiisimu kama vile nahau, methali na sitiari zinazotumika katika kazi ya kifasihi. Aina ya nne ni msimbo wa kiutamaduni. Msimbo huu unajengwa kutokana na matumizi ya viashiria vya utamaduni katika kazi ya kifasihi. Viashiria mbalimbali vya kiutamaduni vinavyotumika katika kazi ya kifasihi huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu vinavyoeleweka

miongoni mwa wasomaji au watazamaji, hivyo kuipa kazi ya kifasihi nguzo za kiutamaduni. Msomaji/mtazamaji anaposema anaelewa akisemacho mtunzi huwa anasema hivi kutokana na viashiria vya msimbo huu.

## **2.6 Hitimisho**

Katika sura hii tumepitia na kuhakiki maandishi yaliyohusiana na mada ya utafiti pamoja na kiunzi cha kiNadharia. Kutokana na mjadala uliopo kwenye sura hii, imeelezwa na kuthibitishwa kuwa ingawa wataalamu mbalimbali wamethubutu kuchunguza vipera anuai vya sanaa jadiya ya Kiafrika, hakuna utafiti wa kina uliofanywa kuhusu utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Vilevile, misingi ya kiNadharia iliyojadiliwa imetumika katika mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti kwenye sura ya tatu, nne, na tano. Katika sura ifuatayo, tumejikusisha na mjadala wa matokeo ya utafiti kwa kuangazia utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika miktadha anuai ya Wasambaa.

## SURA YA TATU

### UTENDAJI WA NYIMBO ZA *MDUMANGE* KATIKA MIKTADHA ANUWAI YA JAMII YA WASAMBAA

#### 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tunakusudia kuwasilisha data kuhusu miktadha ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* tangu katika jamii ya Wasambaa. Aidha, data zinazowasilishwa katika sehemu hii zimemsaidia mtafiti kujibu swali la kwanza la utafiti huu lililouliza kuwa ‘Je, ni miktadha gani ya kijamii imechochea kuibuka na kustawi kwa utendaji wa nyimbo za *mdumange*?’ Katika kulijibu swali hili, maoni ya Wasambaa kuhusu historia ya nyimbo za *mdumange* yalikusanywa kwa njia ya usaili na mijadala ya vikundi. Vilevile, nyimbo za *mdumange* zilizojadili masuala mahsusi ya kihistoria zimechambuliwa.

Kwa ufupi, utafiti huu umebaini kuwa kuna mitazamo mikuu mitatu inayoelezea dhima ya miktadha katika kuchochea kuibuka na kustawi kwa nyimbo za *mdumange*. Mtazamo wa kwanza unadai kuwa nyimbo za *mdumange* zimechimbuka zamani (kabla ya miaka ya sitini) kutokana na turathi simulizi za Wasambaa. Mtazamo wa pili unadai kuwa nyimbo za *mdumange* zimechimbuka hivi karibuni (miaka ya sitini) kutokana na mtagusano baina ya Wasambaa na Wanyamwezi. Aidha, mtazamo wa tatu unadai kuwa nyimbo za *mdumange* zimetokana na matukio ya sherehe za Wasambaa hususan harusi, dini na hafla za kisiasa. Hoja za mitazamo hii zimewasilishwa kwa kina katika sehemu ifuatayo:

#### 3.1 Turathi Simulizi za Wasambaa

Mtazamo huu unadai kuwa nyimbo za *mdumange* zimetokana na fasihi simulizi ya Wasambaa. Aidha, kati ya watafitiwa ishirini na wane (24) waliohojiwa watafitiwa

kumi na watatu (13) sawa na asilimia hamsini na nne nukta moja (54.1%) waliunga mkono hoja hii. Wanaounga mkono hoja hii wanaeleza kuwa kabla nyimbo za *mdumange* hazijaanza, jamii ya Wasambaa walijihusisha na aina mbalimbali za fasihi simulizi hususan *spein*, *bazaa*, na *beni*. Kwa mfano Mzee Shauri alipohojiwa kuhusu chimbuko la nyimbo za *mdumange* alisema:

Hapo mwanzo *mdumange* uliitwa “Spein”, lakini baadaye mimi nilipoanza kujihusisha na sanaa hii watu waliibatiza jina la ‘*mdumange*’, siku zilivyozidi kusonga jina la Spein lilisahaulika na likashamiri jina la *mdumange*. Ukiwa peke yako huwezi kufanya *mdumange*, hata kama wewe utaimba vizuri, unahitaji kundi la watu watakaokusaidia kupiga ngoma, kucheza, kuitikia na kushangilia...

Katika nukuu hii, Mzee Shauri anabainisha kuwa nyimbo za *mdumange* zilitendwa katika sikukuu za mwaka mpya na Krismasii. Kwa mujibu wa Nadharia ya Utendaji wa Maigizo, muktadha una nafasi kubwa ya kutujuza asili na historia ya kuibuka kwa dhana inayochunguzwa (De Vet, 1996; 2008 na Rappaport, 1968). Ni kutokana na msingi huu ambapo nukuu hapo juu inaonyesha kuwa nyimbo za *mdumange* zimechimbuka kutokana na ujumi wa fasihi simulizi iliyojulikana kama ‘spein’. Mzee Shauri anaongeza kwa kusema kuwa zamani nyimbo za *mdumange* ziliitwa ‘spein’ lakini kufikia mwaka 1960 zilibadilishwa na kuitwa ‘*mdumange*’. Kulingana na maoni ya watafitiwa, *spein* ilikuwa na nyimbo chache, wachezaji wachache na haikuwa na mvuto kama ilivyokuwa *mdumange*. Awali, wasanii wa nyimbo za *mdumange* walitumia nyimbo za *spein* ili kunogesha utendaji wao, lakini baadaye walitunga nyimbo mpya. Miongoni mwa nyimbo za *spein* zilizotumiwa na wasanii wa nyimbo za *mdumange* ni **n’tajenga nyumba yangu ya bati, n’teona smol na dada Amina.**

Kimsingi, maelezo ya Mzee Shauri yanaonyesha kuwa nyimbo za *mdumange* zimetokana na uigizaji wa mitindo ya utendaji wa fasihi simulizi ya Wasambaa iliyokuwako kabla, fasihi hiyo iliitwa *spein*.

Kimuundo neno *spein* limekiuka kanuni za uundaji wa maneno ya Kibantu unaofuata mpangilio wa konzonanti na Irabu (KI) katika silabi zake (Kihore, 2002). Hali hii inadokeza kuwa nyimbo za *mdumange* hazikutokana na utamaduni wa Wasambaa, bali zilitokana na utamaduni wa kigeni, hususan wakoloni walioleta Kingereza chenye muundo wa Konzonanti, Konzonanti, Irabu (KKI) badala ya Konzonanti, Irabu , Konzonanti, Irabu (KIKI).

Mbali na nyimbo za *spein*, turathi nyingine za kijamii zilizochochea kuibuka kwa nyimbo za *mdumange* ni ibada au dini za asili, hususan matambiko ya mizimu. Kulingana na usaili pamoja na mahojiano yaliyofanyika kati ya mtafiti na Wasambaa wa Lushoto, imebainika kuwa *mdumange* ni sanaa ya kale mno iliyohusishwa na wahenga (mizimu) wa jamii ya Kisambaa. Katika kushadidia hoja hii, Mwajuma Samakafi kutoka kijiji cha Ngua/Mbuzii anafafanua kwa kusema:

Nijuavyo mimi, *mdumange* ni ngoma ya utamaduni wa Wasambaa iliyoasisiwa na wahenga kama vile Sheuta, Mbegha na Kimweri. Ngoma hii inahusisha sherehe za kuomba na kutoa sadaka kwa mizimu.

Maelezo yaliyotolewa na mtafitiwa hapo juu yanashabihiana na yaliyotolewa na Mzee Shauri kwa kuwa yote yanaonyesha kuwa *mdumange* ni sanaa ya kale iliyochimbuka zamani sana kutokana na utamaduni wa Wasambaa. Ingawa mtazamo huu uliungwa mkono na idadi kubwa ya watafitiwa, utafiti huu unatoa hoja kuwa si rahisi kuthibitika kisayansi ikiwa nyimbo za *mdumange* zilitokana na fasihi ya *spein* au la. Kama ilivyodokezwa hapo awali, muundo wa silabi za aina ya fasihi inayodaiwa

kuwa ya zamani zaidi kuliko *mdumange* (spein) unahitalifiana na muundo wa silabi za Kisambaa na lugha nyingine za Kibantu. Kutofautiana huku kunatufanya tutoe hoja kuwa hoja mtazamo kuwa nyimbo za *mdumange* zimetokana na spein unahitaji data na ushahidi wa kutosha, hivyo tafiti zaidi zifanyike.

Aidha, hoja kuwa nyimbo za *mdumange* zimetokana na turathi simulizi za Wasambaa inabainika pia kupitia mitindo ya kuanza na kuhitimisha utendaji inayotumiwa na wasanii wa nyimbo husika. Baadhi ya wasanii huanza utendaji wao kwa fomula maalum za sala au maombi. Ingawa kuna baadhi ya nyimbo zilizoimbwa kwa kutumia fomula za maombi ya sala za dini ya Kiislamu na Kikristo, kuwoko kwa sala au maombi yaliyojengwa kwenye msingi wa dini za kijadi (ibada ya mizimu) ni ushahidi kuwa kwa kiwango kikubwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* umeathiriwa na itikadi ya jamii kuhusu uwepo wa wahenga na mizimu. Katika nukuu ifuatayo, suala la fomula ya sala au maombi linabainika waziwazi:

### **Mf. 3.1: Wimbo Unaoonyesha Fomula ya Maombi kwa Mizimu**

#### **KISAMBAA**

**MK:** Tamba, tamba, tiase nkoba tiase muungu  
mzimu wa Sheuta neugone ntongo  
**WK:** Tambaa, tiase nkoba tiase muungu  
**MK:** Mzimu ee kagone ee  
**WK:** Eeeee  
**MK:** Uja wa Sheuta neugone ntongo  
**WK:** Tambaa, tiase nkoba tiase muungu  
**MK:** Mzimu ee kagone  
**WK:** Eeeee

#### **KISWAHILI**

**MK:** Tunaomba tukiamini imani ya  
tunguli na miungu mzimu wa  
Sheuta ulale salama  
**WK:** Tunaomba tukiamini tunguli  
na miungu  
**MK:** Mzimu ee ulale ee  
**WK:** Eee ee ee  
**MK:** Wa Sheuta ulale salama  
**WK:** tunaomba tukiamini tunguli na  
miungu  
**MK:** Mzimu ee ulale  
**WK:** Eeeee

Katika nuku hapo juu tunaona jinsi wasanii wa nyimbo za *mdumange* wanavyoamini katika mizimu na wahenga. Aidha, wimbo huu huimbwa wakati wa kuanza utendaji wa nyimbo kwenye hafla za harusi na kisiasa. Heshima kwa mizimu inadhihirika sio



tu kupitia maudhui ya wimbo bali pia kupitia mitindo ya uchezaji. Wakati wa kuimba wimbo huu, badala ya kusimama, wasanii huchuchumaa (taz. Kielelezo hapa chini):



### **Kielelezo na 3.1 : Wasanii wakiwa wamechuchumaa wakati wa kuimba**

Kama inavyoonekana katika kielelezo na. 2 hapo juu, wakati wa kuimba wimbo wa **tamba** wasanii hawasimami wala hawatembeitembei kama ilivyo kwa aina nyingine za nyimbo. Badala yake wanachuchumaa na wakati huo hata ngoma pamoja na ala nyingine za kimuziki hazitumiki. Hii inaashiria kuwa dhamira za wimbo ni ya kipekee zaidi hasa kwa kuwa inatukuza na kuwasilisha maombi kwa wahenga na mizimu. Kwa mujibu wa Nadharia ya Utendaji wa Maigizo (Schechner, 2013), viziada lugha vina nafasi kubwa katika kusaidia kujenga dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa. Kitendo cha waimbaji kukaa chini na kuimba huku wakiwa wametulia ni ishara ya heshima na utii kwa wahenga na mizimu na hivyo ni imani yao kuwa maombi yao yatasikilizwa na kujibiwa.

Vilevile, Wasambaa wanaamini kuwa nyimbo za *mdumange* zimetokana na turathi simulizi za Wasambaa kwa kuwa nyimbo hizo zimesheheni maudhui yanayohusu miviga ya kijadi. Miviga hiyo huhusisha sherehe za kijadi wanazofanyiwa watu walio hai kama vile sherehe ya kuzaliwa mtoto, harusi, na kutawazwa kiongozi. Miongoni mwa nyimbo za *mdumange* zilizosheheni maudhui yanayohusu umuhimu wa miviga ya Wasambaa ni wimbo wa **wenyeji wetu**. Katika nukuu hapa chini mambo haya yamewasilishwa na kusesitizwa kwenye ubeti wa nne:

**Mf. 3.2: Wimbo Unaoonyesha Miviga ya Gao na Nkimbizi**

**KISAMBAA**

24. **E oo e mkae wetu**
25. Mkae wetu ishwi ni Sheuta
26. Na Sheuta yakwe ni miviga
27. Kuna Gao na Nkimbizi
28. Na ndio miviga mikuu
29. Mlezi ni kulea wana
30. Ivi ushe vyoshe hakuna (IV)

**KISWAHILI**

24. **E ooe mhenga wetu**
25. Mhenga wetu sisi ni Sheuta
26. Na Sheuta anataka Miviga
27. Kuna mviga wa Gao na Nkimbizi
28. Hii ndio miviga mikuu
29. Iliyokuwa inatumika kulelea watoto
30. Leo hakuna mvigha wowote (IV)

Katika nukuu ya wimbo hapo juu, utendaji wa nyimbo za *mdumange* umetumika kuwasilishia ujumbe kuhusu wahenga wa Kisambaa na mifano ya miviga inayofaa kufanywa kwa watoto wa kiume na wa kike. Kadhalika, Sheuta ametajwa kama mwasisi wa jadi ya Wasambaa ikiwemo miviga ya *gao* na *nkimbizi*. Kulingana na ufafanuzi uliotolewa na Mama Mjai (kutoka kijiji cha Mlalo) wakati wa mahojiano kati yake na mtafiti, *gao* ni sherehe wanazofanyiwa watoto wa kiume ilhali *nkimbizi* ni sherehe wanazofanyiwa vijana wa kike.

Kutokana na kushamiri kwa vipengele mbalimbali vya matambiko ya kijadi katika nyimbo za *mdumange* utafiti huu unatoa hoja kuwa nyimbo za *mdumange* zimechimbuka katika muktadha wa ibada za kijadi kwa minajili ya kuwaunganisha wanajamii. Aidha, ili kutekeleza jukumu hili wasanii wa nyimbo za *mdumange* huziunda nyimbo zao kisanaa. Suala hili linaafikiana na maoni yaliyotolewa na wana

Nadharia ya utendaji wa Maigizo kuwa dhima kubwa ya matambiko ni kujenga uzalendo, umoja na mshikamano katika jamii (Malinowski, 1935; Gennep, 1960; Mackie, 2004; Rappaport, 1968; na Geertz, 1973).

Jambo lingine lililochochea kuibuka na kustawi kwa nyimbo za *mdumange* ni utamaduni wa Wasambaa hususan masuala ya uganga na uchawi. Watafitiwa waliohojiwa wanatoa maoni kuwa watu wengi wanaojihusisha na *mdumange* kama wasanii (waimbaji au wapiga ngoma) wana uhusiano wa namna fulani na ama uganga wa kijadi au matambiko ya kijadi. Watu hao hutokea katika familia zenye uganga au katika familia zinazohusika na uongozi wa kijadi (machifu). Mukstadha huu ulichochea kuibuka na kustawi kwa nyimbo za *mdumange* kwa namna kuu mbili ambazo ni ujuzi wa kutengeneza vifaa vya kimuziki na udhihirishwaji wa uganga kama mojawapo ya dhamira muhimu katika nyimbo za *mdumange*.

Kitendo cha kuzaliwa na kukulia katika mukstadha wa jamii zenye fani ya uganga au uongozi kiliwapatia wasanii fursa ya kujifunza kutongoa nyimbo za namna mbalimbali. Wakati wa kutenda na kuwasilisha nyimbo za *mdumange*, miundo michache tu ndiyo ilibadilishwa ili kukidhi mahitaji ya mukstadha mpya. Pia mukstadha huu uliwawezesha wasanii kujua namna ya kutengeneza na kupiga ngoma na vifaa vingine vya kimuziki. Kama itakavyoonyeshwa katika sura ya tano, ngoma na vifaa vingine vya kimuziki vinavyotumika katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* zinashabihiana na ngoma zinazotumika katika shughuli za uganga au tiba asilia, hususan *pungwa*.

Pia mukstadha wa turathi simulizi za Wasambaa umeathiri utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwa kuwa baadhi ya wasanii ambao pia walikuwa waganga wamelitumia jukwaa la utendaji wa nyimbo za *mdumange* kujitangaza, kujisifia na kuwabeza

waganga wengine. Miongoni mwa nyimbo za *mdumange* zenye maudhui yanayoelezea dhamira za majigambo ya uganga na uchawi ni wimbo wa **wajinaki bure** ulioimbwa na Shauri wakati wa mahojiano kati yake na mtafiti tarehe 18/12/2015. Katika wimbo huu msanii anasema:

**Mf. 3.3: Wimbo Unaoonyesha Majigambo ya Uganga na Uchawi**

1. Wajinaki bure na uganga
2. Umganga gani usio na jina
3. Kama wewe ni mganga
4. Mloge Shauri akifa nikupe zawadi

Kulingana na nukuu ya wimbo huu, dhamira za majigambo ya uganga na uchawi zinabainika waziwazi. Aidha, dhamira hii iliwasilishwa kwa namna mahsusii ya utendaji uliowawezesha wasanii kujadili tajriba za wasanii na mafanikio yao dhidi ya makundi mengine. Hivyo, kupitia nukuu hii na pia kutokana na maelezo yaliyotolewa na mtafitiwa ni dhahiri kuwa muktadha wa utendaji wa nyimbo za *mdumange* ulifungamana na mashindano ya Wasambaa kuhusu uganga na uchawi. Mzee Shauri anazidi kufafanua kuwa **wajinaki bure** ni miongoni mwa nyimbo za *mdumange* zilizoimbwa zamani kabla ya miaka ya sitini (1960). Katika wimbo huu, msanii anaonyesha jinsi dhamira ya uganga na uchawi ilivyochochea majigambo ya *mdumange*. Kadhaika, neno “uganga” katika wimbo huu limetumika kama msimbo wa kihemenitiki ambao kulingana na Barthes (1964) fanani anapokutana nalo anajenga taswira kuhusu dhima ya uganga na athari yake katika maisha ya Wasambaa.

Kwa ujumla, kulingana na mjadala huu imebainika kuwa kwa kiwango kikubwa Wasambaa wanaamini kuwa nyimbo za *mdumange* zimetokana na muktadha wa turathi simulizi. Pamoja na maelezo haya, utafiti huu unatoa hoja kuwa licha ya

mchango mkubwa wa turathi simulizi ni muhimu pia kuzingatia mchango wa miktadha mingine katika nyimbo za *mdumange*, hususani mtagusano wa kijamii.

### 3.2 Mtagusano wa Kijamii

Mtazamo wa pili unadai kuwa nyimbo za *mdumange* zimechimbuka kipindi cha ukoloni kutokana na fasihi simulizi ya Wanyamwezi iliyoitwa ‘hiari ya moyo’. Aidha, kati ya watafitiwa ishirini na wanne (24) waliohojiwa, watafitiwa saba (7) sawa na asilimia ishirini na tisa nukta mbili (29.2%) waliunga mkono hoja hii. Kimsingi, kundi hili la Wasambaa linaamini kuwa nyimbo za *mdumange* zimeanza kutokana na mtagusano baina ya Wasambaa na Wanyamwezi katika kipindi cha mkoloni, hususan kipindi cha kati ya 1884 – 1959, yaani kabla ya uhuru. Kwa mfano katika mahojiano kati ya mtafiti mmoja wa watafitiwa (Hondo Bakari) kutoka kijiji cha Kihitu maoni yafuatayo kuhusu chimbuko la nyimbo za *mdumange* yalitolewa:

Hapo mwanzo nyimbo za *mdumange* ziliitwa hiari ya moyo. Hii ni sanaa iliyoletwa Lushoto na Wanyamwezi kutoka Tabora wakati wa kufanya kazi kwenye mashamba ya katani.

Maelezo yanayotolewa na mtafitiwa hapo juu, yanaelekea kusesitiza kuwa nyimbo za *mdumange* zimechimbuka kutokana na mtagusano wa kijamii baina ya wenyeji (Wasambaa) na wageni (Wanyamwezi). Aidha, hoja hii pia inaungwa mkono na Mayai Omari kutoka Kijiji cha Kivilicha ambaye anasema:

kuingia kwa wageni katika Wilaya ya Lushoto kunahusishwa zaidi na harakati za kikoloni hususan kuanzishwa kwa kilimo cha chai na katani ambacho kilihitaji vibarua kutoka maeneo mengi ndani na nje ya mkoa wa Tanga. Wanyamwezi, Wazaramo, Wagogo na watu wengine wa bara walikuja Lushoto ili washiriki kama vibarua kwenye mashamba ya chai na katani.

Katika msingi huu, Wanyamwezi walikuja Lushoto ili washiriki katika shughuli za uzalishaji mali kwenye mashamba ya chai na katani. Vibarua hao walijulikana kama ‘manamba’.

Jina lingine linalohusishwa na nyimbo za *mdumange* ni “gongwe” ambayo ni sauti iliyopatikana kutokana na uigizaji wa ngoma iliyotumika wakati huo. Kulingana na maoni ya Zuberi Dhahabu (wakati wa mahojiano):

ngoma ya asili ya Wasambaa iliitwa *gongwe* kutokana na mlio wa sauti iliyotolewa na ngoma hiyo. Jina hili lilitumika kuiwakilisha ngoma ya asili ya Wasambaa wa Lushoto.

Kutokana na nukuu hii, *gongwe* ndilo jina la asili la *mdumange*. Jina hili lilitumika zamani sana na kwa muda mrefu kabla ya kuanza kwa *hiari ya moyo* (miaka kabla ya 1960) na *mdumange* (katika miaka ya 1960).

Hivyo, nyimbo za *mdumange* zilichimbuka kutokana na fasihi simulizi ya Wasambaa pamoja na ya makabila mengine kama vile Wanyamwezi. Aidha, aina mbalimbali za majina zinaonyesha kuwa tangu kale nyimbo hizi zimekuwa zinabadilika kifani na kimaudhui. Ingawa nyimbo zote zilihusishwa na matumizi ya ngoma, aina ya nyimbo na ufundi wa kuimba umekuwa unabadilikabadilika kutoka zama hadi zama. Kadhalika, kitendo cha kutajwa kabila la Wanyamwezi na maelezo kuwa wao ndio walioleta nyimbo za *mdumange* kinahitaji kuchunguzwa na kudadisiwa zaidi. Jambo hili linazua maswali mengi yasiokuwa na majawabu. Kwa mfano, je, ni kweli kuwa kabla ya kuja Wanyamwezi jamii ya Wasambaa haikuwa na sanaa zao za kifasihi simulizi. Jambo lililo wazi ni kuwa pamoja na fasihi simulizi ya Wasambaa, kulikuwa wageni wenye tabia na utamaduni wao wa ngoma iliyoitwa *hiari ya moyo*. Hali hii ilifanya kuwe na aina nyingi za ngoma na fasihi simulizi ndani ya jamii moja. Kulikuwa na fasihi za wenyeji (*mdumange*) na fasihi za wageni (*hiari ya moyo*).

Aidha, mchango wa mtagusano wa kijamii katika kuchochea utendaji wa nyimbo za *mdumange* unaonekana kupitia dhamira ya ushindani kati ya wenyeji na wageni kwenye nyimbo husika. Hali ya ushindani miongoni mwa wanajamii (wenyeji na

wageni) inadhihirika kupitia baadhi ya nyimbo za *mdumange* kama vile wimbo ufuatao ambao uliimbwa na kikundi kimoja cha *mdumange* wakati wa wakati wa sherehe za mwenge tarehe 1/05/2016.

**Mf. 3.4: Wimbo Kuonyesha Ushindani wa Wasanii**

1. Nipeni yamini
2. Na viapo vyote
3. Nikishindwa nitavunja vyungu
4. Hata mjinaki
5. Mwajinaki bure Tamiwai *hemumdahe*

Katika wimbo huu ambao unapoimbwa, mwimbaji hutamba kwa kinua juu kidole huku akiwa anachezeshwa kichwa na shingo, suala la ushindani linabainika. Kwa mujibu wa Nadharia ya Utendaji wa Maigizo, kitendo cha kuinua kidole juu kinaashiria kuwa msanii huyo ni namba moja na hakuna msanii mwingine mwenye uwezo wa kuimba au kufanya jambo jingine zuri kama yeye. Aidha, wimbo huu pia unaonyesha kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* bado unaambatana na madoidoi ya kimajigambo. Kupitia wimbo huu msanii aitwaye Tamiwai anajisifu kuwa hakuna wa kumpiku katika kutunga nyimbo na kucheza ngoma. Hii inaonyesha kuwa hali au muktadha wa kutokea na kustawi kwa nyimbo za *mdumange* kumeambatana na uwepo wa aina nyingine ya sanaa za kifasihi simulizi, zikiwemo za wageni na za wenyeji pia.

Aidha, kutokana na nukuu hii, ni dhahiri kuwa ingawa inaaminika kwamba nyimbo hizo ni za zamani, data inaonyesha kuwa ziliimbwa kwa Kiswahili. Jambo hili linatufanya tutoe hoja kuwa matumizi ya Kiswahili katika nyimbo za majigambo ya kiushindani yanathibitisha kuwa hadhira iliyokuwako wakati huo ilijumuisha wasiojua na waliojua Kisambaa, yaani wageni na wenyeji.

Kwa upande mwingine, ingawa maelezo ya watafitiwa yanasisitiza kuwa nyimbo za *mdumange* zilitokana na fasihi ya Wanyamwezi maelezo hayo hayathibitishi ni lini hasa Wanyamwezi walikuja Lushoto. Aidha, licha ya kuwa watafitiwa wanawataja Wanyamwezi peke yao, ushahidi uliopatikana kwenye nyimbo zinazoimbwa unaonyesha kuwa jamii ya Wasambaa imekuwa na uhusiano na jamii nyingine kando na Wanyamwezi, hususan Wamakonde:

**Mf. 3.5: Wimbo wa Uhusiano kati ya Wasambaa na Wamakonde**

**KISAMBAA**

1. Wamakonde mtejinaki nakio
2. Ubwanga wenyu siunee

**KISWAHILI**

1. Wamakonde mmejigamba bure usiku
2. Ujeuri wenu sijauona

Nukuu ya wimbo katika mfano namba 3.5 inaonyesha kuwa kando na Wanyamwezi, Wasambaa wamekuwa na uhusiano na jamii ya Wamakonde. Aidha, ingawa wimbo huu hauonyeshi bayana wakati gani Wamakonde walikuja lakini kutokana na maudhui ya wimbo tunafahamu kuwa jamii hizi mbili zimetangamana kwa namna fulan, na utangamano huo umezua aina maalum ya utamaduni wa kujigamba kwa kusifia makabila yao. Wimbo huu pia unaonyesha kuwa, utendaji wa nyimbo za *mdumange* ulitumika kama jukwaa la kuonyesha ufahari au utambulisho wa makabila ya Kiafrika, ikiwemo Wasambaa na Wamakonde. Tunaelewa vizuri zaidi wimbo huu kutokana na matumizi ya msimbo wa kiutamaduni ambapo kupitia majina ya makabila tajwa mna viashiria kadhaa vya kujigamba na kujisifu. Mathalani, Wasambaa ni watu ambao wanasifika sana kwa uganga na Wamakonde pia hawapo nyuma wakidaiwa kuwa uganga wao wameutoa Msumbiji (mahojiano na watafitiwa). Jambo hili linathibitisha kuwa mtangusano wa jamii ya Wasambaa na jamii nyingine una mchango mkubwa katika kukuza utendaji wa nyimbo za *mdumange*.



Kimsingi, kuwako kwa maudhui yanayotaja kwa kubeza au kusifia makabila yanayopatikana Tanzania kunaonyesha pia kuwa utendaji wa nyimbo umezuka wakati ambapo kulikuwa na utamaduni wa utani baina ya kabila moja na lingine. Nyimbo za *mdumange* zimetumika pia kuendeleza jadi hiyo ya utani, ambapo kabila moja hubeza kabila lingine kwa minajili ya kukuza undugu au umoja kati yao. Kwa mfano katika wimbo ufuatao wasanii wa nyimbo za *mdumange* wanawataja Wabena (kabila linalopatikana Iringa, Tanzania) kwa kusema:

**Mf. 3.6: Wimbo ambao unaonyesha Utani kati ya Wasambaa na Wabena**

**KISAMBAA**

**MK:** Ngoma yabanighwa

**WK:** N'Wabena ee ee ee

**MK:** E yabanighwa

**WK:** N'Wabena ee ee ee

**KISWAHILI**

**MK:** Ngoma inaharibiwa

**WK:** Na Wabena ee ee ee

**MK:** E inaharibiwa

**WK:** Ni Wabena ee ee ee

Nukuu hapo juu ni mfano wa wimbo unaoimbwa kama kibwagizo cha utendaji wa nyimbo mbalimbali za *mdumange*. Kibwagizo hicho huimbwa mwishoni mwa wimbo kama hitimisho la wimbo mmoja na kama kianzio cha wimbo mwingine. Ingawa ndani ya wimbo huu Wabena wanatajwa, ujumbe na mantiki ya utendaji wake inatumika kukuza furaha na ushiriki wa hadhira.

**3.3 Matukio ya Sherehe za Wasambaa**

Mtazamo mwingine unaoelezea dhima ya miktadha ya jamii ya Wasambaa katika kuchochea kuibuka na kustawi kwa nyimbo za *mdumange* ni matukio ya sherehe. Kati ya watafitiwa ishirini na wane (24) waliohojiwa, hoja kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* unakuzwa na kuendelezwa na matukio ya sherehe iliungwa mkono na watafitiwa wanne (4) pekee. Hii ni sawa na asilimia kumi na sita nukta saba (16.7%) ya Wasambaa waliohojiwa. Aidha, ingawa idadi hii ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya watafitiwa waliounga mkono hoja zilizotangulia, ukweli ni kuwa mtazamo huu unaonyesha umuhimu wa tukio la utendaji katika kuathiri ujumi wa fasihi.

Kulingana na Wasambaa waliohojiwa, ilielezwa uwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* huambatana na utokeaji wa matukio ya sherehe za Wasambaa hususan sherehe za harusi, dini, na hafla za kisiasa. Nyimbo zinazowasilishwa kwenye miktadha hii zimewawezesha wasanii kusawiri dhamira anuai kuhusu mapenzi, siasa, mazingira, afya na dini.

### 3.3.1 Harusi

Sherehe za harusi ni miongoni mwa matukio yanayotumiwa katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Utendaji katika muktadha huu umeathiriwa na mtazamo au itikadi ya Wasambaa kuhusu mapenzi, ndoa, uzazi na malezi. Mtazamo wa Wasambaa kuhusu maisha yao umeathiri mikakati anuai ya kiutendaji ikiwemo uteuzi wa mahali pa kutendea, uteuzi wa dhamira, haiba za fanani na hadhira.

Katika jamii ya Wasambaa, sherehe za harusi hufanyikia nyumbani kwa bibi harusi. Jambo hili pia limeathiri utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwa kuwa hata utendaji wake hufanyikia katika sehemu hiyo hiyo. Hii ni kwa sababu kusudio kuu la uwasilishwaji wa nyimbo hizi ni kuwapongeza wazazi wa bibi harusi, umuhimu wa tabia njema, nafasi ya mahari katika ndoa pamoja na mambo ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa na vijana kabla hawajaoa. Kwa mfano, wimbo ufuatao ambao uliimbwa na bwana Abedi wakati wa sherehe za harusi iliyofanyika katika kijiji cha Kivilicha tarehe 10/09/2015 msanii anasema:

#### Mf. 3.7: Wimbo Ulioimbwa wakati wa Harusi

##### KISAMBAA

1. Ukihua mvyee uwee tabia Saadia ee
2. Ukihua mvyee uwee tabia Saadia ee

##### KISWAHILI

1. Ukitaka kuoja mke chunguza kwanza tabia zake Saadia ee
2. Ukitaka kuoja mke chunguza kwanza tabia zake Saadia ee

Katika nukuu hapo juu, vijana wanasisitizwa kuzingatia tabia ya wachumba wanaotarajia kuwaoa. Msimbo wa kiseme wa Nadharia ya Semiotiki ya Kijamii unajipambanua vizuri katika wimbo huu ambapo neno tabia kwa maana pana ya kisemantiki linarejelea roho ya kudumu kwa maisha ya ndoa. Maisha ya ndoa yana changamoto kubwa kutokana na wanandoa kila mtu kuwa na tabia yake lakini tabia zao zikiwa nzuri ndoa itadumu kwa miaka mingi mpaka kifo kiwatenganishe.

Katika wimbo mwingine suala la tabia njema pia linasisitizwa ambapo msanii anasema kuwa kitu muhimu cha kuzingatia wakati wa kuoa ni moyo wa mtu badala ya sura. Moyo unaotajwa katika wimbo ufuatao ni wa ukarimu, upendo, na uvumilivu. Kadhalika, kupitia wimbo wasanii wanatumia mkutadha wa harusi kuwaasa vijana na jamii kwa ujumla isiwabague watu kwa misingi ya ulemavu:

**Mf. 3.8: Wimbo ambapo Mwimbaji anasisitiza Tabia Njema kwa Wanandoa**

**KISAMBAA**

1. Eooe sura n'maua ee aa ee tiweea moyo
2. Eooe sura n'maua ee aa ee tiweea moyo
3. Eooe kiema hashekwa ee aa ee tiweea moyo
4. Hangwe kiema hashekwa ee aa ee tiweea moyo

**KISWAHILI**

1. Eooe sura n'maua ee aa ee tunaangalia moyo
2. Eooe sura n'maua ee aa ee tunaangalia moyo
3. Eooe kilema hachekwi .... tunaangalia moyo
4. Eti kilema hachekwi ....tunaangalia moyo

Katika wimbo ulionukuliwa hapo juu suala la kuzingatia upendo na mwenendo bora linahimizwa kama msingi wa mapenzi na kukuzia asasi ya ndoa. Hili linabainika kutokana na neno “moyo” kurudiwa mara kadhaa katika wimbo huo na kujenga msimbo wa kihemenitiki wa Nadharia ya Semiotiki ya Kijamii (Barthes, 1964; Eco, 1984). Kwa upande mwingine, wasanii wa nyimbo za *mdumange* hufanya utendaji wao siku moja kabla ya ndoa kufungwa. Jambo hili limefafanuliwa vyema na Zakati Hassani aliposema:

Sherehe za harusi huweza kufanyika mchana au usiku. Sherehe hizo hufanyika siku moja kabla ndoa rasmi haijafungwa. Wanaohudhuria ni bibi harusi, wazazi wa bi harusi, ndugu wengine wa karibu na bi harusi na majirani.

Kutokana na nukuu hapo juu, tunafahamu kuwa washiriki wa utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika sherehe za harusi ni bi harusi, wazazi wake, majirani na wasanii wa nyimbo za *mdumange*. Wasanii huutumia muktadha huu kuteua na kuwasilisha nyimbo zenye maudhui yanayoendana na tukio la harusi. Kutokana na muktadha huu uwasilishaji wa nyimbo za *mdumange* husisitiza dhamira zinazohusu umuhimu wa kuo au kuolewa na kuchagua mchumba. Aidha, nafasi ya mahari katika ndoa pamoja na maisha ya ndoa, malezi bora husisitizwa sio tu kwa bibi harusi bali pia kwa wanajamii wote kwa ujumla. Kwa mfano katika wimbo ufuatao, umuhimu wa upendo na mapenzi ya dhati umesisitizwa:

**Mf. 3.9: Wimbo Unaoonyesha Dhamira ya Mapenzi ya Dhati**

**KISAMBAA**

1. Unyumba ni kukundana
2. na uko kuhembezana
3. Unyumba ni kukundana
4. na uyo mpenzi wako

**KISWAHILI**

1. Unyumba ni kupendana
2. na pia kubembelezana
3. Unyumba ni kupendana
4. na huyo mpenzi wako

Pamoja na kutoa nasaha kuhusu umuhimu wa upendo na kubembelezana miongoni mwa wanandoa, nyimbo za *mdumange* zinazoimbwa kwenye harusi pia zinasisitiza umuhimu wa heshima na adabu kwa bibi harusi. Katika jamii ya Wasambaa, mke mwema hutazamwa kulingana na tabia yake ya uwajibikaji na utii kwa wanajamii wenzake. Dhamira hii inabainika waziwazi katika wimbo ufuatao:

**Mf. 3.10: Wimbo wa *Mdumange* Unaosisitiza Utii na Uwajibikaji**

**KISAMBAA**

1. Iwe ng'wai utende na ishima
2. N'kughulie tenge ja imia
3. Aee n'kughulie tenge ja imia

**KISWAHILI**

1. Wewe mwali uwe na heshima
2. Nikununulie kitenge cha kulimia
3. Aee nikununulie kitenge cha kulimia

Katika wimbo huu, mwimbaji anamwelekeza mwali awe na heshima, kisha anamuahidi kuwa atapokuwa na heshima atamnunulia kitenge cha kulimia. Ni dhahiri kuwa mbali na kusisitiza umuhimu wa tabia njema, nyimbo za *mdumange* pia huutumia muktadha wa harusi kusisitiza umuhimu wa kufanya kazi.

Kwa ujumla, maudhui ya nyimbo za *mdumange* zinazoimbwa kwenye harusi yanaendeleza na kukuza itikadi ya Wasambaa kuhusu usawa wa kijinsia baina ya wanawake na wanaume. Kama ilivyoonyeshwa katika sehemu hii, itikadi ya Wasambaa inaelekea kumkweza mwanamume kwa upande mmoja, na kumtweza mwanamke kwa upande mwingine. Aidha, itikadi za Wasambaa kuhusu asasi hii zimejengwa juu ya misingi wa mfumo wa ubabedume unaowapa wanaume hadhi na mamlaka ya juu zaidi kuliko wanawake. Kadhalika, itikadi ya Wasambaa inayosawiriwa kupitia utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwenye harusi inaenzi malezi bora ya mtoto wa kike kuliko mtoto wa kiume.

### **3.3.2 Sikukuu za Kidini**

Kando na asasi ya ndoa na harusi, asasi nyingine iliyoathiri na kuchangia maendeleo ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni dini. Katika Wilaya ya Lushoto kuna watu wanaofuata imani ya dini za Kikristo, Kiislamu na Kijadi. Jambo hili limeathiri maudhui na utendaji wa nyimbo kwa ujumla. Aidha, maudhui ya nyimbo za *mdumange* yanasawiri mitazamo mikuu ya mfumo wa dini: za Kikristo, Kiislamu na Kijadi. Hivyo, Wilaya ya Lushoto ina kitu ambacho tunaweza kukiita “Uvumilivu wa Kidini” mahali ambapo mtu wa imani moja humheshimu mtu wa imani nyingine, na kwa sababu hiyo watu wa imani tofauti wanaweza kuishi mahali pamoja bila kikwazo chochote.

Kimsingi, kuna sherehe kuu tatu zinazohusishwa na nyimbo za *mdumange* katika muktadha wa dini. Sherehe hizo ni Ubarikio, Krismasi na Idi el-fitri. Ubarikio na Krismasi huwahusu zaidi waumini wa dini ya Kikristo ilhali idi el-fitri huwahusu waumini wa dini ya Kiislamu. Mafundisho ya dini hizi mbili yanakataza mtu kujihusisha na ibada za kijadi pamoja na utamaduni wake. Kwa hiyo, hata nyimbo za *mdumange* pamoja na aina nyingine za dansi au muziki wa asili zinapingwa vikali. Pamoja na hali hii, waumini wake wanapenda sana nyimbo za *mdumange* na kwamba wakati wa hafla zilizotajwa, hunogesha sherehe zao kwa njia ya kucheza na kuimba nyimbo za *mdumange*.

Ubarikio ni sherehe wanazofanyiwa watoto wa waumini wa dini ya Kikristo baada ya watoto hao kuhitimu mafunzo ya awali kuhusuiana na dini yao. Watoto hufanyiwa tafrija fupi kama ishara ya kuwapongeza kwa kufikia hatua hiyo. Vilevile, tafrija hii ni ishara ya kuwahimiza watoto na wanajamii wote kwa ujumla wasipuuze masomo ya dini, na baada ya kuhitimu sasa wanapaswa kuyafanyia kazi mafunzo waliyoyapata katika maisha yao.

Ibada rasmi ya sherehe ya Ubarikio hufanyika siku ya Jumapili, nyakati za asubuhi katika maeneo ya kanisani. Baada ya hapo, watu hutawanyika na kwenda majumbani mwao kwa ajili ya tafrija mbalimbali kama vile vyakula na sherehe ndogondogo za kidini. Waumini wa dini ya Kikristo hutumia fursa hii kualika kikundi cha wasanii wa nyimbo za *mdumange* kuja kutumbuiza majumbani mwao nyakati za mchana. Kwa hiyo, katika siku ya sherehe ya Ubarikio nyimbo za *mdumange* huimbwa wakati wa mchana, wakati ambapo ibada rasmi ishafanyika huko kanisani.

Aidha, Krismasi ni sherehe inayowahusu waumini wote wa dini ya Kikristo duniani. Sherehe hii hufanyika kila mwaka ifikapo tarehe ishirini na tano mwezi Disemba kwa

minajili ya kusherehekea na kuadhimisha kuzaliwa kwa Yesu Kristo. Kwa upande mwingine, Idi elfitri ni sikukuu za waumini wa dini ya Kiislamu. Idi el-fitri hufanyika kila mwaka baada ya waumini wa dini hiyo kumaliza ibada ya kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhan (mwezi wa kumi katika kalenda ya Kiislamu).

Kulingana na Nadharia ya Utendaji wa Maigizo, siku zote fasihi simulizi huwasilishwa katika tukio mahsusi kwenye wakati mahsusi (Finnegan, 1997; Mulokozi, 2002; Ngadala, 2003; na Kitogo, 2005). Aidha, ni kutokana na mtazamo huu ambapo Finnegan (1977) anafafanua kuwa ili fasihi simulizi iwafikie walengwa ni lazima iwasilishwe kwenye tukio mahsusi la kijamii. Tukio la utendaji huathiri namna ya kuteua mahali pa kutendea na kubainisha aina za wanajamii wanaopaswa kushiriki utendaji.

Ni kutokana na msingi huu ambapo katika sherehe za kidini utendaji wa nyimbo za *mdumange* hufanyika nyakati za mchana katika mandhari maalum tofauti na mandhari ya kanisani au msikitini. Utendaji wa nyimbo za *mdumange* hutokea baada ya ibada au sala rasmi za waumini husika kukamilika. Wakati wa sherehe ya Krismasi, waumini wa dini hiyo huutumia mchana wa siku hiyo kujifurahisha kwa kutumia nyimbo za *mdumange*.

Kadhalika, utendaji wa nyimbo za mdumage unafanyikia kwenye maeneo ya wazi kama vile viwanja vya mipira, barabarani na katika majumba ya waumini. Hali hii huwaruhusu watu ambao hata kama si waumini wa dini ya Kikristo kuhudhuria na kushiriki burudani ya nyimbo za *mdumange*. Kwa upande mwingine, katika sikukuu za Idi-elfitri pia iko hivyo hivyo. Hafla za nyimbo za *mdumange* huanza muda wa mchana mara baada ya kumalizika kwa ibada rasmi ya sikukuu hizo msikitini.

Kando na kutambulisha mahali pa kutendea, muktadha wa tukio la utendaji pia huelekeza katika haiba za fanani na hadhira. Kulingana na maoni ya Okpewho (1992) tukio la utendaji linasaidia kupambanua haiba za fanani na hadhira. Aidha, Okpewho anaongeza kuwa pamoja na haiba za fanani utendaji wa fasihi simulizi pia unaathiriwa na ushiriki wa hadhira. Hii ni kwa sababu utendaji wa fasihi simulizi nyimbo za *mdumange* zikiwemo haukamiliki bila kushirikisha hadhira. Mtazamo kuwa hadhira inashirikiana na fanani katika kuwasilisha fasihi unaelezwa vyema na Finnegan (1992) anayetoa hoja kuwa hadhira ni miongoni mwa vipashio muhimu vya utendaji wa fasihi simulizi.

Ni muhimu kusesitiza kuwa kutokana na umuhimu wa hadhira, washiriki wa utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwenye sherehe za kidini si waumni wa dini husika peke yao, badala yake wanajamii mbalimbali pia huhudhuria. Ushiriki katika hafla hizi ni huria, mtu anaweza kushiriki au la. Kwa kuwa nyimbo za *mdumange* zinapigwa vita na watu wa dini za Kikristo na Kiislamu, kiwango cha ushiriki wa wazee kwenye halfa za sikukuu za dini ni kidogo zaidi ikilinganishwa na idadi ya vijana. Vilevile, vijana wanaoshiriki huteua maeneo yaliyo kando kidogo na nyumba za ibada kwa ajili ya burudani hiyo. Kwa kuzingatia hali halisi ya muktadha wa sherehe na hafla za kidini, fanani na hadhira wa nyimbo za *mdumange* huteua muda na mahali pa kufanyia utendaji wao ili kukidhi matakwa ya washiriki wake.

Kulingana na taathira za mafunzo ya dini kwa washiriki, fanani na hadhira hubuni nyimbo maalum zinazoelezea umuhimu wa dini. Utokeaji wa dhamira za kidini katika nyimbo za *mdumange* kwa kiwango kikubwa ni hoja iliyobainika zaidi katika muktadha huu. Mfano wimbo ufuatao ulioimbwa wakati wa sherehe za Ubarikio na kikundi cha *mdumange* cha Bwana Hoza:



**Mf. 3.11: Wimbo Ulioimbwa kwenye Sherehe ya Ubarikio****KISAMBAA**

1. Chonge hangwe ni isho
2. Chonge usheeke dini
3. Ukieka dini
4. Chonge usheuye kaya

**KISWAHILI**

1. Baba yako anakugiza Chonge
2. Chonge usiache dini
3. Ukiacha dini
4. Chonge usirudi nyumbani

Ni wazi kuwa suala la umuhimu wa kufuata mafunzo ya dini linasisitizwa sana sio tu katika dini ya Ukristo bali pia hata katika dini ya Uislamu. Kwa hiyo, wimbo huu pia ungeweza kutumika hata katika sikukuu ya dini ya Kiislamu. Kadhalika, wakati wa sikukuu za dini ya Kiislamu dhamira kama vile umuhimu wa kusali na kuacha kulewa pombe unahimizwa sana. Kwa mfano, katika wimbo ufuatao, msanii anaonyesha mtazamo wa wanadini kuhusu pombe na uharamu wake katika jamii:

**Mf. 3.12: Wimbo Unaoonya Wanajamii Kuacha Pombe****KISAMBAA**

1. Ukikundauzikwe vyedi
2. Mnaa kubali ueke mphombe
3. Siku ya kufa waimu  
washekuona seze

**KISWAHILI**

1. Ukitaka uzikwe vizuri
2. Mama kubali uache pombe
3. Siku ya kufa walimu  
wasikuone kinyaa

Wimbo huu huimbwa wakati wa sherehe za sikukuu ya Idi-elfitri. Hata hivyo, dhamira zinazokuzwa na kuendelezwa zinahusu mtazamo wa dini zote kuhusu uharamu wa pombe na umuhimu wa kusali. Katika wimbo huu, kuna sharti linalowekwa na watu wa dini kuwa kama muumini anataka viongozi wa dini wamhudumie vizuri siku atakapokufa inampasa akubali kuacha pombe, na ashiriki katika ibada ya sala nyinginezo. Vinginevyo, siku atakapokufa viongozi wa dini wataweka vikwazo mbalimbali kama vile faini ndipo washiriki katika mazishi yake.

Kutokana na hali hii, miktadha ya kidini hususan utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika Ubarikio unaonekana kumbana msanii wa nyimbo za *mdumange* kiasi cha kutoweza kuchanganya maudhui ya kidini na maudhui ya aina nyingine. Nyimbo

zinazoimbwa wakati huo ni zile tu zinazohusu kumsifu Mungu na kuelezea umuhimu wa kushika dini.

Kwa upande mwingine, sherehe za sikukuu za Krismasi, na Idi-elfitri zinatoa uhuru kwa watendaji sio tu kuimba nyimbo za dini, bali pia kujadili dhamira mbalimbali za maisha ya mwanadamu kama vile mapenzi, siasa na maadili kwa ujumla. Kutokana na hali hii, utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwenye muktadha wa sherehe ya sikukuu ya Krismasi unahusisha pia nyimbo zenye maudhui yanayojali hisia za vijana hususan dhamira za kisiasa na mapenzi. Kwa mfano, wimbo ufuatao:

**Mf. 3.13: Wimbo wa Siasa Uliombwa kwenye Sikukuu za Kidini**

1. Kule kijijini
2. Kule kijijini tunapata tabu tunateswa na viongozi wa kijiji na kamati zao
3. Tunachoimba
4. Tunachoimba serikali yetu iunde tume huru ichunguze waharibifu

Kama inavyoonekana katika nukuu hii, ingawa wimbo huu uliimbwa kwenye sherehe za sikukuu ya Krismasi, lakini unajadili suala la uongozi na uwajibikaji kwenye serikali za vijiji. Hii inaonyesha kuwa muktadha wa sikukuu za kidini pia umewawezesha wasanii wa nyimbo za *mdumange* kujadili dhamira za siasa na uongozi.

Kulingana na Nadharia ya Utendaji wa Maigizo, maudhui ya kazi ya kifasihi hayaathiriwi tu na utashi wa fanani bali pia yanaathiriwa na ushiriki wa hadhira. Ni kutokana na athari ya ushiriki wa hadhira ya vijana ndio maana wakati wa utendaji wa nyimbo kwenye sherehe za kidini fanani huchanganya dhamira za dini na siasa. Imebainika katika utafiti huu kuwa washiriki wa nyimbo za *mdumange* wakati wa sikukuu za dini si lazima wawe waumini wa dini husika, bali watu wa imani

nyinginezo pia wanakuwepo. Bila shaka, muktadha huu ndio umeziweshwa nyimbo za *mdumange* kuchanganya aina mbalimbali ya dhamira wakati wa utendaji wake.

Jambo lingine muhimu kuhusiana na muktadha wa kidini ni kuwa ingawa nyimbo za *mdumange* hujadili masuala ya kidini, na kwa kiwango kikubwa washiriki wake ni watu wa dini lakini haziimbwi katika maeneo ya ibada rasmi kama vile kanisani na misikitini, badala yake utendaji wa nyimbo hizo hufanyikia kwenye maeneo yaliyo pembezoni na maeneo ya ibada kama vile majumbani mwa waumini na kwenye viwanja au maeneo ya wazi. Hoja hii inathibitisha kuwa haiba za washiriki, haja zao, muda na mahali pa kutendea yameathiri utendaji wa fanani na hadhira wakati wa utendaji wa nyimbo kwenye sikukuu za kidini.

### **3.3.3 Hafla za Kisiasa**

Siasa ni moja kati ya matukio ya kijamii yaliyoathiri utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwa kiasi kikubwa sana. Katika hafla za kisiasa na pia katika hafla nyingine za kijamii, utendaji wa nyimbo za *mdumange* huchukuliwa kama tukio la burudani. Kutokana na hali hii, utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni huru kwani wanajamii wanaweza kuamua ama kuwasilisha au kutowasilisha nyimbo katika matukio kama vile ya siasa. Hali ya muktadha wa sherehe unaambatana na uhuru miongoni mwa wanajamii inaafikiana na maelezo ya Kitogo (2005) pamoja na Wanyama (2005). Kwa mfano, kulingana na Wanyama utendaji wa fasihi simulizi unaweza kutokea katika muktadha huru au usio huru.

Kwa ujumla, utafiti huu umebaini kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika muktadha wa kisiasa umehusisha matukio ya kampeni za uchaguzi, sikukuu ya Wafanyakazi na mbio za mwenge. Muktadha hii imeathiri namna ya uteuzi wa

dhamira, mahaki pa kuwasilishia na aina ya hadhira. Maelezo ya kina kuhusu dhima ya muktadha wa matukio ya sherehe za kisiasa yametolewa katika sehemu ifuatayo.

### **3.3.3.1 Kampeni za Uchaguzi**

Tangu mwaka 1992, nchi ya Tanzania imeingia katika mfumo wa siasa ya vyama vingi ambapo uchaguzi wa viongozi huhusisha ushindani wa chama zaidi ya kimoja. Mojawapo ya michakato ya uchaguzi huru na wa haki ni kuweco kwa kampeni za uchaguzi. Katika kampeni hizo viongozi wanaogombea nafasi mbalimbali za uongozi, hujinadi na kufafanua sera zao kwa wananchi kama njia ya kuwaomba wawapigie kura.

Mchakato wa kampeni nchini Tanzania hufanyika miezi michache kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu, ambao pia hufanyika kila baada ya miaka mitano. Katika uchaguzi mkuu, viongozi wanaotarajiwa kuchaguliwa ni rais, wabunge na madiwani. Aidha, kampeni hizo huhusisha pia uwasilishwaji wa nyimbo na sanaa mbalimbali za kifasihi simulizi. Makusudio ya uwasilishwaji wa nyimbo za *mdumange* kwenye hafla za kisiasa, hususan kampeni za uchaguzi ni kuwasifia baadhi ya viongozi wa kisiasa na pia kuwakejeli baadhi yao kutegemea na kiwango cha uwajibikaji wao. Kwa mfano kulingana na maelezo yaliyotolewa na Mzee Shauri wimbo ufuatao uliimbwa na kikundi chake 1972 ambapo kusudio lake lilikuwa ni kumsifia rais wa wakati huo, Mwalimu J.K Nyerere. Msanii anasema:

#### **Mf. 3.14: Wimbo wa Kumsifu Kiongozi**

1. Viongozi wote
2. Viongozi wote ni wazuri sana Nyerere umetia fora
3. Uliomba maji na sabuni moja Tanzania ukaitakasha
4. Mpanda ngazi
5. Mpanda ngazi anakwenda mbele kisha anarudi nyuma
6. Nani alijua gavana wetu siku gani atarudi kwao

Nukuu ya wimbo huu inaonyesha kuwa wasanii wa nyimbo za *mdumange* huutumia muktadha wa kisiasa kuelezea hisia zao dhidi ya watawala. Katika wimbo huu Nyerere anasifiwa kulingana na mchango wake mkubwa wa kuongoza harakati za kudai uhuru, hadi kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kidemokrasia. Katika kampeni za uchaguzi mkuu mwaka 2015 wasanii wa nyimbo za *mdumange* waliimba nyimbo nyingi kuwasifia na kuwapongeza viongozi wa chama cha CCM. Hata hivyo, kutokana na athari ya utendaji wa nyimbo hizi uliofanywa miaka ya sabini mpaka miaka ya tisini, wasanii huwa wanabadilisha tu majina ya viongozi lakini ujumbe na mtindo wa kucheza unakuwa wa namna moja. Kwa mfano, wakati wa kampeni za mwaka 2015 wasanii walipoimba kumsifia kiongozi aliyekuwa anagombea nafasi ya urais badala ya kusema **Nyerere umetia fora**, wao walisema **Magufuli ametia fora**. Hali hii inaonyesha kuwa wasanii wa nyimbo za *mdumange* wanaoimba nyimbo husika mwaka 2015 kwa namna fulani wameathiriwa na wasanii walioimba nyimbo hizo miaka ya sabini (1972).

Utafiti huu umebaini kuwa utendaji wa nyimbo umetumika kama mbinu ya kuwatangaza viongozi kwa wananchi. Ili kuhakikisha kuwa viongozi watarajiwa wanawashawishi wananchi kiasi cha kuridhisha, mbinu mbalimbali hutumika. Miongoni mwa mbinu hizo ni kukodisha wanamuziki, wasanii na vyombo vya habari na kuvitumia katika kutangaza sera na ilani ya kiongozi au chama husika. Kwa hiyo, wasanii wa nyimbo za *mdumange* pia hukodishwa na chama au mgombea huzunguka na msafara wa mgombea huyo kwa ajili ya kumnadi mbele ya wananchi. Hali hii inabainishwa na wimbo ufuatao ambapo kikundi cha wasanii wa nyimbo za *mdumange* kinaonyesha furaha na upendo kwa kiongozi kama ishara ya kumkubali:

**Mf. 3.15: Wimbo Unaoonyesha Upendo wa Raia kwa Kiongozi**

Ee ndugu Makamba tunavyokupenda hatujui tutakupa nini  
Nyoyo za watu kama ni kitabu tungekupa ukasomasoma

Kiongozi anayetajwa katika wimbo huu ni kada wa chama wa CCM nchini Tanzania. Kutokana na ukweli kuwa wasanii wanapewa posho mbalimbali na viongozi hulazimika kuimba nyimbo za kuwasifia viongozi hao, badala ya kuonyesha udhaifu wa uwajibikaji wao.

Aidha, kitendo cha wasanii kuonyesha hisia za kumkubali kiongozi kinaonyesha kimetumika kama aina mahsusi ya mikakati inayotumiwa na wasanii hao kuwashawishi wanajamii wengine nao wamkubali kiongozi, na hatimaye wamchague kwa kumpigia kura. Hili pia linabainika kutokana na Nadharia ya Utendaji wa Maigizo inayosisitiza kuwa sauti za waigizaji huwa ni sauti za umma au jamii nzima. Kwa hiyo, kupitia wimbo huu tunapata kufahamu kuwa sauti inayotoka ni kama sauti ya wanajamii wote. Wajamii wengine hata kama wao hawakusema kuwa wanampenda kiongozi huyo lakini hapa na wao wamesemewa na baadhi yao huchukua mkondo huo na hatimaye kumpigia kura mlengwa katika wimbo husika.

Ni kutokana na hali hii ambapo utafiti huu unatoa hoja kuwa matumizi ya nyimbo za *mdumange* katika majukwaa ya kampeni za uchaguzi yanawahitaji viongozi wa kisiasa wenye uwezo mkubwa wa kiuchumi na kiushawishi. Uwezo wa kiuchumi huwafanya viongozi wawapatie wasanii fedha kama posho maalum kwa kazi kubwa ya kuwatangaza. Kwa namna hii, mara nyingi chama tawala ndicho kilichokuwa kikiwatumia wasanii na hatimaye kushinda vyama vingine vya upinzani.

Muktadha wa kampeni za uchaguzi ambao umewahusisha viongozi wenye uwezo mkubwa na wenye uwezo mdogo wa kiuchumi umeathiri mtazamo wa wasanii kuhusu chama tawala na vyama vya upinzani mutawalia. Kimsingi, utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika kampeni za uchaguzi unaonyesha mamlaka ya juu waliyo nayo viongozi wa chama cha CCM, dhidi ya mamlaka ya chini waliyo nayo

viongozi wa vyama vya upinzani kama vile CHADEMA. Kutokana na ushindani wa kimamlaka, wasanii wa nyimbo za *mdumange* huwa wanaimba nyimbo zinazotukuza CCM kwa upande mmoja, na kukejeli chama cha upinzani (CHADEMA) kwa upande mwingine. Ingawa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 zilihusisha vyama zaidi ya thelathini na mbili (32) nchini Tanzania, upinzani na ushindani mkubwa ulionyeshwa kati ya chama cha CCM na chama cha CHADEMA. Hali hii inawasilishwa vyema na wimbo ufuatao:

**Mf. 3.16: Wimbo unaosifia CCM Kukejeli CHADEMA**

**KISAMBAA**

1. CHADEMA waaghushana na CCM,  
CCM ni isho enyu
2. CHADEMA waiya waiya,  
CHADEMA, CCM ni isho enyu

**KISWAHILI**

1. CHADEMA mnakimbizana na  
CCM, CCM ni baba yenu
2. CHADEMA nalia mimi jamani,  
CHADEMA, CCM ni baba yenu

Wimbo ulionukuliwa katika mfano namba 3.16 unaonyesha dhima ya muktadha wa kisiasa katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Kutokana na ukweli kuwa chama cha CCM kina viongozi wenye fedha, na wenye nafasi za juu katika utawala, wasanii wanaona ni vyema kuwaunga mkono kwa kuwasifia ili kuwa karibu na wenye mamlaka. Kwa upande mwingine, wasanii wanaonyesha mamlaka ya chini walio nayo wanachama wa chama cha CHADEMA kwa kuwaonya wasishindane na CCM kwa kuwa CCM ni sawa na baba yao. Hapa kuna matumizi ya msimbo wa Nadharia ya Semiotiki ya Kijamii ambapo kutajwa kwa vyama hivi vikubwa vya siasa nchini Tanzania kunaashiria kwamba hawa ndio washindani pekee wenye nguvu katika siasa za Tanzania. Hata hivyo, CCM inaonekana kuwa na nguvu zaidi kuliko CHADEMA kutokana na kuwepo madarakani kwa kipindi kirefu na hivyo kuishinda si kitu chepesi.

Kwa ujumla, muktadha wa kampeni za uchaguzi umechochea kuwako kwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* zinazofafanua hisia za wananchi kwa viongozi wao, matarajio yao na kujenga itikadi ya utawala bora na demokrasia. Kulingana na utafiti huu, kiongozi bora ni yule anayewatumikia wananchi, na kwamba ustawi wa jamii unategemea uhusiano mzuri kati ya wananchi na viongozi wao.

Kadhalika, utafiti huu pia umebaini kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* pia umetumika kuonyesha mamlaka ya juu waliyonayo watawala, ikilinganishwa na mamlaka ya chini ya vyama vya upinzani. Kwa namna fulani, wasanii wanadokeza kuwa watawala wanayatumia madaraka yao vibaya kwa kuwakandamiza wananchi wanyonge wenye mamlaka ya chini.

Kwa ujumla, utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika kampeni za uchaguzi umezua mabadiliko kadhaa kwa wasanii, nyimbo na ufundi wa kuwasilisha nyimbo. Tangu siasa za vyama vingi zilipoanza miaka ya tisini nchini Tanzania, kumekuwa na mwamko mpya wa kuwasilisha nyimbo zenye kutumia mbinu ya kejeli na ucheshi. Mbinu hizi zimewawezesha wasanii kuwakosoa viongozi wao hadharani bila kikwazo chochote. Hii ni tofauti na iliyokuwa hapo awali (kabla ya miaka ya tisini) ambapo chama kimoja tu ndicho kilishika hatamu ya uongozi. Wananchi hawakuwa na uhuru wa kuelezea hisia zao kwa viongozi.

Kwa mujibu wa Selemani Kijemkuu (kutoka kijiji cha Soni), muktadha mpya wa kisiasa uliozuka miaka ya tisini pia umesababisha kutokea kwa aina mpya za mitindo ya uchezaji, miundo ya jukwaa la steji na mavazi maalum (sare) miongoni mwa wasanii wa nyimbo za *mdumange*. Kwa hiyo, athari ya muktadha mpya wa kisiasa haionekani tu katika maudhui ya nyimbo bali pia inaonekana hata katika mitindo ya jukwaa na uchezaji.



Ingawa maelezo ya kina kuhusu mitindo hii ya utendaji imeelezwa katika sura ya tano yafaa kudokeza kwa ufupi hapa kuwa maelezo ya watafitiwa yanaonyesha kuwa kabla ya miaka ya tisini (1990) utendaji wa nyimbo za *mdumange* ulifanyika katika maeneo yasio rasmi, watu walicheza kwa kuzunguka duara la wapiga ngoma na kamwe hakukuwa na sare maalum kwa wasanii. Aidha, watafitiwa wanaendelea kufafanua kuwa kutokana na kuongezeka kwa ushindani wa kuimba nyimbo miongoni mwa vikundi, baadhi ya wasanii waliona bora kutumia jukwaa la steji ambalo linawaruhusu viongozi kuona utendaji hai wa fanani na hadhira.

### **3.3.3.2 Hafla za Sikukuu ya Wafanyakazi**

Hafla za sikukuu ya wafanyakazi huadhimishwa kila mwaka ifikapo tarehe moja mwezi wa tano duniani kote. Nchini Tanzania, kila mwaka viongozi wa serikali kuu huchagua mahali sherehe hizo zitakapofanyikia kitaifa, ingawa kila mkoa na kila Wilaya huandaa sherehe fupifupi katika maeneo yao.

Tofauti na ilivyo katika sherehe za harusi na sikukuu za kidini ambapo utendaji wa nyimbo huweza kufanyika ama usiku au mchana, katika hafla za sikukuu ya wafanyakazi utendaji hufanyika mchana peke yake. Aidha, mandhari yanayotumika ni viwanja vya michezo na maeneo mengine ya wazi. Washiriki wakuu wa utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwenye sherehe hizi ni viongozi na wananchi, wake kwa wanaume.

Miongoni mwa masuala yanayohimizwa na wasanii wakati wa sherehe hizi ni kufanya kazi kwa bidii, uwajibikaji, utunzaji wa mazingira, pamoja na kuonya jamii dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI na madawa ya kulevya. Kwa mfano, wimbo ufuatao ulioimbwa kwenye sherehe za hizi mnamo tarehe moja mwezi wa tano mwaka 2016 katika kijiji cha Mlalo:

**Mf. 3.17: Wimbo Unaosisitiza Suala la Uwajibikaji****KISAMBAA**

1. Eee tate Magufuli azan'ghambia
2. Ndiman'ndiman' ee
3. Tate Magufuli azan'ghambia
4. Kazi n'kazi wene ng'wana (I)
5. Eee tate Magufuli azan'ghambia
6. Ndiman'ndiman' ee
7. Tate Magufuli azan'ghambia
8. Ndiman'ndiman' Magoma iyoo (II)
9. Tate Magufuli azan'ghambia
10. Ndiman'ndiman' ee
11. Tate Magufuli azan'ghambia
12. Kazi n'kazi Tanzania (III)
13. Ee jeshi ja polisi mzaghambiwa
14. Ndiman'ndiman' ee
15. Jeshi ja polisi mzaghambiwa
16. Ndiman'ndiman' Tanzania (IV)

**KISWAHILI**

1. Eee baba Magufuli ameniambia
2. Kazi ni kazi ee
3. Baba Magufuli ameniambia
4. Kazi ni kazi mwanangu (I)
5. Eee baba Magufuli ameniambia
6. Kazi ni kazi ee
7. Baba Magufuli ameniambia
8. Kazi ni kazi katika Magoma (II)
9. Baba Magufuli ameniambia
10. Kazi ni kazi ee
11. Baba Magufuli ameniambia
12. Kazi ni kazi nchini Tanzania (III)
13. Ee jeshi la polisi mmeambiwa
14. Kazi ni kazi ee
15. Jeshi la polisi mmeambiwa
16. Kazi ni kazi nchini Tanzania (IV)

Wimbo ulionukuliwa hapo juu unaonyesha umuhimu wa kufanya kazi na uwajibikaji kwa wananchi wote. Katika wimbo huu suala la kufanya kazi limesisitizwa ambapo Watanzania wameaswa wasichague aina ya kazi. Kitu cha muhimu ni kufanya kazi, iwe kilimo, viwandani au biashara. Kwa ujumla kupitia wimbo huu suala la uwajibikaji linadhihirishwa na kusisitizwa miongoni mwa wanajamii.

Pamoja na kujadili umuhimu wa kufanya kazi na uwajibikaji, wasanii wa nyimbo za *mdumange* huzitumia hafla za sikukuu za wafanyakazi kujadili itikadi ya Wasambaa kuhusu utawala na uongozi kwa ujumla. Wasanii hutumia jukwaa la utendaji wa nyimbo kuuhoji utawala kunako uwajibikaji wao. Kwa mfano katika wimbo ufuatao:

**Mf. 3.18: Wimbo Unaodadisi Uwajibikaji wa Viongozi**

- |   |  |
|---|--|
| 1. Mheshimiwa mtukufu rais sisi wana<br><i>mdumange</i> | 8. Ahadi ya pili ni mamlaka ya mji<br>mdogo hapa Mombo |
| 2. Tunakumbushia ahadi tatu                             | 9. Kuwa halmashauri kamili                             |
| 3. Zile ulizotuahidi mwaka elfu mbili na<br>kumi        | 10. Hilo tunataka majibu                               |
| 4. Kwenye kampeni hapa Mombo                            | 11. Mtukufu ndugu rais .....                           |
| 5. Ahadi ya kwanza ni maji safi                         | 12. Ahadi ya tatu Bonde Mkomazi                        |
| 6. Hiyo tunakushukuru                                   | 13. Umwagiliaji kilimo kwanza                          |
| 7. Kwa kuwa inatekelezwa                                | 14. Manga wanalalamika .....                           |

Katika nukuu hii, wasanii wa nyimbo za *mdumange* wamemkumbusha rais kuhusu ahadi alizoahidi mwaka 2010. Ahadi hizo ni upatikanaji wa maji safi, kuifanya Mombo iwe halmashauri kamili na kuboresha kilimo. Aidha, ndani ya wimbo huu, wasanii wanatoa pongezi pamoja na kero kwa viongozi husika. Pongezi zimetolewa kwa kutaja ahadi zilizotekelezwa (rejea mishororo ya 5, 6 na 7) na kero zimeelezwa kwa kutaja ahadi ambazo bado hazijatekelezwa (rejea mishororo ya 10 na 14) katika wimbo huu.

Ingawa nyimbo za *mdumange* zinazoimbwa kwenye hafla za sikukuu za wafanyakazi zinatekeleza majukumu ya kuelezea diskosi ya uongozi, afya, na uwajibikaji, kwa kiwango kikubwa nyimbo hizi huimbwa kwa minajili ya kuburudisha hadhira. Ili kutekeleza jukumu hili Nadharia ya Utendaji wa Maigizo inatufahamisha kuwa, wasanii hutumia ustadi wa hali ya juu katika sauti, mpangilio wa ala za muziki. Vilevile wasanii hutumia mitindo ya uchezaji inayoibua hisia na kushirikisha hadhira. Kadhalika, wasanii hutumia jukwaa lenye muundo wa mstatili (steji) kama ilivyo katika kampeni za uchaguzi. Jukwaa hili huwaruhusu wasanii kuonyesha mbwembwe zao kwa viongozi kwa uwazi zaidi kuliko kama wangetumia jukwaa la umbo la duara.

### **3.3.3.3 Hafla za Mbio za Mwenge**

Kwa upande mwingine, mbio za mwenge ni hafla maalum zinazofanywa kila mwaka na serikali ya Tanzania ambapo viongozi wa kamati za ulinzi huzunguka nchi nzima kwa minajili ya kuhamasisha maendeleo. Aidha, katika hafla hizo mwenge ambayo ni ishara ya uhuru wa nchi ya Tanzania huwashwa na kutembezwa katika vijiji na halmashauri zote nchini.

Viongozi huhamasisha maendeleo kwa kuonya jamii kuhusu mambo anuai ya kijamii kama vile madhara ya uasherati, UKIMWI na madawa ya kulevya. Kwa mfano katika wakati wa halifa za mwenge mwaka 2015 katika kijiji cha Kwemhafa wasanii waliimba wimbo ufuatao:

**Mf. 3.19: Wimbo Unaotahadharisha Jamii Kuhusu UKIMWI**

1. Twendeni wote tukapime tujue hali zetu,
2. Tuepukane na ngono UKIMWI utatumaliza (I)
3. Ooh twendeni wote tukapime baba tujue hali zetu,
4. Tuepukane na ngono UKIMWI utatumaliza ee (II)
5. Ooh twendeni wote tukapime leo tujue hali zetu,
6. tuepukane na ngono UKIMWI utatumaliza aa (III)

Katika nukuu hapo juu inaelezwa kuwa UKIMWI ni ugonjwa unaopatikana kutokana na tabia ya uasherati na pia imeshauriwa kupima afya mara kwa mara. Aidha, wimbo huu pia unajenga falsafa ya Wasambaa kuhusu UKIMWI kuwa ni tishio kwani huua watu kwa kiwango kikubwa sana. Hili linathibitika kutokana na matumizi ya msimbo wa kihemenitiki ambapo neno UKIMWI limetumiwa kuonyesha msisitizo kuwa ni ugonjwa hatari na ni vizuri kila mtu akapima ili kujitambua kama anao au la kwa lengo la kuchukua hatua stahiki.

Kando na UKIMWI wasanii wa nyimbo za *mdumange* pia huimba nyimbo zinazosisitiza madhara ya madawa ya kulenya hususan pombe na bangi. Kwa mfano, wimbo ufuato uliimbwa wakati wa mbio za mwenge mwaka 2015 katika kijiji cha Mtae. Aidha, licha ya kuwa madawa ya kulevya ni hatari kwa watu wote, mtazamo wa wasanii wa nyimbo za *mdumange* ni kuwa wanaoathirika zaidi na madawa haya ni vijana kuliko wazee. Hali hii imeonyeshwa hapa chini:

**Mf. 3.20: Wimbo Unaotahadharisha Vijana na Madawa ya Kulevya****KISAMBAA**

1. Mwenge utausia ee, mwenge utausia ee
2. Vijana wa leo ee, Mwenge utausia ee, tieke mphombe na bange
3. Unu mwenge uteusia ee, Mwenge wa uhulu ee
4. Kangi uzausia ee, tieke mphombe na bange

**KISWAHILI**

1. Mwenge unausia ee, mwenge unausia ee
2. Vijana wa leo ee, Mwenge unatusia ee, tuache pombe na bangi
3. Huu mwenge umeusia ee, Mwenge wa uhuru ee
4. Tena umeusia ee, tuache pombe na bangi

Katika nukuu ya wimbo hapo juu inabainika jinsi utendaji wa nyimbo unavyofanywa kwa minajili ya kuihofisha jamii juu ya madhara ya madawa ya kulevya, hususan pombe na bangi. Ingawa wasanii wanasema ‘**mwenge umeusia vijana waache pombe na bangi**’ ukweli ni kuwa wosia huo unatolewa na wasanii kwa niaba ya viongozi. Aidha, kitendo cha kutajwa kwa mwenge kinaonyesha kuwa wasanii walitaka kuikumbusha hadhira kuwa makusudio ya mbio za mwenge ni kuhamasisha jamii iachane na madawa ya kuleya.

Kando na wimbo huu kuna nyimbo nyingi zinazoimbwa kwenye muktadha wa mbio za mwenge ambazo hudhamiria kuelimisha jamii kwa njia ya kuiburudisha. Kwa mfano, wimbo ufuatao ambao uliimbwa katika kijiji cha Magoma wakati wa sherehe za mwenge za mwaka 2015. Katika wimo huu wasanii wanaonya jamii kuhusu rushwa, ubakaji na uhujumi uchumi:

**Mf. 3.21: Wimbo Unaokemea Rushwa, Ubakaji na Uhujumi Uchumi****KISAMBAA**

1. Huo mwenge ee ee ee mwenge uwo mwenge
2. Huo mwenge ee ee ee nauje umulike Tanzania
3. Huo mwenge ee, Mwenge uwo mwenge
4. Mwenge wetu wa uhuru, mulika wala rushwa Tanzania

**KISWAHILI**

1. Huo mwenge ee. mwenge huo mwenge
2. Mwenge wa uhuru, mulika wabakaji Tanzania
3. Huo mwenge e, mwenge uwo mwenge
4. Mwenge wa uhuru, mulika wahujumu Tanzania

Katika nukuu hii mambo yanayokemewa na wasanii ni rushwa, ubakaji na uhujumu uchumi. Kimsingi, mambo haya hayafai na ndio maana mwenge umetumiwa kama ishara ili kupaza sauti kwa wanajamii wenye tabia hizo. Kama ilivyokuwa katika mfano wa wimbo hapo juu mwenge ndio uliopewa jukumu la kuwamulika wala rushwa, wabakaji na wahujumi uchumi. Hii ina maana utendaji wa nyimbo za *mdumange* unatumika kama nyenzo kufichulia maovu na waovu. Tofauti na kampeni za uchaguzi ambazo hufanyika kila baada ya miaka mitano, mbio za mwenge na sherehe za sikukuu za wafanyakazi hufanyika kila mwaka. Hii inaonyesha kuwa, matukio ya sherehe za wafanyakazi na mbio za mwenge yanachukua nafasi kubwa katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*.

### **3.4 Hitimisho**

Katika sura hii tumeshughulikia miktadha ya kijamii na dhima yake katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Miktadha iliyochunguzwa imehusisha masuala anuai aliyobainishwa na watafitiwa na pia yaliyodhihirika kwenye dhamira za nyimbo za *mdumange*. Kulingana na mjadala wa sura hii imebainika kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* umeathiriwa na turathi simulizi, mtagusano wa kijamii na matukio ya sherehe au hafla za kijamii. Imeelezwa pia kuwa miktadha hii imechochea na kuathiri utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwa kuwa kwayo watafitiwa wameweza kubainisha chimbuko la nyimbo, mandhari, dhamira na washiriki wake. Katika sura ifuatayo mtafiti anachanganua matumizi ya mikakati ya lugha katika kuwasilisha ujumi wa nyimbo na ulimwengu wa Wasambaa.

## SURA YA NNE

### MITINDO YA LUGHA NA DHIMA YAKE KATIKA KUWASILISHA

#### UJUMBE KWA HADHIRA

#### 4.0 Utangulizi

Lugha ni nyenzo pekee ya mawasiliano miongoni mwa jamii za wanadamu (Fenner, 2019). Aidha, kulingana na Hymes (2007) lugha hubeba utamaduni, mila na desturi za wanajamii. Kutokana na hali hii, sura hii inajadili jinsi mitindo anuai ya lugha inatumika kufanikisha utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Mjadala uliopo kwenye sura hii umedhamiriwa kujibu swali la pili la utafiti huu lililouliza kuwa “Je, ni ipi dhima ya mitindo ya lugha katika kuwasilisha nyimbo na kusawiri maisha ya Wasambaa?”. Katika kutekeleza kusudio hili, matumizi ya vipengele mahsusi vya mitindo ya lugha yamejadiliwa.

#### 4.1 Mtindo wa Kuchanganya Misimbo

Katika jamii ya Wasambaa wa Lushoto, lugha kuu inayotumiwa ni Kisambaa. Aidha, Kiswahili ambacho ni lugha ya taifa pia hushirikishwa katika lugha ya Kisambaa. Hali hii imeathiri utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwani kwa kiwango kikubwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* hufanywa kwa kutumia lugha ya Kisambaa lakini baadhi ya wasanii hutumia pia lugha ya Kiswahili. Kwa ujumla, utendaji wa nyimbo za *mdumange* umehusisha matumizi ya lugha za namna tatu kwa pamoja: Kisambaa, Kiswahili na Kingereza. Utafiti huu umebaini kuwa Kisambaa kimetumika kwa kiwango kikubwa, kikifuatiwa na Kiswahili na Kingereza. Kati ya nyimbo tisini (90) zilizochunguzwa nyimbo sabini na tano (75) sawa na asilimia themanini na tatu nukta tatu (83.3%) ziliimbwa kwa Kisambaa. Kwa upande mwingine utafiti huu umebaini kuwa kati ya nyimbo tisini (90) zilizochunguzwa matumizi ya Kiswahili yamedhihirika katika nyimbo kumi na tano (15) ambayo ni sawa na asilimia kumi na

sita dukta saba (16.7%) ya nyimbo zote. Hatimaye, utafiti huu umegundua kuwa wasanii wa nyimbo za *mdumange* wanachanganya Kingereza katika utendaji wao ili kufikisha ujumbe kwa hadhira. Hata hivyo, matumizi ya Kingereza ni ya kiwango kidogo ikilinganishwa na ilivyo katika Kisambaa na Kiswahili. Kwa ufupi, utafiti huu umebaini kuwa kati ya nyimbo tisini (90) ni nyimbo nne (4) ambazo zimetumia msamiati na miundo ya lugha ya Kingereza. Idadi hii ni sawa na asilimia nne nukta nne (4.4%) ya nyimbo zote zilizochunguzwa na kuchambuliwa. Kwa ujumla, utafiti huu umebaini ruwaza za namna tatu za mtindo wa uchanganyaji misimbo. Ruwaza hizo ni kati ya Kisambaa na Kiswahili, Kisambaa na Kingereza na Kiswahili na Kingereza.

#### **4.1.1 Kisambaa na Kiswahili**

Ruwaza hii imejitokeza katika nyimbo zilizowasilishwa kwa lugha ya Kisambaa. Hata hivyo, kutokana na athari ya kiutendaji wasanii wamechanganya utendaji wao na Kiswahili. Miongoni mwa nyimbo zilizotumia mtindo huu ni wimbo wa **wenyeji wetu** kama ifuatavyo:

#### **Mf. 4.1: Wimbo ambapo Waimbaji wametumia Kisambaa na Kiswahili**

- i. Wenyeji wetu hapa Msamaka wote wake kwa waume
- ii. Wakubwa kwa wadogo mbiu ya mgambo imelia
- iii. Asiyekuwa na mwana leo aeleke jiwe
- iv. **Ngoma Kanyawana izaiza** Shauri na kikosi chake
- v. Chenye sifa mbalimbali
- vi. ee na mitindo ya kisasa **waume soi na kunu**

Nukuu hapo juu imedondolewa kutoka katika wimbo wenye beti tisa. Aidha, wimbo huu unahusu umuhimu wa kuhifadhi na kuenzi utamaduni wa Kisambaa, na mara nyingi huimbwa kwenye mikutano ya kisiasa hususan sherehe au hafla za mbio za mwenge. Katika wimbo huu mbinu ya kuchanganya Kiswahili na Kisambaa imetumika kuwatambulisha wasanii pamoja na kuikaribisha hadhira. Mbinu hii pia



imetumika ili kuvuta umakini na ushiriki wa hadhira ambayo kimsingi imechanganya wanaojua na wasiojua Kisambaa mahali pamoja. Kuwepo kwa hadhira ya wasiojua Kisambaa kumewafanya wasanii waanze kwa Kiswahili. Aidha, kwa sababu sehemu kubwa ya ujumbe uliwalenga Wasambaa, beti zote isipokuwa ubeti wa kwanza zimeimbwa kwa Kisambaa.

Pamoja na kuchanganya lugha ya Kisambaa na Kiswahili, wasanii wamehakikisha kuwa ujumbe wao unaifikia hadhira barabara. Hili limefanyika kwa kugawa matumizi ya lugha zote katika nafasi mbalimbali. Kwa mfano katika kipande cha kwanza cha mshororo wa tano msanii ametumia Kiswahili lakini pia amechopeka kitenzi cha Kisambaa, ambacho hakiwazuii hadhira kuelewa ujumbe wake. Msanii anasema **ngoma kanyawana izaiza** yaani ngoma inayowakanya (kuwaonya) watoto imewasili. Kwa upande mwingine mishororo mingine minne ya awali imeimbwa kwa Kiswahili.

Kwa upande mwingine, Kisambaa kimetumika kwa minajii ya kusisitiza kuwa ujumbe huu unawahusu Wasambaa zaidi. Lugha ya Kisambaa pia imetumika ili kutoa ilani kwa Wasambaa, kuwaalika na kuwataka washiriki katika uitikiaji na uchezaji. Hili linaonekana katika kipande cha pili cha mshororo wa mwisho ambapo msanii anasema **waume soi na kunu** yaani **jamani njooni huku**.

Nadharia ya Utendaji wa Maigizo inasisitiza kuwa utendaji wa kifasihi ni tukio hai na halisi ambalo linafungamana na hali halisi ya maisha ya jamii. Ni jambo gumu sana katika jamii ya leo kuona jamii ambayo inatumia lugha moja tu bila ya kuchanganya na lugha nyingine katika miktadha mbalimbali. Hii ni kwa sababu uhalisia katika jamii ni kwamba jamii zinaingiliana sana na kutegemeana katika mambo mbalimbali.

#### 4.1.2 Kiswahili na Kingereza

Mbali ya kuchanganya Kisambaa na Kiswahili, utendaji wa nyimbo za *mdumange* pia umehusisha mbinu ya kuchanganya Kiswahili na Kingereza. Matumizi haya yanapatikana katika wimbo wa **Chagua CCM** ulionukuliwa hapa chini:

**Mf. 4.2: Wimbo ambapo maneno ya Kiswahili na Kingereza yametumika**

1. Chagua CCM nambari wani Tanzania sote tunajua
2. Wanaoleta fitina na hata majungu CCM ndio baba yao
3. Na hata mwalimu Raisi Nyerere alisema
4. Viongozi bora watatoka chama mapinduzi

Katika nukuu hii, mtindo wa uchanganyaji msimbo unabainika kwenye mshororo wa kwanza ambapo msanii anasema ‘Chagua CCM nambari wani Tanzania sote tunajua’. Maneno “**nambari wani**” yametokana na lugha ya Kingereza (**Number One**). Hapa tunaona jinsi maneno ya Kingereza yalivyofanyiwa mabadiliko ya kiuandishi, lakini matamshi yamebaki vilevile. Katika muktadha huu, mbinu ya kuchanganya misimbo haijatumika kuwabagua wala kuwajumuisha watu wa kundi fulani, bali mbinu hii imetumika kumtambulisha msanii kuwa anajua lugha ya Kingereza, na kuisitiza ujumbe wa kukisifia chama cha CCM. Kwa ufupi, lugha za Kiswahili na Kingereza izimetumika ili kuonyesha hisia za kisiasa walizo nazo wasanii na hivyo kuishawishi hadhira pia iwe na hisia za namna hiyohiyo. Matumizi ya maneno “nambari wani” yanarejelewa na kufafanuliwa vizuri na msimbo wa kiutamaduni wa Nadharia ya Semiotiki ya Kijamii. Maneno haya yanatoka katika lugha ya Kiingereza ambapo inasadikika kuwa ni lugha ya watu waliostaarabika na kuendelea. Hivyo chama cha CCM nacho kinatajwa kuwa ni chama cha watu makini na chenye uwezo wa kuwaletea wananchi maendeleo endelevu kuliko vyama vingine.

### 4.1.3 Kisambaa na Kingereza

Kando na matumizi ya uchanganyaji Kisambaa na Kiswahili na pia Kiswahili na Kingereza, utendaji wa nyimbo za *mdumange* pia umefanywa kwa kuchanganya Kisambaa na Kingereza. Kimsingi, mbinu hii imejitokeza katika nyimbo zilizoimbwa kwa Kisambaa, lakini ili kuibua ujumi wa kifasihi wasanii wamechopeka maneno na miundo ya Kingereza. Kwa mfano:

#### Mf. 4.3: Wimbo ambapo maneno ya Kisambaa na Kingereza yametumika

##### KISAMBAA

1. N'teona **smol** nane
2. Aa ee n'teona **smol**
3. N'teona **smol** aa ee ee

##### KISWAHILI

1. Nimeona kitu kidogo jamani
2. Aa ee nimeona kitu kidogo sana
3. Nimeona kitu kidogo aa ee ee

Katika nukuu hii inabainika jinsi matumizi ya Kisambaa yamechanganywa na Kingereza. Neno 'small' ambalo katika lugha ya Kingereza hutumika kama kivumishi limepachikwa mahali pa mtendwa kwenye muundo wa sentensi ya Kisambaa. Aidha, ingawa matamshi ya neno hili yamebakia kuwa ya namna moja kati ya Kisambaa na Kingereza, ukweli ni kuwa katika uandishi linakuwa na miundo tofauti kwani sauti /a/ na /l/ zimedondoshwa katika Kisambaa na wakati huo huo sauti /o/ imeongezwa ili kufidia udondoshaji wa /a/ na /l/. Kulingana na maoni ya Mzee Shauri, 'smol' ni kitu kizuri. Kwa hiyo wimbo huu uliimbwa kwa minajili ya kusifia vitu vilivyoonekana kuwavutia wasanii.

Wimbo mwingine ambao umeimbwa kwa Kisambaa lakini kutokana na sababu za kijumi umechanganya na matumizi ya Kingereza ni **gangwe**. Katika wimbo huu Kingereza kimejitokeza ambapo msanii amechopeka neno 'taimu' kama ifuatavyo:

**Mf. 4.4: Wimbo ambapo maneno ya Kisambaa na Kingereza yametumika**

**KISAMBAA**

1. Hati ugangwe ugangwe
2. Ushezan'taimu na ngoma
3. Wene ng'wana kizibiti ng'wenye
4. Mphombe sio chai bwana

**KISWAHILI**

1. Ikiwa wewe ni jeuri ujeuri wako sio hapa
2. Usijenifanyia fujo katika ngoma
3. Tafadhali kijana jizuie mwenyewe
4. Kwani pombe sio chai

Katika nukuu hii Kisambaa kimechanganywa na Kingereza ili kunogesha utendaji.

Msanii katika mshororo wa pili anasema *Ushezan'taimu na ngoma*. Neno taimu limetokana na neno la Kingereza 'time' likiwa na maana ya wakati au muda. Licha ya kuwa kiuandishi neno hili limefanyiwa mabadiliko ili liweze kuandikika na kutamkika kwa urahisi hata maana yake ya asili imeumbwa upya. Katika Kingereza 'time' ni wakati au muda lakini katika wimbo huu neno hili limetumika kumaanisha fujo au ghasia.

Wasanii wa nyimbo za *mdumange* waliimba wimbo huu kuwaonya wanachama waliokuwa wamelewa wasijefanya fujo kwenye sherehe. Onyo la msanii ni aina fulani ya kejeli anayoitoa kwa wenzake waliolewa kuwa pombe si chai, ambayo lazima uinywe. Unaweza kuamua kuacha ukitaka.

Mtindo wa kuchanganya misimbo uliojadiliwa kwenye sehemu hii unaonyesha kuwa wasanii wa nyimbo za *mdumange* wamezaliwa na kukulia katika jamii yanye kiwango kikubwa cha wingi lugha. Matumizi ya wingi lugha yamehusisha lugha za Kiswahili, Kingereza na Kisambaa.. Kutokana na utafiti huu imebainika kuwa licha ya kuwako kwa kiwango kikubwa cha wingi lugha miongoni mwa lugha asili za Wasambaa (Kisambaa), Wambugu (Kimbugu) na Wapare (Kichasu), utendaji wa nyimbo hizi haujaathiriwa na lugha husika. Kwa maneno mengine, kutokana na utafiti huu imedhihirika kuwa hakuna matumizi ya Kichasu wala Kimbugu yaliyoonekana katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* badala yake lugha za Kisambaa, Kiswahili na

Kingereza ndio zimetumika. Aidha, utafiti huu pia umebaini kuwa kiwango cha uchanganyaji misimbo ya Kiswahili na Kisambaa ni kikubwa zaidi ikilinganishwa na Kiswahili na Kingereza, na Kisambaa Kingereza.

Matumizi ya lugha hizi yanathibitisha hoja iliyowahi kutolewa na mwanaNadharia ya Semiotiki ya kijamii (Eco, 1984) kuwa kulingana na majukumu yanayotekelezwa na lugha, matumizi yake katika jamii huweza kutokana na nguvu za kiitikadi zaidi kuliko kuzingatia idadi ya wajua lugha. Mtazamo huu unaelekeza katika hoja kuwa ingawa idadi kubwa ya Wasambaa hutumia Kisambaa katika mawasiliano yao ya kila siku, wakati wa utendaji wa nyimbo za *mdumange* wasanii hutumia pia Kiswahili na Kingereza kwa minajili ya kuonyesha kuwa wao wanajua lugha hizo na pia kwa sababu lugha hizo zimepewa hadhi ya juu na mamlaka zinazohusika.

#### **4.2 Mitindo ya Arudhi za Kishairi**

Kumekuwa na mielekeo anuai kuhusu dhana ya arudhi za kishairi na nafasi yake katika kupambaua ujumi wa kifasihi. Katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili mielekeo inayotambulika sana ni miwili: mwelekeo wa kimapokeo (Mayoka, 1986; Nasiri, 1972 na Abeid, 1991) kwa upande mmoja na mwelekeo wa kisasa (Kezilahabi, 1981; Senkoro, 1988 na Mulokozi, 2002) kwa upande mwingine. Mwelekeo wa kimapokeo ulielemea zaidi kwenye misingi ya fasihi andishi katika kubainisha vipashio vya arudhi za kishairi ilhali mwelekeo wa kisasa ulielemea kwenye misingi ya kifasihi simulizi.

Katika utafiti huu, ubainishaji wa arudhi za kishairi zilizotumiwa na wasanii wa nyimbo za *mdumange* umefanyika kwa kutumia misingi ya utendaji wa fasihi simulizi. Mkakati huu umefanywa ili kuepuka dosari za kiutendaji zilizosababishwa na wanamapokeo. Kwa mfano, kulingana na wanamapokeo dhana mbalimbali za

arudhi za kishairi kama vile mshororo, ubeti, na kibwagizo zimefasiiwa kama ifuatavyo:

- (i) Mshororo ni vifungu vya maneno vinavyojenga beti za wimbo.
- (ii) Ubeti ni kifungu cha maneno au mkusanyiko wa mishororo kadhaa unaojitosheleza kimaana. Wimbo unaweza kuwa na ubeti mmoja au zaidi.
- (iii) Kibwagizo ni sehemu ya wimbo inayoimbwa kama kiitikio katika uwasilishaji wa nyimbo.

Kimsingi, fasili zilizotolewa hapo juu zinaelekea kujikita mno katika nyimbo zilizoandikwa kuliko ambazo hazijaandikwa. Si rahisi kujua ukomo wa mshororo wala ubeti wa wimbo unaowasilishwa kwa njia ya mdomo. Ili kubaini mchango wa arudhi hizi katika utendaji wa nyimbo, utafiti huu umezingatia kuwa nyimbo za *mdumange* zinatungwa papo kwa papo wakati wa uwasilishaji mbele ya hadhira. Kwa hivyo hata ubainishaji wa arudhi hizi umezingatia uhusiano kati ya fanani na hadhira wakati wa kuwasilisha nyimbo kwa hadhira.

Kwa kuzingatia hali halisi ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* dhana hizi zimefasiliwa kwa kuegemezwa kwenye misingi ya utendaji wa fasihi simulizi ambayo ni ushirikiano unaodhihirika kati ya fanani na hadhira. Ushirikiano huo unaifanya hadhira iwasiliane na wasanii kwa njia ya kiupokezanaji zamu. Kwa kuzingatia muktadha huu dhana hizi zimefasiliwa kama ifuatavyo:

- (i) Mishororo ni vifungu vya maneno vinavyotamkwa na ama MK au WK kama tamko moja bila kurejelewa au kukaririwa.
- (ii) Ubeti ni kifungu cha maneno au mkusanyiko wa mishororo kadhaa inayodhihirika kabla au baada ya upokezanaji zamu baina ya MK na WK.

(iii) Kibwagizo ni sehemu ya wimbo inayorudiwarudiwa na kupokezanwa kati ya fanani na hadhira wakati wa kuwasilisha nyimbo.

Kwa kuzingatia misingi hii aina mbalimbali za arudhi za kishairi zimepambanuliwa hususan vina na mizani, muundo wa mishororo, beti na kibwagizo kama ifuatavyo:

#### 4.2.1 Vina na Mizani

Mojawapo ya vipengele vinavyotumiwa na wasanii kuwasilisha ujumbe kwa hadhira ni matumizi ya vipengele mbalimbali vya kisanaa vinavyoundwa kwa kutumia kaida za ujumi wa kishairi. Ujumi huo umejumuishia matumizi ya arudhi za kishairi hususan mpangilio wa sauti ili kuunda mishororo, beti, vina, mizani na kibwagizo. Utafiti huu umebaini kuwa kwa kiwango kikubwa nyimbo za *mdumange* hazina urari wa vina na mizani. Aidha, nyimbo chache zenye urari wa vina na mizani zinatumiwa kuibua mapigo ya kimuziki zaidi ikilinganishwa na ambazo hazina urari huo. Ili kujadili athari ya mitindo ya arudhi za kishairi, sehemu ifuatayo imeelezea kwa kina jinsi fanani na hadhira hutumia mitindo hii katika utendaji wao.

Mizani ni idadi ya silabi zinazopatikana katika mishororo ya nyimbo. Aidha, katika muktadha wa utendaji wa nyimbo za *mdumange* vina ni silabi za mwisho au za kati katika mishororo ya nyimbo. Utafiti huu umebaini kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* unatawaliwa na ruwaza mbili za vina na mizani katika mishororo na beti:

(i) vina na mizani tofauti na (ii) vina na mizani mfanano. Mtindo wa vina na mizani tofauti umedhihirika katika nyimbo ambazo mishororo yake inatofautiana urefu.

Mfano wa nyimbo za *mdumange* zenye vina na mizani tofauti ni kama vile **uteasha wanao** ulionukuliwa hapa chini:

**Mf. 4.5: Wimbo wenye Vina na Mizani Tofauti****KISAMBAA**

1. Uteasha wanao Zaina Maisha ya Bongo ni mabaya
2. Kuna kufa weangu Zumiai wa lelo tije dumange (I)
3. Kuna kufa wa baba Zumia wa lelo tije dumange (II)

**KISWAHILI**

1. Umeacha wanao Zaina Maisha ya Bongo ni mabaya
2. Kuna wakati utafika tutakufa jamani Leo itikieni tufurahie dumange (I)
3. Kuna wakati utafika tutakufa Kaka itikieni tufurahie dumange (II)

Katika mfano hapo juu, maneno **Uteasha wanao Zaina, Maisha ya Bongo ni mabaya** ndiyo huunda wa kwanza. Wakati wa utendaji, kila mshororo hurudiwa mara mbili na fanani pamoja na hadhira. Aidha, tukichunguza kwa makini wimbo huu tunabaini kuwa idadi ya silabi (mizani) zilizomo katika kila mshororo zinatofautiana. Mshororo wa kwanza una silabi ishirini **U-te-a-sha-wa-na-o-Za-i-na, Ma-i-sha-ya-Bo-ngo-ni-ma-ba-ya** na mshororo wa pili ambao ni **Kuna kufa weangu Zumiai wa lelo tije dumange** una silabi kumi na tisa. Hii ina maana kuwa wimbo huu una mizani zinazobadilikabadilika kutoka mshororo mmoja hadi mwingine. Kadhalika, wimbo huu hauna vina vya katikati, bali una vina vya mwisho peke yake, na vina hivyo si vya namna moja.

Mtindo wa vina na mizani tofauti pia unapatikana katika wimbo wa **Salamu twazituma** ulioimbwa na kikundi cha *mdumange* wa Shauri tarehe 28/04/2016 kwenye hafla za mbio za mwenge katika kijiji cha Kivilicha:

**Mf. 4.6: Wimbo wenye vina na mizani Tofauti**

1. Salam twazituma kwa wazazi wetu walioko mkoani Tanga
2. Wilaya yetu ya Lushoto
3. Tudumishe kilimo cha mbogamboga na mazao yetu
4. Mbalimbali pamoja na misitu yetu
5. Tualinde mazingira yetu
6. Tunawapongeza wananchi wote walioko mkoani Tanga
7. Kwa kazi wanazozifanya viwandani hata mashambani

Kama inavyoonekana katika wimbo huu MK ametumia vina vinavyobadilika katika mshororo wa kwanza, pili sita, na wa saba. Katika mshororo wa kwanza na wa sita



kina kinaishia na silabi [-nga] ilhali kina cha mshororo wa pili na saba ni [-to] na [ni] mutawalia. Mtindo wa kutumia vina vinavyobadilika kutoka mshororo mmoja hadi mwingine umezuliwa na ujumbe wa wimbo ambao unabainisha eneo ambalo wimbo huu umeimbwa pamoja na kutambulisha jografia ya washiriki.

Kulingana na wimbo huu washiriki wa nyimbo za *mdumange* wanatokea mkoa wa Tanga, Wilaya ya Lushoto. Pia, katika wimbo huu, viwandani na shambani kumetajwa ili kubainisha sehemu au vyanzo vikuu vya uchumi miongoni mwa Wasambaa.

Kwa upande mwingine utendaji wa nyimbo za *mdumange* unaambatana na matumizi ya mtindo wa vina na mizani mfanano. Aina hii ya mtindo imeshamiri katika nyimbo ambazo zina beti zenye mishororo yenye idadi sawa ya mizani na mpangilio wa vina unaofanana kutoka mshororo mmoja hadi mwingine.

Katika wimbo ulionukuliwa kwenye mfano namba 4.6 mtindo huu umetumika mno hasa katika mshororo wa tatu, nne na wa tano. Kina kilichotumika katika mishororo yote hii ni [-tu]. Aidha, mtindo wa vina mfanano umetokana na matumizi ya neno //yetu// lililotumiwa na msanii kwa minajili ya kuonyesha sanaa ya umbuji wa lugha. Kadhalika, neno //yetu// limetumika kuonyesha dhamira ya umiliki wa rasilimali za misitu, mazingira na uchumi. Kulingana na wimbo huu, rasilimali hizi zinamilikiwa na jamii nzima, na kwamba zinahitaji kulindwa na kuhifadhiwa na watu wote ili ziwafae wanajamii wote kwa ujumla.

Kando na kuibua dhamira ya umiliki wa rasilimali, matumizi ya vina mfanano katika wimbo huu pia yamezua athari ya mapigo ya sauti za kimuziki. Wakati wa utendaji wa wimbo huu, MK na WK hurudiarudia mishororo ya wimbo. Kutokana na athari ya

utendaji wa namna hiyo, hadhira huelewa kwa haraka na hushiriki pamoja na MK na WK katika kuimba mishororo ya wimbo, kutegemea maelekezo ya MK.

Ingawa utafiti huu umebaini kuwa kwa kiwango kikubwa nyimbo za *mdumange* hazina urari wa vina na mizani, yafaa kudokeza kuwa hali ya kukosekana kwa urari wa vina mizani inachochewa na matumizi ya ala za muziki kama vile ngoma, manyanga na filimbi. Kadhalika, kwa mujibu wa mahojiano kati ya mtafiti na Wasambaa, na pia kutokana na ushahidi wa data nyanjani ingawa nyimbo nyingi hazina urari wa vina na mizani nyimbo zinaimbika na fanani na hadhira huimba kwa kupokezana kutegemea mpangilio wa mapigo ya kimuziki. Maelezo haya yanaonyesha kuwa, mbali na uimbaji wa fanani na hadhira utendaji wa nyimbo unatekelezwa zaidi kwa kutumia ala nyingine za mitindo ya viziada lugha, hususan uchezaji na muziki. Maelezo ya kina kuhusu mitindo ya viziada lugha yametolewa katika sura ya tano.

#### **4.2.2 Mshororo, Ubeti na Kibwagizo**

Ufafanuzi wa dhana husika katika utafiti huu umetuwezesha kubaini mitindo ya matumizi ya mishororo, beti na kibwagizo. Kimsingi, utendaji wa nyimbo za *mdumange* unaonyesha kutawaliwa na ushirikiano kati ya fanani na hadhira. Fanani na hadhira hushirikiana na kupokezana katika kuimba sehemu mbalimbali za wimbo hususan mishororo, beti na kibwagizo. Katika utafiti huu imebainika kuwa mishororo, beti na kibwagizo imewasaidia fanani na hadhira kuimba kwa njia ya kiupokezanaji zamu. Aidha, upokezanaji zamu hutokea kati ya makundi mbalimbali ya wanaoshiriki utendaji wa nyimbo. Kadhalika, utafiti huu umebaini kuwa kuna aina mbili za mitindo ya kiupokezanaji zamu inayodhihirika ambayo ni:

- (i) Upokezanaji zamu kati ya mwimbaji mkuu mmoja na waitikaji

(ii) Upokezanaji zamu kati ya waimbaji wakuu wawili na waitikiaji

#### 4.2.2.1 Mwimbaji Mkuu Mmoja na Waitikiaji

Aina hii ya uimbaji huhusisha urudiaji wa vipashio au dhamira kuu mara kadhaa miongoni mwa fanani na hadhira. Aidha, katika aina hii ya uimbaji, MK huanza utendaji kwa kuimba ubeti mzima wa wimbo kisha WK huitikia ama kwa kukariri maneno yaleyale yaliyotamkwa na MK au hutumia maneno tofauti kabisa. Maelezo haya yanaonyesha kuwa kuna aina mbili za uimbaji huu. Kuna uimbaji ambao beti zinazoimbwa na MK hufanana kabisa na beti zinazoitikiwa na WK. Kadhalika, kuna uimbaji ambao beti zinazoimbwa na MK hutofautiana na beti zinazoimbwa na WK wakati wa kuitikia. Katika aina ya kwanza, hali ya upokezanaji zamu baina ya fanani na hadhira hutawala uimbaji lakini hakuna mabadiliko yoyote yanayotokea katika beti za wimbo. Hali hii inabainika waziwazi kwenye wimbo ufuatao:

**Mf. 4.7: Wimbo ambapo waimbaji wametumia beti kuunda kibwagizo au kiitikio**  
**34. Wanafunzi**

#### KISAMBAA

1. Wanaashule waekei wanaashule
2. Wakina Maumba wazashungighwa
3. Chimanya wanaashule (I)
4. Wanaashule waekei wanaashule
5. Viongozi wengi wazashungighwa
6. Chimanya wanaashule (II)
7. Wanaadodo , waekei wanaadodo
8. Hata babu Sea azashungighwa
9. Chimanya wanaashule (III)

#### KISWAHILI

1. Wanafunzi waacheni wanafunzi
2. Wakina Maumba wamefungwa jela
3. Ni kwa ajili ya wanafunzi (I)
4. Wanafunzi waacheni wanafunzi
5. Viongozi wengi wamefungwa jela
6. Ni kwa ajili ya wanafunzi (II)
7. Watoto wadogo waacheni watoto wadogo
8. Hata babu Sea amefungwa jela
9. Ni kwa ajili ya wanafunzi (III)

Nukuu ya wimbo hapo juu inaonyesha aina ya mtindo wa uimbaji unaotumia beti kuunda kibwagizo au kiitikio cha wimbo. Kimuundo wimbo huu una beti tatu, na kila ubeti unaundwa na mishororo mitatu. Kiutendaji, wimbo huu huimbwa kwa njia ya upokezanaji zamu wa beti baina ya fanani na hadhira. Wakati wa kuimba wimbo huu, kila mshororo hurudiwa mara mbili, na baada ya MK kumaliza kuimba ubeti mmoja WK huitikia kwa kufuatishia maneno yaleyale yaliyotumiwa na MK. Katika muundo

wa namna hii tunaweza kusema kuwa ama wimbo huu hauna kibwagizo au wimbo mzima uliimbwa kama sehemu ya kibwagizo kwa kuwa kila kifungu kinachounda ubeti kwanza kiliimbwa na MK kama ubeti wa wimbo na pili kiliimbwa na WK kama kiitikio.

Kwa upande mwingine, utendaji wa nyimbo za *mdumange* pia unahusisha muundo wa upokezanaji zamu kati ya fanani na hadhira ambapo beti zinazoimbwa na MK hutofautiana na kiitikio cha WK. Aina hii ya utendaji haina kiwango kikubwa cha urudiaji wa mishororo wala beti kwa kuwa kila mara MK anapomaliza kuimba ubeti maalum, WK hawarejelei ubeti huo tena bali wao wanaitikia kwa kutumia ubeti maalum. Ubeti huu unaotumiwa na WK mara zote na ambao haubadiliki toka mwanzo hadi mwisho ndio huwa kibwagizo cha wimbo kama inavyoonyeshwa hapa chini:

**Mf. 4.8: Wimbo unaoonyesha jozi ya kianzio (MK) na kiitikio (WK)**

**KISAMBAA**

**MK:** Ni mdodo Tate Shauri ni mdodo  
**WK:** Aa uwa uwaa  
**MK:** Tate Shauri ni mdodo  
**WK:** Aa uwa uwaa  
**MK:** Ni mdodo  
**WK:** Aa uwa uwaa  
**MK:** Hati n'waana ana nao

**KISWAHILI**

**MK:** Ni mdogo baba Shauri ni mdogo  
**WK:** Aa uwa uwaa  
**MK:** Baba Shauri ni mdogo  
**WK:** Aa uwa uwaa  
**MK:** Ni mdogo  
**WK:** Aaa uwa uwaa  
**MK:** Kama ni watoto anao

Kama inavyoonekana katika mfano huu, maneno yanayotumiwa na MK ni tofauti na yanayotamkwa na WK. Aidha, kimuundo wimbo ulionukuliwa hapo juu una mishororo ishirini ambapo mishororo kumi iliimbwa na MK ilhali mishororo kumi iliimbwa na WK (Rejea wimbo mzima katika kiambatisho). Kadhalika, beti za wimbo huu zinaundwa na jozi ya kianzio cha MK pamoja na kiitikio cha WK. Kwa hiyo, wimbo huu una beti kumi zinazohusisha upokezanaji zamu baina ya MK na WK.

Kimsingi, katika uimbaji wa namna hii WK hawarejelei maneno yaliyotamkwa na MK, bali maneno yao ni kama yanaendeleza ubeti ulioanzishwa hapo kabla. Muundo huu wa nyimbo za *mdumange* hauruhusu takriri ya maneno baina ya fanani na hadhira, bali takriri hutokea ambapo kila mmoja huwa na maneno yake.

Aidha, katika mfano uliotolewa hapo juu, wakati MK anao uhuru wa kubadili maudhui yatokanayo na beti zake, kwa upande mwingine WK hawako huru kwani maneno yao ni ya namna moja tu. Katika mfano hapo juu utikiaji wa WK umetumia maneno **Aa uwa uwaa**. Maneno haya yameundwa kitanakali za sauti na dhima yake kubwa ni kuunga mkono kilichosemwa na MK. Hapa ndipo mawazo ya Nadharia ya Utendaji wa Kimaigizo hasa yanayoelezwa na Rappaport (1968); Foley (1988; 1995 na 2002) pamoja na Austin (1965) wanaposhadidia kuwa ili utendaji wa kisanaa uweze kufanikisha lengo lake ni lazima uishirikishe hadhira na fanani. Hali hii ndiyo imetawala utendaji wa nyimbo za *mdumange* ambapo ushirikiano baina ya fanani na hadhira ni wa kiwango kikubwa. Katika mfano ulionukuiwa hapo juu, fanani anaanzisha wimbo lakini yale anayoyasema yanaungwa mkono na hadhira kitu ambacho kinaufanya wimbo husika kuwa ni tukio hai na halisi.

Kando na upokezanaji zamu unaotokea katika beti na mishororo, aina nyingine upokezanaji zamu hudhihirika katika kibwagizo. Utendaji wa nyimbo za *mdumange* unatumia vibwagizo ama wakati wa kubadilisha wimbo au wakati wa kuhitimisha utendaji. Kama ilivyo kwa ubadilishanaji zamu wa beti na mishororo, MK ana uhuru mwingi kwenye upokezanaji zamu wa kibwagizo. Wakati wa uimbaji, maneno yanayotamkwa na MK yanaweza kubadilikabadilika kutegemea dhamira anayoikuza na kuiendeleza, lakini maneno yanayotamkwa na WK hayabadiliki. Licha ya mabadiliko hayo, maneno ya MK pamoja na maneno ya WK huunda kibwagizo cha

wimbo husika. Kwa mfano wimbo ufuatao unaonyesha jinsi ushrikiano kati ya fanani na hadhira unavyochochea uundwaji wa kibwagizo cha wimbo:

**Mf. 4.9: Wimbo unaonyesha kibwagizo wakati wa utendaji**

**KISAMBAA**

**MK:** E hayaa hayaa ee  
 Mounti Usambara zumia kagoma  
 Angwe kuna ngoma hayaa  
 Mounti Usambara Mzantamia  
 Nshezaiva Mweia oiye  
**WK:** Nshezaiva mweiyaae  
 Eooe nane nshezaiva mweiyaae  
**MK:** Angwe senionge nini iwe mame  
 Mwenye mbui naaonge  
 Nshezaiva mweia wene ng'wana  
 Mzantamia shazaiva mweia oiee  
**WK:** Nshezaiva mweiyaae  
 Eooe nane nshezaiva mweiyaae

**KISWAHILI**

**MK:** E hayaa hayaa ee  
 Mouti Usambara itikieni ngoma  
 Eti kuna ngoma haya  
 Mouti Usambara Mmenifurahisha  
 Nisijekusikia anayelia  
**WK:** Nisijekusikia anayelia  
 Leo jamani nisijekusikia anayelia  
**MK:** Eti sina la kusema wewe mama  
 Mwenye tatizo na aliseme  
 Nisijekusikia anayelia wewe mtoto  
 Mmenifurahishanisijekusikia anayelia  
**WK:** Nisijekusikia anayelia  
 Leo jamani nisijekusikia anayelia

Mfano hapo juu ni kibwagizo cha wimbo ambacho hutumiwa na wasanii wa nyimbo za *mdumange* kwa minajili ya kuburudisha hadhira yao. Kama inavyoonekana maneno ya MK hubadilika kutegemea na matakwa ya utendaji ilhali maneno ya WK hayabadiliki. Kwa njia hii, upokezanaji zamu wa kibwagizo huwa kama taswira kuu au wazo kuu la wimbo husika. Mbali na kusisitiza ujumbe, upokezanaji zamu wa kibwagizo humpatia fursa MK hufanya ufaraguzi wa namna mbalimbali kadri atakavyo kwa minajili ya kuzua hisia za furaha, shangwe na nderemo katika sherehe za utendaji wa nyimbo za *mdumange*.

Kupitia wimbo ulionukuliwa hapo juu urudiaji wa maneno “*n'shezaiva mweiaa ee ee*” unaonekana bayana na athari yake ilionekana wazi wazi wakati wa ushuhudiaji ri kwa hadhira. Hadhira inapata wasaa wa kuzingatia maudhui ya utendaji kupitia mkakati wa kiupokezanaji zamu wa kibwagizo pamoja na mkakati wa uradidi. Kupitia utendaji wa namna hii utafiti huu unatoa hoja kuwa katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* jukumu la MK sio tu kuanzisha nyimbo na kutambulisha hatua

mbalimbali za utendaji, bali pia MK anawajibika kufanya mabadiliko mbalimbali wakati wa utendaji ili kuufanya utendaji uwe hai, na wa kuvutia zaidi.

Hivyo, mbinu ya upokezanaji zamu wa beti na kibwagizo huonyesha kuwa kiutendaji fanani wa nyimbo za *mdumange* anayo mamlaka ya juu zaidi ikilinganishwa na mamlaka ya chini ya hadhira. Mamlaka aliyonayo MK yanamuwezesha kuingiza kitushi chochote katika wimbo kama vile kumtaja yeyote miongoni mwa watu wanaoshiriki utendaji. Katika mfano uliotolewa, tumedondoa tu sehemu ndogo ambapo Mzee Shauri ndiye aliyetajwa na kusifiwa na waimbaji. Kadhalika, MK ndiye mwenye mamlaka ya kuamua muda na namna ya kuhitimisha/kukomesha uimbaji kwani anaweza kuanzisha na kuukatisha wimbo muda wowote.

#### **4.2.2.2 Waimbaji Wakuu Wawili na Waitikiaji**

Ingawa kwa kiwango kikubwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* huwa na muimbaji mkuu mmoja pamoja na waitikiaji wengi kuna wakati utendaji huo huwahusisha waimbaji wakuu kwa wakati mmoja. Kila mmoja kati ya waimbaji (wasanii) hao huanzisha wimbo kwa nafasi yake, huku akiitikiwa na hadhira. Msanii mmoja anapomaliza kutongoa wimbo/ubeti wake, hadhira huitikia. Kisha inafuata zamu ya msanii mwingine kuimba kwa njia ya kujibu au kuendeleza dhamira au wazo lililoanzishwa na msanii wa kwanza. Kama ilivyokuwa kwa msanii wa kwanza, hadhira huitikia utendaji wa msanii wa pili mara anapomaliza kutongoa ubeti wake. Waimbaji wote wawili wanashirikiana kuimba wimbo mmoja kwa nyakati tofautitofauti huku kila mmoja akiitikiwa na hadhira.

Hali hii ya uimbaji wa namna hii imeathiri utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwa kuwa upokezanaji zamu unaopatikana huwa kama aina maalum ya uigizaji wa tabia za wahusika wa kidrama. Aidha, mtindo huu huchochea ushiriki wa hadhira kwa

kiwango kikubwa kuliko ilivyo wakati wa kutumia muimbaji mkuu mmoja peke yake.

Athari ya uimbaji wa namna hii inabainika waziwazi katika wimbo ufuatao:

**Mf. 4.10: Wimbo unaoimbwa na waimbaji wakuu wawili**

**WEWE MWALI (A)**

**WEWE MWALI (B)**

**MK 1:** Iwe ng’wai utende na ishima  
n’kughulie tenge jaimia  
Aee n’kughulie tenge jaimi

**MK 2:** Iwe Juma utende na ishima  
tikuighae Boma kwe vinyange  
Aee tikuighae Boma kwe vinyange

**WK:** Iwe ng’wai utende na ishima  
n’kughulie tenge jaimia  
Aee n’kughulie tenge jaimi

**WK:** Iwe Juma utende na ishima  
tikuighae Boma kwe vinyange  
Aee tikuighae Boma kwe vinyange

Wimbo ulionukuliwa hapo juu una sehemu kuu mbili (A) na (B). Sehemu A iliimbwa na msanii aliyemnasihwa mwali awe na tabia njema na B iliimbwa na msanii mwingine aliyeigiza uhusika wa mwali. Katika mifano hii, tunaona jinsi MK 1 anavyotoa nasaha zinazosisitiza utii, adabu na heshima kwa bibi harusi, baada ya washiriki kumaliza kuitikia anaibuka mshiriki mmoja na kumjibu MK 1. Huyu ni sawa na MK 2 kwa kuwa anaimba kwa niaba ya bibi harusi na anasisitiza kuwa umuhimu wa adabu, nidhamu na heshima si kwa bibi harusi peke yake bali ni kwa watu wote akiwemo MK 1.

Kupitia mfano huu, nguvu ya utendaji wa kiupokezanaji zamu inaonekana kutawala hisia za washiriki wa nyimbo za *mdumange*. Tunapochunguza wimbo huu, tunapata kufahamu kuwa muimbaji mkuu wa kwanza ni mwanaume ambaye katika wimbo huu anaitwa Juma. Pia ‘Boma’ ni jina la mahali ambapo harusi ilifanyikia. Mawazo ya Nadharia ya Utengaji wa Maigizo yanatufanya tuelewe kuwa kitendo cha kutaja jina ya mshiriki pamoja na jina la mahali harusi imefanyikia kinaufanya utendaji wa nyimbo za *mdumange* uwe hai zaidi kuliko kama nyimbo husika zingewasilishwa kwa njia ya maandishi.



Ushirikiano kati ya waimbaji wakuu wawili na waitikiaji pia umedokezwa na namna waimbaji wanavyowashurutisha fanani kufanya mambo mahsusu ya kiutendaji. Katika hali hii hakuna waimbaji wawili wanaoonekana dhahiri bali kunakuwa na kauli mbili au semi zinazojibizana. Kauli moja inatoa maelekezo na kauli au sauti nyingine inatekeleza amri husika. Mbinu hii tumeuita mbinu ya kidialojia kwa kuwa inahusisha majibizano ya washiriki kama inavyoonekana katika wimbo ufuatao:

**Mf. 4.11: Wimbo unaotendwa Kidialojia**

**MK:** Neja ng'wai toa nkeeghee n'kubendui hadodo

**WK:** Aee n'kubendui hadodo

**Mame mwali:** (anapiga vigelegele)

Nukuu iliyoonyeshwa katika mfano namba 4.11 inabainisha wazi kuwa utendaji wa kidialojia umedhihirika kutokana na jinsi MK na WK wanavyomshurutisha mame mwali apige vigelegele na vilevile kutokana na mame mwali anavyotekeleza amri hii. Kwa upande mwingine, MK na WK wanamuahidi tuzo mame mwali kuwa endapo atapiga vigelegele watammegea. Tuzo yenyewe imewasilishwa kwa kutumia lugha ya kisitiari. Msanii anasema '**N'kubenduie hadodo**' akiwa na maana nikumegee kidogo, yaani wamchezee mame mwali kiasi. Kwa ujumla, utendaji unaotumia miundo ya kidialojia umesaidia kuzifanya nyimbo za *mdumange* ziifurahishe hadhira na pia umemsaidia msanii kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Aidha, aina hii ya muundo inaonyesha kuwa kwa kiwango kikubwa utunzi na uwasilishwaji wa nyimbo za *mdumange* unasisitiza umoja, ushirikiano na mshikamano wa washiriki wote, akiwemo fanani na hadhira. Finnegan (1970) anaeleza kuwa utendaji ni uti wa mgogo wa fasihi simulizi ya Kiafrika ambapo hadhira huweza kushiriki kwa namna mbalimbali ikiwemo kupiga makofi, kuuliza maswali, na kupiga vigelegele. Hivyo, kitendo cha mama mwenye mwali (mame mwali) kupiga vigelegele ni ithibati tosha kuwa utendaji katika nyimbo za *mdumange* ni shirikishi.

### 4.3 Mtindo wa Mianza na Miisho ya Kifomula

Fomula ni kipengele cha kisanaa ambacho kimetumika kwa muda mrefu katika fasihi simulizi. Kwa mara ya kwanza Nadharia ya fomula simulizi ilibuniwa na Miliman Pary pamoja na Lord (1960). Kwa mujibu wa Parry na Lord matumizi ya fomula simulizi katika fasihi simulizi kama vile tendi ni ishara kuwa fasihi hiyo imetokana na jadi simulizi. Kadhalika, wataalamu hawa wanasisitiza kuwa fomula hizo ni ushahidi kuwa watunzi wake walitunga sanaa husika kwa njia ya kukariri. Kimsingi, Nadharia ya fomula simulizi iliyoasisiwa na Parry na baadaye ikaendelezwa na Lord haikuzingatia ubunifu wa fanani na hadhira katika kuzalisha tungo mpya za kifasihi. Tofauti na mtazamo huu, utafiti huu umebaini kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* umehusisha matumizi ya fomula maalum zinazotumika wakati wa kuanza, kuhitimisha na kubadilisha nyimbo wakati wa utendaji. Fomula hizo zimeonyesha kuwa utendaji wa nyimbo umesheheni ujumi wa namna mbalimbali. Katika sehemu ifuatayo, mifano maridhawa imetolewa kwa kila aina ya fomula na matumizi yake katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* yamejadiliwa.

#### 4.3.1 Fomula za Ufunguzi

Wasanii wa nyimbo za *mdumange* hutumia mbinu mbalimbali kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Mojawapo ya mbinu hizo ni matumizi ya fomula maalum wakati wa kuanza uwasilishaji wa nyimbo. Utafiti huu umegundua kuwa wakati wa kuanza uimbaji wasanii hutunga nyimbo zenye muundo wa maombi au sala. Kuna sala zilizojengwa juu ya imani ya dini za Kijadi na kuna sala zilizojengwa juu ya imani ya dini za Ukristo na Uislamu. Nyimbo zifuatazo zinadhihirisha bayana jinsi fomula za ufunguzi zinajengwa kwa kutumia itikadi dini za Kijadi, Kiislamu na Kikristo:

**Mf. 4.12: Mianza ya Kifomula (Dua)****KISAMBAA**

**MK:** Tamba, tamba, tiase nkoba tiase  
muungu mzimu wa Sheuta  
neugone ntongo

**WK:** Tambaa , tiase nkoba tiase  
muungu

**MK:** Mzimu ee kagone ee

**WK:** Eeeee

**MK:** Uja wa Sheuta neugone ntongo

**WK:** Tambaa, tiase nkoba tiase  
muungu

**MK:** Mzimu ee kagone

**WK:** Eeeee

**KISWAHILI**

**MK:** Tunaomba tukiamini imani ya tunguli  
na miungu, mzimu wa Sheuta ulale  
salama

**WK:** Tunaomba tukiamini tunguli na  
miungu

**MK:** Mzimu ee ulale ee

**WK:** Eee ee ee

**MK:** Wa Sheuta ulale salama

**WK:** Tunaomba tukiamini tunguli na  
miungu

**MK:** Mzimu ee ulale

**WK:** Eeeee

Nukuu hapo juu ni mfano wa wimbo ulioimbwa na Mama Bilali pamoja na kikundi chake cha mdumange (kutoka kijiji cha Soni) wakati wa hafla za uchaguzi mkuu Oktoba mwaka 2015. Katika nukuu hii fomula zitokanazo na imani ya dini ya Kijadi zinadhihirika. Aidha, kupitia matumizi ya fomula hizi itikadi ya Wasambaa kuhusu mizimu na dini ya Kijadi inabainika waziwazi. Katika jamii ya Wasambaa, Sheuta ndiye muasisi wa jamii hiyo na kwamba hata ingawa alikufa zamani sana wanajamii wanapaswa kumuomba na kumtegemea katika kuleta neema na kuwaondolea balaa. Ndiyo maana hata katika kuanza mambo yao kama vile uimbaji wa nyimbo za *mdumange* wanamtaja na kumsifia.

Kutajwa na kusifiwa kwa mzimu wa Sheuta kunasisitiza dhamira ya umoja na ushirikiano baina ya watu walio hai na waliokufa. Kwa ujumla, fomula za sala zilizoainishwa zinatumiwa kutambulisha hatua ya awali ya utendaji wa nyimbo, kuhamasisha umoja na undugu na kuchochea ushiriki wa hadhira. Fomula hizi zinatumiwa tu wakati wa kuanza utendaji kwa kuwa Wasambaa wanaamini kuwa utendaji unafanikiwa endapo tu tukio la utendaji linahamasisha kiwango kikubwa cha ushiriki wa hadhira.

Kando na fomula zilizoundwa kwa kutumia dini ya Kijadi, wasanii wa nyimbo za *mdumange* pia wanatumia miundo ya fomula za sala au maombi yatokanayo na imani ya dini za Kiislamu na Kikristo. Katika fomula za namna hii, mzimu wa Sheuta hautajwi wala kusifiwa badala yake wasanii wanamtukuza na kumuomba Mungu kulingana na imani za dini zao. Fomula za maombi ya sala za dini ya Kijadi hutumika kwenye hafla za siasa na harusi ilhali fomula za dini za Ukristo na Uislamu hutumika katika hafla za kisiasa na harusi. Kamwe fomula hizi hazitumika kwenye sherehe za harusi.

**Mf. 4.13: Mianza ya Kifomula (Dua ya Dini ya Kiislamu na Kikristo)**

1. Sisi tukianza ngoma, Jambo la kwanza
2. ni lazima tumuombe Mungu
3. Kwa jinae la babae, Na la mwana, Na la roho mutakatifu
4. Wale ndugu zetu islamu, E ndugu zetu islamu ‘Swalie mtume

Nukuu hii inaonyesha miundo ya fomula za sala na maombi zilizojengwa juu ya misingi ya dini za Kikristo na Kiislamu. Aidha, katika nukuu hii msanii anaeleza bayana kuwa ni desturi ya wasanii kuanza utendaji wao kwa kuomba au kusali kwanza. Lengo la utendaji unaomtukuza Mungu kwa misingi ya dini zote ni kutengeneza undugu na utangamano wa kijamii usiojali itikadi za kidini, kikabila na hata kisiasa. Hii inaonyesha kuwa, fomula zinazotumika katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* sio tu kwamba zinaonyesha kuanza kwa utendaji bali pia zina dhima ya kuhamasisha umoja, undugu na ujamaa. Msimbo wa kimatukio wa Nadharia ya Semiotiki ya Kijamii (Escarpit, 1974; Greene & Cushman, 2006; na Fenner, 2010) ambao wanaeleza kuwa matukio katika kazi za fasihi huwafanya watunzi wajenge dhamira kwa namna inayofikisha ujumbe kwa hadhira ilivyokusudiwa. Matumizi ya fomula za sala na maombi katika nyimbo za *mdumange* ni kitendo cha kuivuta jamii na kuifanya hadhira na jamii kwa ujumla iamini na ikubali ujumbe unaoelezwa kwenye tukio husika.

### 4.3.2 Fomula za Uhitimishaji

Kama ilivyo wakati wa kuanza utendaji, wasanii wa nyimbo za *mdumange* pia hutumia fomula maalum wakati wa kumaliza au kuhitimisha utendaji wao. Lengo la kutumia mtindo huu wa uimbaji ni kurahisisha mawasiliano miongoni mwa waimbaji, wachezaji na wapiga ngoma pamoja na ala nyingine za kimuziki. Kwa mfano wimbo ufuatao:

#### Mf. 4.14: Fomula za Uhitimishaji

##### KISAMBAA

**MK:** Waume tiagane  
**WK:** Tiagane kwa usaama  
**MK:** N’kunda tiagane  
**WK:** N’kunda tiagane kwa usaama  
**MK:** Wauya mzumie ngoma  
**WK:** Mzumie ngoma kwa usaama  
**MK:** N’kunda tiivane  
**WK:** N’kunda tiivane kwa usalama  
**MK:** Ooh tate Abedi toa ngoma ee  
**WK:** Toa ngoma kwa usaama  
**MK:** N’tende zeze baba  
**WK:** N’kunda tiagane kwa usaama..  
**MK:** Ooh tate wauya tiivane  
**WK:** Tiivane kwa usaama

##### KISWAHILI

**MK:** Jamani tuagane  
**WK:** Tuagane kwa amani  
**MK:** Nataka tuagane  
**WK:** Ninataka tuagane kwa amani  
**MK:** Wasanii itikieni ngoma  
**WK:** Itikieni ngoma kwa amani  
**MK:** Nataka tuelewane  
**WK:** Ninataka tuelewane kwa amani  
**MK:** Ooh baba Abedi piga ngoma ee  
**WK:** Piga ngoma kwa amani  
**MK:** Nifanyeje kaka  
**WK:** Ninataka tuagane kwa amani  
**MK:** Ooh baba wasanii tuelewane  
**WK:** Tuelewane kwa amani

Kupitia nukuu ya wimbo huu, tunaona jinsi msanii anavyosisitiza suala la amani, umoja na undugu pamoja na dhana nzima ya kuagana. Wakati wa kuimbwa kwa wimbo huu, ngoma pamoja na ala nyingine za kimuziki hupigwa katika mwendo wa harakaharaka zaidi. Hali hii inaonyesha kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* unaambatana na matumizi ya uimbaji wa fomula maalum sio tu wakati wa kuanza, bali pia wakati wa kuhitimisha utendaji.

Katika muktadha mwingine wasanii huunda fomula za uhitimishaji kwa kutumia ruwaza tofauti na iliyoainishwa katika mfano namba 4.14 hapo juu. Kwa mfano, katika nukuu ifuatayo msanii badala ya kusisitiza suala la amani na umoja, huhitimisha utendaji wake kwa kuwapongeza wanachama na kuwaomba radhi, au

kuwataka watoe madukuduku yao. Pia katika nukuu hii, wasanii wanaonyesha kuisitiza umuhimu wa wazazi wa kike na wa kiume katika jamii. Msanii anasema

**Mf. 4.15: Wimbo unaohitimishwa kwa Kuwaomba radhi wanachama**

**MK:** Ee oiye mame haya ee  
Mouti Usambara hayani mame  
Wabwanga mame kuna ngoma haya ee  
Mouti Usambara hayani mame  
Angwe kuna ngoma haya ee  
zumiangoma

**WK:** Ee haya ee  
Ee haya ee  
Waiya lelo ee

**MK:** E mwena mbui naaonge nguzu  
Mwena mbui naaonge nguzu  
N’kunda niite na kwetu  
Wabwanga n’kunda niite na kwetu  
Wabwanga n’kunda niite na kwetu  
Mwena mbui naaonge nguzu  
Mwena mbui naaonge nguzu  
N’kunda niite na kwetu  
Wabwanga n’kunda niite Mgwashi  
Wabwanga n’kunda niite na kwetu  
Ee kuna ngoma mame Jaia Jaia

**WK:** E Jaia Jaia ee  
Aee nane Jaia Jaia ee

**MK:** E oiye mama hayaa ee  
Mouti Usambara hayani mama  
Na vijana mama kuna ngoma haya ee  
Mouti Usambara hayani mama  
Eti kuna ngoma haya ee itikieni ngoma

**WK:** Ee haya ee  
Ee haya ee  
Waiya lelo ee

**MK:** E mwenye tatizo la aseme haraka  
Mwenye tatizo na aseme haraka  
Nataka kwenda kwetu  
Vijana nataka niende kwetu  
Vijana nataka niende kwetu  
Mwenye tatizo na aseme haraka  
Mwenye tatizo na aseme haraka  
Nataka niende kwetu  
Vijana nataka niende Mgwashi  
Vijana nataka niende kwetu  
Ee kuna ngoma mama Jaia Jaia

**WK:** E Jaia Jaia ee  
Aee nane Jaia Jaia ee

Data iliyonukuliwa katika mfano namba 4.15 hapo juu inaonyesha aina nyingine ya fomula za uhitimishaji zinazotumika katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Katika utendaji wa namna hii, wasanii wanataja na kusifia wasanii wengine, na pia wanaitaja na kuisifia hadhira. Kwa ufupi, fomula ya uhitimishaji iliyotumika katika nukuu hii hairejelei mizimu wala miungu wanaotukuzwa katika fomula za sala au maombi. Aidha, fomula hii pia inaonyesha jinsi fanani na hadhira huwasiliana na hushirikiana ili kukamilisha utendaji wao. Katika fomula hii, maneno yanayotaja mama na baba yamerudiwa mara kwa mara kama ishara ya kuonyesha umuhimu wa kuwaenzi wazazi katika maisha ya Wasambaa.

### 4.3.3 Fomula za Kibwagizo cha Kubadilishia Wimbo

Kando na miundo ya fomula za ufunguzi na uhitimishaji, utendaji wa nyimbo za *mdumange* pia unahusisha fomula changamani. Fomula hizo hutumika mwanzo, katikati au mwishoni mwa utendaji, hususan wakati wa kuhitimisha wimbo au kubadilisha wimbo. Kwa kiwango kikubwa kundi hili la fomula lina muundo wa swali – jawabu baina ya fanani na hadhira. Fanani huimba nyimbo zao kwa njia ya kuiuliza hadhira maswali. Kadhalika, kwa vile hadhira pia huitikia utendaji kwa njia ya kujibu maswali kutoka kwa fanani, tunaweza kusema kuwa fomula mchanganyiko pia zina muundo wa kidialojia (majibizano) miongoni mwa washiriki wa nyimbo za *mdumange*. Aidha, utafiti huu umebaini kuwa kuna aina mbili za fomula za namna hii: (i) fomula zilizoundwa kwa muundo wa swali – jawabu (majibizano) kati ya fanani na hadhira; na (ii) fomula zisizoundwa kwa njia ya swali – jawabu.

#### Mf. 4.16 (a): Uimbaji wa Kibwagizo (1)

**MK**

Ee hayani mwatimula,  
Ee hayani mwatimula ngoma Dereva  
(ee hayani mwatimula ngoma wanangu wa  
chama ee)

**WK**

Ee waiyaa eo nane waiyaa

#### Mf. 4.16 (b): Uimbaji wa Kibwagizo (2)

**MK**

Ee ho tate  
Ee ho mame

**WK**

Shauri yao

Nyimbo zilizonukuliwa katika mfano namba 4.16 (a) na (b) zinawakilisha fomula mchanganyiko zilizoundwa kwa kutumia muundo wa majibizano yasio na umbo la swali – jawabu. Katika mfano namba 4.16 (a) MK anaimba mishororo miwili kisha WK wanafuatishia uimbaji kwa kuimba mshororo mmoja pekee. Aidha, idadi ya mizani zinazounda mishororo ya mfano namba 4.16 (a) ni kubwa ikiliganishwa na idadi ya mizani za mishororo iliyopo katika mfano namba 4.16 (b).

Kwa upande mwingine, wasanii wa nyimbo za *mdumange* pia hutumia fomula mchanganyiko zenye muundo wa swali – jawabu kwa minajili ya kuonyesha mwanzo wa utendaji, kuisha kwa wimbo mmoja na kuanza kwa wimbo mwingine na pia kwa minajili ya kuhitimisha utendaji. Wakati wa utendaji wao, MK huwauliza maswali WK kama vile niimbe au nisiimbe, na niseme au nisiseme. Katika mifano ifuatayo aina hii ya muundo wa fomula inabainishwa waziwazi:

**Mf. 4.17 (a): Beti zinazotumika mwanzoni, katikati au mwishoni (1)**

**KISAMBAA**

**MK:** Ee [-tate] niimbe [-imi] hambu nieke

**WK:** ee imbaa

**MK:** ee ee ee (oi nane)

**WK:** e imba ee hambu titeiza [weizie] wenye  
(ee imba mwenge wa uhulu uzabua)

**KISWAHILI**

**MK:** Ee niimbe au nisiimbe

**WK:** Ee imbaa

**MK:** Eee ee ee

**WK:** Imba kwa kuwa tumekuja  
wenyewe/ee imba mwenge wa  
uhuru umewasili

**Mf. 4.17 (b): Beti zinazotumika mwanzoni, katikati au mwishoni (2)**

**KISAMBAA**

**MK:** Ee [tate] nionge [-imi] hambu nieke

**WK:** Ee onгаа

**MK:** ee ee ee (Oi nane)

**WK:** Ee onгаа ee hambu tiizie [weizie]  
wenye

**KISWAHILI**

**MK:** Ee baba niseme au nisiseme

**WK:** Eee sema

**MK:** E eee ee

**WK:** Ee sema ee kwani tumekuja  
wenyewe

Beti zilionukuliwa katika mifano namba 4.17 (a) na (b) zinatumiwa na wasanii wa nyimbo za *mdumange* katika hatua mbalimbali za utendaji kama vile wakati wa kuanza, kubadilisha wimbo na kumalizia utendaji. Katika mfano namba 4.17 (a) msanii anaiuliza hadhira yake impatie ruhusa ya kuimba na katika mfano namba 4.17 (b) msanii anaiuliza hadhira yake impatie ruhusa ya kusema. Mawazo ya Nadharia ya Utendaji wa Maigizo yametusaidia kuelewa kuwa mbinu ya uulizaji maswali katika utendaji wa nyimbo hapo juu imetumika kujenga taharuki katika utendaji kwani ingawa msanii anaouwezo wa kuimba na kusema, anaiuliza hadhira kwa minajili ya kuifanya hadhira ihisi kuwa inayo mamlaka ya juu katika utendaji. Chochote atakachofanya msanii hakitakuwa na maana ikiwa hadhira haitakitambua. Kwa



ujumla, fomula zote za 4.17 (a) na (b) huweza kutumika mwanzoni, katikati au mwishoni mwa utendaji.

#### **4.4 Mitindo ya Tamathali za Usemi, Methali, Nahau na Misemo**

Kipengele kingine cha mitindo ya lugha ni tamathali mbalimbali za usemi. Kadhalika, utendaji wa nyimbo za *mdumange* huenda sambamba na matumizi ya methali, nahau na misemo. Mulokozi (2002) anaeleza kuwa ni vigumu sana kutenganisha tanzu za fasihi simulizi wakati wa kuwasilisha tanzu fulani. Uwasilishaji wa nyimbo huenda sambamba na methali, nahau, misemo, miviga na kadhalika. Hivi ndivyo utendaji wa fasihi simulizi unavyojidhihirisha vinginevyo hutenganishwa kwa lengo la kufafanua tu lakini kiuhalisia hazitenganishwi.

##### **4.4.1 Tamathali za Usemi**

Katika utafiti huu tumebaini kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* unaambatana na matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi kama vile tanakali za sauti, takriri, tashititi, tasfida na tashihisi. Mbinu hii imetumika ili kuibua taswira katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Aidha, mbinu za kisanaa zilizojengwa kwa kutumia tamathali za usemi zimetumika kuwasilishia ujumbe unaohusu mambo nyeti ya kijamii kama vile mapenzi na ndoa, kwa lugha ya upole, ukarimu na ucheshi. Sehemu ifuatayo imejadili kwa kina matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*

##### **4.4.1.1 Tanakali za Sauti**

Tanakali za sauti ni tamathali ya usemi ambayo imesheheni matumizi ya vipashio vya kiisimu visivyokuwa na maana zinazojitegemea. Maana za vipashio hivyo zimeumana na muktadha wa utendaji. Aidha, kutokana na hali hiyo, si rahisi kutafsiri vipashio

vya tamathali ya tanakali za sauti nje ya muktadha wa utendaji. Miongoni mwa nyimbo zilizotumia mbinu ya tanakali za sauti ni wimbo ufuatao:

**Mf. 4.18: Wimbo ambapo mbinu ya tanakali za sauti zimetumika**

**KISAMBAA**

1. Ee waiya eooo oeee
2. Lele lele lele leleee
3. Kimphanga chakwea mwemti
4. Chikishea chakema hayeye (I)
5. Kimphanga chakwea mwemti
6. Chikishea chakema hayeye
7. Kimphanga chakwea mwemti
8. Chikishea chakema hayeye (II)
9. E awo wana wake wadodo
10. Wakikua neze wahaawe
11. Awo wana wake wadodo,
12. Wakikua neze wahaawe (III)

**KISWAHILI**

1. Ee nalia eooo oeee
2. Lele lele lele leleee
3. Mwewe amepanda juu ya mtii
4. Akiteremka hulia hayeye (I)
5. Mwewe amepanda juu ya mti
6. Akiteremka hulia hayeye
7. Mwewe amepanda juu ya mti
8. Akiteremka hulia hayeye (II)
9. E hao watoto bado ni wadogo
10. Wakikua wataondoka
11. Hao watoto bado ni wadogo
12. Wakikua wataondoka (III)

Kama inavyoonekana hapo juu, maneno ya mshororo wa kwanza **Ee waiya eooo oeee, e lele lele lele leleee** hayana maana ya moja kwa moja, bali yanatumika kwa minajili ya kukidhi mahitaji ya kiutendaji. Maneno yaliyopo katika mshororo wa kwanza yametumika kutoa sauti za kimuziki ili kuvuta nadhari za hadhira, na hatimaye kuwasilisha ujumbe kwa njia inayovutia. Kadhalika, maneno yaliyotumika katika mshororo wa pili kwenye ubeti huo **Kimphanga chakwea mwemti, chikishea chakema hayeye** yametumika ili kuwasilisha ujumbe kwa njia yenye mvuto zaidi.

*Kimphanga* ni ndege mwenye tabia ya kuchukua vifaranga wa kuku. Ndege huyu anafanana na kunguru au mwewe. Katika wimbo huu, mbinu ya tanakali za sauti imetumika kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kuigiza sauti zinazotolewa na mwewe anapokuwa mawindoni na wakati anapofurahia kupata kifaranga. Kupitia mbinu hii, msanii ameelezea furaha ya mwewe kwa njia ya kuigiza jinsi ndege huyo anavyolia. Tanakali za sauti iliyotumika katika mshororo wa kwanza inaigiza jinsi ndege huyu anavyolia wakati akiwa mawindoni, na tanakali iliyopo katika mshororo wa pili

inaonyesha jinsi ndege huyu anavyolia mara baada ya hunyakua vifaranga wa kuku. Sauti ya kwanza ni ya huzuni ilhali sauti ya pili ni ya furaha.

Kwa ufupi, ingawa sauti zilizotumika zimeigiza milio ya ndege, ujumbe unaowasilishwa unaelekeza namna ya kuwalea na kuwatunza watoto. Dhamira hii inafafanuliwa vyema na msanii katika ubeti wa tatu anaposema kuwa: **Awo wana wake wadodo, wakikua nezewahaawe** akimaanisha kuwa **Hao watoto bado hawajakua, wakikua watakujaondoka**. Ujumbe unaopatikana katika wimbo huu unawahusu wazazi wasiozijali familia zao. Onyo na tahadhari inatolewa kuwa kama anavyofanya mwewe, ndivyo watoto watafanya. Kwa kuwa sasa hawana uwezo, wanalalamika lakini siku wakipata nguvu wataondoka kwa shangwe kama mwewe anavyoshangilia baada ya kupata chakula.

Mbali na wimbo wa **mwewe**, nyimbo nyingine zilizotumia tanakali za sauti ni pamoja na wimbo wa **sitaweza, kaka Wile** na **mheshimiwa**. Katika nyimbo hizi, sauti za viumbe, matendo au hali mbalimbali zimeigizwa na kutumika kama mbinu ya kuwasilishia ujumbe kwa hadhira. Matumizi ya mbinu hii yameufanya utendaji wa nyimbo za *mdumange* kuwa hai, na wa kuvutia. Kwa ufupi, mbali na kufanikisha utendaji, mbinu hii imechochea kufahamika kwa ujumbe kwa hadhira na pia kuiburudisha jamii kwa ujumla. Utafiti huu unatoa hoja kuwa matumizi ya tanakali za sauti kama mkakati wa kiutendaji yana mchango mkubwa kwani huzifanya nyimbo husika zivutie, huonyesha msisitizo katika ujumbe, na husaidia katika kusawazisha hitilafu za urari wa vina na mizani ndani ya nyimbo za *mdumange*.

#### **4.4.1.2 Tashititi**

Tashititi ni mbinu ya kisanaa ambapo msanii huuliza swali lisilohitaji jawabu. Kusudio la swali linaloulizwa katika kazi ya kisanaa ni kuibua usikivu na hamasa ya

kushiriki katika utendaji. Katika mbinu hii, msanii anakuza wazo na hisia zake kwa kupandisha na kushusha kiwango cha sauti au mawimbi ya sauti wakati wa uimbaji. Mbinu ya kitashtiti imetumika katika wimbo wa **ninawauliza** kama inavyodhihirikka hapa chini:

**Mf. 4.19: Wimbo ambapo mbinu ya tashiti imetumika**

1. *Ninawauliza*
2. Ninawauliza Gonjwa la UKIMWI
3. Duniani limetoka wapi
4. *Ninawauliza*
5. Ninawauliza Gonjwa la UKIMWI
6. Duniani limetoka wapi

Katika nukuu hii, swali linaloulizwa na msanii linakusudia kudadisi kitendawili kilichopo kuhusu asili na chimbuko la ugonjwa hatari wa UKIMWI. Licha ya kuwa ugonjwa huu umekuwako Tanzania tangu miaka ya 1980 mpaka leo, bado asili yake haijafahamika vyema. Kitendo cha kuuliza swali lisilohitaji jawabu kinazua hali ya taharuki kwa hadhira. Kwa kutumia swali, dhamira inayofafanua ugonjwa wa UKIMWI imewasilishwa kwa msisitizo mkubwa zaidi kuliko kama ingewasilishwa kwa kutumia mtindo mwingine. Kwa hiyo, matumizi ya mbinu hii katika kuwasilisha ujumbe wa nyimbo za *mdumange* yamesaidia kuibua dhamira kuhusu tahadhari ya ugonjwa wa UKIMWI. Mbali ya kutumika katika kuisitiza ujumbe unaohusu athari ya ugonjwa wa UKIMWI, tashiti pia zimetumika kwa minajili ya kufafanua dhamira ya umuhimu wa kutunza utamaduni wa Kisambaa. Suala hili linadhihirika katika wimbo wa **wanaume wa Mponde**, ubeti wa kwanza:

**Mf. 4.20: Wimbo ambapo mtindo wa tashtiti umetumika****Wanaume wa Mponde****KISAMBAA**

1. E ooe waghoshi wa Mponde
2. Waghoshi wa Mponde
3. Na wa Shambaai taawauza nenywi munijibu.
4. Icho cheeka muke miviga.
5. Watate nenywi munijibu.
6. Na wamame nenywi munijibu.
7. Kwani kuuliza si ujinga.
8. Aulizaye ataka kujua (I)

**KISWAHILI**

1. E ooe wanaume wa Mponde
2. Wanaume wa Mponde
3. Na wa Shambaai tunawauliza mnipe jawabu
4. Kwa nini mmeacha kufanya miviga
5. Nanyi Baba mnipe jawabu
6. Mama pia mnipe jawabu
7. MUK
8. MUK (I)

Katika nukuu hapo juu kuna aina mbalimbali za maswali zilizotumika kuwasilishia ujumbe. Kwanza ni kutoka mishororo ya 2, 3 na 4 ambapo msanii anawauliza wanaume wa vijiji vya Mponde na Shambaai kwa nini wameacha kufanya miviga ya Kisambaa? Msanii anasema: **Waghoshi wa Mponde, na wa Shambaai taawauza nenywi munijibu, icho cheeka muke miviga.** Maana ya maneno haya ni kuwa **Wanaume wa Mponde na wa Shambaai nanyi tunawauliza mnipe jawabu, kwa nini mmeacha kufanya miviga?** Katika awamu ya pili swali hilo limeelekezwa kwa wazazi wa kiume na wa kike.

Kitendo cha kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kuuliza maswali makundi mbalimbali ya hadhira kinazifanya nyimbo ziburudishe na ujumbe wake ueleweke kwa urahisi. Aidha, kitendo cha kuuliza hadhira maswali kinaonyesha kuwa wakati wa utendaji, fanani anaweza kutangamana na uimbaji (nyimbo) pamoja na hadhira yake. Ili kuonyesha umuhimu wa maswali yake kwa hadhira, msanii anamalizia ubeti kwa kusema: **kwani kuuliza si ujinga, aulizaye ataka kujua.** Hali hii inaonyesha kuwa maswali yalikusudiwa kuifanya hadhira ielewe kuwa jamii imekumbwa na kasumba ya kudharau mila zao ikiwemo miviga.

Tashititi zilizojadiliwa katika nyimbo za **ninawauliza** na **wanaume wa Mponde** zimetumika katika muktadha wa hafla za kisiasa, hususan katika sherehe za sikukuu ya Wafanyakazi. Katika sherehe hizo pamoja na mambo mengine masuala ya utamaduni pamoja na afya hupewa kipaumbele sana. Kando na muktadha huu, mbinu ya tashititi pia imetumika katika sherehe za harusi. Katika utendaji wa nyimbo hizi, tashititi hutumika kuimarisha mapigo ya kimuziki pamoja na kuelezea umuhimu wa binti kwa wazazi wake. Hali hii inadhihirika waziwazi katika wimbo wa **tumekupa mkono wetuu** ambapo msanii anasema:

**Mf. 4.21: Tumekupa mkono**

**KISAMBAA**

**MK:** Tizakunka uyo mndee

**WK:** Uzaghua mkono wetu

**MK: Ndiye aite nkuni ni ndai**

**WK:** Uzaghua mkono wetu

**MK: Ndiye aite mtoi ni ndai**

**WK:** Uzaghua mkono wetu

**MK: Ndiye aime nkoi ni ndai**

**WK:** Uzaghua mkono wetu

**MK:** Tizakunka uyo mndee

**WK:** Uzaghua mkono wetu

**KISWAHILI**

**MK:** tumekupatia huyo msichana

**WK:** Umechukua mkono wetu

**MK:** Nani ataenda kutafuta kuni

**WK:** Umechukua mkono wetu

**MK:** Nan ataenda kuteka maji

**WK:** Umechukua mkono wetu

**MK:** Nani ataenda shambani

**WK:** Umechukua mkono wetu

**MK:** Tumekupatia huyo msichana

**WK:** Umechukua mkono wetu

Katika wimbo huu mbinu ya kuuliza maswali bila kuyatolea majibu imedhihirika mara tatu. Tashititi imejitokeza katika mishororo ya 3, 5 na 7. Swali lililoulizwa katika hali zote tatu linaibua hisia ya upendo wa wazazi kwa binti yao. Aidha, katika wimbo huu, tashititi imetumika kuibua mapigo ya kimuziki kwa sababu mara zote swali limetumika kama kiitikio cha wimbo. Muktadha wa mapigo ya kimuziki umechochea hali ya kurudiwarudiwa kwa tashititi mara tatu ndani ya wimbo mmoja. Mbali na kuibua athari ya kimuziki, tashititi iliyotumika katika wimbo huu imesaidia kufafanua ujumbe kwa hadhira lengwa, hasa kuhusu nafasi ya mtoto wa kike katika familia. Kwa mujibu wa desturi za Wasambaa, mtoto wa kike ni raslimali kubwa sana kwani yeye ndiye anayetarajiwa kusaidiana na familia katika shughuli za kilimo,

kuteka maji, kuchunga mifugo na kutafuta kuni. Kwa hiyo, ingawa anapopata mchumba wazazi hufurahi, siku ya harusi wazazi huonyesha hisia za upendo wao kwa binti yao. Pia huonyesha umuhimu wa binti huyo katika maisha yao. Ndiyo maana maswali yaliyoulizwa katika wimbo huu yamejikita katika shughuli za uzalishaji mali ambapo msanii anasema **Ndiye aite nkuni ni ndani? Ndiye aite mtoi ni ndai? Na ndiye aite nkoi ni ndai?**

Maswali haya yanadadisi kuwa ikiwa binti kabla ya kuolewa alisaidia katika shughuli za kutafuta kuni, kuteka maji na kwenda shambani, je leo akiolewa ni nani atafanya shughuli hizo? Kwa ufupi, mbinu hii inaonyesha kuwa licha ya kuwa wazazi walimpenda sana binti yao, lakini muda ukifika hakuna jinsi ni lazima aolewe. Ni kutokana na msingi wa umuhimu wa ndoa katika maisha ya Wasambaa ndiyo maana hata maswali yaliyoulizwa hayakustahili kujibiwa. Kitendo cha kuuliza maswali hayo ambayo hayahitaji majibu ya papo kwa papo ni namna nzuri ya utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Katika maswali hayo bwana harusi makini atakuwa amepata uelewa kuwa pamoja na kwamba yeye sasa ndiye mume na mwenye maamuzi juu ya mkewe basi afahamu kuwa wazazi nao wanahitaji msaada fulani kutoka kwake na kwa binti yao pia. Nadharia ya Utendaji wa Maigizo inaeleza kuwa hadhira hushirikishwa kwa namna mbalimbali ambapo wakati mwingine ni akili tu ya hadhira ndiyo inayoshirikishwa. Kuuliza maswali ambayo hayahitaji majibu kutoka kwa hadhira ni utendaji ambao umeihusisha akili ya hadhira na majibu atakuwa nayo ndani ya nafsi yake. Suala hili linaafikiana kwa namna fulani na mtazamo wa Nadharia ya Uchanganuzi Nafsiya kuwa kitendo cha kuhusisha akili ya wahusika huathiri zaidi tabia na mienendo ya mwanadamu (Jung, 1933 na Jones, 2007).

Kutokana na namna mbinu hii ilivyotumika tunaweza kusema kuwa tashititi ni miongoni mwa mikakati ya kisanaa iliyotumiwa na wasanii wa nyimbo za *mdumange*

kuumba na kuwasilisha ujumbe kwa njia inayovutia. Maswali yalioulizwa yanaonyesha kiwango cha utangamano wa fanani na hadhira wakati wa utendaji. Aidha, maswali hayakujibiwa ndani ya nyimbo kutokana na ukweli kuwa lengo lake ni kuibua hisia za udadisi na tafakuri kuhusu dhamira husika.

#### 4.4.1.3 Tasfida

Tasfida ni tamathali ya usemi ambapo msanii hutaja na kufafanua mambo kwa kutumia lugha ya upole ili kuwasilisha ujumbe unaohusu masuala nyeti ya kijamii. Miongoni mwa masuala nyeti ya kijamii yaliyowasilishwa kwa kutumia mbinu ya tasfida ni suala la mapenzi. Katika jamii ya Wasambaa, masuala mbalimbali ya mapenzi yanachukuliwa kuwa ni mambo ya siri na ni mwiko kuyataja hadharani. Kitendo cha kutaja au kuzungumzia masuala ya mapenzi baina ya mume na mke hadharani kinaonekana kama ni kukosa adabu. Ili kuweka msingi imara katika falsafa hii ya malezi na mafundisho ya jamii ya Wasambaa, wasanii wanatumia lugha ya kitaswira, hususan kwa njia ya tasfida. Ili kuwasilisha dhamira hii kwa lugha ya upole (tasfida) zimetumika:

#### Mf. 4.22: Matumizi ya Tasfida (1)

##### KISAMBAA

1. Ooh ng'wana ni mdodo ee aalilia unyumba aa e
2. Eeh ng'wana ni mdodo nane aalilia unyumba aa e
3. Ooh ukishemlinda ee mame utakoma ubishi
4. Ukishemlinda iwe mamee utakoma ubishi ng'wenye

##### KISWAHILI

1. Ooh mtoto ni mdogo ee analilia unyumbaa e
2. Eeh mtoto ni mdogo jamani analilia unyumbaa e
3. Ooh usipomlinda ee mama utakoma ubishi
4. Usipomlinda wewe mama utakoma ubishi mwenyewe

Katika nukuu hapo juu “unyumba” limetumika kitasfida ili kuficha na kupunguza ukali wa maneno yanayofafanua raha anazopata mwanandoa. Vilevile mbinu hii



imetumika kuweka misingi ya malezi kwa watoto kwa kuyasawiri mapenzi kama kitu cha hatari sana kwa watoto kwa upande mmoja na kuyasawiri mapenzi kama kitu muhimu kwa watu wazima. Aidha, katika wimbo huu msanii anajadili wajibu wa wazazi pamoja na jamii kwa ujumla katika kuwalea na kuwalinda watoto wasijihusishe na masuala ya mahusiano ya kindoa. Hivyo, neno **Unyumba** limetumika kurejelea ndoa, kuolewa, na starehe za ndoa kwa ujumla kwa minajili ya kuficha au kupunguza ukali wa maneno hayo. Kwa kufanya hivyo, wasanii wanaonekana watu wastaarabu na waliotelewa kwenye mfumo wa maadili ya jamii.

Maneno mengine yaliyotumika kufafanua maana na ujumbe unaohusu masuala ya mapenzi kwa njia ya lugha ya upole (tasfida) kwenye utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni “**huduma**” . Neno hili limetumika sawa na neno ‘unyumba’ lilivyotumika katika mfano uliofafanuliwa hapo juu. Katika mfano ufuatao muktadha wa matumizi ya neno hili umefafanuliwa vyema.

#### **Mf. 4.23: Matumizi ya Tasfida (2)**

##### **KISAMBAA**

1. Iwe baba n’hudumia wa lelo
2. Wakeoi ng’wenye nen’teie
3. Afazali kughuighwa mdodo kuiko ifu ja ubweni
4. Aee jaagyea wasiwasi

##### **KISWAHILI**

1. Wewe kaka nihudumie leot tu
2. Kesho mwenyewe nitajua la kufanya.
3. Bora kuolewa mdogo kuliko kupata mimba kabla ya ndoa
4. Mimba kabla ya ndoa inaleta wasiwasi

Wimbo ulionukuliwa katika mfano namba 4.23 umetumia neno “**huduma**” ili kuficha aina ya uhusiano unaodhihirika baina ya mabinti na vijana ambao bado hawajaoana. Kwa hiyo, huduma inayotajwa katika wimbo huu ni tasfida inayodhamiriwa kufafanua hali ya mapenzi yanayofanywa na vijana kabla hawajao au kuolewa. Kwa kuwa jambo hilo halikubaliki katika jamii, vijana wengi hulifanya kuwa la siri mno

kwa kuhofia kugombeza na wazazi wao, na pia kuhofia kupata uja uzito. Ndio maana katika mshororo wa mwisho wa wimbo huu msanii anasema “**afazali kughuighwa mdodo kuiko ifu ja ubweni jaagyea wasiwasi**” akimaanisha kuwa ni afadhali kuolewa angali mtoto kuliko kupata uja uzito kabla ya ndoa. Matumizi ya tasfida pia yamedhihirika katika kuelezea dhamira ya shida anazozipata mtu asiyeoa na raha anazozipata mtu aliyeoa/olewa. Katika kuelezea dhamira hii, msanii ametumia picha ya kukwea mlima kama ilivyo katika mfano hapa chini:

**Mf. 4.24: Matumizi ya Tasfida (3)**

**Nitapanda nani katika mlima**

**KISAMBAA**

1. N’kwea na ndai mweaka kaima weangu ee
2. N’kwea na ndai mweaka kaima
3. Nen’ghue sen’vidahe (I)
4. N’kwea na ndai mweaka kaima Zaituni
5. N’kwea na ndai mweaka kaima
6. Zaituni sen’vidahe (II)

**KISWAHILI**

1. N’tapanda na nani katika kilima hiki jamani
2. N’tapanda na nani katika kilima hiki
3. Nitaoa peke yangu sitaweza (I)
4. N’tapanda na nani katika kilima hiki mimi Zaituni
5. N’tapanda na nani katika kilima hiki mimi
6. Zaituni peke yangu sitaweza (II)

Sauti inayosikika katika wimbo hapo juu ni ya mwanamume anayelalama kuhusu upweke na tabu za kukwea mlima. Michakato ya kimaisha kwa ujumla imeelezwa kwa kutumia taswira ya kupanda mlima, na hali ya kutokuwa na mwenza imewasilishwa kwa kutumia swali “**n’kwea na ndai**” ikiwa na maana kuwa je, nitapanda mlima huu pamoja na nani. Wimbo huu unaonyesha jinsi taswira ya taabu anazozipata mwanamume asiyeoa ilivyofananishwa na taabu azipatazo mtu wakati akipanda mlima mrefu. Bila shaka mtu anayepanda kwenye mlima anahitaji kutembea polepole, na hahitaji kuwa na mzigo mzito. Katika mshororo wa pili, msanii anasema **ne’nghue sen’vidahe** akiwa na maana kuwa ni bora aoe ili aondokane na tabu hizo.

Kando na kutumia mbinu ya tasfida kurejelea raha na shida za wanandoa, mbinu hii ya tasfida pia imetumika kurejelea aina mbalimbali za taabu na mateso ya maisha kwa ujumla wake. Aidha, tofauti na ilivyo katika mfano namba 4.25 ambapo tasfida ya

namna hii imejengwa kwa kutumia taswira ya **kupanda mlima**, katika kutaja aina nyingine za taabu na mateso ya maisha kwa ujumla imejengwa kwa kutumia taswira ya “**hakwea**” yaani sehemu yenye mlima. Kwa ufafanuzi zaidi tazama mfano hapa chini:

**Mf. 4.25: Matumizi ya tasfida**

**KISAMBAA**

1. Se n'dahe hakwea ee, Se n'dahe hakwea ee
2. Waiya iya baba ee, se n'dahe hakwea ee
3. Ooe waiya iya baba ee, se n'dahe hakwea
4. Kweli se n'dahe hakwea ee (I)

**KISWAHILI**

1. Sitaweza sehemu yenye mlima
2. Kaka nalia sitaweza sehemu yenye mlima
3. Ooe nalia kaka
4. Kweli sitaweza sehemu yenye mlima (I)

Katika nukuu hapo juu, msanii ameelezea mateso katika maisha kwa ujumla kwa njia ya kutotaja waziwazi mateso mahsusi. Aidha, tasfida ya mateso au taabu za maisha imejengwa kwa njia ya lugha ya picha ambapo taabu hizo zimefananishwa na sehemu yenye mlima.

Kwa ujumla, kitendo cha kutotaja hadharani masuala nyeti kinawafanya watu wa rika na jinsia zote washiriki utendaji bila kikwazo. Falsafa ya kijamii inayojengwa kupitia nyimbo zilizokuliwa katika sehemu hii ni kuwa mapenzi ni haki ya msingi kwa watu wazima, pia ni haki ya msingi kwa wanandoa bali sio haki ya watoto. Watoto na watu wengine wasioo wala kuolewa wanapaswa kuzuiwa na kulindwa dhidi ya vishawishi vitakavyosababisha waingie katika mahusiano ya kindoa, ikiwemo uasherati, na kupata au kusababisha uja uzito. Suala hili linaelezwa pia na Mbiti (1975) pamoja na Mazrui (2007) hasa wanapojadili kuhusu muundo wa falsafa ya Kiafrika. Wataalamu hawa wanasisitiza kuwa Waafrika huwaza na kutenda kulingana na mahitaji ya muktadha wa mazingira yanayowazunguka. Kwa ujumla matumizi ya neno “kupanda mlima” yamejenga msimbo wa kimatukio ambapo tukio hilo linahitaji

mtu mwenye nguvu na asiyesumbuliwa na maradhi ya aina yoyote. Utafiti huu unatoa hoja kuwa tukio hili linarejelea tendo la ndoa ambalo nalo huwahitaji wahusika kuwa na nguvu ya kutosha ili waweze kutimiza azma yao vinginevyo hawawezi kufanikiwa.

#### 4.4.1.4 Tashihisi

Kando na tasfida, wasanii wa nyimbo za *mdumange* wamedhihirisha utendaji wao wa kujenga taswira kuhusu masuala muhimu ya kimaisha kwa kutumia mbinu ya tashihisi. Katika mbinu hii, vitu, na viumbe visivyo na uhai vimepewa sifa ya kutenda na kusema kama binadamu. Kama ilivyo kwa mbinu nyingine, tashihisi pia zimetumika kuongeza umakini wa hadhira pamoja na kuonyesha msisitizo kuhusu dhamira kwa hadhira lengwa. Katika utafiti huu matumizi ya tashihisi yamedhihirika katika wimbo wa **nkondo** yaani vita ambapo msanii anasema:

#### Mf. 4.26: Ujenzi wa maana kwa kutumia tashihisi

| KISAMBAA                        | KISWWAHILI                       |
|---------------------------------|----------------------------------|
| <b>MK:</b> Nkondo nkondo nkondo | <b>MK:</b> Vita vita vita        |
| <b>WK:</b> Tegheezai mame       | <b>WK:</b> Akina mama sikilizeni |
| Uyu mgheni UKIMWI               | Huyu mgeni UKIMWI                |
| Wengi wazamfikiza               | Watu wengi wamemfikiza           |
| Azaonea n'kaya                  | Amepata makazi                   |
| Azaemea kughotoka (I)           | Amekataa kwenda kwao (I)         |

Katika nukuu hapo juu ugonjwa wa UKIMWI umefananishwa na mgeni aliyekaribishwa katika mji fulani, baadaye mgeni huyo akakataa kuondoka. Mbinu ya tashihisi imeufanya UKIMWI ueleweka kama ugonjwa wa hatari zaidi. Kutokana na mbinu hii utafiti huu unatoa hoja kuwa nyimbo za *mdumange* zimetumika kuionya jamii ijihadhari dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Kadhalika katika wimbo huu, ugonjwa wa UKIMWI umesawiriwa kama janga kubwa lililoivamia jamii. Jamii inaaswa ijihami dhidi ya janga na uvamizi wa mgeni huyu. Katika mshororo wa kwanza na wa pili msanii anasema **Uyu mgheni UKIMWI, wengi wazamfikiza**

akiwa na maana kuwa huyu mgeni UKIMWI, watu wengi wamempokea na kumpa makazi. Kitendo hiki pia kinaonyesha kuwa vishawishi vinavyosababisha ugonjwa huu vinaelekea kuwavutia watu wengi, na kwa hiyo idadi kubwa ya watu wameathirika. Kwa kutumia mbinu hii, jamii haina budi kuogopa vishawishi hivyo.

Kwa ujumla, wasanii wa nyimbo za *mdumange* wamefanikiwa kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa kwa kutumia taswira mbalimbali. Pia wamefanikiwa kujenga itikadi ya Wasambaa kuhusu masuala nyeti ya jamii kama vile mapenzi, ndoa, utamaduni na maradhi. Taswira zilzotumiwa na wasanii zimechimbuka kutokana na muktadha wa jamii ya Wasambaa ambao ndio uliowalea na kuwakuza watendaji wa nyimbo za *mdumange*.

#### **4.4.2 Matumizi ya Methali**

Kando na matumizi ya tamathali za usemi, ujumi wa nyimbo za *mdumange* pia umeimarishwa kwa kutumia methali za namna mbalimbali. Baadhi ya methali zimetokana na Kisambaa na nyingine zimetokana na Kiswahili. Kwa kiwango kikubwa methali za Kiswahili zimetumika sana katika nyimbo zilizowasilishwa kwenye hafla za kisiasa ilhali methali za Kisambaa zimetumika zaidi kwenye sherehe za harusi.

Kwa kiwango kikubwa methali zimetumika katika wimbo wa **wenyeji wetu**. Katika wimbo huu, methali kadhaa zimetumika katika ubeti wa kwanza na wa tatu. Aidha, katika wimbo huu utendaji umeambatana na matumizi ya methali mbili ndani ya muktadha mmoja. Kwanza ni katika ubeti wa kwanza ambapo msanii anasema:

**Mf. 4.27: Matumizi ya Methali (1)****KISAMBAA**

1. E oo e wenyeji wetu
2. Wenyeji wetu hapa Msamaka
3. wote wake kwa waume
4. Wakubwa kwa wadogo
5. mbiu ya mgambo imelia
6. Asiyekuwa na mwana
7. leo aeleke jiwe
8. ngoma ya Kanyawana izaiza
9. Shauri na kikosi chake
10. chenye sifa mbalimbali
11. ee na mitindo ya kisasa
12. waume soi na kunu (I)

**KISWAHILI**

1. MUK
2. MUK
3. MUK
4. MUK
5. MUK
6. MUK
7. MUK
8. Ngoma ionyayo watoto imewasili
9. MUK
10. MUK
11. MUK
12. Jamani njooni huku (I)

Kulingana na nukuu hapo juu matumizi ya methali yanadhihirika kwenye mshororo wa tano na sita. Kwanza kuna **Mbiu ya mgambo imelia**, na pili kuna **Asiyekuwa na mwana aeleke jiwe**. Methali hizi zimetumika kama utangulizi katika wimbo. Makusudio ya kufanya hivyo ni kuvuta usikivu wa hadhira na kuionyesha hadhira kuwa fanani anajua namna ya kuzungumza kwa hekima huku akiongozwa na turathi nyingine za kijamii ikiwemo methali. Msanii ameteua aina mahsusi ya methali za kutumia mwanzoni mwa utendaji na pia ameteua aina maalum ya methali za kutumia katikati mwa utendaji wake.

Baada ya kutumia methali zinazolenga kuiandaa hadhira iwe tayari kufuatilia utendaji, katika ubeti wa tatu, msanii anatumia methali nyingine inayofafanua zaidi ujumbe wake. Msanii anasema:

**Mf. 4.28: Matumizi ya Methali (2)****KISAMBAA**

1. E ooe waghoshi wa Mponde
2. Waghoshi wa Mponde
3. Na wa Shambaai taawauza munijibu.
4. Icho cheeka mueke miviga.
5. Watate nenywi munijibu.
6. Na wamame nenywi munijibu.
7. Kwani kuuliza si ujinga.
8. Aulizaye ataka kujua (I)

**KISWAHILI**

1. E ooe wanaume wa Mponde
2. Wanaume wa Mponde
3. Na wa Shambaai tunawauliza mnipe jawabu
4. Kwa nini mmeacha miviga
5. Nanyi Baba mnipe jawabu
6. Mama pia mnipe jawabu
7. MUK
8. MUK (I)

Katika ubeti ulionukuliwa hapo juu kuna methali inayosema kuwa **kuuliza si ujinga, aulizaye ataka kujua**. Kauli hii ya kimethali imetumiwa na wasanii ili kuongeza uzito wa swali lililoulizwa kabla yake. Kabla ya kutumika kwa methali hii, msanii alitumia mbinu ya tashititi kwa kuiuliza hadhira kwa nini wameacha kufanya miviga ya Kisambaa. Katika kuendelea kudadisi tatizo hili, msanii anatumia methali ili kuonyesha kuwa swali lake ni la msingi na kwamba hadhira inapaswa kuzingatia.

Mbali na methali za Kiswahili, wasanii wa nyimbo za *mdumange* pia wametumia methali za Kisambaa. Kuna wakati methali zimetumika katika nyimbo zilizoimbwa kwa Kisambaa peke yake na kuna wakati methali za Kiswahili zimechopekwa mahali ambapo nyimbo ziliimbwa kwa Kisambaa. Kwa mfano, katika wimbo wa **wenyeji wetu** methali zote zimewasilishwa kwa Kiswahili licha ya kuwa idadi kubwa ya beti za wimbo huu ziliimbwa kwa Kisambaa. Hali hii inaonyesha jinsi Wasambaa walivyoathiriwa na matumizi ya muktadha wa uwingi lugha. Vilevile, hali hii inadhihirisha kiwango kikubwa cha utangamano wa Kiswahili na lugha za asili, hususan Kisambaa.

Kwa ujumla, matumizi ya methali yamezua athari ya kimwingiliano matini baina ya nyimbo na turathi nyingine za Kisambaa, ikiwemo methali na miviga. Imedhihirika jinsi methali na miviga ya Wasambaa inavyochangia katika utendaji wa nyimbo kwa kurutubisha fani na maudhui ya nyimbo hizo. Vipashio hivi vimetumika kuendeleza utamaduni wa Kisambaa. Pia vimesaidia kuburudisha hadhira kupitia utendaji wa nyimbo na pia zimesaidia kufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Kutokana na hali hii inahalisi kusema kuwa, utendaji wa nyimbo za *mdumange* umeonyesha kiwango kikubwa cha muumano kati ya aina mbalimbali za turathi za kijadi hususan lugha, methali na miviga.

#### 4.4.3 Matumizi ya Misemo na Nahau

Miongoni mwa mbinu zilizotumiwa na fanani kuwasilisha ujumbe kwa jamii ni uteuzi wa maneno ili kuunda nahau za namna mbalimbali. Maneno maalum yaliyotumika kuunda nahau katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* yanapatikana katika wimbo wa **hana hasira** kama ifuatavyo:

#### Mf. 4.29: Maneno Maalum Kuunda Nahau

##### KISAMBAA

- 1, Eoe ee nane waume
2. ng'wanangu wa ngoma hana maya
3. Ee nane waume (I)
4. Hati una maya tua nyungu ee nane waume
5. Hati una umshai tua nyungu ee
6. Wanangu wapate kaugima (II)
7. Wanangu wa ngoma waaia ee nane waume
8. Wanangu wa chama waaia
9. Ee nane waume (III)
10. Hati umshai tua nyungu ee waume
11. Hati walogha tua nyungu ee
12. Wanangu wapate kaugima(IV)
13. Ho tate tate Abedi aaiia ee weangu sionga
14. E tate Abedi aaia ee
15. Nane sionga (V)

##### KISWAHILI

1. Eoe ee jamani
2. mwanangu wa ngoma hana hasira
3. Ee jamani (I)
4. Kama una hasira vunja chungu jamani
5. Kama una ni mchawi vunja chungu ee
6. Wanangu wapate uzima (II)
7. Wanangu wa ngoma wanalia ee jamani
8. Wanangu wa chama wanalia
9. Ee jamani (III)
10. Kama wewe ni mchawi vunja chungu ee
11. Kama unaroga vunja chungu ee
12. Wanangu wapate uzima (IV)
13. Baba Abedi analia ee sina la kusema
14. Baba Abedi analia ee
15. Sina la kusema (V)

Katika wimbo hapo juu, nahau ya **Kuvunja chungu** imedhihirika katika mshororo wa ubeti wa pili na katika mshororo wa ubeti wa nne. Nahau hii inatokana na misemo miwili iliyotumiwa katika wimbo huu ambapo msanii anasema **hati umshai tua nyungu** na **hati una maya tua nyungu**. Misemo hii imetafsiriwa kama **ikiwa wewe una hasira vunja chungu**, na **ikiwa wewe ni mchawi vunja chungu**. Aidha, misemo hii imesaidia kudhihirisha nahau ya **Kuvunja chungu** kwa minajili ya kuufanya ujumbe ueleweke vyema.



Kimsingi, wimbo huu huwa unaimbwa katika hafla za mwaka mpya na katika hafla za kidini. Katika hafla hizi, wimbo ulionukuliwa hapo juu unatumika kukemea wanajamii wenye tabia ya hasira kali na wanaojihusisha na masuala ya kiuchawi. Hizi ni tabia zenye madhara kwa mtu mmojammoja na kwa jamii nzima. Mtu mwenye tabia ya kuwa na hasira kali anashindwa kutangamana vizuri na watu, na wakati mwingine hutokea mtu huyo akachukua maamuzi ya kuua mtu mwingine au hata kujiua. Vivyo hivyo, tabia ya uchawi inakemewa sana kwani ina madhara makubwa katika jamii. Katika wimbo huu, msanii ametumia nahau ya **Kuvunja chungu** kwa maana ya kujinyonga au kujitundika. Kuvunja chungu ni adhabu anayojipa mtu bila kushurutishwa ambapo anaamua kujiua. Aidha, katika hali ya kawaida, masuala ya uchawi, kunyonga na kujinyonga ni nyeti sana na hayatakiwi kujadiliwa hadharani. Kutokana na unyeti wake, mila za utamaduni wa Wasambaa zinakataza kumtuhumu mtu kuwa ni mchawi bila ushahidi wa kutosha.

Mfano mwingine wa nahau zilizoundwa kutokana na uteuzi wa maneno maalum ni **kuja ukiwa** ambayo inapatikana katika wimbo wa **nachekea wageni na kuuia ubweni** mutawalia. Katika nukuu hapa chini muktadha uliochochea utokeaji na uteuzi wa maneno yanayounda nahau hizi umefafanuliwa vyema:

**Mf. 4.30: Wimbo kuonyesha misemo na nahau** (*kutoka ubeti wa tano*)

**KISAMBAA**

**KISWAHILI**

- |   |  |
|---|--|
| 5. Hangwe kiema hashekwa ee aa ee<br>tiweea moyo (VI) | 5. Eti kilema hachekwi ee aa ee<br>tunaangalia moyo (VI)   |
| 6. Eooe ubweni wa uia ee aa ee wagyea<br>mawazo       | 6. Eooe useja wa kukariri ee aa ee<br>unaleta mawazo       |
| 7. Eooe ubweni wa uia ee aa ee wagyea<br>mawazo (VII) | 7. Eooe useja wa kukariri ee aa ee<br>unaleta mawazo (VII) |

Katika wimbo huu kuna misemo miwili iliyotumika kuwasilishia ujumbe. Katika mshororo wa tano ubeti wa sita msanii anasema '**kilema hachekwi, tunaangalia moyo**'. Msemo huu umetumika kusesitiza umuhimu wa kuwajali watu wote bila kujali

dosari waizo nazo. Aidha, wimbo huu unaonyesha kuwa Wasambaa wanatumia nyimbo kuhamasisha suala la haki na usawa miongoni mwa wanadamu. Kwa upande mwingine nahau ya ‘**kukariri useja**’ imetumika katika wimbo wa **sura ni maua**. Katika muktadha wa wimbo huu nahau hii imetumika kuwakemea wanandoa ambao licha ya kuwa tayari wameshaoa bado wana mienendo inayofanana na ya watoto wadogo, ambao bado hawajaoa.

Kadhalika, katika mshororo wa sita msanii anasema ‘**useja wa kukariri unaleta mawazo**’. Msemu huu unawahimiza watu wazima wasiige tabia za watoto wadogo. Nahau nyingine iliyotumiwa na wasanii wa nyimbo hizi ni **kuja ukiwa**. Nahau hii imetumika katika wimbo wa **nachekea wageni** kama ifuatavyo:

**Mf. 4.31: Wimbo kuonyesha nahau “wanangu wanakula ukiwa”**

**KISAMBAA**

**MK:** Ee shekeshoke n’shekea wageni ee mame

**WK:** Wanangu waaja ukiwa

**MK:** Angwe shekeshoke n’shekea wageni wanangu waaja e mame

**WK:** Wanangu waaja ukiwa

**MK:** Shekeshoke n’shekea wageni wanangu waia e mame

**WK:** Wanangu waaja ukiwa

**MK:** Oie niikaia wanangu baba iwe

**WK:** Niikaia wanangu ee ee ee

**MK:** Niikaia wangu ee ee ee

**WK:** Niikaia wanangu ee ee ee Mghoshingwa ni beyu ajiia hotei Niikaia wanangu ee

**MK:** Niikaia wanangu ee ee ee

**WK:** Niikai wanangu ee ee ee

**MK:** Ee niikaia wanangu mame

**KISWAHILI**

**MK:** Hahah nacheka ila nachekea wageni mama

**WK:** Wanangu wanakula ukiwa

**MK:** Eti hahah nacheka la nachekea wageni wanangu wanakula mama

**WK:** Wanangu wanakula ukiwa

**MK:** Hahah nacheka ila nachekea wageni wanangu wanakula mama

**MW:** Wanangu wanakula ukiwa

**MK:** Oie ninakalia wanangu kaka

**WK:** Ninakalia wanangu ee ee ee

**MK:** Ninakalia wanangu ee ee ee

**WK:** Ninakalia wanangu ee ee ee Mheshimiwa ni kupe analia hotelini

Ninakalia wanangu ee

**MK:** Nnakalia wanangu ee ee ee

**WK:** Ninakalia wanangu ee ee ee

**MK:** Ninakalia wanangu mama

Kama inavyoonekana katika nukuu hapo juu, ‘**wanangu wanakula ukiwa**’ ni nahau iliyotumika kurejelea mateso wanayoyapata watoto kutokana na kutelekezwa na baba

yao. Katika wimbo huu baba mwenye tabia ya namna hii amesawiriwa kama **kupe** kwa kuwa badala ya kutafuta chakula aende akale na watoto wake yeye anaenda hotelini kula peke yake.

#### **4.5 Hitimisho**

Sura hii imepambanua mitindo ya lugha na dhima yake katika uwasilishwaji wa ujumbe kwa hadhira. Imeelezwa kuwa ili kutimiza lengo la kuwasilisha ujumbe kwa hadhira, fanani hutumia mikakati anuai ya mitindo ya lugha kama vile uchanganyaji misimbo, arudhi za kishairi, tamathali za usemi, mianzo na miisho ya kifomula, methali na nahau. Mikakati hii imewawezesha fanani na hadhira kuwasiliana wakati wa utendaji wa nyimbo. Kupitia matumizi ya mikakati hii utafiti huu umethibitisha kuwa nyimbo za *mdumange* zina ujumi wa kipekee unaozipambanua kama sanaa mahsusi iliyosheheni vipashio mbalimbali vya itikadi za ulimwengu wa Wasambaa. Ndani ya sura hii pia ilidokezwa kuwa matumizi ya mitindo ya lugha huambatana na viziada lugha ili kukamilisha uwasilishaji wa nyimbo. Katika sura ya tano aina mbalimbali za mitindo ya viziada lugha pamoja na nafasi yake katika utendaji wa nyimbo vimeelezwa na kujadiliwa bayana.

## SURA YA TANO

### NAFASI YA MITINDO YA VIZIADA LUGHA KWA WASANII NA JAMII YA WASAMBAA KWA UJUMLA

#### 5.0 Utangulizi

Sura hii inakusudia kujadili mitindo ya viziada lugha na nafasi yake katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Azma ya mjadala wa sura hii ni kumuwezesha mtafiti kulikabili swali la tatu la utafiti lililouliza kuwa ‘Je, mitindo ya viziada lugha ina nafasi gani katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*?’ Katika kulishughulikia suala hili mtafiti ameongozwa na misingi ya Nadharia za Utendaji wa Maigizo (Okpewho, 1992) pamoja na Semiotiki ya Kijamii (Barthes, 1964 na Eco, 1984). Kwa mujibu wa Okpewho (1992) viziada lugha ni mtindo wa kiutendaji unaotumiwa na fanani kuwasilisha ujumbe kwa hadhira usioegemea katika matumizi ya vipashio vya kiisimu. Mitindo ya viziada lugha iliyojadiliwa kwenye sura hii ni pamoja na miondoko, maleba, uchezaji dansi, muziki na uigizaji.

#### 5.1 Miondoko ya Fanani na Hadhira

Miondoko ya utendaji hujumuisha tabia za kiuigizaji na mwendo au mijongeo. Mitindo hii hudhihirishwa na fanani pamoja na hadhira kwa kutumia uso, kichwa, mikono au kiungo chochote cha mwili. Kulingana na Nadharia ya Utendaji wa Maigizo, miondoko hutumiwa na watendaji ili kuwasilisha au kufafanua ujumbe kwa hadhira kwa njia ya vitendo badala ya maneno peke yake (Okpewho, 1992; Miruka, 1994).

Utafiti huu umebaini kuwa kwa kiwango kikubwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* umeambatana na miondoko ya watendaji. Kutokana na athari za utendaji wa namna hii, hakuna wimbo hata mmoja katika nyimbo za *mdumange* ambao unaweza

kuwasilishwa kwa maneno peke yake bila kutumia miondoko ya watendaji. Miondoko hiyo imesheheni viashiria vya matendo ya kuigiza. Kwa ujumla, utafiti huu umebaini aina tatu za miondoko ya utendaji kulingana na uamilifu wake katika uwasilishaji wa nyimbo ambazo ni miondoko inayofafanua ujumbe, inayodokeza ushiriki wa hadhira na inayotambulisha mawasiliano kati ya fanani mmoja na mwingine. Sehemu ifuatayo inajadili aina hizi za miondoko ya watendaji.

### **5.1.1 Miondoko Inayofafanua Ujumbe wa Nyimbo**

Miondoko inayofanywa na watendaji wa nyimbo za *mdumange* inatekeleza majukumu mbalimbali. Moja kati ya majukumu hayo ni kufafanua ujumbe unaodhamiriwa kuwasilishwa na wimbo ndani ya muktadha mahsusi. Kwa mfano, katika wimbo wa **ninawauliza** waimbaji pamoja na wachezaji huimba kwa kuonyesha ishara mbalimbali kwa kutumia vidole, kichwa na nyuso zao. Watendaji hawa hufanya hivyo ili kufafanua ujumbe wa wimbo ambao ni kufafanua dalili za ugonjwa wa UKIMWI na madhara yake katika jamii.

Aidha, utafiti huu unatoa hoja kuwa kumekuwa na changamoto kubwa katika namna ya kuwasilisha miondoko ya watendaji kwenye lugha ya maandishi. Hii ni kwa sababu, sehemu kubwa ya miondoko ya watendaji inadhihirishwa kwa kutumia matendo badala ya maneno. Ili kukabiliana na changamoto hii, mkakati maalum wa kuwasilisha miondoko umependekezwa. Katika nukuu ifuatayo, maneno yaliyoambatana na miondoko yameandikwa kwa wino mweusi ilhali miondoko iliyodhihirishwa imeandikwa kwa *hati mlazo* ndani ya mabano:

**Mf. 5.1: Wimbo Unaoonyesha Miondoko ya Fanani na Hadhira**

1. Ninawauliza
2. Ninawauliza Gonjwa la UKIMWI duniani limetoka wapi
3. **Mara ya kwanza kuharisha** (*huinua juu kidole kimoja cha shahada mkono wa kulia*)
4. **Mara pili kutapika** (*huinua juu vidole viwili; cha shahada na cha katikati mkono wa kulia*)
5. **Mara ya tatu ni kwa heri unakwenda zako** (*huinamisha migongo yao chini na kuelekeze kidole cha shahada ardhini*)

Kama inavyoonekana katika nukuu hapo juu, watendaji wanapofikia sehemu inayosema “**mara ya kwanza kuharisha, mara ya pili kutapika**” huinua na kunyoosha juu kidole kimoja na vidole viwili mutawalia. Watendaji hufanya hivyo ili kufafanua ujumbe kuwa dalili ya kwanza ya ugonjwa wa UKIMWI ni kuharisha na dalili ya pili ni kutapika. Kadhalika wanapofika sehemu inayosema “**mara ya tatu ni kwa heri unakwenda zako**” hunyoosha vidole vyao kuelekea kwenye ardhi. Kutokana na utendaji huu waimbaji pamoja na wachezaji husisitiza dhamira kuwa UKIMWI unaua. Bila shaka, uigizaji unaofanywa na watendaji kwa kutumia mikono, vidole, migongo na macho unasisitiza maudhui ya kuwataka wanajamii wachukue tahadhari kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI.

Ingawa wakati wa kuimbwa wimbo huu watu hufurahia mapigo ya kimuziki yatokanayo na sauti za waimbaji, ala za muziki na uchezaji, maudhui ya utendaji wa miondoko ya watendaji yanatoa tahadhari kwa wanajamii dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Hii inaonyesha kuwa pamoja na mambo mengine, dhima ya utendaji wa namna hii ni kuielimisha na kuiburudisha jamii.

Kadhalika miondoko ya watendaji imetumika kuisitiza na kufafanua ujumbe wa fanani kwa hadhira katika wimbo wa **mheshimiwa**. Katika wimbo huu watendaji wanatumia ishara mbalimbali kufafanua na kuelezea hisia zao kuhusu muundo wa serikali unaopendekezwa kwenye katiba mpya. Hisia hizo huwasilishwa kwa kutumia

ishara za viungo vya mwili kama vile mikono, kichwa na mgongo kama ilivyoonyeshwa hapa chini:

**Mf. 5.2: Miondoko katika wimbo wa Mheshimiwa**

1. Tusije sahai bunge la katiba
2. Tunaomba liwe la amani
3. Twasubiri katiba safi
4. Wale wanaohitaji
5. **Kuwa na serikali tatu** (*hunyoosha juu vidole vitatu vya mkono wa kulia*)
6. Tunasema
7. **Wana lao jambo** (*hunyoosha na kuelekezea hadhira kidole cha shahada*)
8. Serikali tatu ni mzigo
9. Ni sawa na kulea watoto
10. **Mapacha walio watatu** (*huina na kuelekeza mikono yao miwili mgongoni*)
11. **Ni mzigo usiobebeka** (*hujitwisha mikono yao miwili kichwani*)

Kulingana na nukuu ya wimbo hapo juu matumizi ya mtindo wa miondoko yanadhihirika waziwazi katika mshororo wa tano, saba, kumi na kumi na moja. Katika mshororo wa tano, maneno **kuwa na serikali tatu** yameambatishwa na miondoko ya watendaji. Watendaji walinyoosha juu vidole vitatu vya mkono wa kulia kufafanua muundo wa serikali tatu inayoelezwa kwenye wimbo. Aidha, katika mshororo wa saba maneno **wana lao jambo** yamefungmanishwa na miondoko ya watendaji kwa hunyoosha na kuelekezea hadhira kidole cha shahada kama ishara ya onyo na tahadhari kuhusu hatari ya kuwa na serikali tatu. Katika kushadidia ugumu wa kuendesha serikali tatu waimbaji pamoja na wachezaji wanapofikia sehemu inayosema **mapacha walio watatu** huinama na kuelekeza mikono yao miwili mgongoni, kuonyesha ishara ya kubeba mtoto, na kulea, kisha humaliza ubeti kwa kusema “**ni mzigo usiobebeka**” huku wakiwa wamejitwisha mikono yao miwili kichwani.

Wimbo huu mara nyingi huimbwa katika miktadha ya kisiasa, hususan katika hafla za mbio za mwenge na kampeni za uchaguzi. Katika utafiti huu wimbo uliimbwa kwenye mbio za mwenge ambapo wasanii walitoa maoni yao kuhusu mchakato wa kupata katiba mpya nchini Tanzania. Katika muktadha huo mambo mengi hufasiriwa kulingana na itikadi ya siasa za vyama vingi, demokrasia na utawala bora. Ni kutokana na muktadha huu ambapo wasanii huzitumia nyimbo za *mdumange* kama jukwaa la majadiliano baina yao na viongozi. Aidha, wananchi pia hupata fursa ya kutoa maoni yao kuhusu harakati za kisiasa zinazoendelea nchini. Mtazamo wa wasanii ni kuwa uendeshaji wa serikali tatu ni mgumu, ikilinganishwa na uendeshaji wa serikali mbili zilizopo kwa sasa (serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

Vilevile matumizi ya miondoko ya waimbaji yamejitokeza katika wimbo wa **sijadhulumu haki ya mtu**. Mtafiti alishuhudia wimbo huu ukiimbwa kwenye sherehe za harusi katika kijiji cha Lwandai. Kulingana na muktadha huu, wimbo husika huweza kuwa na maana ya jumla kuhusu maisha kwa ujumla wake, au huweza kuwa na maana ya kutoa nasaha kwa bi harusi. Katika kuwasilisha ujumbe huu wasanii hutumia maneno pamoja na matendo (miondoko) kama inavyoonekana hapa chini:

**Mf. 5.3: Miondoko katika wimbo wa “Sijadhulumu haki ya mtu”**

**KISAMBAA**

1. Hati uzaja onгаа
2. Oiye hati uzaja ee
3. Hati uzaja onгаа
4. baba e hati uzaja ee
5. Sijie cha mntu
6. **Naasona shanga**

**KISWAHILI**

1. ikiwa umedhumu sema
2. Sema tafadhali ikiwa umekula
3. Ikiwa umedhulumu sema
4. Kaka ikiwa umedhulumu haki ya mtu sema tafadhali
5. Sijadhulumu haki ya mtu
6. **Ninalamba udongo** (*huinama, husugua kidole ardhini na hukilamba*)

Kulingana na nukuu hapo juu, miondoko ya watendaji inabainika katika sehemu mbalimbali za wimbo. Msanii na washiriki wengine wanapofika katika sehemu



isemayo **naasona shanga** huinamisha migongo yao huku wakiashiria kuchukua udongo ardhini kwa kutumia kidole chao cha shahada mkono wa kulia, halafu huashiria kulamba kidole chenye udongo, na hunyoosha mkono pamoja na kidole cha shahada kuelekea mbinguni. Kulingana na maoni ya watafitiwa, **sijie cha mtu** ina maana sijala mali ya mtu au sijamdhulumu mtu. Dhuluma inayorejelewa katika wimbo huu huweza kuwa kitendo cha zinaa (ama kwa mume au mke) endapo wimbo utaimbwa kwenye harusi au huweza kurejelea mambo mengine ya kijamii kama vile wizi, unafiki, uongo na utawala mbaya endapo utaimbwa nje ya muktadha wa sherehe za harusi.

Kulingana na utafiti huu, miondoko ya kulamba udongo imetumika kuashiria hali ya kula kiapo. Kwa mujibu wa desturi za Wasambaa, mtu anapotakiwa kuthibitisha ukweli wa jambo huamriwa kula kiapo kwa njia ya kugusa udongo kwa kidole chake, kisha kukilamba kidole hicho, na kukiinua juu. Wakati wa kufanya hivyo, mtu huyo huwa anasema “haya ninayoyasema ni ya kweli, ikiwa si kweli basi udongo huu nilioulamba unilaani”. Aidha, ni kosa kubwa kwa mtu yeyote kuiba mali ya mtu mwingine, na ikibainika hivyo mtu huyo atalipishwa faini. Kama anayetuhumiwa kosa atakana, italazimika kula kiapo.

Kwa ujumla, miondoko ya watendaji iliyojadiliwa hapa imeathiriwa na muktadha wa kiutendaji. Kwa mfano, muktadha wa kisiasa umesaidia kutafsiri ishara zitokanazo na miondoko ya wasanii katika nyimbo za **mheshimiwa** na **ninawauliza**. Kwa upande mwingine, muktadha wa sherehe za harusi umesaidia kuzua maana nyingi katika ishara zinazowasilishwa kwenye wimbo wa **sijadhulumu haki ya mtu**. Miondoko inayotumiwa na watendaji katika wimbo wa **mheshimiwa** imesaidia kujenga itikadi ya Wasambaa kuhusu muundo wa serikali tatu, ilhali katika wimbo wa **ninawauliza**

wasanii wametumia miondoko hiyo kujenga falsafa yao kuhusu afya, maradhi na kifo. Kadhalika, miondoko iliyotumika katika wimbo wa **sijadhulumu haki ya mtu**, imeibua ishara zinazoakisi mtazamo wa Wasambaa kuhusu motifu ya dhambi na mapatilizi ambapo kila mtenda dhambi huapizwa, hulipizwa kisasi na hupatwa na laana. Kwa ujumla, utendaji unaambatana na miondoko ya watendaji umesaidia kufafanua ujumbe wa nyimbo na kujenga mtazamo wa Wasambaa kuhusu falsafa ya uongozi bora, kutunza afya, na uaminifu kwa wanandoa na jamii kwa ujumla.

### 5.1.2 Miondoko ya Hadhira Kupongeza Utendaji wa Fanani

Kando na kufafanua ujumbe wa fanani, miondoko pia hutumiwa kwa minajili ya kuchochea na kudhihirisha ushiriki wa hadhira. Katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* miondoko hii imebainika kwa kutumia ishara mbalimbali hususan kupeana mikono, kuonyesha dole gumba na kukumbatiana. Aina hizi za miondoko zinaonekana wazi wazi katika vielelezo vifuatavyo:



**Kielelezo na 5. 1: Picha Inayoonyesha Ushiriki wa Hadhira**

Katika kielelezo hapo juu picha za watu wawili waliolekana zinaonyesha kuwa wanasalimiana au wanapeana mikono. Hii ni ithibati kuwa washiriki wa utendaji wa nyimbo za *mdumange* (rejea mtu mwenye mshale mweupe) wanawapongeza wasanii (rejea mtu mwenye mshale mweusi) kwa kupeana nao mikono. Miondoko hii ilidhihirika wakati wa uwasilishaji nyimbo za *mdumange* kwenye hafla za mbio za mwenge zilizofanyika Aprili 2016, katika kijiji cha Magoma. Kitendo cha hadhira kupeana mikono na fanani wakati wa utendaji kinaonyesha athari ya utendaji wa nyimbo katika kuibua hisia za shangwe na furaha kwa jamii. Pia hii ni ishara ya hadhira kumpongeza fanani kutokana na usanii wake.

Miondoko ya washiriki kupeana mikono pia ilidhihirika kwa upande wa wasanii wanawake. Katika kielelezo kifuatacho hadhira ileile inaonekana ikipeana mikono na wasanii wanawake.



**Kielelezo na 5. 2: Picha Inayoonyesha Hadhira ikipeana Mikono na Wachezaji**

Katika kielelezo hiki, picha zilizozungushiwa duara zinaonyesha mwanamume akipeana mikono na wanawake wanaocheza. Hii ni picha iliyochukuliwa wakati wa utendaji wa nyimbo za *mdumange* kuonyesha jinsi hadhira inavyoshiriki kwa kutumia miondoko ya kusalimiana na kupongezana na wasanii. Matumizi ya mbinu hii huwatia moyo wasanii na kuufanya utendaji mzima uvutie. Mbali na miondoko ya kupeana mikono na fanani, hadhira pia huweza kuwakumbatia na kuwashangilia wasanii kwa kuwapigia vigelegele. Nadharia ya Utendaji wa Maigizo inaeleza kuwa utendaji wa fasihi simulizi hufanyika kwa njia ambayo huwafanya hadhira na fanani kuwa kitu kimoja. Kitendo cha fanani na hadhira kupeana mikono huwaweka karibu na kuaminiana na hatimaye kufurahia tukio la kifasihi ambalo linatendeka kwa wakati huo. Kitendo hiki pia humfanya fanani kujituma zaidi katika utendaji akiamini kuwa kile ambacho anakifanya kinathaminiwa na hadhira yake.

### **5.1.3 Miondoko Inayowezesha Mawasiliano Miongoni mwa Fanani**

Mbali na miondoko inayotumiwa kufafanua ujumbe, kuonyesha pongezi za hadhira kwa fanani utafiti huu pia umebaini kuwa miondoko inatumika kwa minajili ya kuimarisha mawasiliano kati ya wasanii wenyewe kwa wenyewe. Kwa mfano, ikiwa MK angetaka kusaidiwa kuimba na mmojawapo kati ya wasanii wenzake waliopo asingeomba msaada huo kwa kutamka maneno, wala asingeacha kuimba kwanza bali wakati utendaji unaendelea huwa anaelekeza ombi hilo kwa kutumia ishara za uso, kichwa, macho na mikono kama inavyoonekana katika kielelezo kifuatacho:



Muimbaji  
anawasili  
ana kwa  
ishara na  
muimbaji  
mwingine

### **Kielelezo na 5.3: Picha Inayoonyesha Mawasiliano ya Wasanii kwa ishara**

Katika kielelezo hiki, MK anawasiliana kwa ishara au muondoko wa kunyoosha kidole na kumtazama muimbaji mwingine ili asaidiwe kuimba. Kulingana na ukweli huu, ni desturi ya wapiga ngoma kumtazama MK wakati mwingi. Aidha, wapiga ngoma wanapoona MK amechoka na ametoa ishara maalum kwa muimbaji mwingine, huhamisha nadhari zao kutoka kwa muimbishaji wa kwanza na kuzielekea kwa muimbishaji mpya. Mtindo huu unathibitishwa pia na Omari Shauri ambaye mara nyingi ameshiriki utendaji wa nyimbo za *mdumange* kama MK:

Ninapoimbisha naweza kumuashiria mchezaji yeyote aanzishe wimbo mpya, hivyo hata wapigaji ngoma humfuata yeye kwani mpiga ngoma asipofuatisha mwendo wa muimbishaji ladha ya mdumamnge huparaganyika.

Nukuu ya bwana Omari inaonyesha kuwa miondoko ya wasanii huwasaidia kuimarisha mawasiliano baina yao na kuhakikisha kuwa utendaji unafanikiwa.

Kadhalika, wasanii hutumia miondoko maalum kuwaamrisha wasanii wenzao watekeleze masuala nyeti ya kiutendaji. Kwa mfano, wakati wa uwasilishaji wa

nyimbo za *mdumange* kwenye sherehe za harusi zilizofanyika katika kijiji cha Kihitu, mtafiti alishuhudia MK akiwaamrisha wasanii wachezaji waonyeshe miduno maalum ya kiuchezaji. Katika kufanya hiyo hakuongea nao kwa maneno bali alionyesha kwa ishara za vidole pamoja na filimbi (taz. kielelezo hapa chin)i:



**Kielelezo na 5.4: MK akiwaamrisha wasanii**

Kielelezo hapo juu kinaonyesha jinsi MK anawasiliana na wasanii wengine hususan wachezaji kwa kutumia filimbi na ishara za mikono. Kutokana na mawasiliano yanayofanywa kwa ishara kati ya muimbaji na wasanii wengine, wasanii wachezaji na wasanii wanaopiga ngoma daima wanakuwa makini kuona kuwa kile anachowaza muimbaji ndicho kinatokea katika jukwaa la utendaji. Aidha, kutokana na mbinu hii, wasanii wachezaji huweza kucheza kwa kunengua, kutembea, au kusimama kulingana na maelekezo ya muimbaji mkuu.

Kadhalika, ikitokea, wapiga ngoma wamejisahau, mwimbishaji wa kwanza huwakumbusha kwa kutumia ishara za namna hiyohiyo. Waimbishaji huelekeza

macho na mkono yao kwa wasanii wengine endapo wangehitaji kusaidiwa. Hii ni ishara au msimbo maalum unaotumiwa na wasanii wa nyimbo za *mdumange* kuimarisha mawasiliano baina yao. Vilevile, wasanii waimbaji huwa wanaendelea kuwatazama wapiga ngoma kwani utendaji wa nyimbo hizi unaambatana na uimbaji na upigaji wa ngoma. Katika hali ya kutazamana, wasanii hupeana ishara za namna mbalimbali kuhusiana na mwenendo mzima wa utendaji. Nadharia ya Utendaji wa Maigizo inaeleza kuwa utendaji katika nyimbo unawataka wasanii kuwa wazingativu sana ili kuhakikisha utendaji unakamilika. Uzingativu huo unawataka kutumia milango yao ya fahamu na kuchukua maamuzi ya haraka ili kuhakikisha mambo hayaharibiki. Kwa upande wa mwimbishaji, huyu ndiye ambaye anatakiwa kuwa makini kwelikweli kwa kuwa baadhi ya waimbaji wanaweza kujisahau na kuharibu utendaji na yeye ndiye mtu wa kuwakumbusha. Tumeona katika kielelezo hapo juu namna mwimbashaji anavyofanya kazi yake kwa umakini mkubwa na kuwezesha utendaji kukamilika na dhamira lengwa kuifikia jamii.

## **5.2 Utendaji wa Kimuziki**

Mitindo ya utendaji wa kimuziki ina nafasi kubwa sana katika uwasilishaji wa ujumbe na maana katika nyimbo na fasihi simulizi ya Kiafrika kwa ujumla. Kulingana na Alembe (2002) muziki ndio uti wa mgongo wa waimbaji wa tendi simulizi. Umuhimu wa muziki katika fasihi simulizi ya Kiafrika upo katika kuchochea hamasa za ushiriki wa watendaji pamoja na kukoleza ujumbe unaowasilishwa katika fasihi hiyo. Kwa hivyo, mfungamano wa muziki na nyimbo za Kiafrika unapatikana katika utendaji wake. Mapigo ya kimuziki yana dhima kubwa katika kusesitiza ujumbe wa nyimbo, kuufanya ujumbe huo ueleweke vyema na kuufanya utendaji mzima uvutie.

Kutokana na athari ya mfungamano baina ya maana na sauti zinazojitokeza wakati wa uwasilishaji wa nyimbo, utafiti huu unatoa hoja kuwa muziki ni kiambajengo muhimu cha utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Hivyo basi, ili utendaji wa kifasihi simulizi ufanikiwe, muziki na maneno yanayotamkwa katika nyimbo vinahitaji kuwa na muwala wa namna maalum. Katika uwasilishaji wa tanzu mbalimbali za kifasihi simulizi kwa kiwango kikubwa hadhira pamoja na washiriki wengine huupata ujumi wa fasihi hiyo kutokana na kiwango cha ubora wa sauti za kimuziki zinazosikika wakati wa kuimba na wakati wa kutumia ala za muziki.

Aidha, Alembe anaongeza kwa kusema kuwa utendaji wa nyimbo za fasihi simulizi ya jamii nyingi za Kiafrika unaambatana na matumizi ya aina mbili za muziki. Kuna muziki utokanao na ala za muziki na pia kuna muziki utokanao na sauti mbalimbali za mitindo ya wimbaji. Katika sehemu ifuatayo tumejadili aina hizi mbili za utendaji wa kimuziki kwa kurejelea utendaji wa nyimbo za *mdumange* miongoni mwa jamii ya Wasambaa.

### **5.2.1 Muziki wa Sauti za Uimbaji**

Sauti za uimbaji zina nafasi kubwa katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Mojawapo ya dhima zake ni kusaidia kutoa mapigo ya kimuziki wakati wa uwasilishaji wa nyimbo husika. Aidha, sauti hizo pia huvuta umakini wa hadhira pamoja na kusesitiza ujumbe unaowasilishwa kwa hadhira. Kadhalika, muziki wa sauti una dhima ya kutambulisha muktadha wa kutendaji baina ya fanani na hadhira. Kwa ujumla, ujumi wa utendaji wa nyimbo za *mdumange* unaimarishwa kwa kutumia vipashio mbalimbali vya muziki wa sauti za wimbaji kama vile mifumo ya uimbaji wa nyimbo, ubora wa sauti na mawimbi ya sauti. Vipashio vyote hivi husaidia kukoleza na kunogesha fani na maudhui ya nyimbo za *mdumange*.



Uimbaji wa nyimbo za *mdumange* unafanywa kwa kufuata mfumo wa upokezanaji zamu. Kulingana na mfumo huu suala la uimbaji linategemea ushirikiano baina ya mwimbishaji na waitikiaji wake. Wimbo mmoja au kikundi kimoja cha *mdumange* kinaweza kuwa na muimbishaji mmoja au zaidi. Aidha, ingawa hakuna masharti yoyote ya nani awe mwimbishaji, katika vikundi vingi vya kisanaa tulivyochunguza tumebaini kuwa waimbishaji wake ni wanaume. Hii inaashiria kuwa sanaa ya nyimbo za *mdumange* ina muelekeo wa kumilikiwa na jinsia ya kiume zaidi kuliko jinsia ya kike. Kwa upande mwingine, wanawake wameonekana kushiriki kama waitikiaji, washangiliaji na wachezaji. Hali hii inawakilisha hali ya kutegemeana baina ya wanawake na wanaume katika sanaa ya nyimbo za *mdumange* na katika nyanja nyingine za kimaisha kama vile uongozi, malezi, uzazi na mapenzi. Kamwe, hakuna jinsia inayojitosheleza au inayoweza kufanya kazi kwa ufanisi bila kupata ushirikiano wa jinsia nyingine.

Mwimbishaji ndiye mwenye mamlaka ya kuteua aina ya wimbo kulingana na aina ya tukio, na pia ndiye mwenye mamlaka ya kuchagua mfumo wa uimbaji. Anaweza kuanzisha uimbaji kwa kutumia mawimbi ya juu, kati au ya chini kutegemea ujumbe anaotaka kuwasilisha. Vilevile, mwimbishaji anao uhuru wa kuamua muda unaofaa kutumika katika wimbo mmoja. Pamoja na kuanzisha wimbo, mwimbishaji pia analo jukumu la kudokeza ubeti unaofuata katika wimbo.

Kwa upande mwingine, mapigo ya kimuziki katika nyimbo za *mdumange* pia yanapata uhai wake kutokana na ushiriki wa hadhira. Hadhira inaweza kuitikia kwa kukariri maneno yaliyotamkwa na fanani bila kubadili chochote au inaweza kukariri baadhi tu ya maneno ya fanani. Kadhalika, hadhira inaweza kuitikia kwa kukariri maneno yaliyotamkwa na mwimbishaji pamoja na kuongeza maneno mengine. Njia

hii ya kuongeza maneno mengine huathiri mpangilio wa wimbo, kwani kutokana na mfumo huu kianzio kinakuwa kifupi na kiitikio kinakuwa kirefu.

Ingawa mara nyingi muundo unaotumika katika kuimba ni wa kiupokezanaji zamu, ni vema kuelezea kuwa si mara zote mfumo huu unatumika mwanzo hadi mwisho. Kuna wakati waimbishaaji wa nyimbo wanaonyesha ubunifu wao kwa njia ya kughani mashairi kwa kushirikiana na fanani, bila uchezaji wala upigaji ala wa aina yoyote. Kiwango cha matumizi ya muundo huu si kikubwa sana kwani mara nyingi uimbaji wa nyimbo za *mdumange* unaambatana na uchezaji pamoja na upigaji wa ala. Kuwako kwa mfumo huu wa uimbaji kunaonyesha kuwa nyimbo za *mdumange* zinaweza kughanwa tu bila kuhusishwa na mapigo ya ala za muziki au zinaweza kuwasilishwa kwa njia ya uimbaji unaambatana na upigaji ala za muziki pamoja na uchezaji.

Uteuzi wa mfumo wa uimbaji haufanyiki kiholela, bali unatokea kulingana na mikakati ya kuwasilishaji katika muktadha mahsusi wa kiutendaji. Fanani wa nyimbo za *mdumange* huamua kutumia mfumo wa kughani mashairi kwa minajili ya kutoa ilani, dhamira au ujumbe unaotarajiwa kuwasilishwa kwenye nyimbo. Kwa hiyo, wakati wa kughani inatarajiwa kuwa hadhira iko makini zaidi na kuna usikivu mkubwa kwani hakuna kelele wala hakuna ngoma zinazolia. Mwimbishaaji huwaongoza wasanii wenzake katika kufafanua ujumbe kwa njia ya kughana mashairi. Wakati wa kughani mashairi kwa njia hii, jukumu kuu la mwimbishaaji ni kudokeza mwanzo, muendelezo na hitimisho la wimbo. Kwa njia ya kudokeza, hadhira hudakia na kuungana na mwimbishaaji, badala ya kusubiri mwimbishaaji amalize ubeti au wimbo mzima.

Kadhalika, mfumo wa kuimba kwa kutoa sauti za kughani bila kutumia ala yoyote ya kimuziki hutumiwa na fanani inapotokea ngoma au ala nyingine ya kimuziki inahitaji ukarabati fulani au kama kuna dosari yoyote ya kiufundi imejitokeza katika safu ya ala na uchezaji. Katika mazingira hayo, mwimbishaji huchukua jukumu la kuimba nyimbo kwa njia ya kughani. Dhima kuu ya uimbaji wa namna hii ni kutangaza na kufafanua ujumbe wa wimbo ambao muda si mrefu utawasilishwa kwa njia ya kuimbwa na kucheza. Kwa hivyo, hata kama mbinu ya kughani inatumika, mbinu hii hutumika sambamba na mbinu ya kuimba, na kucheza ala za muziki.

Pamoja na sauti za uimbaji, utendaji wa nyimbo za *mdumange* unaambatana pia na aina nyingine za sauti zisizotoa maneno maalum hususan ufaraguzi, vigelegele na miluzi . Kwa kiwango kikubwa sauti hizo zinatokana na mbinu ya ufaraguzi wa fanani na hadhira. Ufaraguzi sio mtindo wala mbinu ya kiutendaji peke yake, bali ni mkakati maalum wa kisanaa unaotumiwa na wasanii kwa minajili ya kutimiza matakwa anuai ya kiujumi. Ni mkakati kwa kuwa wasanii hutumia sauti na viungo vyao vya mwili kuelezea tajriba zao kisanii. Katika nyimbo za *mdumange*, ufaraguzi umetumiwa kwa njia mbalimbali hususan katika kutoa sauti za kimuziki.

Ufaraguzi hutumika kama mbinu ya utunzi na uwasilishaji kwa wakati mmoja. Nyimbo za zamani zinakaririwa, zinaendelezwa na kubadilishwa kwa kuchagua na kupangilia upya vipashio mwafaka vya mishororo, au maneno katika nyimbo. Wakati huohuo, nyimbo mpya kabisa zinatongolewa kila mara kunapokuwa na tukio au sherehe kama vile harusi, sikukuu za kidini na katika hafla za kisiasa. Kulingana na matumizi ya mbinu hii, kipande chochote cha wimbo wa *mdumange* hakiwezi kurejelewa kwa namna ileile kinapowasilishwa kwenye miktadha tofautitofauti. Hata kama wimbo ulikuwa na maudhui ya namna moja, lakini unapotendwa kwenye

miktadha tofautitofauti vipashio mbalimbali vya wimbo huo hubadilishwa ili kukidhi mahitaji ya kusudio la utendaji.

Kando na ufaraguzi, mapigo ya kimuziki pia hudhihirishwa kwa kutumia sauti zinazodhamiriwa kusesitiza dhamira au ujumbe, na pia zinatolewa kwa minajili ya kushangilia utendaji wa waimbaji, wapiga ngoma na wachezaji. Miongoni mwa sauti hizo ni vigelegele, miluzi na maoni ya mwimbaji au hadhira. Mara nyingi wakati utendaji ukiwa unaendelea, washiriki hupiga vigelegele pamoja na miluzi. Ingawa hatuwezi kuziwakilisha sauti hizi kimaandishi, lakini ni dhahiri kuwa athari ya utokeaji wake katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni kubwa. Kwa mfano, sauti za miluzi zinazosikika katika wimbo huongeza ladha ya kimuziki, na kuchochea hisia za ubunifu wa fanani na ushiriki wa hadhira. Sauti hizo ni ishara kuwa washiriki wanafurahia utendaji unaoendelea. Kadhalika, vigelegele vinavyopigwa huashiria hisia zao katika utendaji na ni ithibati ya kuwapongeza waimbaji, wachezaji na wapiga ala za muziki. Sauti hizi vilevile, humfanya mwimbaji apunguze kasi ya kuimba kwa sekunde kadhaa, ili sauti ya uimbaji wake isikinzane na sauti ya wapiga vigelegele.

Vilevile, mwimbishaji anaweza kuacha kuimba kwa sekunde kadhaa na kutoa maoni ya waziwazi kwa hadhira mithili ya mtu anayetoa hotuba. Maoni yake yanaweka msisitizo juu ya ujumbe unaowasilishwa kwenye wimbo husika. Anaweza kutoa maoni kwa kutumia lugha ileile anayoitumia wakati wa kuimba, au anaweza kutumia lugha nyingine anayoifahamu na inayofahamika zaidi miongoni mwa hadhira.

Sauti zinasaidia kupasha habari na kutoa ujumbe kulingana na hali au muktadha kama ni wa furaha, huzuni au maombolezo. Sauti zinashirikiana na mfumo wa lugha ishara katika kutatua utata utokanao na kauli zinazonenwa wakati wa utendaji wa nyimbo.

Kuwako kwa sauti za uimbaji kunasisitiza namna lugha ya kisanaa inavyoshirikiana na lugha ishara katika kuwasilisha nyimbo. Aidha, lugha ishara zinazotumiwa na fanani huwasilisha na kudhibiti mpangilo wa taarifa na kuufanya uwasilishaji ubadilikebadilike kulingana na makusudio ya utendaji husika. Mawimbi ya sauti na msisitizo wa sauti hizo ni vidokezo mwanana vya hisia za waimbaji pamoja na mtazamo na itikadi zao. Kwa hiyo, katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*, maana hupatikana kutokana na utangamano wa vipashio vya utendaji unaotumia lugha ya kisanaa na lugha ishara ndani ya muktadha maalum wa kijamii.

Kadhalika, kutokana na ladha ya kimuziki, fanani wa nyimbo za *mdumange* hutumia ujuzi wake na ustadi wa hali ya juu kuumba maana kwa kutumia sauti yake. Sauti nyorororo na iliyochangamka ikiambatana na maneno maalum huvutia hadhira na pia hunogesha mpangilio wa maana iliyokusudiwa. Zana zote hizi huwa kama nyenzo muhimu zinazomsaidia fanani kuwasilisha ujumbe maalum kwa njia ya nyimbo, hususan zinapochanganyika na matumizi ya ala za muziki. Okpewho (1992) anaeleza kuwa utendaji katika fasihi simulizi hujitokeza bayana kutokana na matumizi ya sauti ya mwimbaji pamoja na waitikiaji. Fanani katika wimbo huimbisha wimbo kwa sauti ya kupanda na kushuka yote hii ikiwa na lengo la kuisitiza dhamira fulani kwa hadhira iliyokusudiwa. Mawazo haya pia yanaungwa mkono na wana Nadharia ya Utendaji wa Maigizo pale wanapodai kuwa sauti ni hazina muhimu katika kufanikisha utendaji wa fasihi simulizi ikiwemo nyimbo. Hii inatokana na ukweli kuwa fasihi simulizi hutumia lugha inayotolewa kwa sauti za mdomo. Jambo hili linaloonyesha kuwa sauti ni kitu muhimu sana katika utendaji wa nyimbo kwa jumla, na za *mdumange* kwa umahsusi wake.


## **5.2.2 Muziki wa Ala katika Nyimbo za Mdumange**

Pamoja na muziki wa sauti, utendaji wa nyimbo za *mdumange* pia huambatana na matumizi ya ala mbalimbali za kimuziki. Tunaweza kuzigawa ala hizo katika makundi mawili kutegemea jinsi zinatumiwa kutoa sauti na mapigo ya kimuziki. Makundi hayo ni ala zinazotoa sauti za kimuziki kwa njia ya kupigwa na zinazotoa muziki kwa njia ya kupulizwa. Ala zinazopigwa ni ngoma na manyanga ilhali ala zinazopulizwa zinajumuisha vipaza sauti, filimbi, pembe au gunda na tarumbeta. Kati ya aina zote hizi za ala za muziki, ngoma ndicho chombo kikuu kinachotumika kuzitambulisha nyimbo za *mdumange* kama sanaa maalum ya kiutendaji. Hii ni kwa sababu bila ya ngoma hakuna utendaji wa nyimbo za *mdumange*.

### **5.2.2.1 Ala Zinazotoa Sauti za Kimuziki kwa Njia ya Kupigwa**

#### **5.2.2.1.1 Ngoma za Asili**

Kuna makundi mawili ya ngoma zinazotumika katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Kuna ngoma za asili na ngoma za kisasa, zinazojulikana kama ngoma za bendi. Aidha, utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwa kutumia ngoma za asili unahusisha ngoma za aina tatu kwa wakati mmoja. Ngoma hizi zimetofautishwa kutokana na ukubwa wa umbo lake pamoja na sauti zinazotokana na ngoma husika. Kwa ufupi, utendaji wa nyimbo za *mdumange* unahusisha ngoma za namna nne kwa wakati mmoja kama inavyoonekana katika kielelezo hapa chini:



**Kielelezo na 5.5: Maumbo ya ngoma za Utendaji wa Nyimbo za *Mdumange***

Kielelezo hicho hapo juu kinaonyesha maumbo mbalimbali ya ngoma zinazotumika katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Kama inavyoonekana hapo juu namba moja ni goma kuu ambayo Wasambaa huiita *goma*. Ngoma hii ina urefu wa kati ya futi 3 mpaka 4, na imetengenezwa kwa kutumia ndoo au pipa la chuma. Ndoo hiyo inaweza kuwa imekatwa ufuniko wa upande mmoja au inaweza kuwa imeondolewa funiko pande zote mbili. Baada ya hapo, huchukuliwa ngozi ya mnyama (mara nyingi ni ngozi ya mbuzi au ng'ombe) kisha hukazwa kwa kutumia kamba za ngozi nyingine kuhakikisha kuwa wakati ikipigwa inatoa sauti.

Kadri ngoma itakavyokuwa na kipenyo kikubwa ndivyo uzito wa sauti yake utakavyokuwa mkubwa. Kwa hiyo, wasanii huhakikisha kuwa kipenyo cha ndoo au pipa la ngoma hii ni kikubwa kuliko ngoma nyingine. Kulingana na muundo wake, ngoma hii hutoa sauti nzito zaidi ikilinganishwa na ngoma nyinginezo. Katika kielelezo hiki ngoma kuu ziko mbili, moja inatumika na nyingine imewekwa kama ya akiba.

Kwa upande mwingine kielelezo kinaonyesha kuwa mbali na ngoma kuu kuna ngoma nyingine tatu. Ngoma hizo zina ukubwa wa wastani, na katika kielelezo hiki kuna ngoma namba mbili, tatu na nne. Ngoma namba mbili iko kuliani mwa mpiga ngoma. Aidha, ngoma namba tatu iko upande wa kushoto. Maumbo ya ngoma namba mbili na namba tatu ni ya ukubwa wa wastani. Aidha, utaratibu wa kutengeneza ngoma hizi unafanana sana na wa kutengeneza ngoma kuu. Tofauti yake ni ukubwa wa kipenyo cha ndoo au pipa. Kutokana na udogo wa kipenyo cha ndoo/pipa, ngoma hii hutoa sauti kali na nyororo ikilinganishwa na ngoma kuu. Aidha, ngoma kuu na ngoma ya katikati hupigwa na mtu mmoja kwa kutumia mikono yote miwili wakati wa utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Midundo ya ngoma hizi mbili huweza kuimarishwa kwa kufuatishiwa na mapigo ya kimuziki yanayotokana na upigaji ngoma kwa kutumia fimbo ama pembezoni mwa ngoma kuu au pembezoni mwa ngoma ya kati na kati.

Picha na. 4 inaonyesha umbo la ngoma ndogo kabisa ijulikanayo kama *Mkibi*. Jina la ngoma hii limetokana na uigizaji wa sauti inayosikika wakati wa kupigwa kwake. Kimuundo, ngoma hii ni ndogo kabisa kuliko ngoma nyingine zilizokwishaelezwa. Pia, ngoma hii imetengezwa kwa kutumia mti mkubwa ambao umechongwa na kutobolewa upande mmoja. Tundu lililopatikana katika kipande hiki cha mti hufunikwa kwa kutumia ngozi ya mnyama. Kutokana na muundo wake, ngoma hii hutoa sauti nyororo zaidi kuliko aina nyingine za ngoma. Aidha, ngoma hii inapigwa kwa kutumia mikono yote miwili, na kwa hivyo mtu anayepiga ngoma hii hana uwezo wa kupiga ngoma nyingine kwa wakati mmoja kwa kuwa midundo yake hupigwa kwa mwendo kasi zaidi. Hatimaye, utendaji wa nyimbo za *mdumange* unahusisha ngoma za aina tatu, zinazopigwa na watu watatu au wawili kwa wakati mmoja. Ngoma kuu na ngoma ya kati na kati zinapigwa na mtu mmoja au wawili, ilhali *mkibi* au ngoma ndogo kabisa inapigwa na mtu mwingine mmoja.



Kulingana na Wasambaa waliohusika katika utafiti huu, matumizi ya ngoma za asili yaliasisiwa na wahenga zamani sana tangu kabla ya ukoloni. Ngoma hizo zilitumika kwenye shughuli mbalimbali za kijadi kama vile matambiko, miviga na kwenye shughuli za kiuganga, hususan *pungwa*. Kadhalika, matumizi ya ngoma za asili yanahusishwa na utawala wa kijadi uliokuwako katika jamii ya Wasambaa siku nyingi kabla ya utawala wa kikoloni.

Kwa hiyo, matumizi ya ngoma za asili katika nyimbo za *mdumange* yanasawiri mila na utamaduni wa asili wa Wasambaa. Utamaduni huo unaenzi maisha asilia na turathi jadiya za Wasambaa kuhusu utawala, uganga, na sherehe mbalimbali za ibada za matambiko ya kijadi. Kadhalika, ngoma za asili zinaashiria dhamira ya kuendeleza na kuhamasisha ustawi wa utamaduni wa kijadi katika enzi hizi za utandawazi, sayansi na teknolojia. Pia ni ishara ya umoja, uzalendo na ujamaa kwani kutokana na matumizi yake, si rahisi mtu mmoja kuwasilisha nyimbo za *mdumange*.

Utafiti huu umegundua kuwa, ili uwasilishaji wa nyimbo za *mdumange* ukamilike lazima kuwepo na kikundi cha watu wenye nia moja na dhamira maalum. Watu hao hugawana majukumu na hushirikiana katika majukumu mbalimbali ya kiutendaji kama vile kuimba, kucheza na kupiga ngoma au ala nyingine ya kimuziki. Aidha, kutokana na maoni ya watafitiwa, imeelezwa kuwa katika utamaduni asilia wa Wasambaa ngoma pamoja na ala nyingine za kimuziki ni jukumu la wanaume. Aidha, utafiti huu umegundua kuwa hali ilivyo katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni tofauti na maoni haya kwani utendaji umewawezesha wanawake kufanya majukumu ambayo wasingeweza kuyafanya nje ya muktadha wa kiutendaji. Utafiti huu umebaini kuwa wanawake na wanaume wanatumia ala za muziki kama mbinu ya kutambulisha utu na uwezo wao katika jamii. Kila kundi miongoni mwa wanawake na wanaume

wanaotenda nyimbo za *mdumange* linajitambulisha na kudhihirisha uwezo wake. Katika uimbaji, wanawake wanapendelea nyimbo zinazobainisha dosari za wanaume katika ndoa ilhali wanaume wanajitahidi kutongoa nyimbo zinazoonyesha uvivu wa wanawake na mamlaka ya wanaume katika kulea na kuwatunza wanawake.

Aidha, matumizi ya ala za muziki miongoni mwa wanawake na wanaume yanasawiri hali ya mapambano ya kimamlaka. Kutokana na mabadiliko ya kijamii, na pia kutokana na muktadha wa utendaji ngoma ambayo hapo awali ilipigwa na wanaume peke yao, sasa hata wanawake wanapiga ngoma. Kwa mfano, katika kielelezo kifuatacho tunaona jinsi wanawake wanavyoshiriki upigaji wa ala hii:



**Kielelezo na 5.6: Picha Inayoonyesha Wanawake wakipiga ngoma**

Kielelezo hapo juu kinaonyesha wanawake na wanaume wakishiriki utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwa njia ya kupiga ngoma. Hali hii inadokeza kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* unawapatia wanawake fursa ya kufanya matendo ambayo nje ya muktadha wa utendaji wasingeweza kuyafanya. Kutokana na hali hii tunaweza

kusema kuwa wanawake wanajitafutia uhuru na uwezo wa kimamlaka kama njia ya kufanya majukumu ya wanaume. Hii inaweza kuitwa kuwa ni njia mojawapo wanayotumia wanawake kupinga mgawanyo wa majukumu katika misingi ya jinsia.

#### **5.2.2.1.2 Ngoma za Kisasa**

Kulingana na mabadiliko ya kijamii kuanzia miaka ya 1940 na 1950 serikali za kikoloni ziliimarisha mfumo mpya wa maisha barani Afrika. Katika muktadha wa fasihi simulizi, mfumo huo ulizua aina mpya ya ala za muziki. Miongoni mwa ala za muziki zilizozuka wakati wa kipindi cha serikali ya kikoloni ni ngoma za bendi. Ngoma hizi zimetengenezwa kwa ustadi mkubwa ikilinganishwa na ngoma za asili. Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na Wasambaa waliohusishwa kwenye utafiti huu ngoma za bendi zimeingizwa katika nyimbo za *mdumange* kutoka katika ngoma ya *Beni*. Hii ni ngoma ya kisasa iliyokuwa ikichezwa na askari wa serikali ya kikoloni katika miaka ya 1950 nchini Tanzania. Kimuundo, utendaji unaotumia ngoma hizi unahusisha ngoma mbili na tarumbeta tatu kama inavyoonekana katika kielelezo na 5.7 hapa chini.



**Kielelezo na 5.7: Picha Zinazoonyesha Ngoma ya Bendi**

Katika kielelezo hapo juu picha na. 5.7 inaonyesha ngoma za bendi. Kifaa hiki cha kimuziki hupigwa na wanaume peke yake. Aidha, kulingana na muundo wa ala hii kuna mambo yanapaswa kuzingatiwa kuhusiana na utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Mambo hayo yanahusu ushirikiano wa wasanii wakati wa utendaji. Kutokana na ushirikiano tunaona kuwa kila ngoma hupigwa na mtu mmoja. Hii inaonyesha kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni mchakato unaopaswa kushirikisha kundi la wasanii, badala ya msanii mmoja peke yake. Muundo wa ngoma hizi pia unaonyesha kiwango kikubwa cha ushiriki wa wanaume katika kupiga ngoma wakati wa utendaji.

**5.2.2.1.3 Manyanga**

Manyanga ni kifaa kingine cha kimuziki kinachotumika sambamba na ngoma za asili. Kifaa hiki kimetengenezwa kwa kutumia makopo ya chuma. Mara nyingi watengenezaji wake huchukua makopo yaliyokuwa yamewekewa mafuta ya taa au

makopo yoyote yenye uwezo wa kutoa sauti maalum ya kimuziki. Wasanii wa nyimbo za *mdumange* hutoboa tundu dogo katikati mwa mfuniko wa kopo. Umbo la kifaa hiki linaonekana waziwazi katika kielelezo na. 5.8.

Katika kielelezo hicho, tunaona picha ya msanii anayepiga manyanga kwa kutumia mkono na wakati huohuo anapuliza filimbi mdomoni. Kwa kutumia mpini wa manyanga, msanii huizunguusha manyanga kulia na kushoto kwa kutumia mkono mmoja ili itoe sauti. Aidha, msanii mmoja anaweza kuwa na manyanga moja au mbili, na anaweza kupuliza filimbi au filimbi inaweza kupulizwa na mtu mwingine. Hali hii itategemeana na muktadha wa utendaji na idadi ya wasanii waliopo.



**Kielelezo na 5.8: Picha ya Msanii anayepuliza Manyanga**

### **5.2.2.2 Ala Zinazotoa Muziki kwa Njia ya Kupulizwa**

#### **5.2.2.2.1 Tarumbeta**

Tarumbeta ni kifaa kinachotumika sambamba na ngoma za bendi katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Ujumi wa kifaa hiki unapatikana baada ya kupulizwa na MK pamoja na wasaidizi wake kama inavyoonekana katika kielelezo na. 5.9.

Katika utendaji wa nyimbo, msanii anayetumia tarumbeta hatoi sauti au maneno yanayosikika kwa mdomo bali huimba kwa kutumia sauti za tarumbeta. Aidha, wakati mwimbishaji anapomaliza kuimba, wapiga tarumbeta wengine pamoja na hadhira hudakia wimbo husika.

Kwa ujumla, matumizi ya ngoma za bendi na tarumbeta ni ishara ya mabadiliko katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Hapo awali, ngoma za bendi pamoja na tarumbeta zilitumika katika ibada na sherehe za kidini, hususan kwenye makanisa lakini wasanii wameamua kuzitumia katika uimbaji wa nyimbo za *mdumange*. Hii ni ishara kuwa nyimbo za *mdumange* ni sanaa yenye uhai na yenye umuhimu mkubwa katika jamii ya Wasambaa.



#### **Kielelezo na 5 9: Matumizi ya Tarumbeta katika Nyimbo za Mdumange**

Matumizi ya ngoma na ala nyingine za kimuziki katika utendaji wa nyimbo yanaonyesha tabia ya kimwingiliano matini ndani ya utendaji. Kutokana na tabia hii utafiti huu unatoa hoja kuwa ujumi wa nyimbo za *mdumange* umeimarishwa na

mfungamano wa tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya Wasambaa. Ndiyo maana utendaji wa nyimbo umehusisha pia ngoma na tarumbeta.

#### **5.2.2.2 Filimbi, Gunda na Kipaza sauti**

Kando na tarumbeta, vifaa vingine vinavyotoa mapigo ya kimuziki kwa njia ya kupulizwa ni filimbi, gunda na kipaza sauti. Gunda ni kifaa kilichotokana na pembe za wanyama kama vile ng'ombe na wanyama wengine wa porini. Kifaa hiki hutumika katika utendaji unaotumia ngoma za asili. Aidha, kifaa hiki hupulizwa kwa mdomo huku kikiwa kimeshikiliwa na mpulizaji kwa mikono miwili. Matumizi yake ni kutoa sauti kubwa inayoashiria kuwepo kwa hafla au sherehe mahali husika. Kifaa hiki kinaweza kutumika mwanzoni, katikati au mwishoni mwa utendaji ili kutekeleza majukumu mbalimbali ya kupasha hadhira habari pamoja na jamii kwa ujumla. Kwa ujumla, gunda hutumika sambamba na ngoma za asili ilhali tarumbeta hutumika sambamba na ngoma za kisasa.

Mbali na filimbi, manyanga na gunda, wasanii pia hutumia kipaza sauti. Kipaza sauti hutumiwa kwa minajili ya kuongeza sauti na kuvutia hadhira. Aidha, kifaa hiki hutumiwa sawa na ambavyo tarumbeta hutumiwa kwa kuanzishia wimbo au kwa kuitikia. Kwa upande mwingine, filimbi hutumiwa na wasanii wanaotumia ngoma za kisasa na wanaotumia ngoma za asili kwa minajili ya kunogesha utamu wa nyimbo pamoja na kuwasilisha ujumbe maalum. Kati ya vifaa hivi, filimbi ni kifaa chepesi kutumia na kinaweza kutumiwa pamoja na ala nyingine kama vile ngoma na manyanga. Kwa ujumla, vifaa vya kiumziki vilivyoainishwa hapa, hutumiwa na wasanii kutekeleza majukumu mahsusi ya kiutendaji yakiwemo haya yafuatayo:

Mosi, matumizi ya ala hizi yanasawiri uwasilishaji wa ujumbe na dhamira zinazohusu itikadi za ulimwengu wa Wasambaa kwa njia mbalimbali. Mojawapo ya njia hizo ni

kuwasilisha ujumbe kwa kuidokeza hadhira hatua mbalimbali za utendaji kama vile kuanza kwa uimbaji, kubadilisha wimbo, na kuhitimisha uimbaji. Mara tu ngoma zinapoanza kupigwa, wasikilizaji na hadhira kwa ujumla hupata ujumbe kuwa katika eneo hilo kuna sherehe. Hata kabla hawajawaona watendaji, waimbaji, wala wapiga ngoma hadhira hutambua kuwa katika sherehe hiyo, nyimbo za *mdumange* zitaimbwa na kuwasilishwa. Hii ni kwa sababu midundo ya ngoma inayopigwa inahusishwa na mitindo ya uimbaji pamoja na uchezaji unaojulikana katika jamii ya Wasambaa.

Watendaji wa nyimbo za *mdumange* huanza utendaji wao kwa namna mbalimbali. Mara nyingine huanza kwa msimbo maalum wa kupiga ngoma taratibu huku midundo ya ngoma hiyo ikifuatishiwa na uimbaji. Ngoma inapopigwa polepole, watu wanapata ujumbe kuwa sasa sherehe imekaribia kuanza. Katika mazingira mengine ya kiutendaji, tarumbeta, filimbi au gunda ilianza kupulizwa kwa sauti kubwa bila kuimba wala kupiga ngoma. Sauti hizo hufika mbali zaidi kuliko ngoma na uimbaji. Hivyo, sauti za ala za kupulizwa huwa kama tangazo maalum kuwa mahali fulani kutakuwa na burudani ya *mdumange*, hatimaye watu huharakisha kufika kwenye eneo lenye sherehe.

Pili, matumizi ya ala za muziki zilizowasilishwa hapo juu yamechochea ubainishaji wa mitazamo ya utunzi na uwasilishaji wa nyimbo za *mdumange*. Kwa upande mmoja, kutotumika kwa manyanga na gunda katika utendaji wa nyimbo unaotumia ngoma za kisasa kunatokana na imani kuwa hivi ni vifaa vya kijadi vinavyonasibishwa na utamaduni asili wa Wasambaa, hususan *pungwa*. Hivyo, matumizi ya kipaza sauti, tarumbeta na filimbi yamezua aina mbili za watendaji wa nyimbo za *mdumange*: wanamabadiliko na wahafidhina. Wanamabadiliko ni wasanii wanaotumia ngoma za asili kwa kuwa hawaoni shida kutumia filimbi, ngoma za asili,



na kipaza sauti kwani wanaamini kuwa *mdumange* ni sanaa hai inakua na kubadilika kila uchao. Kulingana na mtazamo wa kundi hili, si vibaya kuchukua mtindo wa kisasa na kuingiza katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* ikiwa hauna athari hasi kwa jamii.

Kwa upande mwingine, wasanii wa kundi la kihafidhina linajumuisha wasanii wanaotumia ngoma za kisasa ambapo *mdumange* unatazamwa kama sanaa mpya na ya kisasa isiokuwa na uhusiano wowote na utamaduni asilia wa Wasambaa. Kundi hili linaamini kuwa *mdumange* ni sanaa kwa ajili ya kuelimishia, kuburudishia na kuliwazia jamii. Kutokana na mtazamo huu, wasanii wa kihafidhina hawatumii gunda wala manyanga wakati wa utendaji wao kwa kuwa hivi ni vifaa vya kijadi na vinawakilisha utamadui wa Wasambaa.

Tatu, ngoma pamoja na ala nyingine za kimuziki zinazopatikana katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* zinaingia katika kundi la ishara/misimbo ambayo kwa mujibu wa Peirce amezifafanua kuwa ni ishara za kisemiotiki. Hii ni kwa kuwa zinahusiana sana na masuala ya utamaduni wa jamii inayochunguzwa (Wasambaa). Ishara hizo zimetumiwa na wasanii kuwasilisha dhamira ya mgawanyo wa majukumu katika jamii ya Wasambaa kwa misingi ya kijinsia. Kulingana na utamaduni wa jamii hii, kuna majukumu maalum yanayopaswa kufanywa na wanaume na kuna majukumu mengine maalum yanayopaswa kufanywa na wanawake. Upigaji wa ngoma pamoja na ala nyingine za kimuziki kama vile gunda, manyanga, tarumbeta na filimbi ni miongoni mwa majukumu yanayohusishwa na jinsia ya wanaume. Ngoma ni ishara ya utawala na ni kiwakilishi cha itikadi ya mfumodume. Kwa hiyo, hata katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* wanaohusika na upigaji ngoma ni wanaume zaidi kuliko wanawake. Kwa ujumla, nyenzo hizi za kimuziki zinarutubisha utendaji wa nyimbo kwa kuchochea uchezaji, uimbaji na ushirikishwaji wa hadhira.

### 5.3 Maleba na Vifaa vya Kuigizia

Kipengele kingine kinachotoa ujumbe kwa njia ya lugha – ishara ni mavazi pamoja na vifaa vya kuigizia. Wasanii pamoja na washiriki wengine wa nyimbo za *mdumange* hujipambanua kutokana na namna wanavyoonekana wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kiutendaji. Kwa ujumla, utendaji wa nyimbo za *mdumange* umeathiriwa na matumizi ya maleba na vifaa mbalimbali vya kuigizia kama vile *mwengo*, *pembe* na *ngao ya Sheuta*. Aidha, mbali na matumizi ya zana hizi za kuigizaji, wasanii wa nyimbo za *mdumange* pia hutumia mavazi maalum ya kiutendaji kama vile *kofia ya kishadda* au ya *usinga*, *kaniki/sufi*, *kibwebwe* na *masegele*. Sehemu ifuatayo imeeleza kwa kina matumizi ya nyenzo hizi katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*.

#### 5.3.1 Maleba ya Wasanii na Washiriki

Mavazi na vifaa vya kuigizia ni misimbo inayotoa fununu kwa watu au wahakiki kuhusu utambulisho wa makundi ya watu na majukumu yao katika utendaji. Misimbo hii imesaidia kutambulisha makundi ya washiriki wa nyimbo za *mdumange* pamoja na majukumu yao kwa njia mbalimbali. Kutokana na matumizi ya aina mbalimbali za mavazi tumefanikiwa kubainisha makundi makuu mawili ya washiriki wa nyimbo za *mdumange*: (i) washiriki wasanii na; (ii) washiriki hadhira. Katika kundi la kwanza pia kuna mgawanyo wa vijikundi vidogovidogo kulingana na majukumu wanayoyafanya wakati wa kuwasilisha nyimbo. Hapa kuna wasanii waimbaji, wapiga ngoma na wachezaji. Vikundi vyote vya washiriki wasanii vinapaswa kushiriki katika utendaji pamoja na washiriki hadhira. Wasanii waimbaji hujipambanua kutokana na mitindo yao ya mavazi pamoja na jinsi wanatumia ala mbalimbali za kuigizia.

Katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* imebainika kuwa wasanii waimbaji huvaa mavazi maalum hususan *kofia ya kishadda* au ya *usinga*, *masegele*, *kaniki/sufi* na

*lubega*. Kofia ya *kishadda* ni aina maalum ya kofia iliyotengenezwa au kushonwa kwa kutumia sindano ya moto, badala ya sindano ya uzi. Kofia hii inahusika na mila na utamaduni wa waumini wa dini ya Kiislamu, na ni ishara ya heshima na uanazuoni. Kwa upande mwingine, kofia ya *usinga* ni aina ya kofia iliyotengenezwa kwa kutumia manyoya ya ndege aitwaye singa au kipanga. Kofia hii inahusishwa na nguvu za kiuganga na ushirikina miongoni mwa jamii hii. Miundo na aina za kofia zinazotumiwa na wasanii wa nyimbo za *mdumange* imewasilishwa katika kielelezo na. 5.10 hapa chini:



**Kielelezo na 5.10: Picha Zinazoonyesha Kofia ya Usinga na y a Kishadda**

Kama inavyoonekana katika kielelezo hapo juu, (A) ni kofia ya Usinga, (B) ni kofia ya Kishadda na (CH) ni kofia aina ya kapelo. Kofia za Usinga na Kishadda huvaliwa na wasanii waimbaji ilhali kapelo huvaliwa na wasanii wapiga ngoma na manyanga. Kusudio la kofia hizi ni kutambulisha na kutofautisha wasanii dhidi ya hadhira. Aidha, kofia hizi hutumika kumjengea uwezo wa kujiamini na kujikinga dhidi ya mionzi ya jua. Kadhalika, kuna imani miongoni mwa wasanii kuwa kofia ya Usinga

ina uwezo wa kumpatia msanii nguvu ya kuimba na kuwasilisha nyimbo kwa kujiamini na ustadi mzuri. Kutokana na mtazamo huu, ni nadra kuona msanii asiyevaa kofia ya aina yoyote katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*.

Aina nyingine za mavazi yanayowatambulisha watendaji wa nyimbo za *mdumange* ni *kibwebwe* na *masegele*. *Kibwebwe* ni mtindo wa kuvaa kanga kwa kuisokota vyema kiasi cha kuifanya ionekane kama vile kamba, kisha hufunga kiunoni (tazama kielelezo na. 5.11). Mtindo huu huvaliwa sana na wasanii waimbaji, wapiga ngoma na wachezaji. Aidha, *kibwebwe* ni vazi la asili linalovaliwa ili kuonesha madoido ya unenguaji na uchezaji kwa njia ya kukata kiuno. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Wasambaa waliohojiwa, *kibwebwe* pia huvaliwa hata katika utendaji wa nyimbo nyingine kama vile za wanawake (kidembwa).

Kwa upande mwingine *masegele* (rejelea kielelezo na. 5.12) ni aina ya vazi la kisanii lililotengenezwa kwa majani au mbegu maalum za miti. Kadhalika, utafiti huu pia umebaini kuwa wakati mwingine shanga pia hutumika kutengenezea *masegele*. Majani, mbegu au shanga hizo hufungwa kwa kutumia kamba maalum na kisha huingirishwa kiunoni mwa msanii. Wakati wa kuimba, kucheza au kupiga ngoma au kifaa kingine kama vile *filimbi* au *manyanga*, *masegele* hutoa sauti yenye mapigo ya kimuziki. Kimsingi, *masegele* yanaelekea kukaribiana na *kibwebwe*, tofauti yao ni kuwa *kibwebwe* ni vazi la asili zaidi, lakini *masegele* ni vazi la hivi karibuni.



**Kielelezo na 5.11: Picha Zinazoonyesha Kibwebwe**

Kama inavyoonekana katika kielelezo hapo juu wachezaji wanawake wamevaa kibwebwe viunoni mwao wakati wa utendaji. Aidha, kwa kiwango kikubwa kibwebwe kinavaliwa na wanawake zaidi kuliko wanaume. Tofauti nyingine kati ya masegele na kibwebwe ni kuwa wakati masegele hutoa sauti za namna fulani, kibwebwe hakitoi sauti ila kinasaidia kuvuta nadhari za hadhira wakati wa kucheza. Wakati wa utendaji, msanii hujitikisa kwa utaratibu maalum unaoyafanya masegele yatikisike pia. Masegele na kibwebwe humsaidia mtendaji kuwa na kiuno kikubwa kuliko watu wengine wasiovaa zana hizo. Kwa njia hii, masegele na kibwebwe huchochea hisia na midadi (ungoya) ya msanii na huvuta nadhari za hadhira.



**Kielelezo na 5.12: Picha za Wasanii waliovaa Masegele**

Aidha, badala ya kufungwa kiunoni, wakati mwingine, masegele hufungwa katika mabega ya msanii (kama inavyoonekana katika 5.12) kwa kutumia mtindo wa uvaaji unaotumiwa na Wamasai. Ikiwa kutakuwepo na masegele mengi, msanii muimbaji huweza kuvaa aina zote za masegele; kiunoni na lubega. Pia kama masegele ni mengi, hata wasanii wengine kama vile wachezaji na wapiga ngoma huweza kuvaa masegele au lubega. Ikiwa msanii ataingia katikati ya duara hali ya kuwa hana kibwebwe wala masegele, msanii yeyote kati ya waliopo huvua segele au kibwebwe chake na humfunga yeye. Hii inaonyesha kuwa uchezaji wa nyimbo za *mdumange* haukamiliki bila kutumia mtindo wa uvaaji kibwebwe.

Kwa upande mwingine, waimbaji, wachezaji na wasanii wanaopiga ala za muziki hujipambanua dhidi ya hadhira kwa kuvaa sare maalum. Sare hizo zinaweza kuendana na makusudio ya tukio la utendaji au zinaweza kuwa za kawaida. Kadhalika, sare ya

wasanii wa nyimbo za mdumange huweza kufanana au kutofautiana kulingana na tofauti za kijinsia baina ya wanawake na wanaume. Mara nyingi katika sherehe za harusi na Ubarikio wanawake huvalia sare maalum ya magauni yajulinayo kama madira. Kwa upande wa wanaume huweza kuvaa nguo zozote za heshima na nadhifu, lakini zinazofanana. Hivyo hivyo, katika hafla za kisiasa kama vile mbio za mwenge na kampeni za uchaguzi suala la mavazi linachukua nafasi kubwa sana.

Wasanii wa nyimbo za *mdumange* huweza kuvaa sare ya fulana au tisheti maalum. Fulana na tisheti hizo huwa na maandishi yanayofafanua kusudio la tukio husika. Kwa minajili ya kuisitiza dhamira ya kutunza utamaduni wa Wasambaa, wasanii wa nyimbo za *mdumange* pia huweza kuvaa sare ya kaniki au sufi (kama ilivyo katika kielelezo na. 5.13). Sufi ni vazi linalofanana na kitenge, lakini lenyewe lina rangi nyeusi. Vazi hili hupendelewa kuvaliwa na waganga wa jadi wakati wa kuwahudumia wateja wao.



**Kielelezo na 5.13: Picha Zinazoonyesha Wasanii waliovaa Sare ya Kaniki**

Katika kielelezo na. 5.13 tunaona wasanii wanawake waliovaa sare ya kanga nyeusi (kaniki) wakati wa hafla za mwenge katika kijiji cha Magoma, Lushoto. Kwa upande mwingine, kielelezo (5.14) ni sare ya wasanii wa kiume. Wasanii wakiume walitumia ngoma za bendi na matarumbeta wakati wa utendaji wao. Kimsingi, utendaji wa nyimbo za *mdumange* unaambatana na aina maalum ya mavazi yanayotofautisha hadhira, waimbaji, wapiga ngoma na wachezaji. Aina hizi za mavazi huweza kuwatofautisha wasanii wanawake na wanaume. Aidha, mavazi hayo hutoa ujumbe unaopaza sauti isemayo kuwa wasanii/watendaji wanayo nafasi maalum katika *mdumange* ikilingansihwa na washiriki wengine wasio kuwa na mavazi wala ala za kuigizia. Hata hivyo, aina maalum ya mavazi hupunguza kiwango cha ushiriki wa watu wengine, kwa kuwa wao hujiona kama si watu muhimu sana na kuwafanya washiriki wasiwe huru kama ilivyo kwa wasanii. Kulingana na matumizi ya sare maalum za wasanii (maleba) masuala anuai ya kiutendaji yamebainika. Sare wanazovaa wasanii wa nyimbo za *mdumange* zinachangia katika kufahamu ujumbe wanaoutoa kwa mawanda mapana. Kwa mfano, katika sherehe za harusi wasanii huvaa sare maalum iliyoshonwa kwa ajili ya sherehe hiyo.





**Kielelezo na 5.14: Picha Zinazoonyesha Sare Maalum za Watendaji**

Kitendo hiki kinaonyesha ukuruba uliopo baina yao na waandaaji wa sherehe. Katika hafla za kisiasa kama vile mbio za mwenge, wasanii huvaa nguo maalum zilizoshonwa kwa ajili ya tukio hilo. Sare zinazotumika kwenye hafla ya mbio za mwenge huwa zina maandishi na michoro ya mwenge wa uhuru. Kadhalika, wasanii wanapoalikwa kwenye hafla za kisiasa yenye lengo la kuhamasisha masuala ya kiutamaduni huvaa sare mbalimbali za kiutamaduni kama vile mashati ya vitenge na kaniki/sufi. Aina hizi za mavazi tunaweza kuziita kuwa ni misimbo maalum ya kiutamaduni. Aidha, kulingana na maoni ya Mwana Nadharia ya Semiotiki ya Kijamii, Barthes (1964) anafafanua kuwa msimbo wa kiutamaduni unatufanya tuelewe kuwa matumzi ya mavazi maalumu katika nyimbo za *mdumange* ni muhimu sana katika kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyolengwa. Mavazi hayo yanatoa viashiria fulani kwa hadhira na kuwapatia hisia na kuvutiwa kusikiliza nyimbo husika na hatimaye kupata dhamira iliyokusudiwa katika utendaji wa nyimbo.

Aina za mavazi yanayovaliwa na wasanii wa nyimbo za *mdumange* yanaakisi mfumo wa maisha ya jamii ya Wasambaa. Ni marufuku kuvaa mavazi yasio ya heshima kama vile kuvaa nguo zenye kuonyesha sehemu za siri, au kuvaa nusu uchi. Mtindo wa utendaji wa nyimbo hizi unazingatia mfumo wa maadili ya Wasambaa kuwa mtu anapaswa kujisitiri kwa kuvaa mavazi nadhifu na ya heshima. Kitendo hiki kimezifanya nyimbo hizi zithaminiwe tangu enzi hadi enzi na idadi kubwa ya wanajami ambao wanaona kuwa mavazi ni sehemu muhimu ya maadili ya jamii. Hii ni tofauti na mitindo ya mavazi inayotumika katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya kama vile MBF ambapo wasanii wake hujipambanua kwa kuvaa sketi fupi, kaptula na majinzi yanayoning'inia matakoni (Omari, 2009). Kulingana na maoni ya wasanii wa nyimbo za *mdumange*, mitindo hii ya kisasa inabomoa maadili asilia ya jamii.

Mavazi yanayotumika katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* yamechochea hali ya unusura katika nyimbo hizi. Ingawa nyimbo hizi ni za zamani sana, lakini mpaka leo zingali zinaenziwa na makundi yote ya wanajamii. Licha ya mabadiliko madogomadogo yanayojitokeza katika nyimbo hizi, wasanii wanaamini kuwa nyimbo hizi bado ni za asili na zinatukuza utamaduni wa asili bila kupuuza mambo mazuri ya utamaduni wa kisasa. Miongoni mwa masuala ya kisasa yaliyoingizwa kwenye utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni pamoja na matumizi ya filimbi, kipaza sauti, mavazi yaliyoshonwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa badala ya mavazi ya ngozi.

Kadhalika, usasa ndani ya nyimbo hizi umejitokeza hata katika maudhui hususan kulingana na kuibuka kwa mahitaji mapya ya kijamii kama vile maradhi ya UKIMWI, demokrasia ya vyama vingi na umuhimu wa kutunza mazingira. Dhamira zote hizi ni mpya na zinaashiria hali ya usasa. Kwa hivyo, ingawa nyimbo za *mdumange* zinaenzi mfumo wa maisha ya kijadi, bado hazijapuuza hali mpya zinazotokea katika kijamii.

Hii ni kuonyesha kuwa, nyimbo za *mdumange* pamoja na aina nyingine za kifasihi simulizi ni sanaa hai, pevu na zinazobadilika kulingana na mahitaji mapya ya kijamii.

### **5.3.2 Vifaa vya Uigizaji wa Fanani**

Kando na matumizi ya aina mbalimbali za mavazi ya kisanaa, wasanii wa nyimbo za *mdumange* pia hujipambanua dhidi ya washiriki wengine kwa kutumia vifaa anuai vya kuigizia. Vifaa vinavyotumika katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni pamoja na *mwengo*, *pembe* na *ngao ya Sheuta*. Mwengo na pembe ni vifaa cha kuigizia vinavyohusishwa na uganga wa kijadi miongoni mwa Wasambaa. Vyote vina rangi nyeusi, na vimeundwa kutokana na malighafi za wanyama. Umbo la mwengo linafanana na ufagio, na limetengenezwa kwa kutumia manyoya ya wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi au mnyama yoyote mwenye rangi nyeusi. Kwa upande mwingine pembe ni kifaa cha kiutendaji kilichotengenezwa kwa kutumia pembe za wanyama hususan wanyama wa porini.

Kimundo kifaa hiki kinashabihiana na gunda, lakini kimatumizi hivi ni vifaa viwili tofauti kabisa. Gunda hutumika kama kifaa cha kimuziki ilhali pembe hutumika kama kifaa cha kuigizia matendo ya kimila kama vile tiba asilia.



**Kielelezo na 5.15: Picha inayoonyesha msanii aliyeshika mwengo**

Kielelezo hapo juu kinaonyesha kundi la wasanii, ambapo msanii wa katikati ameshika kifaa cha kuigizia kiitwacho mwengo. Wakati wa uwasilishaji wa nyimbo, msanii muimbaji hushikilia mwengo kwa mkono mmoja na huuzungusha mwengo upande wa kulia na kushoto. Uzungushaji wake unaendana na mapigo ya sauti za uimbaji pamoja na uimbaji.

Licha ya kuwa mwengo humfanya muimbaji ajiamini, kwa kiwango kikubwa mwengo hutumika kama ishara ya uganga na ulinzi dhidi ya wachawi. Hii inadhihirika kwa jinsi ambavyo kifaa hiki kimekuwa kinatumika miongoni mwa wasanii ambao ama wao wenyewe ni waganga wa tiba asilia, au wazazi wao ni waganga wa kijadi wanaosifika kutokana na uganga wao.



**Kielelezo na 5.16: Picha za Pembe na Gunda**

Aidha katika kielelezo na. 5.16 tunamuona msanii aliyeshika mwengo (mkono wa kushoto) na pembe (mkono wa kulia). Wakati wa utendaji wa nyimbo za *mdumange*, wasanii waimbaji huwa wamezihifadhi pembe mahali maalum kwa ajili ya ya kujihami dhidi ya uovu unaoweza kutokea. Kwa hiyo, dhima na nafasi ya pembe inafanana na dhima ya mwengo.

Aidha, wasanii wa nyimbo za *mdumange* pia huwa wanatumia kifaa maalum cha kuigizia kiitwacho ngao ya Sheuta (tazama kielelezo na. 5.17). Hii ni fimbo maalum iliyozungushiwa shanga za rangi mbalimbali kutoka juu mpaka chini. Upande mmoja wa fimbo una ncha, na unatumika kuisimika fimbo chini ya ardhi huku uimbaji ukiwa unaendelea. Upande wa juu, umeundwa kwa kukunjwa mithili ya bakora, lakini mkunjo wake ni mdogo sana kuliko ilivyo mkunjo wa bakora ya kawaida.



**Kielelezo na 5.17: Picha inayoonyesha Muundo wa Ngao ya Sheuta**

Kielelezo hapo juu kinaonyesha picha ya ngao ya Sheuta. Kulingana na maoni ya Wasambaa waliohojiwa wakati wa kuwasilisha nyimbo, ngao ya Sheuta husimikwa katikati ya duara au husimikwa karibu na wapiga ngoma. Kwa ujumla, ngao ya Sheuta hutumika kama alama inayoashiria mila na utamaduni wa jadi ya Wasambaa. Ngao hii imetumika kama msimbo wa kiutamaduni kuonyesha namna kiongozi huyo wa kimila wa jamii ya Wasambaa anavyoheshimiwa na pia ni mtu mwenye nguvu kubwa katika jamii ya Wasambaa. Uwepo wa ngao hiyo katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni ishara ya kuwapatia waimbaji ujasiri na kujiamini katika kutimiza wajibu wao.

Aidha, Wasambaa wanasimulia kuwa Sheuta ndiye mhenga wa mwanzo aliyeasisi taifa na dola ya Wasambaa miaka mingi iliyopita. Miongoni mwa mambo yaliyoasisiwa na mhenga huyu na ambayo hadi leo yanaaminika kuwa ndio nguzo za ustawi wa maisha ya Wasambaa ni miviga, matambiko na ibada nyingine za mizimu.

Kwa hiyo, kitendo cha kuweka ngao hii katikati au karibu ya wapiga ngoma kinaashiria umuhimu wake, na jinsi wasanii wanavyoamini juu ya uwezekano wa kupata msaada wa kiulinzi, kisanaa na kiutendaji kutoka kwake.

Kwa ujumla, ala za kuigizia na mitindo ya mavazi yanayovaliwa na wasanii pamoja na washiriki wengine yana nafasi kubwa katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Mitindo hii hushirikiana na mitindo ya matumizi ya lugha kuisitiza ujumbe, kufafanua maana na kufumbua maana za taswira au mafumbo yanayojitokeza wakati wa utendaji. Kadhalika, mitindo hii inasharabu na kuibua mwitiko wa hadhira kutegemea na aina ya dhamira inayokuzwa katika nyimbo.

#### **5.4 Jukwaa na Uchezaji Dansi**

Kuna uhusiano mkubwa baina ya uchezaji na uigizaji wa matendo mbalimbali yanayoonyeshwa na wasanii wa nyimbo za *mdumange*. Kulingana na Okpewho (1992:47) uchezaji ni mbinu maridhawa ya kuufanya utendaji uvutie na upendeze. Hata hivyo, pamoja na kuufanya utendaji uvutie, aina mbalimbali za mitindo ya uchezaji katika nyimbo za *mdumange* huchangia katika kufafanua ujumbe na maana inayojengwa kwenye nyimbo hizo. Kwa ujumla, uwasilishwaji wa nyimbo za *mdumange* katika matukio mbalimbali ya kijamii ikiwemo harusi, sikukuu za kidini na hafla za kisiasa unaambatana na matumizi ya jukwaa, uchezaji na uigizaji.

##### **5.4.1 Miundo ya Jukwaa la Utendaji**

Jambo la kwanza kabisa katika kuchunguza uhusiano wa mitindo ya uchezaji, uigizaji na uwasilishaji wa nyimbo za *mdumange* ni muundo wa jukwaa. Muundo huo unakusudia kutujaza mpangilio wa eneo la utendaji kabla na wakati wa utendaji. Aidha, jukwaa ni kipengele muhimu sana cha kisemiotiki kinachowahusisha pamoja fanani, hadhira na vifaa mbalimbali vya kiutendaji kama vile vifaa vya kimuziki na

kiugizaji. Kimsingi, kuna aina kuu mbili za miundo ya jukwaa la utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Kwanza kuna muundo wa duara, na pili kuna muundo wa mstatili, maarufu kama jukwaa la steji.

#### 5.4.1.1 Jukwaa la Muundo wa Duara

Jukwaa la duara ndilo jukwaa la asili katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Katika hatua za awali za uwasilishwaji wa nyimbo, jukwaa hili linaonekana katika muundo wa nusu duara. Hii ni kwa sababu vile vifaa vya utendaji vilivyotajwa vinakuwa vimepangwa kulizunguka duara la uonyeshaji. Kadri washiriki wanavyoingia kwenye eneo la utendaji ndivyo mzunguko wa duara unavyokamilika. Hii ni kusema kuwa kabla utendaji kuanza, jukwaa la asili la utendaji wa nyimbo za *mdumange* linaonekana likiwa wazi au nusu duara kama inavyoonekana hapa chini:



#### Kielelezo na 5.18: Muundo wa Jukwaa (Nusu duara)

Kielelezo na. 5.18 kinaonyesha jinsi hali ya jukwaa ilivyo wakati wa kuanza utendaji. Katika wakati huu watendaji wamezunguka na kutengeneza umbo la nusu duara.



Kwa upande mwingine, jukwaa la utendaji wa nyimbo za mdumange huonekana kama duara kamili kama ilivyobainishwa katika kielelezo kifuatacho:



**Kielelezo na 5.19: Muundo wa Jukwaa (duara kamili)**

Kama inavyoonekana katika kielelezo na. 5.19 hapo juu, wasanii na washiriki kwa pamoja wamezunguka na kutengeneza duara kamili. Muundo huu wa duara kamili unapatikana baada ya muda mwingi kupita tangu utendaji ulipoanza. Katika muundo huu inakuwa rahisi kuona watendaji wanaocheza kwa kulizunguka duara na si rahisi kuwaona wasanii wapiga ngoma, kwani wao wako katikati.

**5.4.1.2 Jukwaa la Muundo wa Steji**

Kwa upande mwingine jukwaa la steji au mstatili huwapanga fanani na hadhira katika mistari anuai. Kwanza kuna mstari wa waitikiaji na wachezaji unaokuwa mbele

kabisa na hutazamana na mistari mingine ya waimbaji na wapiga ala za muziki. Muundo huu umeonyeshwa dhahiri katika vielelezo na. 5.20 na 5.21

Kulingana na kielelezo na. 5.20 hali ya jukwaa la steji wakati wa kuanza utendaji huonyesha wasanii wakiwa kwenye mistari mbalimbali. Aidha, katika kielelezo na. 5.21 tunaona muundo wa jukwaa la steji wakati utendaji ukiwa unaendelea, hasa wachezaji. Muundo huu wa jukwaa unatoa fursa kwa watazamaji kushuhudia uchezaji, na kuwaona wasanii wapiga ngoma.

Kimsingi, aina hizi mbili za miundo ya jukwaa la utendaji wa nyimbo za *mdumange* hutokea kulingana na tofauti za muktadha wa tukio. Mara nyingi jukwaa la steji hutumika mahali penye hadhira rasmi kama vile viongozi wa chama na serikali wakati wa mikutano na hafla za kisiasa. Miundo hii ya jukwaa huelekeza na huathiri pia mitindo mbalimbali ya uchezaji wa wasanii wa nyimbo za *mdumange* kama ifuatavyo.



**Kielelezo na 5.20: Muundo wa Jukwaa la Steji**



### **Kielelezo na 5.21: Mistari ya Wachezaji katika Jukwaa la Steji**

Miundo ya uchezaji inaonekana katika mitindo mikuu miwili ya utendaji. Mtindo wa duara hutumika sana katika hafla za harusi, na sikukuu za kidini ilhali jukwaa la steji hutumika karika siasa. Aidha, itaonekana wazi kuwa jukwaa la steji ni rasmi kwani linawagawa washiriki katika watendaji na watazamaji. Kulingana na jinsi lilivyo watu wengine huona ugumu wa kuingia kwenye safu za mistari ya wasanii na hivyo kushindwa kushiriki uchezaji. Kwa ufupi, hili ni jukwaa jipya na linatumiwa na vikundi vichache vya *mdumange*. Kwa kiwango kikubwa, utendaji wa nyimbo za *mdumange* unafanyika katika jukwaa la duara (la asili). Majukwaa yote yanachangia kufasiri ulimwengu wa Wasambaa kwa namna tofauti tofauti.

Kwa upande mmoja jukwaa la muundo wa duara husaidia kujenga mtazamo na itikadi ya umoja, undugu na ujamaa kutokana na ukuruba uliopo baina ya fanani na hadhira wake. Kutokana na jukwaa kuwa na umbo la duara, dhana inayojengeka miongoni mwa washiriki ni kuwa kati ya fanani na hadhira hakuna mwenye hadhi ya juu wala ya chini kiutendaji. Pamoja na kujenga ukuruba miongoni mwa washiriki, matumizi

ya jukwaa la duara pia yanachochea ushiriki wa hadhira zaidi ikilinganishwa na jukwaa la steji. Kulingana na muundo huu wa jukwaa, hadhira inahamasishwa kushiriki utendaji kwa kiwango kikubwa.

Kwa upande mwingine, jukwaa lenye muundo wa steji lina athari hasi zaidi kwa hadhira kwa kuwa jukwaa hili hujenga dhana ya matabaka katika utendaji. Kutokana na muundo wa jukwaa hili, uhuru wa hadhira kushiriki utendaji ni mfinyu mno, kwani tofauti na ilivyokuwa katika jukwaa la duara, katika jukwaa hili hadhira inajiona kama wametengwa na kwamba utendaji huo unakuwa umeandaliwa kwa watu wengine kutazama na wengine kutenda kwa kushiriki. Katika vielelezo namba 5.20 na 5.21 miundo hii ya jukwaa la utendaji wa nyimbo za *mdumange* imeonyeshwa waziwazi.

Pamoja na kutofautiana kwa miundo ya majukwaa, dhima zao katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni kubwa sana. Kupitia mpangilio wa jukwaa hususan jukwaa la duara, mtazamo wa fanani na hadhira kuhusu mwonoulimwengu wa jamii unawasilishwa. Hii ina maana kuwa jukwaa la namna hii hutengeneza muktadha maalum wa kisaikolojia baina ya makundi ya washiriki wa sanaa husika, na ambao pia huimarisha na kurahisisha utangamano wao.

Kupitia matumizi ya majukwaa haya, wataalamu kama vile Karim (1999; 2007) na Johansson (2009) wanaeleza kuwa urazini mbwete wa fanani na hadhira yake (unconscious) unafichuliwa wakati wa kuwasilisha nyimbo za *mdumange*. Kupitia utendaji huo, utambulisho wa kila mmoja kati ya fanani na hadhira hubainishwa. Kwa hiyo, nyimbo pamoja na uwepo wa hadhira na fanani unakidhi matamano fiche ya wanajamii kwa kuwezesha wasanii kusema na kutenda mambo ambayo nje ya muktadha wa kiutendaji wasingeweza kuyasema na kuyatenda. Mahala pengine,

fanani anabuni na kuwasilisha dhamira zake katika muktadha wa kidhahania na hatimaye kuishirikisha hadhira njia ya uimbaji, uchezaji na uigizaji.

#### **5.4.2 Mitindo ya Uchezaji Dansi**

Dhima nyingine ya matumizi ya aina hizi za majukwaa katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni uzalishaji wa mitindo mbalimbali ya uchezaji dansi. Kama ilivyokwishasemwa hapo awali kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* hutokea katika muktadha wa sherehe za harusi na matukio mengine ya furaha kama vile sikukuu za kidini na hafla za kisiasa. Kulingana na muktadha huu wa sherehe na sikukuu, suala la kucheza linachukua nafasi kubwa kwa kuwa kucheza ni sehemu ya kudhihirisha furaha miongoni mwa wanajamii.

Wasanii pamoja na watu wengine wanaoshiriki katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* hudhihirisha madoido yao ya kucheza kwa minajili ya kuwasilisha ujumbe maalum. Si rahisi kuona uwasilishwaji wa nyimbo usioambatana na uchezaji wa dansi. Katika uwasilishaji huo, uchezaji hufanyika kwa kufuata midundo ya ala za muziki pamoja na ridhimu ya uimbaji wa nyimbo. Kwa kiwango kikubwa, wasanii na watu wengine hucheza kwa kuzunguka duara au jukwaa. Huanzia upande wa kushoto kuelekea upande wa kulia. Aidha, uchezaji kwa njia ya kulizunguka duara pia unaambatana na uchezeshaji wa sehemu nyingine za viungo vya mwili hususan mabega, mikono na kiuno. Baadhi ya washiriki huvaa au hufunga nguo maalum ijulinayo kama kibwebwe viunoni mwao ili kuvifanya viuno vyao vionekane vikubwa, na kuwafanya waonekane waziwazi na watu wengine wakati wa kucheza kwao.

Mbali na mtindo wa kucheza kwa kuzunguka duara, kutegemea na aina ya wimbo kuna baadhi ya wakati uchezaji hufanyika kwa njia ya kusimama na kupiga makofi.

Katika mtindo huu, washiriki wa nyimbo za *mdumange* huwa wanatazamana kulingana na jinsi walivyojipanga katika duara la utendaji. Uchezaji wa namna hii ni maalum kwa ajili ya kumtaja mtu mmojammoja na kumpigia makofi huku washiriki wakiendelea kuimba. Mtu anayetajwa huingia katikati ya duara na kuonyesha ufundi wake wa kucheza, hususan kwa njia ya kukata viuno. Uchezaji kwa njia ya kukata viuno unawafanya wachezaji wacheze kama vile wanajikunjakunja huku wakiinama chini kuanzia juu (wakiwa wamesimama wima) mpaka mtu anapiga magoti au mpaka anafikia hatua ya kuchuchumaa, kisha mchezaji huinuka juu tena. Aidha, ili kuufanya uchezaji uvutie zaidi, muimbaji kiongozi huwa anataja watu wawiliwawili, na mara nyingi anataja watu wa jinsia tofauti. Uchezaji wa namna hii ni maarufu sana katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*, na unajulikana kama *Shambi*.

Kulingana na taratibu za utamaduni wa Wasambaa, hairuhusiwi kucheza kwa kukumbatiana. Kwa hivyo, watendaji huweza kubuni namna mbalimbali za kuonyesha furaha yao lakini huwa wanachunga sana nidhamu hii. Vilevile, utendaji wa nyimbo za *mdumange* unapaswa kuwa wa kistarabu na kwamba ikiwa uchezaji wa shambi utahusisha watu wa jinsi mbili tofauti, basi wimbo unaoimbwa ukimalizika tu kila mmoja kati ya watu wawili hao waliokuwa wanaonyesha shambi zao anatakiwa kurejea mahali pake pa kuchezea. Hatakiwi kubaki pale katikati ya duara. Mara nyingine si lazima wimbo umalizike, inategemea na namna muimbaji kiongozi atakavyoimba wimbo wake. Kama amemtaja mtu, na mtu huyo tayari ashaingia katikati ya duara kuonyesha madoido yake, basi anapomtaja mtu mwingine yule wa mwanzo huondoka mahali hapo. Wanaoingia katikati kucheza hutajwa kwa njia ya kuimba, na maneno, lakini wanapofika katika eneo la kuchezea wanazungumzishwa kwa njia ya filimbi na ishara za mikono.

Katika jukwaa la steji, uchezaji hufanyika kwa njia na mitindo ileile ya uchezaji kwenye jukwaa la duara. Hata hivyo, kulingana na muundo wa jukwaa hili kuna mabadiliko madogomadogo hususan katika namna ya mtindo wa uchezaji uitwao Shambi. Katika mtindo huu, badala ya kuingia katikati, wanaopaswa kuonyesha shambi husogea mbele, na mara nyingi husogea karibu na muimbaji kiongozi. Wakifika eneo hilo ndipo huonyesha madoido yao ya uchezaji.

Uchezaji unaofanyikia katika jukwaa la steji unawapatia washiriki wengine (watazamaji) nafasi ya kuwaona, kuwashangilia na kuwatunza wanaonengua kwa uwazi zaidi kuliko ilivyo katika jukwaa la duara. Katika jukwaa la duara, wanaonengua huwa hawaonekani (kwa watu walio nje ya duara), kwani wanakuwa wapo katikati ya duara na wanakuwa wamezungukwa na washiriki wengine. Kwa ujumla, mitindo ya uchezaji dansi inasaidia kuwasilisha maana mbalimbali ndani ya utendaji wa nyimbo za *mdumange*.

Miongoni mwa dhima za mitindo ya uchezaji katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* ni kusaidia katika kuwasilishia ujumbe uliokusudiwa kwa njia inayovutaia sana na inayojenga taharuki. Ujumbe huo unategemea aina ya sherehe au tukio la kiutendaji. Hii ina maana kuwa mitindo mbalimbali ya uchezaji inaakisi maoni na matarajio ya wanajamii kuhusiana na dhamira ya sherehe husika. Kwa mfano, sherehe mbalimbali zinazofanywa kwenye harusi huwa zinatoa mawaidha mbalimbali kwa bibi harusi mtarajiwa pamoja na bwana harusi. Sherehe hizi pia zinawapongeza wazazi wa watoto wanao oana.

Kulingana na muktadha huu hata uchezaji unaotokea katika muktadha wa sherehe za harusi unatumika kutimiza malengo yanayofanana na hayo. Katika sherehe hizi, wanawake pamoja na wanaume hukusanyika katika nyumba ambamo mnatarajiwa

kufanyikia ndoa baina ya binti na kijana. Kwa hiyo, katika muktadha huu uchezaji ni ishara inayotangaza tukio la harusi, na kulifanya tukio hilo lisiwe la siri, bali lifahamike kwa wanajamii wote. Kulingana na mila na utamaduni wa jamii hii, mapenzi ya sirisiri yanachukuliwa kama kitendo kisichofaa, na kwamba mapenzi ya dhahiri yanaenziwa na ndiyo yanayoheshimika.

Siku ya harusi pia huambatana na hafla za kuandaa karamu kwa wageni mbalimbali. Katika hali ya namna hii, kuna uchezaji maalum unaofanywa na wageni mara wanapomaliza kula. Uchezaji huu huashiria shukrani pamoja na furaha ya tukio lenyewe la harusi. Pongezi na shukrani hutolewa kwa wazazi wa bibi/bwana harusi, hususan kwa mzazi wa kike. Pia uchezaji hufanywa kwa minajili ya kuwafurahisha na kuondoa uchovu kwa watu mbalimbali walioshiriki kwenye maandalizi ya sherehe hiyo.

Kwa upande mwingine, katika hafla na mikutano ya kisiasa, mitindo mbalimbali ya uchezaji hutumika sambamba na mitindo mingine ya kiutendaji ili kuwasilisha ujumbe wa namna mbalimbali. Uchezaji hufanya kazi ya kukuza, kutangaza na kueneza utamaduni wa asili. Vilevile, utendaji hufanywa kwa minajili ya kuonyesha na kuwafurahisha wageni waalikwa (wanasiasa) utamaduni asilia wa Wasambaa. Nyimbo pia hutumika kama daraja la kuelimishia jamii kwa kutoa ujumbe maalum kulingana na kauli mbiu ya hafla husika. Miongoni mwa kaulimbiu zinazotangazwa kwenye majukwaa ya wanasiasa kupitia nyimbo za *mdumange* ni demokrasia, kujikinga na ugonjwa wa UKIMWI, uongozi bora na uwajibikaji. Vilevile, uchezaji wa nyimbo za *mdumange* katika majukwaa ya siasa unatoa ujumbe na nasaha kwa jamii kuhusiana na madhara ya madawa ya kulevyo kama vile pombe na bangi.



Mitindo ya uchezaji inayopatikana katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* pamoja na matumizi yake katika kufikisha ujumbe kwa jamii inatofautiana na aina nyingine za uchezaji katika jamii nyingine miongoni mwa Waswahili. Kwa mfano, uchezaji wa dansi unaofanywa na Waswahili Mombasa katika utendaji wa nyimbo za harusi unawahusisha wanawake peke yake, badala ya kuwahusisha na wanaume pia. Vilevile, tofauti na ilivyo katika utendaji wa nyimbo za *mdumange*, uchezaji wa nyimbo za harusi miongoni mwa Waswahili wa Mombasa huwaruhusu wanawake wacheze wakiwa wamevaa nusu uchi.

### **5.5 Hitimisho**

Sura imejihusisha na upambanuzi wa mitindo ya viziada lugha na nafasi yake katika kufanikisha utendaji wa wasanii na kujenga itikadi za wanajamii. Katika kutekeleza azma hii, mitindo ya utendaji kama vile miondoko, muziki, maleba, jukwaa na uchezaji wa dansi imechambuliwa. Aidha, imedhihirishwa kuwa nyenzo za viziada lugha zimemsaidia fanani kuumba ujumbe, kutagusana na hadhira yake na kujenga itikadi mbalimbali za Wasambaa. Imeonyeshwa bayana kuwa viziada lugha hushirikiana na vipashio vya kiisimu (lugha) kuzifanya nyimbo za *mdumange* zitekeleza wajibu wa kuelimisha na kuburudisha jamii. Sura ifuatayo inaelezea kwa muhtasari matokeo na mapendekezo ya utafiti huu.

## SURA YA SITA

### MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 6.0 Utangulizi

Katika utafiti huu tuliazimia kuchunguza nafasi ya mitindo ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika maisha ya Wasambaa. Aidha, utafiti ulifanyikia katika vijiji teule ya Wilaya ya Lushoto mkoa wa Tanga, nchini Tanzania. Katika sura hii masuala anuai yameelezwa kwa muhtasari. Masuala hayo yamejumuishwa muhtasari wa tasnifu, mahitimisho, mchango wa utafiti, na mapesndekezo ya utafiti.

#### 6.1 Muhtasari wa Tasnifu

Masuala mbalimbali yaliyojadiliwa kwenye kazi hii yameelezwa katika sura sita. Katika sura ya kwanza tumefafanua suala la utafiti pamoja na usuli kuhusu utendaji wa nyimbo, na fasihi simulizi ya Wasambaa. Kadhalika, ndani ya sura ya kwanza, suala la utafiti, na madhumuni ya utafiti yamebainishwa. Vilevile, katika sura ya kwanza ilifafanuliwa kuwa maswali yaliyokusudiwa kushughulikiwa ndani ya utafiti huu ni pamoja na:

- (i) Ni kwa namna gani miktadha ya jamii ya Wasambaa imechochea utendaji wa nyimbo za *mdumange*?
- (ii) Je, ni ipi dhima ya mitindo ya lugha katika kuwasilisha nyimbo na kusawiri maisha ya Wasambaa?
- (iii) Je, mitindo ya viziada lugha ina nafasi gani kwa wasanii na jamii ya Wasambaa kwa ujumla?

Vilevile, katika sura ya kwanza tulijadili mikakati mbalimbali ya uteuzi wa mbinu za utafiti. Ilielezwa kuwa mbinu kuu zilizotumika katika utafiti huu ni uchunguzi shiriki,

usaili na mijadala ya vikundi. Vifaa vya utafiti kama vile kamera, kinasa sauti na redio kaseti vilitumika kurekodia data zilizokusanywa nyanjani.

Katika sura ya pili tulijikita kwenye uhakiki wa maandiko pamoja na kiunzi cha kiNadharia. Masuala mahsusi yaliyojadiliwa kwenye sura hiyo yaliangazia dhana za sanaa jadiya, sanaa za maonyesho na vipera mbalimbali vya fasihi simulizi, hususan nyimbo. Kutokana na upitiaji pamoja na uhakiki wa maandishi, ilibainishwa kuwa wahakiki wengi wanaelekea kusesitiza kuwa utendaji ndio msingi mkuu wa kisanaa unaowezesha kupambanua ujumi wa kazi za kifasihi. Pia maandishi yaliyohakikiwa yalidhihirisha namna nyimbo kama kipera kimojawapo cha fasihi simulizi zinavyotumiwa na wanajamii kwa minajili ya kuburudisha na kuelimisha. Hata hivyo, sura hii ilihitimishwa kuwa licha ya kuwa nyimbo za *mdumange* zimekuwa na bado zinaendelea kuwa amali muhimu ya Wasambaa, hakuna utafiti wa kina uliofanywa dhidi yake. Ni kutokana na kukosekana kwa utafiti wa kina kwenye nyimbo za *mdumange* ambapo utafiti huu umefanyika. Aidha, ili kuyakabili madhumuni ya utafiti huu Nadharia za Utendaji wa Maigizo na Semitoiki ya Kijamii ziliteuliwa. Misingi na matumizi ya Nadharia hizi yalijadiliwa kwa kina katika sura hii ya pili.

Uwasilishwaji na uchanganuzi wa matokeo ya utafiti uliangaziwa katika sura za tatu, nne na tano. Katika sura ya tatu mtafiti aliwasilisha na kujadili matokeo yaliyowezesha kujibu swali la kwanza la utafiti huu. Mjadala wa sura hii ulijikita juu ya miktadha ya kijamii na dhima yake katika kuchochea utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Suala la muktadha wa kijamii liliangaziwa kwenye utafiti huu kama kipashio kikuu cha Nadharia za Utendaji wa Maigizo na Semiotiki ya Kijamii. Hivyo, sura ya tatu ilielelza kuwa utafiti huu umebaini kwamba utendaji wa nyimbo za *mdumange* umechochewa na miktadha mikuu mitatu ya jamii ya Wasambaa ambayo

ni turathi simulizi za Wasambaa, mtagusano na wageni pamoja na matukio ya sherehe za Wasambaa. Sura hii ilihitimishwa kwa maelezo kuwa kamwe ujumi na historia ya nyimbo za *mdumange* haiwezi kueleweka vyema bila kuzingatia miktadha iliyopambanuliwa. Miktadha hiyo iliathiri muundo wa mitindo ya utendaji (lugha na viziada lugha) pamoja na uamilifu wake katika utendaji wa nyimbo za Wasambaa, hususan nyimbo za *mdumange*.

Matokeo kuhusu mitindo ya lugha na dhima yake katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yalijadiliwa katika sura ya nne. Aidha, sura hii ilijikita katika vijejezi mbalimbali vya matumizi ya lugha vilivyomuwezesha mtafiti kujibu swali la pili la utafiti. Kutokana na maelezo ya watafitiwa, na pia kutokana na uchambuzi wa nyimbo utafiti huu umebaini kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* unaongozwa na mitindo mikuu ya saba ya matumizi ya lugha. Mitindo hiyo ni uchanganyaji misimbo, arudhi za kishairi, tamathali za usemi, methali, nahau pamoja na misemo. Mitindo hii ya lugha imeweza mawasiliano baina ya wasanii na hadhira yao. Kadhalika, mitindo ya lugha iliyojadiliwa imewaafanya wasanii wawasilishe nyimbo kwa njia inayovutia zaidi na hatimaye kuburudisha na kuelimisha jamii.

Katika utafiti huu pia imebainika kuwa wasanii hutumia mitindo ya lugha kujadili masuala muhimu kuhusu maisha ya Wasambaa kama vile ndoa, mapenzi, uwajibikaji, uongozi, madawa ya kulevya, magonjwa na mazingira. Mwisho, katika sura ya nne ilihitimishwa kuwa ingawa wasanii hutumia mitindo ya lugha kuwasilisha ujumbe wa namna mbalimbali, utendaji wao pia unategemea nyenzo nyingine za kimawasiliano zisizotumia lugha ya mdomo (viziada lugha). Dhima na nafasi ya nyenzo hizo ilijadiliwa katika sura ya tano.

Kimsingi, sura ilianza kwa kufafanua umuhimu wa misingi ya Nadharia za Utendaji wa Maigizo na Semiotiki ya Kijamii katika kukabiliana na uchunguzi wa mitindo ya viziada lugha. Mitindo ya viziada lugha iliyojadiliwa katika sura hii ala za muziki kama vile ngoma, manyanga, gunda, na filimbi. Mitindo mingine ni miondoko, uchezaji na uigizaji. Kwa ufupi, sura ya tano ilimuwezesha mtafiti kujibu swali la tatu la utafiti lililouliza kuhusu dhima na nafasi ya mitindo ya viziada lugha kwa wasanii na jamii ya Wasambaa kwa ujumla. Ilikezwa katika sura hiyo kwamba, fanani, hadhira na washiriki wengine wa nyimbo huwasiliana wao kwa wao kwa kutumia mitindo ya viziada kugha iliyobainishwa na kujadiliwa. Aidha, mitindo hiyo pia hujenga falsafa za Wasambaa kuhusu utamaduni wao, uhusiano wa kijinsia na mamlaka ya kisiasa. Sura hii pia imeonyesha jinsi mbinu za viziada lugha zinavyochangia katika kufasiri ishara za utamaduni wa Wasambaa. Vipengele vya utamaduni wa Wasambaa vilivyowasilishwa kwa kutumia mitindo ya viziada lugha ni malezi, mapenzi, uongozi na masuala ibuka (maradhi, mazingira na madawa ya kulevya).

Baada ya kueleza na kujadili masuala yaliyojadiliwa kwenye utafiti huu kutoka sura ya kwanza mpaka ya tano mtafiti amemaliza kwa kutoa muhtasari kwenye sura ya sita. Katika sura ya sita vipengele mbalimbali vya utafiti vimeelezwa kwa muhtasari. Miongoni mwa vipengele hivyo ni muhtasari wa utafiti, mchango wa utafiti, hitimisho pamoja na mapendekezo ya utafiti. Sehemu ifuatayo imefafanua kwa muhtasari mahitimisho na matokeo ya utafiti.

## **6.2 Mahitimisho ya Utafiti**

Kulingana na michakato ya ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu, tunatoa mahitimisho kuhusu madhumuni na maswali ya utafiti kama ifuatavyo:

### 6.2.1 Jinsi Miktadha ya Kijamii Iliyochochewa Utendaji wa Nyimbo

Katika utafiti huu tumebaini kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* umechochewa na miktadha anuai ya Wasambaa. Aidha, miktadha hii pia imeathiri mitazamo ya Wasambaa kuhusu kuibuka na kustawi kwa nyimbo za *mdumange*. Miktadha hiyo ni pamoja na turathi simulizi za Wasambaa, mtagusano na wageni na matukio ya sherehe za Wasambaa. Miktadha wa turathi simulizi za Wasambaa umezua vichocheo vya utunzi na uwasilishaji wa nyimbo kama vile dhamira, mitindo ya uwasilishaji na vifaa vya kiutendaji. Kwa ufupi, kutokana na utafiti huu imebainika kuwa kati ya watafitiwa ishirini na wanne (24) waliohojiwa, watafitiwa kumi na watatu (13) ambao ni sawa na asilimia hamsini na nne desimali moja (54.1%) waliunga mkono hoja kuwa nyimbo za *mdumange* zimetokana na turathi simulizi za Wasambaa. Turathi zilizohusishwa na kuzuka pamoja na kustawi kwa nyimbo za *mdumange* ni miviga, matambiko, uganga, uchawi na mashindano ya vikundi vya kisanaa. Mtazamo wa Wasambaa wanaounga mkono hoja hii ni kuwa nyimbo za *mdumange* zilianza siku nyingi sana, hata kabla ya ukoloni na kwamba mitindo ya utendaji wa nyimbo hizi imekuwa ikibadilikabadilika toka zama hadi zama.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tumetoa hoja kuwa, ingawa kwa kiwango kikubwa ujumi wa nyimbo za *mdumange* umetokana na turathi simulizi zilizoainishwa, kuna uwezekano baadhi ya vipashio vya kifasihi vikawa vimetoka kwenye makabila mengine. Ni kutokana na msingi huu ambapo, utafiti huu ulibaini kuwa baadhi ya watafitiwa wanaona kuwa nyimbo za *mdumange* zimezuka kutokana na fasihi iliyoitwa 'hiyari ya moyo' kutoka jamii ya Wanyamwezi miaka ya 1884 - 1959. Hoja hii iliungwa mkono na watafitiwa saba pekee kati ya watafitiwa ishirini na wanne waliohojiwa. Hii ni sawa na asilimia ishirini na tisa desimali mbili (29.2%).

Wanaounga mkono hoja hii wanafafanua kuwa kabla ya kuletwa kwa ‘hiyari ya moyo’, Wasambaa walikuwa na sanaa yao ya asili iliyoitwa ‘gongwe’. Kwa ujumla, Wasambaa wanaoona kuwa awali, *mdumange* uliitwa ‘gongwe’ na baadaye ukabadilishwa na Wanyamwezi ukawa ‘hiyari ya moyo’. Mtazamo huu umetufanya tuhoji kuwa yamkini sanaa za *mdumange* au hiyari ya moyo zilikuwa na mvuto zaidi kiutendaji kiasi kwamba watu wengi walivutiwa nazo na hatimaye zikasababisha kutoweka kwa ‘gongwe’ pamoja na ‘spein’. Kwa ujumla, utafiti huu umebaini kuwa falsafa ya Wasambaa inaelekea kusisitiza kuwa tanzu mbalimbali za kifasihi zimekuwa zinazuka na kutokweka tangu kale kutokana na mahitaji ya wanajamii. Hii ndiyo sababu iliwafanya waachane na gongwe na hatimaye wakajihusisha na hiyari ya moyo ambayo kwa sasa inajulikana kwa jina la *mdumange*.

Kadhalika, kutokana na maelezo ya watafitiwa, mtafiti ametoa hoja kuwa yamkini makundi yote mawili yanaafikiana kuwa hata kabla ya kuanza kwa *mdumange* kulikuwa na aina nyingine za sanaa ambazo ndizo zilizozua utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Hii ni kusema kuwa, kwa vyovyote vile, utendaji wa nyimbo za *mdumange* haukuanza katika ombwe, bali umeanza na kustawi katika muktadha wa jamii ya Wasambaa. Muktadha huo ulikuwa umesheheni fasihi ya wenyeji na fasihi za wageni, hususan fasihi ya Wanyamwezi.

Maelezo ya watafitiwa yanashadidia hoja kuwa nyimbo za *mdumange* ni sanaa ya kijamii ambayo imekuwako siku nyingi. Katika kuwako kwake imekuwa ikibadililabadilika. Zamani sana nyimbo hizi ziliitwa ‘gongwe’. Aidha, katika miaka ya kabla ya sitini jina la nyimbo hizi lilibadilika na kuwa ‘spein’. Hata hivyo, tangu miaka ya sitini mpaka leo jina kuu linalotumika kuzitambulisha nyimbo zilizochunguzwa ni ‘*mdumange*’.

Pia tumegundua kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* umechochewa na matukio ya sherehe za jamii ya Wasambaa kama vile harusi, sikukuu za dini na hafla za kisiasa. Ushahidi kutoka nyanjani unaonyesha kuwa hoja hii inaungwa mkono na idadi ndogo ya watafitiwa kwa kuwa kati ya watafitiwa ishirini na wanne (24) waliohojiwa ni watafitiwa wanne (4) tu waliohusisha utendaji na sherehe za kijamii. Hii ni sawa na asilimia kumi na sita desimali saba (16.7%) ya watafitiwa wote. Licha ya kuwa hoja hii iliungwa mkono na watafitiwa wachache zaidi, utafiti huu unatoa hoja kuwa kimsingi matukio ya sherehe hususan hafala za kisiasa, dini na harusi yamechochea kustawi kwa nyimbo kwa kiwango kikubwa.

Mchango wa sherehe zilizoainishwa umeonekana katika kubainisha maudhui, mahali pa kutendea, washiriki na mitindo ya uwasilishwaji. Wasanii wa nyimbo za *mdumange* wamekuwa na ujuzi wa hali ya juu kwa vile wanajua muktadha ndio msingi wa utendaji wao. Kwa kila muktadha wamebuni aina mahsusi ya nyimbo na mitindo ya utendaji inayobadilika ili kukidhi haja za hadhira lengwa. Mabadiliko ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* yanaakisi uhusiano uliopo kati ya fasihi na jamii.

Kwa upande mwingine, muktadha wa matukio ya kiutendaji umedokeza uamilifu wa nyimbo za *mdumange* katika jamii ya Wasambaa. Ilionyeshwa kuwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* unafanyika katika matukio yanayoambatana na itikadi ya mfumo wa maisha ya Wasambaa. Itikadi hiyo imeugawa ulimwengu wa Wasambaa katika sehemu kuu mbili: Furaha na huzuni. Kutokana na mfumo au muundo wa itikadi hii, nyimbo za *mdumange* ni kiwakilishi cha sanaa inayotendwa kwenye matuko ya furaha na ni jukwaa maalum linalowapatia fursa wanajamii kufurahika, kutoa hisia zao na kuwasiliana miongoni mwao kwa njia ya kisanaa.



Muktadha mwingine uliochangia udhihirishwaji wa ujumi na diskosi ya Wasambaa ni Utendaji wa Maigizo. Kutokana na athari za muktadha huu, utafiti huu umetoa hoja kuwa kwa kiwango kikubwa nyimbo za *mdumange* zinawasilishwa kwa kutumia miundo ya utendaji wa kimaigizo, na hivyo hata upataji maana hauna budi kuzingatia hali hii. Kimsingi, utafiti huu umetoa hoja kuwa, nyimbo za *mdumange* ni sanaa inayotendwa katika matukio ya furaha, na kamwe nyimbo hizi haziwasilishwi kwenye misiba. Kutokana na msingi huu, hata mitindo yake ya uwasilishwaji imekuwa na dhima za kuburudisha na kuelimisha. Mitindo hiyo ni lugha na viziada lugha.

### **6.2.2 Mitindo ya Lugha na Dhima yake katika Kuwasilisha Ujumbe**

Utafiti huu umebaini kuwa uwasilishaji wa nyimbo za *mdumange* unajumuisha pamoja matumizi ya mitindo mbalimbali ya kiutendaji inayotumia lugha na viziada lugha. Mitindo hii hutegemeana na hukamilishana katika kuwasilisha ujumbe au maana zinazolandana na muktadha wa tukio la kiutendaji.

Kutokana na utafiti huu, tumebaini kuwa lugha hutumika kama nyenzo kuu ya utendaji wa nyimbo za *mdumange*. Nyenzo hii hutumiwa na wasanii kutekeleza malengo makuu mawili: (i) kuburudisha jamii na (ii) kujenga diskosi ya Wasambaa kuhusu masuala nyeti ya kijamii kama vile malezi, ndoa, mahusiano ya kijinsia, siasa, umoja, afya na utunzaji wa mazingira.

Utafiti huu umeweka bayana kuwa katika harakati za kuwasilisha ujumbe kwa hadhira, fanani hutumia mikakati anuai ya mitindo ya lugha kama vile uchanganyaji misimbo, arudhi za kishairi, tamathali za usemi, mianzo na miisho ya kifomula, methali na nahau. Kwa kiwango kikubwa, utendaji wa nyimbo za *mdumange* umetawaliwa na matumizi ya matumizi ya lugha ya kimaigizo. Miundo ya utendaji wa kimaigizo ilijumuisha vipengele vya fomula maalum, arudhi za kishairi na

upokezanaji zamu. Utafiti huu pia umetoa hoja kuwa upokezanaji zamu ndio muundo mkuu unaotumika katika kuwasilisha nyimbo za *mdumange* mbele ya hadhira.

Aidha, ndani ya muktadha wa kiutendaji, mpangilio wa muundo wa nyimbo za *mdumange* unaathiriwa na michakato mingine ya kiutendaji kama vile ufaraguzi wa fanani, ubadilishaji mada na uradidi. Mikakati hii imewawezesha mawasiliano kati ya fanani na hadhira wakati wa utendaji wa nyimbo. Kupitia matumizi ya mikakati hii utafiti huu umethibitisha kuwa nyimbo za *mdumange* zina ujumi wa kipekee unaozipambanua kama sanaa mahsusi iliyosheheni vipashio mbalimbali vya itikadi za ulimwengu wa Wasambaa.

Kimsingi, imebainika pia kuwa mitindo ya utendaji (matumizi ya lugha) katika nyimbo *mdumange* imebadilika kwa kiwango kikubwa. Tofauti na ilivyokuwa hapo awali, ambapo lugha ya Kisambaa ilitumika sana, katika wakati wa sasa matumizi ya lugha hii yanaenda sambamba na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Aidha, kwa sasa utendaji wa nyimbo hizi umekuwa raslimali ya kiuchumi ambapo vijana wanajipatia kipato. Kubadilika kwa mitindo ya utendaji pamoja na hadhi ya nyimbo za *mdumange* kumechochewa na hali mpya za kijamii, kisiasa na kiuchumi zinazoathiri maisha ya Wasambaa.

### **6.2.3 Nafasi ya Mitindo ya Viziada Lugha kwa Wasanii na Jamii**

Kwa upande mwingine, kando na matumizi ya mitindo ya lugha, utafiti huu pia umegundua kuwa wasanii wa nyimbo za *mdumange* hutumia mitindo ya viziada lugha kutekeleza majukumu mbalimbali. Mitindo hiyo ina nafasi kubwa kwa wasanii wa nyimbo na jamii kwa ujumla. Kwa ufupi, mitindo ya viziada lugha iliyojadiliwa katika utendaji wa nyimbo za *mdumange* ilijumuisha miondoko, muziki, maleba, jukwaa na uchezaji wa dansi.

Aidha, kupitia utafiti huu imedhihirishwa kuwa nyenzo za viziada lugha zimemsaidia fanani kuumba ujumbe, kutagusana na hadhira yake na kujenga itikadi mbalimbali za Wasambaa. Imeonyeshwa bayana kuwa viziada lugha hushirikiana na vipashio vya kiisimu (lugha) kuzifanya nyimbo za *mdumange* zitekeleza wajibu wa kuelimisha na kuburudisha jamii. Mitindo hii imeshirikiana na lugha katika kuzifanya nyimbo za *mdumange* zivutie na ziwasilishe ujumbe unaokuza na kuendeleza itikadi mbalimbali za Wasambaa.

### **6.3 Mchango wa Utafiti**

Katika utafiti huu tumeonyesha kuwa nyimbo za *mdumange* ni chemchemi ya kuufasiri ulimwengu wa wasanii na wa jamii kwa ujumla. Ulimwengu huo unasawiriwa na mikakati ya kiutendaji ambayo ni muktadha, lugha na viziada lugha. Kadhalika, utafiti huu umetoa mchango mkubwa katika jamii kwa kutujuza kuwa, utendaji wa nyimbo za *mdumange* na nyimbo kwa ujumla unaweza kutumika sio tu kuburudisha jamii, bali pia katika kuibua hisia za harakati za ukombozi na ujenzi wa jamii mpya. Vilevile, utafiti huu umechangia katika kukuza taaluma ya uchunguzi wa fasihi simulizi kwa njia ya kurekodi utendaji hai moja kwa moja kutoka kwa jamii inayochunguzwa.

### **6.4 Mapendekezo ya Utafiti huu**

Kutokana na utendaji wa nyimbo za *mdumange* kuwa raslimali muhimu ya maisha ya Wasambaa, Raslimali hii itaendelea kutumika katika maisha ya jamii yake madamu bado ina tija kwa wanaoitenda. Hata hivyo, dhima na mitindo yake inabadilika sana kila siku kutokana na mabadiliko ya kimuktadha katika jamii. Wasanii wa nyimbo za *mdumange* wana wajibu wa kuiendeleza, kuienzi na kuitangaza tunu hii ili isije ikapotea. Mikakati ya kimakusudi inatakikana miongoni mwa vikundi vya wasanii wa

nyimbo za *mdumange* na jamii kwa ujumla katika kukuza na kuendeleza utendaji wa nyimbo za *mdumange* na aina nyingine za fasihi simulizi ya Wasambaa.

Kadhalika, mamlaka za kiserikali zinapaswa kuhimiza matamasha na sherehe zinazochochea uwasilishwaji wa nyimbo za *mdumange*. Katika uhimizaji huo, maarifa ya kijamii kuhusu maisha yao, ustawi wa jamii na wa taifa kwa ujumla yatabainishwa. Kwa mfano, kupitia utendaji wa nyimbo za *mdumange* kwenye matamasha ya kijamii, itabainika wazi jinsi jamii na utamaduni wa Wasambaa unaelekeza katika jitihada za kuihifadhi jamii dhidi ya maambukizi ya maradhi, mmomonyoko wa maadili, kukuza uchumi, falsafa ya uongozi na utunzaji wa mazingira. Kwa hivyo, kitendo hiki kitazifanya nyimbo za *mdumange* na aina nyingine za fasihi zichangie katika ustawi wa taifa kwa njia ya kuburudisha na kuelimisha.

### **6.5 Mapendekezo kwa Ajili ya Tafiti za Baadaye**

Katika utafiti huu tulichunguza utendaji wa nyimbo za *mdumange*, nyimbo ambazo huwasilishwa katika muktadha wa sherehe za harusi, sikukuu za kidini na hafla za kisiasa. Kutokana na hali hii, mtafiti hakuweza kuchunguza hali ya utendaji wa nyimbo zinazotokea katika muktadha mwingine kama vile katika matanga au misiba. Hivyo, ipo haja kwa watafiti wengine kuchunguza utendaji wa aina nyingine za nyimbo na fasihi simulizi ya Wasambaa, hususan nyimbo zinazoimbwa kwenye miktadha ya uganga na misibani. Kadhalika, utendaji wa nyimbo umehusisha aina tatu za nyimbo kwa wakati mmoja (harusi, kidini na za kisiasa), Tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe kwa kujikita katika aina moja mahsusi ya nyimbo zinazoimbwa kwenye muktadha wa sherehe huku zikitumia *mdumange*. kwa mfano, katika harusi, dini na siasa badala ya kuzichunguza zote kwa pamoja.

## MAREJELEO

- Abdallah, A. (1973). "Ushairi wa Kiswahili na Uhusishwe Usiuliwe." Katika *Zindiko*. Dar-es-Salaam: Chama cha Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.
- Abeid, A.K. (1991). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Ajjemy, A.H. (1978). *Habari za Wakilindi*. Nairobi: East Africa Literature Bureau
- Alembi, E. (2002). "The Construction of the Abanyole Perceptions on Death Through Oral Funeral Poetry." *Tasnifu ya Uzamvu*, Chuo Kikuu cha Helsinki (Haijachapishwa).
- Almabrok, I.M. (2004). "Kutathmini Dhima ya Nyimbo katika Kukuza na Kuimarisha Malezi: Mfano wa Kabila la Wakaguru." *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa).
- Askew, J. (2002). *Performing the Nation Through Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania*. London: Heinemann.
- Austin, J. L. (1965). *How to Do Things with Words*. Oxford: Oxford University Press.
- Barthes, R. (1964). *Elements de Semiologie Communications 4*. Seull: Paris.
- Bauman, R. (1975). "Verbal Arts as Performance." Katika *American Anthropology New Series*, juz. 77, na. 2, kur. 290 – 311. Ilisomwa tarehe 15/07/2015 katika <http://www.jstor.org>.
- Bauman, R., & Briggs, C. (2003). "Poetics and Performance as Critical Perspectives on Language and Social Life." Katika *Annual Review of Anthropology*, juz. 19, kur. 59-88.
- Bauman, R., & Sherzer, J. (Wah.). (2011). *Explorations in the Ethnography of Communication*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Baumgardt, U. (2002). *Littératures Africaines: Langue, Mode de Communication et Representations Identitaires*. Paris: INALCO.
- Brecht, J. (1990). "Determining the Focus of Instruction: Content Planning for Intelligent Tutoring System." *Tasnifu ya Uzamivu*. Chuo Kikuu cha Saskatchewan (Haijachapishwa).
- Brown, R.A. (2016). *Structure and Function in Primitive Society*. Glencoe: Free Press.
- Brunott, J.M. (2013). "Orality, Textuality and History Issues in South African Oral Poetry and Performance." *Tasnifu ya Uzamivu*, Chuo Kikuu cha Kwa Zulu Natal (Haijachapishwa).
- Bryman, A. (2004). *Social Research Methods (Toleo la Pili)*. Oxford: Oxford University Press.
- Chomsky, N. (2007). *Aspects for the Theory of Syntax*. Cambridge: MIT Press.

- De Vet, T. (1996). "The Joint Role of Orality and Literacy in the Composition, Transmission, and Performance of the Homeric Texts: A Comparative View." *Katika Transactions of the American Philological Association*, juz. 126, kur. 43-76.
- De Vet, T. (2008). "Context and the Emerging Story: Improvised Performance in Oral and Literate Societies." *Katika Oral Tradition*, juz. 23, na. 1, kur. 159-179.
- Dundes, A. (1971). "Folk ideas as Unit of Worldview." *Katika The Journal of American Folklore*, juz. 84, na. 331, kur. 93-103.
- Eco, U. (1984). *Semiotics & Philosophy of Language*. Bloomington. Indiana University Press.
- Eliasoph, N. (1990). "Political Culture and Presentation of a Political Self: A Study of the Public Sphere in the Spirit of Erving Goffman." *Katika Theory and Society*. Netherlands: Kluwer Academic Publishers, Juz. 19, na. 4, kur. 465-494.
- Escarpit, R. (1974). *Sociology of Literature*. London: Frank Cass and Co. Ltd.
- Fabb, N. (2009). "Why is verse poetry?" *Katika Poetry Nation Review*. Carcanet Press, kur. 52-57.
- Feierman, S. (1972). "Concepts of Sovereignty Among the Shambaa and their Relation to Political Action." *Tasifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Wadham (Haijachapishwa)*.
- Feierman, S. (1974). *The Shambaa Kingdom*. Madison: University of Wisconsin Press.
- Feierman, S. (2000). "Explanation and Uncertainty in the Medical World of Ghaambo." *Katika Bulletin of the History of Medicine*, The Johns Hopkins University Press, kur. 317-344.
- Feierman, S. (2008). *Peasant intellectuals: Anthropology and History in Tanzania*. Madison: University of Wisconsin Press.
- Fenner, M. (2010). *Language as a Social Semiotic: The Social Interpretation of Language and Meaning*. University Park Press.
- Fenton, M. (Ed.) (2003). *Bat Ecology*. Chicago: University of Chicago Press.
- Finnegan, R (1992): *Oral traditions and the verbal arts: a guide to research practices. (ASA Research Methods in Social Anthropology*. London and New York: Routledge.
- Finnegan, R (2015). *Where is Language?* London: Bloomsbury.
- Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Cambridge: Open Book Publishers.
- Finnegan, R. (1997). *Oral Poetry: Its Nature, Significance and Social Context*. Cambridge: Cambridge University Press.

- Finnegan, R. (2007). *How to do things with words: the oral in Africa*, Chicago. Chicago University Press.
- Foley, J. (1988). *The Theory of Oral Composition: History and Methodology*. Bloomington: Indiana University Press.
- Foley, J. (1995). *The Singer of the Tales Performance*. Bloomington. Indiana University Press.
- Foley, J. (2002). *How to Read an Oral Poem*. Urbana: University of Illinois Press.
- Forster, M. (2007). *The Hill of Devi*. Houghton Mifflin: Harcourt Publishing Company.
- Frazer, J. (1890). *The Golden Bough: A Study in Comparative Religion*. London: Macmillan.
- Geertz, C. (1973). *The Interpretation of Culture*. New York: Basic Books.
- Gennep, V.A. (1960). *Les Rites de passage*. Chicago: University of Chicago Press.
- Goffman, E. (1959). *The Presentation of the Self in Everyday Life*. New York: Doubleday. Anchor.
- Goffman, E. (1963). *Behavior in Public Places: Notes on the Social Organization of Gatherings*. Free Press.
- Goffman, E. (1974). *Frame Analysis: an Essay on the Organization of Experience*. New York: Harper & Row.
- Greene, R. & S. Cushman. (2006). *The Handbook of Poetic Terms*. Princeton: Princeton University Press.
- Guba, E.G. (1981). "Criteria for Assessing the Trustworthiness of Naturalistic Inquires." *Katika Educational Communication and Technology*. Juz. 29, kur. 76-92.
- Harding, F. (Mhar.). (2002). *Performance Arts in Africa*, London: Routledge.
- Hoffman, T. (2013). *American Poetry in performance: From Walt Whitman to Hip Hop*. Michigan: University of Michigan Press.
- Honko, L. (Mhar.). (2000). *Textualization of Oral Epics*. Berlin: Mouton de Gruyter.
- Hymes, D. (2007). "Models of the Interaction of Language and Social Life." *Katika* Gumperz, J. J. & Hymes, D. (Wahar.). *Directions in Sociolinguistics: The Ethnography of Communication*. New York: Rinehart & Winston.
- Jakobson, R. (1960). "Concluding Statement: Linguistics and Poetics." *Katika* Sebeok, T. (Mha.). *Style in Language*. Cambridge: MIT Press, kur. 350-77.
- Jameson, F. (2005). *Archaeologies of the Future: The Desire Called Utopia and Other Science Fictions*. London & New York: Verso.

- Johansson, C. (2009). "On Goffman: Researching Relations with Erving Goffman as Pathfinder." Katika O. Ihlen, B. van Ruler, & M. Fredriksson (Wah.). *Public Relations and Social Theory, Key Figures and Concepts*. New York: Routledge, kur. 119–140.
- Jones, R.A. (2007). *Jung, Psychology, Postmodernity*. Hove, East Sussex: Routledge.
- Jung, C.G. (1933). *Modern Man in Search of a Soul*. New York: Harcourt, Brace.
- Karim, B. (1999). *Yoruba Wuyi (with Akin Oyetade)*. A Revised and Substantially Expanded Version of Yoruba Dun un So, Part I. London: Hakuna Matata Press.
- Karim, B. (2007). *The Anthropology of Texts, Persons and Publics: Oral and Written Culture in Africa and Beyond*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Kezilahabi, E. (1981). "Ushairi na Nyimbo katika Utamaduni." Katika *Urithi wa Utamaduni Wetu*. Dar-es-Salaam: Tanzania Publishing House.
- Kihore, Y.M. (2002). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kipury, N. (1983). *Oral literature of the Maasai*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
- Kitogo, S. A. (2005). *KIJA Chungu cha Mwana Mwari wa Gining*, Dar es Salaam: TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- Kitzinger, J. (2000). The Methodology of Focus Groups: The Importance of Interactions Between Research Participants. Katika *Sociology of Health and Illness*, juz. 16, na. 2, kur. 103-21.
- Kobia, J. (2004). "Taswira ya Mwanamke katika Njuno (Methali) za Kimeru." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi (Haijachapishwa).
- Kothari, C. R. (2004), *Research Methodology: Methods and Techniques*, (Toleo la Pili), New Age International Publishers.
- Kristina, R.K. (2009). *The Syntax of Object Marking in Sambia: A Comparative Bantu Perspective*. LOT: Utrecht Netherlands.
- LangHeirinch, S. (1921). *Schambala-Worterbuch*. L. Friederichsen & Company: Princeton University.
- Lawrence, D. (2009). *Tanzania and Its People*. New Africa Press.
- Lewis, J. (2002). *Cultural Studies*. London: Sage Publications.
- Lord, A. (2000). *The Singer of Tales*. Harvard: Harvard University Press.
- Mackie, C. J. (2004). *Oral Performance and its Context*. Leiden: Brill.
- Malinowski, B. (1935). *Gardens and their Magic*. New York: American Book Company.



- Matti, N. (2009). "Sanaa za Maonyesho za Kiafrika za Jadi: Mfano wa Tohara ya Watharaka." *Tasnifu ya Uzamili*, Chuo kikuu cha Moi (Haijachapishwa).
- Mayoka, J. (1986). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mazrui, A.M. (2007). *Swahili Beyond the Boundaries: Literature, Language, and Identity*. Athens: Ohio University Press.
- Mbiti, M. (1975). *An Introduction to African Religion*. Nairobi: Heineman.
- Melnitz, W. (1955). *The Living Stage: A History of the World Theatre*. Prentice-Hall Inc.
- Miruka, O. (1994). *Encounter with Oral Literature*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mlama, P.M. (1983) "A Tanzanian Traditional Theatre as Pedagogical Institution: The Kaguru Theatre as a Case Study." *Tasnifu ya Uzamivu*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Mollel, L.M. (2008). "Utafiti wa Lugha za Asili Tanzania: Semina ya Utafiti kwa Maafisa Utamaduni." Katika Makala za Kongamano la Maafisa wa Utamaduni mjini Dodoma (Haijachapishwa).
- Mulokozi, M. M. (2002). *The African Epic Controversy: Historical, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Poetry and Performance*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.
- Muzale, H. R. T., & Rugemalira, J. M. (2008). "Researching and Documenting the Languages of Tanzania." Katika *Langage Documanting and Preservation*. Dar es Salaam: Languages of Tanzania Project.
- Mvula, E. T. (1994). *Strategy in Ngoni Women Oral Poetry. Critical Arts*. Michigan State University Press.
- Nasiri, S.A.A. (1972). *Al – Inkishafi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Ngadala, D.K. (2003). "Ujenzi na Mmomonyoko wa Maadili ya Taifa." Makala Iliyowasilishwa katika Mkutano wa Sekta ya Utamaduni, Morogoro (Haijachapishwa).
- Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nkondokaya, V. G. (2006). *Asili ya Tanga Pamoja na Asili ya Wadigo, Wasegeju na Wadaiso, Pamoja na koo za kabila Nyingine Ndogondogo Zilizo ndani ya Makabila Haya*. Dar es Salaam: Human Development Centre.
- Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds, Character, and Continuity*. Bloomington: Indiana University Press.
- Omari, S. (2009). "Hip Hop Music as Popular oral Poetry." *Tasnifu ya Uzamivu*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

- Owomoyela, O. (2008). *African Literatures: An Introduction*. Crossroads Press: Waltham, Mass.
- Parry, A. (Mhr.). (1987). *The Making of Homeric Verse: The Collected Papers of Milman Parry*. Oxford: Oxford University Press.
- Peter, M. (2013). "The Usambara Mountains of Tanzania Irente Biodiversity Reserve." Iliyosomwa tarehe 30/06/2016 katika <http://www.Usambara.community.org>.
- Pongwen, A. (2007). "Voicing the Text: South African Oral Poetry and Performance." Katika *Journal of African Cultural Studies*, juz. 14, kur. 175-180.
- Rajwayi, A.C. (2009). "Maudhui na Mtindo katika Nyimbo za Msanii Faustin Munishi." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).
- Rappaport, R.P. (1968). *Pigs for the Ancestors*. New Haven: Yale University Press.
- Rirash, M. (1992). "Somali Oral Poetry as a Vehicle for Understanding Disequilibrium and Conflicts in a Pastoral Society" Katika *Nomadic Peoples*, juz. 30, kur. 114-121. Iliyosomwa tarehe 21/05/2016 katika <http://www.jstor.org>.
- Samwel, M. (2012). "Mabadiliko katika Majigambo ya Jadi na ya Bongo Fleva Tanzania." Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Schechner, R. (1988). *Performance Theory*. New York and London: Routledge.
- Schechner, R. (2013). *Performance Studies: An Introduction*. Routledge: New York.
- Sebeok, T.A. (1959). *Encyclopedic Dictionary of Semiotics*. Berlin: Mouton de Gruyter.
- Sengo, T.S.Y. (2009). *Fasihi za Kinchi*. Dar-es-Salaam: Kiswahili Researcher Products.
- Senkoro, F.E.M.K. (1988). *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*. Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam University Press.
- Silverman, D. (2005) *Doing Qualitative Research: A Practical Handbook* London: SAGE Publications.
- Simiyu, W.F. (2015). "Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa *Embalu na Mwaka Kogwa*." Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).
- Tarsitani, B.A. *et al.* (2010). *Preserving Local Knowledge in the Horn of Africa: Challenges on Prospects for Collaborative Research in Oral Literature, Music and Ritual Practices*. Kyoto: Kyoto University.

- Tsiu, M.W. (2008). *Basotho Oral Poetry at the Beginning of the 21<sup>st</sup> Century*. Pretoria: University of South Africa. Iliyosomwa tarehe 15/02/2015 katika <http://hdl.handle.net/>.
- Turner, V. (1982). *From Ritual to Theatre: The Human Seriousness of Play*. New York: Performing Arts Journal Publications.
- Vansina, J. (1985). *Oral Tradition As History*, Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.
- Wanyama, M.N. (2005). "Form and Content of African music : A case Study of Bukusu Circumcision Music." Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Pretoria (Haijachapishwa).
- Wanyama, M.N. (2005). "Ujumi katika Muziki wa Kiafrika: Mfano wa Muziki wa Tohara ya Wabukusu." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi (Haijachapishwa).
- Winstone, N.J. (2006). "Mwonoulimwengu wa Waswahili Jinsi Unavyojitokeza katika Ngano." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho cha 1: Mwongozo wa Maswali Ya Usaili Nyanjani

#### Utangulizi

Mimi ni mwanafunzi kutoka chuo Kikuu cha Moi, Kenya. Jina langu ni **Ramadhani Thomas Kadallah**. Ninafanya utafiti kuhusu **Utendaji katika Nyimbo za *mdumange* za jmmii ya Wasambaa wa Lushoto, Tanga- Tanzania**. Ili nifanikishe utafiti huo naomba ushirikiano wako kwa kujibu maswali yafuatao:

#### Taarifa za Watafiti waliosailiwa

- i. Jina la Mtafitiwa .....
- ii. Umri wako .....
- iii. Je, Ulizaliwa katika:
  - Kijiji cha .....
  - Kata ya .....
  - Wilaya ya ...
  - Mkoa wa .....

#### Maswali kuhusu Muktadha na Miundo ya Nyimbo za *Mdumange*

- a. Maana ya *Mdumange* ni nini?
- b. *Mdumange*:
  - Ulianzishwa na nani?
  - Ulianza lini?
  - Ulianza katika kijiji/kata/Wilaya gani?
  - Unatendwa katika matukio gani? (harusi, jando, .....
  - Unahusisha watu wa aina gani? (vijana, wazee, wanawake, wanaume)
- c. Je, maudhui ya nyimbo za *mdumange* yanahusu nini? (siasa, dini, malezi au mapenzi?)
- d. Nyimbo za *mdumange* zinahusinaje na:
  - Nyimbo za kupunga mapepo
  - Nyimbo za maombolezo
  - Miviga ya vijana wa kiume (gao) na miviga ya wanawake (Nkimbizi)
  - Dini ya Ukristo na Uislamu
  - Utawala wa kichifu
  - Utawala wa mkoloni

- Utawala baada ya ukoloni (Nyerere, Mwinyi, Mkapa, Kikwete na Magufuli)
- e. Kando na *mdumange*, ni sanaa gani nyingine hutendwa katika jamii ya Wasambaa kwa;
- Kuhusisha uimbaji, upigaji ngoma na uchezaji
  - Kuhusisha uimbaji peke yake
  - Kuwahusisha wanaume peke yao
  - Kuwahusisha wanawake peke yao
  - Kuwahusisha vijana peke yao
  - Kuwajumuisha vijana na wazee mahali pamoja
  - Kuwajumuisha wanaume na wanawake mahali pamoja
- f. Je, Nyimbo za *mdumange* hutendwa:
- Katika matukio gani? (ya furaha au huzuni?)
  - Siku gani (siku yoyote au kuna siku maalum)
  - Wapi (mahali popote au kuna sehemu maalum)
  - Wakati (muda wowote au kuna muda maalum)
- g. Tangu kuanzishwa kwake mpaka leo ni mambo gani katika nyimbo za *mdumange*:
- Yamebadilika sana
  - Yamebadilika kidogo
  - Hayajabadilika kabisa
- h. Kwa nini baadhi ya mambo katika nyimbo za *mdumange* yamebadilika na mengine hayajabadilika?
- i. Unafikiri mabadiliko yaliyotokeza katika nyimbo za *mdumange* yana athari yoyote?
- j. Je, wewe ulijifuzaje uimbaji, upigaji ngoma na uchezaji wa *mdumange*?
- k. Kati ya uimbaji, upigaji ngoma na uchezaji kipi kinatakiwa kianze? Kwa nini?
- l. Je, kuna maneno/nyimbo maalum zinapaswa kuimbwa mwanzoni, kati kati au mwishoni? Kwa nini?
- m. Ni kwa nini katika nyimbo za *mdumange* baadhi ya beti/maneno hurudiwa rudiwa sana?
- n. Je, nyimbo unazoimba zinawakilisha mambo ya kweli au ni ubunifu tu unaoufanya kwa ajili ya kuburudisha?
- o. Wewe unatungaje nyimbo zako?

- Papo kwa papo wakati wa hafla?
  - Unaziandaa kwanza kwenye karatasi na kuzifanyia mazoezi na unazikariri?
  - Unaimba nyimbo unazozikumbuka ambazo ulishawahi kuziimba wewe mwenyewe?
  - Unaimba nyimbo unazozikumbuka ambazo uliwahi kuzisikia zikiimbwa na wasanii wengine?
- p. Ipi ni mbinu bora, kwa vijana kujifunza sanaa ya *mdumange*? je, yafaa wajifunza mapema wakiwa wadogo au wasubiri mpaka wakiwa watu wazima? Je, watajifunzaje?
- q. Eleza jambo lolote unalofikiri limechochea kuibuka, kustawi na kubadilika kwa utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika jamii ya Wasambaa.
- r. Je, una swali lolote ungependa kuniuliza?
- s. Ninakushukuru sana kwa ushiriki wako, maoni yako yatanifaa sana katika utafiti wangu. Kabla hatujafunga mazungumzo yetu kama hutajali ninaomba nikupige picha au tupige picha pamoja.

#### **Maswali Kuhusu Mitindo ya Utendaji wa Nyimbo za *Mdumange***

- a. Ni kitu kinacozitofautisha nyimbo za *mdumange* dhidi ya sanaa nyingine?
- b. Ni mikakat gani inafanywa na fanani ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira?
- c. Je, ni majukumu gani yanafanywa na hadhira ili kuurutubisha utendaji?
- d. Kwa nini nyimbo za *mdumange* zinatumiwa mbinu zifuatazo:
  - Tasfida, Tashihisi, Sitiari
  - Matumizi ya lugha za Kisambaa, Kiswahili na Kingereza
  - Methali na nahau
- e. Viungo vya mwili vinatumikaje kuwasilisha ujumbe?
- f. Viungo vya mwili vina umuhimu gani katika nyimbo za *mdumange*?
- g. Mwengo, ngao ya Sheuta, gunda, filimbi, segele, na kaniki vinawakilisha nini katika utendaji?
- h. Ni sifa zipi zinampambanua mtendaji mwenye ujuzi dhidi ya mtendaji asokuwa na ujuzi?

#### **Maswali Kuhusu Dhima ya utendaji wa nyimbo za *mdumange* katika jamii ya Wasambaa**

- a. Ni maudhui gani yanakuzwa na kuendelezwa katika nyimbo za *mdumange*?
- b. Maudhui hayo yanawasilishwaje?

- c. Maudhui hayo yana nafasi gani katika kuenzi, kukuza na kuendeleza:
- Historia ya Wasambaa
  - Kutambulisha Utamaduni wa Kisambaa (ndoa, mirathi, uganga, malezi)
  - Kuhifadhi maadili ya Wasambaa
  - Kuelezea masuala ibuka (maradhi, mazingira, mapenzi, madawa ya kulevya)
  - Kukuza lugha ya Kisambaa
  - Kupinga unyonyaji wa sampuli mbalimbali
  - Kuhamasisha demokrasia na utawala bora
- d. Kuna uhusiano gani kati ya mitindo ya lugha na viziada lugha vinavyotumika katika nyimbo za *mdumange*?
- e. Una maoni gani kuhusu hatari ya kupotea au kufa kwa sanaa ya *mdumange*?
- Kitu gani kinahatarisha kustawi kwake?
  - Tufanyeje ili tuzinusuru nyimbo na sanaa ya *mdumange*

**ASANTE SANA KWA USHIRIKIANO WAKO**

**Kiambatisho na. 2: Mwongozo wa Maswali katika Mijadala ya Vikundi**

1. Ni nani mtu wa kwanza kuishi katika hii milima ya Usambara? Ilikuwa lini?
2. Kwa maoni yako, unafikiri kuna koo ngapi za Wasambaa?
3. Je, ni mambo gani yanatambulisha koo hizo?
4. Watu wafuatao wana umuhimu gani katika historia ya Wasambaa?
  - Sheuta, Kimweri, Bughe, Wakilindi
5. Tunapozungumzia kuhusu mila/utamaduni wa Msambaa tunarejelea vitu gani
6. Je, ni kwa kiwango gani mila na tamaduni hizo zimeathiriwa na utandawazi, dini za Uislamu na Ukristo?
7. Je, tamaduni za Wasambaa za sasa ni sawa na za zamani? Ipi tofauti yao?
8. Nyimbo za *mdumange* zilianzishwa na nani, mwaka gani?
9. Je, nyimbo hizi zina umuhimu wowote katika jamii?
10. Kwa nini nyimbo za *mdumange* hazitendwi kwenye misiba?
11. Je, lugha inayotumika kwenye nyimbo za *mdumange* ni ya kisanaa au ni ya kawaida?
12. Kwa nini wasanii wa nyimbo za *mdumange* wanatumia tasfida, tashihisi tanakali za sauti. Fomula simulizi na methali katika utendaji wao?
13. Dhana zifuatazo zinawakilisha nini katika utamaduni wa Kisambaa?
  - Mviga wa gao,
  - Mviga wa Nkimbizi
  - Fika ya chekecheke, kirurumo na huto
  - Kutua nyungu
14. Vifaa vifuatavyo vina maana gani katika sanaa ya *mdumange*?
  - Ngoma, vazi la sufi, usinga, kishadda, mwengo, gunda, filimbi, Fimbo ya Sheuta.
15. Je, kuna yeyote kati yenu angetaka kuniliza swali kuhusu utafiti huu?
16. Ninawashukurni sana kwa ushirikiano mawazo yenu yatanifaa sana kaika utafiti wangu.
17. Sasa kabla hatujafunga mjadala wetu, ninakuombeni tutoke nje kwa ajili ya picha ya pamoja (kwa wale watakaokuwa tayari).

**SHUKRAN**



**Kiambatisho na. 3: Watafitiwa Walio Shiriki Usaili na Mijadala ya Vikundi**

| <b>JINA</b>                 | <b>JINSI</b> | <b>UMRI</b> | <b>KIJIJI NA KIKUNDI<br/>CHA MDUMANGE</b> |
|-----------------------------|--------------|-------------|---|
| 1. Abeid Idd                | ME           | 34          | Kijiji cha Kivilicha                      |
| 2. Alhaji Housein           | ME           | 55          | Kijiji cha Kwemhafa                       |
| 3. Bituni Makau             | KE           | 30          | Kijiji cha Ngua/Mbuzii                    |
| 4. Dhahabu Zuberi           | ME           | 40          | Kijiji cha Mgwashi                        |
| 5. Fatuma I. Mdoe           | KE           | 53          | Kijiji cha Magoma                         |
| 6. Halima Athumani          | KE           | 35          | Kijiji cha Mlalo Kaya                     |
| 7. Hasina Shomari           | KE           | 65          | kijiji cha Kwezindo                       |
| 8. Hondo Bakari             | ME           | 46          | Kijiji cha Kihitu                         |
| 9. Imamu Hamisi             | ME           | 45          | Kijiji cha Mlalo Kaya                     |
| 10. Jumaa Shekalage         | ME           | 67          | Kijiji cha Magoma                         |
| 11. Kimweri Ngovi           | ME           | 36          | Kijiji cha Lushoto Mjini                  |
| 12. Kristina M. Singano     | KE           | 54          | Kijiji cha Mgwashi                        |
| 13. Mashina Shine (Mhidini) | ME           | 49          | Kijiji cha Mtae                           |
| 14. Musa Mhidini            | ME           | 22          | Kijiji cha Kwezindo                       |
| 15. Mzee Mayai              | ME           | 39          | Kijiji cha Kivilicha                      |
| 16. Rahel Daniel            | KE           | 55          | Kijiji cha Lwandai                        |
| 17. Rozi S. Fedriki         | KE           | 55          | Kijiji cha Lushoto Mjini                  |
| 18. Sabitina B. Mtunguja    | KE           | 52          | Kijiji cha Soni                           |
| 19. Selemani Kijemkuu       | ME           | 50          | Kijiji cha Soni                           |
| 20. Shauri S. Shemshuza     | ME           | 86          | Kijiji cha Ngua/Mbuzii                    |
| 21. Siti Shewedi            | ME           | 25          | Kijiji cha Kihitu                         |
| 22. Sofia Shauri            | KE           | 33          | Kijiji cha Mtae                           |
| 23. Wiliam Salehe           | ME           | 40          | Kijiji cha Lwandai                        |
| 24. Zakati Hamza            | KE           | 34          | Kijiji cha Kwemhafa                       |

**Kiambatisho cha 4: Nyimbo za Mdumange****1. Sitaweza kupanda mlima****KISAMBAA**

1. Se n'dahe hakwea ee, Se n'dahe hakwea ee
2. Waiya iya baba ee, se n'dahe hakwea ee
3. Ooe waiya iya baba ee, se n'dahe hakwea ee
4. Kweli se n'dahe hakwea ee (I)
5. Sauti ya kinanda ee, sauti ya kinanda ee
6. Ooe waiya iya baba, sauti ya kinanda,
7. Iyee waiya iya babae sauti ya kinanda
8. Kweli sauti ya kinanda ee (II)
9. Imba wewe imba wewe, imba wewe ee
10. Ooe waiya iya kaka ee imba wewe imba wewe
11. Iyee waiya iya kaka imba wewe imba wewe
12. Kweli imba wewe imba wewe ee (III)

**KISWAHILI**

1. Sitaweza kupanda mlimani
2. Kaka nalia sitaweza kupanda mlima
3. Ooe nalia kaka
4. Kweli sitaweza kupanda mlimani (I)
5. Hii ni sauti ya kinanda ee
6. Ooe nalia kaka
7. Iyee nalia kaka ee
8. Kweli hii ni sauti ya kinanda eee (II)
9. Sasa ni zamu yako kuimba eee
10. Ooe nalia kaka eee
11. Iyee nalia kaka
12. Kweli ni zamu yako kuimba (III)

**2. Ni wewe****KISAMBAA**

1. Ni wewe ni wewe ni wewe
2. Ni wewe hongea
3. Uwo moyo wako siukunda
4. Iyo sura yako siikunda
5. Bola du mai ngwa ya mame
6. Ilawe salama

**KISWAHILI**

1. Ni wewe ni wewe ni wewe
2. Ni wewe hongera
3. Huo moyo wako siutaki
4. Hiyo sura yako siitaki
5. Ilimuradi mahari ya mama
6. Itoke kwa amani

**3. Zaina umeacha wanao****KISAMBAA**

1. Uteasha wanao Zaina Maisha ya Bongo ni mabaya
2. Kuna kufa weangu Zumiai wa lelo tije dumange (I)
3. Kuna kufa wa baba Zumia wa lelo tije dumange (II)

**KISWAHILI**

1. Umeacha wanao Zaina Maisha ya Bongo ni mabaya
2. Kuna wakati utafika tutakufa jamani Leo itikieni tufurahie dumange (I)
3. Kuna wakati utafika tutakufa Kaka itikieni tufurahie dumange (II)

#### 4. Hunithamini

##### KISAMBAA

1. Hati n'ng'wanangu uzan'hoka
2. Kwa kuti baba hunifanyanya
3. Imi se n'dahe tabia za mzi
4. N'kunda niite na kwetu

##### KISWAHILI

1. Kama ni mwanagu  
ushaninyang'anya
2. Kwa kuwa kaka hunithamini
3. Mimi sitaweza tabia za mji huu
4. Nataka niende kwetu

#### 5. Ngomani

##### KISAMBAA

1. Siitangiwa kwengoma
2. Bila baba haizie kaya
3. Ae ae baba
4. Labda ukaaghie nyika (I)
5. Kisa cha kutoighwa
6. Sindati n'chielewe bwana
7. Ae ae baba
8. Labda ukaaghie kwenyu (II)

##### KISWAHILI

1. Siitwi ngomani
2. Kabla kaka yako hajaja  
nyumbani
3. Ae ae kaka
4. Labda ukimbilie mjini (I)
5. Kisa cha kupigwa
6. Bado sijakifahamu bwana
7. Ae ae kaka
8. Labda ukimbilie kwenu (II)

#### 6. Juma anatafuta mchumba

##### KISAMBAA

1. Juma aonda mchumba
2. Kaka Juma ng'waka washia
3. Juma ee uonda mchumba
4. Eo nane ng'waka washia (I)
5. Juma nionda mchumba
6. Juma ee ng'waka washia
